

**MABADILIKO YA KIFONOLOJIA NA KISEMANTIKI KATIKA MANENO
YA KISWAHILI YENYE ASILI YA KIARABU**

HUSSEIN ALI HUSSEIN

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SHARTI LA KUKAMILISHA
KUHITIMU SHAHADA YA UZAMIVU (PhD) YA KISWAHILI KATIKA
SKULI YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIGENI YA CHUO KIKUU CHA
TAIFA CHA ZANZIBAR**

DISEMBA 2016

TAMKO

Mwanafunzi

Hii ni kazi yangu asilia na haijawasilishwa kwa ajili ya tunuku ya Shahada au tunuku yoyote katika Chuo chengine chochote.

.....
Saini

Hussein, Ali Hussein

Na.ya Usajili 2012/01/00005/TZ

.....
Tarehe

Wasimamizi :

Sisi tunathibitisha kwamba kazi iliyoelezwa katika tasnifu hii imefanywa na mwanafunzi chini ya usimamizi wetu.

.....
Saini

Abdul-aziz Y. Lodhi

Professor Emeritus,
Dept. of Linguistics & Philology,
Uppsala University, Sweden.

.....
Tarehe

.....
Saini

Dkt. Abubakar M. Fasih

Idara ya Lugha za Kigeni, Chuo Kikuu cha
Taifa cha Zanzibar, Tanzania.

.....
Tarehe

TABARUKU

Kwanza kwa uwezo wake Muumba na shani yake ya kunifikisha hapa nilipo na kama nilivyo hivi sasa, lakini pili kwa wazazi wangu, walezi na walimu wangu wa ngazi zote tangu ya awali hadi hii niliyofikia. Maelekezo, busara na wasia wao kwangu ni hazina endelevu isiyokwisha katika matumizi yote ya maishani mwangu.

SHUKRANI

Kukamilika kwa kazi hii na kuwa tasnifu ni matokeo ya juhudi za watu wengi, kuwataja wote hapa haitakuwa rahisi hata kidogo. Nianzie kutoa shukrani za dharti tena maalumu na za pekee ziende kwa Mwalimu wangu, Msimamizi wangu Mkuu Prof. Profesa Abdul-aziz Y. Lodhi bila ya yeye pamoja na maelekezo, mchango na msaada wake, kazi hii isingekuwa kama hivi ilivyo. Kadhalika shukrani za kiwango kama hicho ni kwa Msimamizi Mwenza Dkt. Abubakar M. Fakih, licha ya majukumu yake mazito tena mengi hayakumwekea kikwazo katika usimamizi wake kwenye kazi hii. Udhaifu, kasoro na nuksani zitakazoonekana katika kazi hii, napenda kukiri kwamba ni za mtafiti mwenyewe binafsi. Pamoja na hali ngumu, hasa ya ukosefu wa fedha, inayokikabili Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar; shukrani za dharti kabisa ninazitoa hasa kwa Uongozi wa juu wa Chuo kwa kuzingatia msembo wetu wa Kiswahili usemao “ Kutoa ni moyo usambe utajiri”, kwa hicho hicho kichache mno kilichokuwepo tulimegewa pamoja na maliwazo mazuri. Asiyeshukuru kidogo hashukuru kwa kingi pia. Hakuna walioguswa na kuathirika kama mke na watoto wangu kutokana na kuwachama kwa muda mkubwa wakati wa shughuli ya ukusanyaji, uchambuzi wa data na uandishi wa kazi hii pamoja na ule muda wa Kozi ya darasni. Kutokana na uvumilivu wa hali juu waliouonesha, nawapongeza bali pia nawashukuru si kwa uvumilivu wao waliouonesha tu bali pia kwa maneno yao ya kunitia moyo na maliwazo mazuri. Ili nisiwe mwizi wa fadhila, nawashukuru walimu wangu hasa wale walionifunza katika ngazi hii na mwenyewe nikiwa kwenye umri wa kuendea uzeeni.

Lakini kama nilivyotangulia kusema kwamba kukamilika kwa kazi hii kunatokana na juhudi za watu wengi, kwa hivyo wale ambao hawajatajwa hapa, nawathibitishia

kwamba maoni, michango na mawazo yao yanathamiwa na kukadiriwa kwa kiasi kikubwa tena nawashukuru sana.

YALIYOMO

TAMKO	i
TABARUKU	ii
SHUKRANI	iii
YALIYOMO	v
MAJADWELI	vii
IKISIRI	viii
SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA JUMLA	1
1.1 Utangulizi	1
1.2 Historia Fupi ya Kiarabu	3
1.3 Historia ya Kiswahili kwa Ufupi	5
1.4 Sauti za Kiswahili na Kiarabu	8
1.5 Mada ya Utafiti	13
1.6 Tatizo la Utafiti	13
1.6.1 Usuli wa Tatizo	13
1.7 Lengo la Utafiti	14
1.8 Malengo Mahsusi	14
1.9 Maswali ya Utafiti	15
1.10 Umuhimu wa Utafiti	15
1.11 Eneo la Utafiti	16
1.12 Mipaka ya Utafiti	17
1.13 Matatizo/changamoto za Utafiti	17
SURA YA PILI: KAZI TANGULIZI	18
2.1 Utangulizi	18
2.2 Kazi Zilizopitiwa	18
SURA YA TATU: NADHARIA ZA UTAFITI	23
3.1 Utangulizi	23
3.2 Nadharia Kongwe Kuu ya Istilahi	23
3.3 Nadharia Jamii ya Uundaji Istilahi	23
3.4 Nadharia ya Saikolojia ya Tabia	24
3.5 Nadharia ya Uhalisia	25
SURA YA NNE: MBINU NA NJIA ZA UTAFITI	26
4.1 Utangulizi	26
4.2 Mbinu ya Maktabani	26
4.3 Mbinu ya Mahojiano	26
4.4 Mbinu ya Kutumia Maswali ya Ana kwa Ana	27
4.5 Uteuzi wa Watafitiwa	27
4.6 Ukusanyaji wa Data	28
4.7 Vifaa vya Utafiti	28
4.8 Uchambuzi wa Data	28
4.9 Nadharia ya Uchambuzi wa Data	29
SURA YA TANO: UCHAMBUZI WA DATA	30
5.1 Utangulizi	30
5.2 Uchambuzi wa Data za Maktabani	30
5.2.1 Maneno ya Kibiashara	30
5.2.2 Maneno ya Kisiasa/utawalaKi	45
5.2.3 Maneno ya Kidini	64
5.2.4 Maneno ya Kitaaluma	86
5.2.5 Maneo ya Kijamii	118

5.2.6	Maneno ya Kiuhasibu / Kifedha	330
5.2.7	Maneno ya Kibaharia / Usafiri.....	342
5.2.8	Maneno ya Kiujenzi na Vifaa vyake.....	351
5.2.9	Muhutitari wa Uchambuzi wa Data za Maktabani	357
5.2.9.1	Utangulizi.....	357
5.2.9.2	Mabadiliko 358	
5.2.9.2	Sababu za Mabadiliko ya Kisemantiki	358
5.2.9.2.1	Kisemantiki	359
5.2.9.2.3	Kifonolojia.....	360
5.3	Uchambuzi wa Data za Uwandani	361
5.3.1	Utangulizi.....	361
5.3.2	Kipengele A - Semantiki	362
5.3.3	Kipengele B - Fonolojia.....	366
5.3.4	Kipengele C - Mofolojia	367
5.4	Uchambuzi wa Data za Njia ya Mahojiano	369
5.4.1	Utangulizi	369
5.4.2	Unasibu wa Dhana na Maana	369
5.4.3	Usahihi wa Utoaji wa Dhana	370
5.4.4	Kubakia kwa Maana Asilia ya Kiarabu	370
5.4.5	Uhusiano wa Maana Mpya na Maana Asilia za Lugha Chanzi	371
5.4.6	Kinyume cha Maana	371
5.4.7	Sababu za Kinyume cha Maana	372
5.4.8	Maoni ya Wahojiwa Juu ya Utoaji wa Maana Iwe Sahihi au si Sahihi	372
	SURA YA SITA: MATOKEOYA UTAFITI	374
6.1	Utangulizi.....	374
6.2	Semantiki	374
6.3	Fonolojia	375
6.4	Matokeo Mengine Kiujumla	376
6.4.1	Semantiki	376
6.4.2	Kipengele B Mofolojia	379
6.5	Mapendekezo na Maoni	381
6.5.1	Utangulizi	381
6.6	Hitimisho.....	384
	MAREJELEO	387
	VIAMBATANISHO	394

MAJADWELI

- Jadweli Na. 1 : Sauti za Kiswahili Konsonanti na Irabu.
- Jadweli Na. 2 : Sauti Konsonantiza Kiswahili.
- Jadweli Na. 3 : Sauti Konsonanti za Kiarabu.
- Jadweli Na. 4 : Maneno ya Kibiashara/ Kiuchumi.
- Jadweli Na. 5 : Maneno ya Kisiasa/ Kiutwala.
- Jadweli Na. 6 : Maneno ya Kidini.
- Jadweli Na. 7 : Maneno ya Kitaaluma.
- Jadweli Na. 8 : Maneno ya Kijamii.
- Jadweli Na. 9 : Maneno ya Kiuhasibu/ Kifedha.
- Jadweli Na. 10 : Maneno ya Kibaharia / Usafiri.
- Jadweli Na. 11 : Maneno ya Vifaa Vya Ujenzi.

IKISIRI

Kazi ya utafiti huu imeanzia kwa kutazama uhusiano wa kihistoria uliopo baina ya wenye lugha mbili hizi, Kiswahili na Kiarabu, pia imeangalia maingiliano ya watu hao kijamii, kiutamaduni na kidini. Maingiliano hayo yametazamwa ni kwa kiasi gani yalivyotoa mchango na kuathiri katika Kiswahili. Kwa kuwa kazi hii imejikita zaidi kwenye lugha kwa ujumla na hasa kwenye maneno yenye usuli wa Kiarabu, ilionekana ni vyema kupata historia fupi mno za lugha mbili hizi. Kutokana na mada ya utafiti huu ambayo ni “Mabadiliko ya Kifonolojia na Kisemantiki katika Maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu”. Kwenye tatizo la utafiti, inaonekana kumekuwa na utaratibu wa kuchukuliwa maneno ya Kiarabu na kuingizwa katika Kiswahili. Imebainika kwamba maneno hayo au baadhi yake yanapewa maana nyengine kinyume na ile maana ya asili au wakati mwingine maana hizo katika Kiswahili zinakuwa hazina usahihi kwa mujibu wa maoni ya mtafiti. Kwa hivyo, lengo kubwa la kazi hii ni kuyachunguza maneno hayo, baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili. Katika hali hiyo, kwa umahasusi utafiti unalenga kuyatazama maneno hayo kwa kuyachunguza, kifonolojia na kisemantiki kwenye Kiswahili na Kiarabu. Umuhimu uliopo kwenye utafiti huu ni kwamba katika utaratibu mzima wa kukopa maneno ni kwa ajili ya kuongeza uelewa zaidi, lakini pia na katika kazi ya uundaji wa maneno yenye umuhimu mkubwa na baadhi ya istilahi. Bilashaka hili ni jambo zito hasa pale maneno na istilahi hizo katika kupatiwa maana, hapa panahitaji uhakika wa maana inayotakiwa na uhalisia wake

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Utangulizi

Kazi hii, kwanza katika kipengele hiki kinaangalia uhusiano wa kihistoria uliopo baina ya Waswahili na Waarabu, maingiliano yao kiutamaduni, kijamii, kiuchumi na kidini. Maingiliano hayo yameangaliwa kwa kiasi gani yalivyotoa mchango, hususan katika lugha ya Kiswahili. Nafasi ya kila nyanja imeangaliwa ni kwa kiasi gani ilivyochangia kutoa taathira katika Kiswahili.

Pamoja na kwamba hawa Waarabu na Waswahili ni watu tafauti, ni wazi kwamba utamaduni wao pia ni tafauti. Lakini kutokana na kuwa na utangamano wa muda mrefu kati yao, (Freeman Greenville 1988) anaona kwamba utamaduni wa Kiswahili ulitokana na ubadilishanaji wa kitamaduni na hatimaye kuwa ustaarabu wa Mwambao huu ukawa wa pekee, sio wote wa kiarabu wala si wa kiafrika peke yake. Ustaarabu wa Kiswahili umetokana na ustaarabu wa kiafrika na kiislamu, utamaduni wa kibiashara pamoja na mtiririko wa jamii za kilimo na kivuvi, na kuushibisha nyenzo za kitamaduni na nasaba ya kibailojia na michango mingine kutoka Bahari ya Hindi, Bara Hindi, Ghuba ya Uajemi na sehemu za Kusini ya Bahari ya Sham. Hali hii inashuhudiwa waziwazi kwa viwango tafauti vya imani kubwa ya Kiislamu ya madhehebu ya Sunni, Fasihi, Muziki, Usanifu majengo, Mavazi, Mapishi, Mila na Silka katika Mwambao wa Afrika Mashariki (Lodhi 2000).

Kwa hivyo ni dhahiri kuwa zilitokea taathira. Je, taathira hizo ni kwa kiasi gani zinaonekana katika lugha ya Kiswahili?.

Suala la uchumi nalo halikuwa nyuma katika shughuli na harakati za watu wa pande mbili hizo. Biashara kati yao ilishamiri, iwe kwa mabadilishano ya bidhaa kwa bidhaa au kwa njia nyengine yoyote. Kwenye Mwambao wa eneo hili la Uswahilini, biashara ilikuwa yenye faida, kwa kiwango cha juu cha ubadilishanaji katika karne ya kumi na nne na kumi na tano zilitoa jamii za wakulima, wavuvi na wafanyabiashara wenyeji walioingiliana na matajiri kwa matumaini ya kutumia nafasi yao ya kujinufaisha wao wenyewe (Spear 2000). Wakati wa nusu ya karne ya 18 (Whiteley 1969), kidogokidogo lakini kwa uhakika, Kiswahili kilipenya ndani ya Mashariki ya Afrika na kufikia Maziwa Makuu, hususan pamoja na ueneaji wa misafara ya kibiashara na usafirishaji wa watumwa, pamoja na mahitaji makubwa makubwa ya pembe za ndovu katika nchi za Magharibi na mahitaji ya kilimo na watumwa wa ndani kutokana na ukuaji wa mashamba ya bara ndani kwenye vituo vya mijini na kwenye Mwambao . Mahusiano hayo ya kiuchumi, kwa upande wa lugha, bila shaka yaliacha athari. Je ni athari gani hizo?, hapana shaka yapo maneno katika nyanja hii, nayo hayakufumbiwa macho, mtafiti aliyaangalia katika kazi yake hii.

Kwa hali yoyote, watu hawa kwa kuwa walikuwa na ukaribu ndani ya jamii waliyoishi, pamoja na kasoro ndogo ndogo za kibinaadamu walizokuwa nazo, walifarijiana, waliliwazana, walipongezana na walisaidiana kwa njia mbalimbali. Hali hii, bila ya kificho, inaonekana kwa kupitia maneno yaliyopo katika nyanja hii.

Asilimia kubwa mno ya Waswahili, ambao ndio wenyewe wa hiyo lugha ya Kiswahili, ni waumini wa Dini ya Kiislamu. Dini hiyo ya Kiislamu ni kiungo muhimu kilichowaweka pamoja watu hawa. Hali hii, (Allen 1981 na Harries 1964) wanaonekana kulishuhudia hilo kwamba Waafrika wenyeji walishirikiana na waliukubali Uislamu kama Dini ya wenyeji iliyounda utamaduni ambao ndani yake

maneno “mswahili” na “muislamu” yamekuwa ni sinonimu. Uislamu umekuwa ni sifa tambukizi ya utamaduni wa Kiswahili. Miji na wenyeji wake waliikumbatia dini mpya pamoja na nufudhi (nguvu) zake kwenye utu uliojaa wema. Walinganiaji na wafanyabiashara wa Kiarabu waliacha alama pekee katika Mwambao wa Zanzibar, pamoja na uchambuzi zaidi katika utamaduni wa Kiswahili. Mtu anaweza kuona mng’ang’anio na ueneaji wa mila za kiafrika kwenye dini ya (eneo la) Mwambao. Misikiti ipo kila mahali katika mwambao wa Afrika ya Mashariki na nufudhi ya kiislamu imepenya na kuenea kwenye vituo vya miji katika sura ya Vyuvo vya Qur-aan, lakini pia na mifumo ya miji inaonesha taathira ya Uislamu (Middleton 1992). Kutokana na hali hiyo yumkini chimbuko kubwa na chanzo cha maneno yenye asili ya Kiarabu, ikawa mwanzo wake ni kutokana na lugha kuu ya Dini ya Kiislamu nayo ni Kiarabu Fasaha, lugha ya Qur-aan tukufu. Ukweli wa mambo ni kuwa bado Waarabu na Viarabu vyao, wanapiga magoti kwa Masheikh wenye Elimu ya Qur-aan na Kiarabu kujifunza kama Waislamu wengine. Katika hali kama hiyo, walinganiaji Waislamu wa mwanzo waliofika pwani ya Afrika Mashariki (maeneo ya Waswahili) lugha yao ilikuwa ni Kiarabu. Wenyeji wa maeneo hayo waliukubali Uislamu, bila shaka walijifunza lugha ya walinganiaji hao kwa njia mbalimbali. Katika upande huu, yaliangaliwa maneno yaliyopo na yanayotumika, na kwa kiasi gani taathira yake imetokea kilughawiya.

1.2 Historia Fupi ya Kiarabu

Kiarabu ni lugha/lahaja pekee iliyoendelea na inayoendelea kuishi kati ya lahaja kongwe katika makundi ya lahaja zilizokuwepo kabla ya Uislamu, lahaja ambazo zilithibitishwa kwamba zina maandishi tangu karne ya nne (4) KK. Kiarabu kama lugha ya maongezi ni ya kale, inathibitishwa hivyo kutokana na maandishi yake.

Kwani maandishi yake makongwe zaidi yanarudi kwenye miaka ya 512 - 568 KK ambapo abjadi ya Kiarabi ilianzishwa kwa Waarabu kupitia kwa wafanyabishara wa Dola ya Bahari ya Kati (Mediterranea), ambapo Waarabu walianza kutumia maandishi katika zama za Ukristo Mashariki ya Kati. Kutoka Kiarabi, Maandishi hayo yaliendelea kwa kupitia Dola mbili za Nabatiya na Palmyran ndani ya eneo hilo. Ndani ya Baraarabu, matumizi ya lugha hii yalikuwepo kwa karne nyingi. Chaker (2012:49) anadai kwamba historia ya maandishi ya Kiarabu mwanzo wa kujulikana kwake hauko waziwazi lakini herufi zake, maumbo yake yalikuwa waziwazi na kujulikana na Waarabu wenyewe hata kabla ya Uislamu. Kwani wakati huo kulikuwa na utamaduni wa mashairi simulizi kabla ya mashairi hayo kuandikwa hapo mwishowe. Ingawa mashairi yao hayo ndani yake yalikuwa na mambo ya kilughawiya yasiyokuwa ya kawaida, lakini mashairi yalihifadhiwa kimaandishi pamoja na kwamba yalikuwa na tafauti ya kitahaja na utamkaji ambao ulitumiwa na maandishi mbalimbali katika kujaribu kurekodi kimaandishi mashairi ambayo hapo mwanzo yalisemwa tu. Bila shaka tafauti hizi, ziliakisi lahaja mbalimbali ambazo zilikuwa na taathira kubwa kwenye Kiarabu Andishi na namna gani matini hizo zilivyorekodiwa kimaandishi. Hali hiyo ya Kiarabu ilinawiri katika karne ya sita (6) pamoja na kwamba maandishi ya kazi hizo hayakuandikwa mpaka kufikia karne ya nane (8) na ya tisa (9).

Katika hali ya kuonesha ukongwe wa lugha ya Kiarabu, Abubakr (1992:11-13) kuna maandishi yaliyogunduliwa Nimara (Mlima Durouz) ya mwaka 328 BK ambayo matini yake ni ya Kiarabu.

Lugha sanifu au Lugha ya Qur-aani kama inavyoitwa ndiyo lugha ambayo ilitumika kabla ya Uislamu ndani ya Baraarabu mpaka kufikia Utawala wa Abbasiya. Lugha hiyo sanifu ndiyo chimbuko hasa la Kiarabu sanifu cha kisasa ambacho kinatumika

kwa upeo mpana katika nyanja mbalimbali rasmi kama vile Mwahala mwa kazi, Maskulini, Vyuoni, Vyuu Vikuu na kwenye Vyombo vya Habari.

Wikipedia , The Free Encyclopedia “ Arabic”. URL : en.wikipedia.org/wiki/Arabic_Language 10 /07 / 2014.

1.3 Historia ya Kiswahili kwa Ufupi

Kabla ya kuangalia historia kwa ufupi ni vizuri, japo kwa muhtasari, kupata chasili cha neno Kiswahili.

Tamko Kiswahili, ni neno la Kiswahili linalomaanisha lugha. Vilevile neno hili hutumiwa katika Kiingereza. Jina Kiswahili linatokana na wingi wa neno la Kiarabu *sawaahil* ambapo umoja wake ni *saahil* likiwa na maana ya ‘ufuo’ au “upwa”. Hutumika kama kivumishi kwa maana ya mkaazi wa pwani. Kiambishi “ki” kinamaanisha lugha. Hiki ni kiambishi awali kiambishwacho na nomino za Ngeli za majina ambazo zimo katika lugha za kibantu.

Kwa mujibu wa Spear na Nurse (1985), Hinnebusch (1993) wanasema kwamba usuli wa Kiswahili unatokana na kundi la Kisabaki la Kaskazini Mashariki la tawi la kundi dogo la kiocha cha lugha za Niger- Congo. Hivi sasa kwa ujumla wanalughawiya na wanahistoria wanalikubali hilo (Mazrui na Shariff 1994, Middleton 1992) kwamba Kiswahili kilijitokeza kama lugha ya mjini katikati mwa melania ya kwanza BK na nafasi yake iliimarishwa na ujio wa Uislamu kwenye Mwambao.

Kiswahili ni lugha ya maeneo ya Pwa za kutoka Somalia ya Kusini mpaka Msumbiji kaskazini yakiwemo maeneo ya pwani ya Tanzania na Kenya. Hapo mwanzo, Kiswahili kilizungumzwa na wenyeji wa mwambao na kikaenea kama lugha za wavuvi kwenye visiwa mbalimbali vinavyozunguuka upwa wa Waswahili. Wafanya biashara wa visiwa hivyo walikuwa na maingiliano makubwa na watu wa pwani toka

karne ya pili (2) BK. Lugha hii ilianza kuenea kwenye upwa wa Waswahili kwenye karne ya sita (6) BK. Kuna ushahidi wa kiutamaduni wa Wazaramo kutoka Dar es salaam ambao ni wakaazi wa mwanzo wa visiwa vya Zanzibar, waafrika wa visiwa hivyo wana utamaduni ambao una asili ya wakaazi hao wa mwanzo. Wahamiaji kutoka Ghuba ya Uajemi na Oman walikuja na wakaeneza Dini ya Kiislamu na hivyo basi yakaongezeka maneno ya lugha hiyo ya Kiswahili. Wahamiaji hao walijenga ngome na miji kwenye vituo vikuu vya biashara na utamaduni maeneo ya Kusini k.v Sofala, Kilwa na kwa Kaskazini k.v Mombasa, Lamu, Visiwa vya Komoro, Madascar na Barawa kusini mwa Somalia. Waarabu wa Oman waliohamia Zanzibar walianzisha kilimo cha mikarafuu katika visiwa vya Zanzibar. Mahitaji ya karafuu, punde tu kwa wakati huo, yalianzisha njia za kimataifa za kibiashara. Wafanyabiashara wazungumzaji wa Kiswahili walistakimu katika vituo vidogovidogo vya kibiashara kwenye njia mpya za kibiashara. Kwa kiasi kikubwa mchakato huu ulianzisha maendeleo ya Kiswahili cha kileo. Pamoja na hayo, kuenea kwa Kiswahili kulikwamishwa na ukoloni wa Ulaya, ueneaji huo haukutokea upande wa Magharibi wa Ziwa Malawi uliojulikana kwa jina la Kongo ya Ubelgiji, hivi sasa Jimbo la Katanga katika Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, kwa hivyo Kiswahili kikawa cha upili badili ya kuwa lugha kuu kweye eneo hilo.

Baada ya Ujerumani kushambulia eneo lililojulikana kama Tanganyika (hivi sasa Tanzania Bara) na kulitawala mwaka 1886, ilibaini ueneaji wa Kiswahili. Kwa hivyo mara tu Kiswahili kikachaguliwa kama lugha ya Koloni hilo, lugha rasmi ya Utawala. Waingereza kwa upande wao, hawakufanya hivyo katika nchi ya Kenya, hata hivyo walifanya jambo fulani katika upande huo. Waingereza na Wajerumani waliupa nguvu utawala wao katika makoloni hayo ambapo wananchi wa nchi hizo kwa madarizeni walizungumza lugha mbalimbali – kwa hivyo wakuu wa kikoloni

waliichagua lugha moja ya kienyeji ambayo walitarajia kwamba wenyeji wangeikubali. Kiswahili ndicho kilichokuwa pekee ndani ya makoloni hayo mawili.

Hatua muhimu katika kuenea kwa Kiswahili ilikuwa ni kuunda lugha ya uandishi sanifu.

Baada ya Vita vya kwanza vya dunia, Uingereza ilihisi kuwa ipo haja yakuwa na lugha sanifu itakayotumiwa katika Utawala na Elimu katika maeneo yake ya Afrika Mashariki. Usanifishaji wa lugha andishi ulifanyiwa kazi na kubadilishwa maandishi ya hati za kienyeji kwa hati za Kiswahili Kiarabu kwa alfabeti za kiromani/kizungu kama hatua ya mwanzo. Huu ni mchakato ulioanzishwa katika miaka ya 1850 na mmisionari wa Kijerumani Ludwing Krapf (Lodhi 2000) kwa ajili ya huduma za Jumuiya ya Misheni ya Kanisa (CMS) lenye makao yake mjini London. Lahaja ya Kimvita ya Mombasa aliitoa kwenye mfumo wa maandishi ya Kiromani. Baada ya kumalizika karne hiyo, zaidi ya darizeni za Sarufi na Makumusi yalitolewa na Biblia kutafsiriwa kwa Kiswahili, tafsiri moja ilikuwa kwa maandishi yote mawili kwa hati za Kiromani na hati za Kiarabu katika kila ukurasa (rudia Lodhi 2000) .

Juni 1928, mkutano wa Makoloni ulifanyika Mombasa, ambapo lahaja ya Zanzibar, Kiunguja mjini kilichaguliwa kuwa ni msingi wa usanifishaji wa Kiswahili. Lahaja hiyo, Kiswahili sanifu cha leo, ikawa inasomeshwa kama ni lugha ya Pili kwa madhumuni ya kivitendo japo kuwa kulikuwa na hitilafu kati ya usanifu wa maandishi na lugha hiyo ya Zanzibar. Wikipedia – The Free Encyclopedia, Swahili Language. URL : en.wikipedia.org/wiki/Swahili_Language 21 / 07 / 2014.

Usanifishaji ulifanywa na Kamati ya Lugha ya Utawala wa Kiingereza katika makoloni, na baadaye kuitwa Kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki hiki kilikuwa ni chombo cha usanifishaji ambapo baadaye kilisita kufanya kazi na kutoweka mwaka

1964 kilipofanyiwa mabadiliko katika Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili ya Chuo Kikuu kishiriki cha Dar-es-salaam, Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki (Lodhi 2000). Kuvunjika kwa Jumuiya ya zamani ya Afrika Mashariki mapema mnamo miaka ya 1970 kulipelekea kuundwa kwa Vyuo Vikuu vya nchi wanachama Kenya, Tanzania na Uganda. Humo vikapatikana vyombo vya usanifishaji ambavyo ni mabaraza ya Kiswahili. Kwa hivyo TUKI ikawa ni Taasisi ya Tanzania katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Na Taasisi kama hizo ziliendelezwa Mjini Zanzibar, Nairobi, Mombasa na Kampala. Hata hivyo, kazi ya uratibu wa maendeleo ya watu unashughulikiwa Tanzania Bara na Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA), Kenya (BAKIKE) na Uganda (BAKIU). Kuna Kamati za Kiswahili kama hizo katika Jamhuri za Komoro, Congo/ DRC, Burundi na Ruanda (Lodhi 2000).

1.4 Sauti za Kiswahili na Kiarabu

Utangulizi

Kwa kuwa katika kazi hii, yanaangaliwa zaidi mabadiliko ya maneno ya usuli wa Kiarabu katika Kiswahili, itakuwa si kukengeuka kusudio kama zitatazamwa sauti za lugha hasa hizi za Kiarabu na Kiswahili. Hali hii ni kutokana na kuwa mabadiliko hayo yanatazamwa katika pembe mbili, kifonolojia na kisemantiki.

Maneno ni sehemu moja tu, lakini ni muhimu, katika viambajengo vya lugha yoyote. Kwa kiasi ambacho si kidogo, kiambajengo hiki kina umuhimu wake katika lugha ya matamshi. Ni maneno, kwa asilimia kubwa zaidi, ndiyo yanayozaa sentensi, maelezo n.k kwa hivyo hiyo ndiyo lugha yenyewe.

Itakuwa ni vyema, japo kwa kadiri ndogo, zikaangaliwa sauti hizo hata kama kwa kuziainisha zile sauti za msingi katika lugha hizi mbili, kwani sauti hizo ndizo

zinazounda maneno hayo yanayo kusudiwa kuchunguzwa mabadaliko yake. Hivyo basi kutoa mwanga mdogo tu kuhusu namna zilivyo, haitakuwa jambo baya.

“Lugha zina sauti, uteuzi wa sauti hizo hauko katika mantiki au vigezo maalumu lakini ni kwa maafikiano ya kimazoea tu kwa watumiaji wa lugha fulani inayohusika”, Massamba na wenziwe (2004 : 1). Kwa hivyo kufanana na kutokufanana kwa sauti za lugha, bila shaka kutakuwepo. Kutokana na maafikiano hayo ya kimazoea, kwa upande wa Kiarabu fasaha na Kiswahili sanifu, hali hiyo ipo. Lengo kubwa kwenye kipengele hiki ni kuziainisha tu sauti za lugha mbili hizi ili kuweza kubaini mfanano na tafauti zilizopo katika lugha hizi, kwani yumkini ndani ya mabadiliko ya maneno hayo yanayochunguzwa kwenye utafiti huu, huenda sauti ikawa ni katika jumla ya sababu ya mabadiliko au pengine ndiyo mabadiliko yenyewe hasa.

Kwa hivyo sauti hizo kwenye Kiswahili ni ishirini na saba (27) Massamba na wenziwe (2004 : 40 - 41), ziko kama ifuatavyo:

	midomo	mdomo- meno	Baina meno	Uf.me	ufizi	Kaakaa.	Ki.tonge	koromeo	koo
Vipasuo									
Ghuna	b				d		g		ʔ
Sio ghuna.	p p ^h				t t ^h		k k ^h		
Vikwamizi.									
Ghuna		v	ð		z	ʃ	ɣ	h	
Sio ghuna.		f	θ			ɲ s ʃ č	x		
Kimadende.					r				
Kitambaza.					l				
Nazali.	m				n	ŋ			
Viyeyusho.	w					y			
Irabu : a ε i ɔ u									

Jadweli Na. 1 sauti za Kiswahili konsonanti na irabu

Sauti irabu za Kiswahili hizi ni tano (5) nazo ni kama hizi zifuatazo:

a ε i ɔ u

Sauti Konsonanti za Kiarabu ni ishirini na nane (28) kama anavyoziainsha Abdel-tawab (1997 : 61), nazo sauti zenyewe ni kama hizi zifuatazo angalia Jadweli Na. 3

:

Sauti irabu za Kiarabu ni sita (6). Tatu fupi na tatu refu, rejea Abdel-tawab (1997), nazo irabu zenyewe ni kama hizi zifuatazo :

a i u , a: i: u:

Sifa za sauti		Mahali pa matamshi									
		midomo	Meno-mdomo	meno	Meno ufizi	Ufizi	Kaakaa gumu	Kaakaa laini	k/tonge	Koromeo	Koo
Vipasuo	ghuna	b ب			d د , ḍ ض , ṭ ط						
	Isiyo ghuna				t ت			k ك		q ق	ʔ ء
Vikwamizi	ghuna			ḏ ذ , ḥ ح	z ز				y غ		
	Isiyo ghuna		f ف	ṯ ث	s س , ṣ ص		j ج , ḍj ج , š ش		x خ	h ه , ḥ ح	ʔ ع
Kati na kati	Ghuna	m م				n ن					
Nazali	Isiyo ghuna										
Kimadende						r ر					
Kitambaza						l ل					
Viyeyushi/nusu irabu		w و					y ي				

Jadweli Na. 2 Sauti konsonanti za Kiswahili

Namna ya matamshi		Mahali pa matamshi							
		Ghuna	Midomo	Midomo- meno	Meno	Ufizi	Kaakaa- gumu	Kaakaa- laini	Koromeo
Vipasuo	ghuna	b				d		g	
	isiyoghuna	P				t		k	
	mpumuo	p^h				t^h			
Vizuio- kikwamizi	ghuna					J			
	isiyoghuna					č			
Vikwamizi	ghuna			v	ð	z		y	h
	isiyoghuna			f	θ	s	ʃ		
Nazali		m				n	ɲ	ŋ	
Vitambaza						l			
Vimadende						r			
Viyeyushi		w					y		

Jadweli Na. 3 Sauti konsonanti za Kiarabu

1.5 Mada ya Utafiti

Mabadiliko ya Kifonolojia na Kisemantiki katika Maneno ya Kiswahili yenye Asili ya Kiarabu.

1.6 Tatizo la Utafiti

1.6.1 Usuli wa Tatizo

Kiswahili hivi sasa kinaonekana kiko katika ukuaji na maendeleo yake. Lakini pia lugha hii inapata umaarufu na kukubalika nje ya mipaka ya maeneo yake ya asili. Hali hii ya sasa ni kinyume na ile hali ya zamani, Kiswahili hivi sasa kwa kukadiria, kinazungumzwa na watu zaidi ya milioni mia moja na arubaini katika maeneo ya Afrika Mashariki na Kati (Wikipedia – The Free Encyclopedia, Swahili Language. URL: en.wikipedia.org/wiki/Swahili_Language 21 / 07 / 2014.).

Kiswahili pia kinatumiwa na Mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Ni kweli kwamba hali hii inachochea kasi kubwa ya maendeleo ya lugha hii. Katika maendeleo ya Kiswahili, kuna juhudi kubwa za nchi zinazozungumza Kiswahili katika kubuni na kuunda maneno kwa lengo la kuikuza lugha hii na kuongezea msamiati wake, aidha na kutayarisha istilahi mbalimbali kwa ajili ya nyanja tafauti za taaluma. Katika mwendelezo wa juhudi hizo; mbali yale maneno yaliyoingia kwenye Kiswahili karne nyingi zilizopita; imekuwa ni jambo la kwaida kuchukua maneno au baadhi ya vishazi kutoka kwenye Kiarabu. Jambo kubwa la kujiuliza hapa, ni je utaratibu huu unaotumika katika kuchukua maneno hayo unakubalika kwa wenye lugha, na unafaa? Kwani wao wenye lugha ndio wenye mamlaka juu ya lugha yao na ndio wanaoijua vilivyo na siyo Taasisi, Taasisi ni ajira na wala si ujuzi. Katika kipindi cha hivi karibuni miaka ishirini

mpaka thalathini iliyopita tumekuwa tukishuhudia idadi kubwa ya maneno ya Kiarabu yaliyoingia kwenye Kiswahili na yanatumika hivi sasa. Mara nyingi maneno hayo, kwa maoni ya mtafiti, yamepewa maana iliyokuwa si sahihi. Pengine yawezekana kuwa hao walioamua kuyatia maneno hayo kwenye lugha hii, maarifa yao katika Kiarabu ni madogo; kwa hivyo wakayapa dhana ambayo kwa kweli ni dhaifu na isiyokuwa sahihi katika uhalisia wa Kiswahili. Mtafiti anadhani kuwa, huu ni utaratibu usiokuwa sahihi katika huo unaoambiwa kuwa ni ukopaji. Bila shaka hili ni tatizo. Anaona ni tatizo kutokana na utoaji wa dhana kwenda kwenye lugha lengwa. Hivyo, huo ndio utaratibu ulivyo kwamba linapochukuliwa neno kutoka lugha fulani na kupelekwa kwenye lugha nyengine kwamba ni lazima dhana halisi ya neno hilo nayo ibadilishwe. Katika msingi huo, hapa ndipo linapojitokeza hilo tatizo. Kwa hivyo linahitaji kuangaliwa kwa umakini zaidi.

1.7 Lengo la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza Mabadiliko ya maneno hayo kwa ujumla baada ya kutoka kwenye Kiarabu na kuingia kwenye Kiswahili.

1.8 Malengo Mahsusi

1. Kuchunguza sauti za maneno hayo kifonolojisi jinsi zilivyokuwa kwenye lugha asili mpaka yanapoingizwa katika Kiswahili.
2. Kuyachunguza kimofolojia jinsi yalivyokuwa kwenye lugha asili hadi yanapoingizwa kwenye Kiswahili.

3. Kuyachunguza kuanzia Kisemantiki yalivyo kidhana katika lugha asilia hadi yanapoingia katika Kiswahili.

1.9 Maswali ya Utafiti

1. Je maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili kidhana yana maana mnasibu?.
2. Mbinu za utoaji dhana za maneno ni sahihi?.
3. Je maana asilia za maneno hayo ya asili ya Kiarabu inabakia kama ilivyo yanapoingizwa kwenye Kiswahili?.
4. Je kuna maneno ambayo yana kinyume cha maana?.

1.10 Umuhimu wa Utafiti

Kiswahili kina idadi kubwa ya maneno yaliyochukuliwa kutoka kwenye Kiarabu, kati ya maneno hayo yapo yale yaliyoundwa kama ni istilahi, ingawa haya si mengi na yapo yale maneno ya kawaida kama msamiati wa lugha hiyo. Umuhimu mkubwa ni kuongeza zaidi uelewa katika utaratibu mzima ambao ni muwafaka kabla ya kuyachukua maneno ya Kiarabu.

Watayarishaji wa istilahi na maneno mengine wanafanya kazi nzito na ngumu katika uundaji wake. Wao wanajaribu kuyapa maneno na istilahi hizo maana inayokusudiwa. Kutokana na kuwa kuna kanuni za ukopaji wa maneno kutoka lugha moja kwenda lugha nyengine, hata hivyo ipo haja kuwa na uhakika wa maana juu ya maneno yanayohitajika kukopwa, kwa kupitia utafiti huu, hilo litapatikana. Hivi sasa, kutokana na kuwa maneno mengi ya Kiarabu yanaingizwa kwenye Kiswahili, katika kuhakikisha, kwa kupitia kwenye utafiti, tafauti za maana au kinyume cha maneno hayo zinajuilikana.

Kiswahili kimekua na kuendelea kwa kasi na kimepata mwelekeo wa kimataifa katika matumizi na siyo kama vile kilivyokuwa hapo mwanzo kuwa ni lugha ya mahali maalumu basi. Katika hali yake ya kukua, kuendelea na kupata mwelekeo wa kimataifa kimatumizi, kuna umuhimu mkubwa wa lugha hii kuwa na msamiati wa kutosha pamoja na istilahi mbalimbali zenye dhana sahihi kimaana. Kutokana na hali hiyo, nyanja hii katika utafiti huu itachangia katika uhalisi wa kuelekeza vizuri katika kutumia njia sahihi kwenye utaratibu mzima wa kuchukua maneno kutoka kwenye Kiarabu. Vilevile utafiti huu, kwa matumaini makubwa, utawapatia watayarishaji wa istilahi na waundaji wa maneno hasa yanayotokana na Kiarabu, uwezo mzuri wa kuchagua maneno na kuyaunda kama istilahi kwa kuzingatia, kwanza maana halisi asilia kabla ya kuyapa dhana mpya katika lugha lengwa. Kwa hivyo, utafiti huu kwa kiasi kikubwa, utaimarisha dhana ambazo hazina usahihi katika utaratibu mzima wa kuchukua maneno kutoka kwenye Kiarabu. Kwa kuzingatia kuwa linalochokuliwa si neno tu, lakini ni pamoja na dhana yenyewe nzima.

Pia utafiti huu ni muhimu sana kwa kuwa ni mpya na haupatikani katika makataba zetu na kwamba haujafanywa kwa mipaka ya uelewa wa mtafiti.

1.11 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanywa katika mawanda mawili, kwanza ndani ya Maktaba katika kukusanya maneno yenye asili ya Kiarabu ambapo mtafiti alipitia vitabu mbali mbali vya Kiswahili na Kiarabu, na magazeti mbalimbali. Pili, kwa sehemu ya uwandani; kijografia utafiti umefanywa Zanzibar – hasa Mjini Unguja.

1.12 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu kitaaluma umejikita kwenye Nomino, umefanywa katika maneno hayo yenye asili ya Kiarabu katika nyanja za kijamii, kidini na kibiashara (kiuchumi), kiutawala (kisiasa), kitaaluma, kifedha na kiujenzi. Katika kila nyanja yalikusanywa maneno yanayohusika, na kila neno limeanishwa mabadiliko yake kifonolojia, kimofolojia na kisemantiki.

1.13 Matatizo/changamoto za Utafiti

- (i) Muda wa utafiti ni mchache, muda halisi uliowekwa kwa progamu hii ya uzamivu ni miaka mitatu. Mwaka mmoja ni wa Kozi ya Darasani, na miaka miwili ni kwa ajili ya Utafiti; lakini kutokana na Kozi ya darasani kuchukua mda wa miaka miwili, hali hii kwa kiasi ilichangia katika kufupika kwa muda huo wa utafiti uliowekwa na kuleta usumbufu kwa mtafiti katika kuharaka kudiriki muda.

SURA YA PILI

2.0 KAZI TANGULIZI

2.1 Utangulizi

Kwenye kipengele hiki, mtafiti alisoma machapisho na vitabu mbalimbali, tasnifu na majarida yanayohusiana na maudhui hii. Vilevile aliangalia majarida na makala mbali mbali katika mitandao. Lengo kubwa la kufanya hivyo lilikuwa ni kupata maarifa na pia taarifa juu ya mada aliyoifanyia utafiti. Pamoja na kwamba, uwanja huu unaotaalaki na utafiti huu unaoneka kuwa bado haujaandikiwa vya kutosha.

2.2 Kazi Zilizopitiwa

Hata hivyo, kile alichokipata mtafiti kilimuelekeza bali na kumuauni katika kuufanikisha na kuukamilisha utafiti huu. Katika kazi zilizompelekea mtafiti kwenye fanaka hiyo ni hizi zifatazo:

Zawawi (2004) anaeleza kwamba, maneno mengi yaliyochukuliwa kwenye Kiswahili yanatokana na Kiarabu cha Oman. Mfano mdogo wa maneno kama hayo tunayapata k.v *kem* kwa maana ya ngapi au kiasi gani, *risim* likiwa na maana ya bei ya kitu kinachouzwa, *darisha* kwa maana ya uwazi ulioachwa katika sehemu maalumu ya ukuta kwenye nyumba ili kupitisha hewa na mwangaza, *shubaka* nafasi au sehemu maalumu iliyowekwa kwenye ukuta kwa ajili ya kuwekea vitu, *bileshi* likiwa na maana ya bila ya chochote ambapo katika Kiswahili lina maana ya pasi na sababu.

Maarifa aliyoyapata hapa mtafiti, yaliongoza katika kuendelea na utafiti huu hususan kwa kuwa hapa mtafiti alichokuwa akiaangalia ni mbadiliko ya kimofolojia na kisemantiki

katika maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu, bila shaka hapa kilikusudiwa Kiarabu kwa upeo wake kwenye pembe zake zote.

Suleiman (2006) kwa kiasi kikubwa anaonesha maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili, ingawa kazi yake kwa njia moja au nyengine ilikuwa inahusiana na utamaduni, mifano mizuri tunayoipata hapa kutokana na maneno hayo ni *mali bila daftari hughibu bila habari, tahadhari kabla ya athari*, (mambo yenda) *shaghala baghala ,muhitaji hanithi lau kana rijali*. Ingawa kazi hii haikusadifu pakubwa katika utafiti huu, imesaidia kwa kiasi kikubwa katika kuangalia mabadiliko yaliyokwisha kutokea kwenye maneno hayo kisemantiki na kimofolojia.

Suweid (1999) Katika kulinganisha na kutafautisha sentensi changamano katika Kiswahili na Kiarabu, anayatumia maneno mbali mbali yenye asili ya Kiarabu katika mjengeko wa sentensi, mfano *mwalimu amehudhuria darasani kwa wakati uliopangwa, Ali amefahamu somo la lugha ya Kiarabu, nimekiona kitabu cha elimu ya dini ya kiislamu ndani ya maktaba*. Kazi hii ilimpa mtafiti nafasi zaidi ya kuendelea kutafiti maneno hayo kwa kuyaangalia zaidi kwenye mabadiliko ya kimaana katika kazi ya utafiti huu wa maneno yenye asili ya Kiarabu.

Omar (1995) Katika kazi yake anavibainisha vishazi kwa kuvilinganisha na kuvitafautisha kati ya Kiswahili na Kiarabu, mfano: *Watoto someni kwa furaha. Nyumba imepata msingi madhubuti. Kajawa na huzuni ya kufiwa na nduguye. Ukipata habari nijulishe haraka. Ewe mwanangu tahadhari fitina za umma*. Bila shaka ndani yake

vishazi hivyo mna maneno yenye asili ya Kiarabu, pamoja na kwamba kazi hiyo haiko bega kwa bega kwa kiasi kikubwa lakini bado ilitoa muongozo kwa mtafiti na kumsaidia kwa namna moja au nyengine katika kuangalia mabadiliko yaliyokwisha kutokea katika maneno hayo ndani ua utafiti huu.

Hussein (1988) katika kazi yake ambayo ilikuwa ni kulinganisha na kutafautisha katika kiwango cha kifonetiki kati ya lugha ya Kiswahili na Kiarabu, lakini anaonesha uhusiano uliopo kati ya lugha mbili hizi kwa kugusia na kubainisha kwamba ndani ya Kiswahili kuna idadi kubwa ya maneno yenye asili ya Kiarabu, kwa mfano kajaribu kuainisha maneno *thamani, thawabu, theluji, dhambi, dhoruba, dhuluma, gharama, ghanima, ghorofa, methali, sahibu, na rafiki*. Ingawa katika kazi yake hiyo, aliyatumia baadhi ya maneno hayo, katika Utafiti huu, yalitazamwa mabadiliko yake jinsi gani yalivyo katika nyanja za kisemantiki na kifonolojia.

Krum (1940) Katika kuyachunguza kifonetiki maneno yenye asili ya kigeni hasa Kiarabu kwenye Kiswahili, anaangalia tahajia, matamshi pamoja na sauti zake ngeni za kimashariki. Maneno hayo aliyoyatazama zaidi kwa upande wa sauti, baadhi ya mifano ya sauti alizoziangalia katika maneno hayo tunazipata kama vile [x], anabainisha kwamba kuna maneno mengi yamechukuliwa kutoka kwenye Kiarabu k.m *khhabari /xabari/, khitilafu /xitilafu/, khatari /xatari/, khamisa /xamsa/, na khamsini /xamsini/*. Anaona kuwa (kwa wakati huo) sauti hii kwa Waswahili haina tatizo katika kuitamka.

Kutokana na kazi yake kubwa na muhimu, bado suala zima la kutazamwa kwa undani kabisa mabadiliko ya maana ya maneno hayo hakulichunguza vya kutosha. Kwa hivyo,

ili kulijaza pengo hilo, japokuwa ni dogo, katika Utafiti huu, kipengele hiki kimempa mtafiti nafasi kubwa katika kuchunguza ndani ya utafiti huu ili kuona mabadiliko hayo.

Mwita (2009) katika kazi yake, jumla ya mambo aliyoyashughulikia ni kutazama kwa kina mfumo wa silabi wa Kiswahili dhidi ya nafasi ya irabu za maneno yaliyokopwa kutoka kwenye Kiarabu. Hapa mjadala uliopo ni juu ya kudhibiti mfumo wa silabiwazi katika Kiswahili kama vile pale linapowekwa neno katika silabi au katika kuzingatia zaidi konsonanti na katika kutia irabu. Katika kazi hii, vilevile Mwita anaweka wazi kwamba Kiswahili kwa kiasi kikubwa kinatumia uingizaji wa irabu katika usilabishaji lakini pia na taratibu nyenginezo kama vile udondoshi wa konsonanti, kuruhusu mkusanyiko wake na mabadiliko ya muundo pia huwa unatumika. Anathibitisha kwamba Kiswahili kwa tabia yake kinakubaliana na mkusanyiko wa konsonanti katika silabi k.m *alfajiri, alhamisi, mstaarabu*; hali hii inatokana na ufungamano wa Kiswahili na Kiarabu kikiwa ni lugha isiyo ya Kibantu. Katika kazi hii, inayaangalia maneno yaliyokopwa kutoka kwenye Kiarabu kwa njia ya uchambuzi kifonolojia.

Kwa hivyo, kazi hiyo ingawa haina mnasaba mkubwa na utafiti huu, ilimpa nguvu zaidi mtafiti kuendelea na utafiti wake. Hivyo aliona ipo haja ya kwenda mbali zaidi ya uwanja huo aliokomea Mwita.

Pamoja na kwamba Kiarabu na Kiswahili ni lugha zenye usuli tafauti, Kidah (2013), anaangalia mabadiliko mbali mbali ya kifonolojia na kisemantiki kwenye maneno yaliyokopwa kutoka kwenye Kiarabu. Katika kazi yake hiyo analenga zaidi katika kutazama michakato mbalimbali iliyohusishwa kwenye ukopaji wa maneno ya Kiarabu

katika Kiswahili. Inadhihirika kwamba kuna wimbi kubwa la maneno yenye asili ya Kiarabu, hilo ni jambo na matokeo ya ukopaji. Mchakato wa ukopaji huo aghalabu unapelekea kwenye uchukuaji wa maneno ya Kiarabu, na pale yanapoingizwa kwenye msamiati wa Kiswahili, baadhi ya wakati hali hii inakuwa pamoja na mabadiliko ya kisemantiki kama vile mpanuko, ufinyu na mbadiliko wa maana. Kwa kaisi kikubwa kazi yake hiyo, ina uhusiano mkubwa na pia itatoa mchango mkubwa kwenye utafiti huu, na pale ambapo Akida hakupagusia kwa undani hasa kwenye mjengeko wa kifonolojia wa maneno hayo, utafiti huu unajaribu kulifanyia kazi eneo hilo kwa kadiri inavyowezekana.

Kutokana na taathira za wageni mbali mbali waliofika Mashariki ya Afrika, k.v. Wairani, Wafursi, Wahindi, Waarabu Waturuki na Wachina; Lodhi (2015) anaangalia mkopo wa maneno ya lugha za Mashariki. Kwenye Kiarabu anatazama kwa kina zaidi kwenye maneno hayo mkopo wa kileksika, kimuundo, vitenzi na mwengezeko wake katika Kiswahili. Mfano: viambishi vitenzi vyaweza kunyambuliwa kutoka kwenye vivumishi, k.v *safi* > *safisha*, *kusafiri* > *kusafirisha*. Vitenzi vilivyokopwa kwenye Kiarabu vilevile vyaweza kuongezewa kweye nomino kwenye maneno ambayo yana asili ya Kiarabu katika Kiswahili, k.v *hesabu* > *-hesabu*, *-hesabia*, *-hesabika*, *-hesabisha*; *dhamiri* > *-dhamiria* ; *fikira* > *-fikiri*, *fikiria*, *fikirika*; *jeraha* > *jeruhi*. Mtafiti anapata fursa zaidi ya kuyaangalia maneno kama hayo katika kuyachunguza mabadiliko yake yaliyotokea ndani ya nyanja hizo alizozitazama mwandishi.

SURA YA TATU

3.0 NADHARIA ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti amezelezea nadharia alizozitumia katika utafiti pamoja na uchambuzi wa data, kama inavyoeleweka kwamba nadharia ni msingi madhubuti unaomuelekeza na kumuongoza mtafiti jinsi ya kufanya utafiti na uchambuzi wa data za utafiti. Kusudio hasa la nadharia hizi ni kuzitumia katika mawanda ya kazi hii. Katika kazi ya utafiti huu kwa jumla, mtafiti ameteua nadharia nne, “Nadharia Kongwe Kuu ya Istilahi”, “Nadharia Jamii ya Uundaji wa Istilahi”, “Nadharia ya Saikolojia ya Tabia”, “Nadharia ya Uhalisia”.

3.2 Nadharia Kongwe Kuu ya Istilahi

Kuna Nadharia Kongwe Kuu ya Istilahi (NKKI) nadharia ambayo mwasisi wake Mwaustralia Woster (1960), ni nadharia inayotilia mkazo juu ya usanifishaji wa lugha kwa kuunda maneno kutokana na dhana. Nadharia hii inachukulia tu kwamba dhana zinafikiria maneno, Kwa hivyo muundaji wa istilahi inampasa alifanyie kazi neno ambalo litaakisi dhana. Vilevile Nadharia hii inapuuza umuhimu wa mawasiliano na maumbile ya watumiaji wa maneno. Katika utafiti huu imetumika nadharia hiyo ya NKKI , hasa katika kuyaangalia yale maneno yaliyopo kama istilahi kidhana.

3.3 Nadharia Jamii ya Uundaji Istilahi

Pia kuna Nadharia Jamii ya Uundaji Istilahi (NJUI). Nadharia hii (NJUI) inatilia mkazo kwamba istilahi haiko kwenye lugha ya kuzushwa ambayo haina utaratibu na kaida zake

(lugha bandia) lakini ina sifa zote za lugha kuu, kutokana na hivyo, ina maana kama ile lugha kuu. Lugha inahitaji kufahamika na kukubaliwa na wazungumzaji, kwa hivyo ni muhimu waundaji wa maneno na istilahi kuzingatia haja ya watumiaji wake wakati wa kuunda maneno na istilahi hizo. Mahitaji hayo yanajumuisha mahitaji ya kikabila, kiutamaduni, kiutambuzi na kilughawiya. Istilahi/maneno hayatakwenda kinyume na kaida za watumiaji wa lugha. Kwa hivyo nadharia hii (NJUI) nayo ilitumika katika utafiti huu na imesaidia kuelekeza utafiti huu katika kuyajibu maswali yaliyotolewa.

3.4 Nadharia ya Saikolojia ya Tabia

Waasisi wahusika wa Nadharia hii ni Pavlov (1957) Mrusi na Skinner (1971) Mmarekani. Pavlov na Skinner walifikia uamuzi wa kuwa mwanadamu na mnyama hujifunza vizuri na kwa hamu kubwa mno pale anapopewa zawadi kila mara anapofanya jambo zuri. Lakini pia hamu ya kujifunza hufifia au kuondoka kabisa akiacha kupewa zawadi. Nadharia hii imemuongoza mtafiti katika kazi yake hii kuwapa fedha chache kiasi cha shilingi alfu kumi, kwanza kwa kutilia maanani muda uliotumika katika shughuli hiyo ya mahojiano ulikuwa ni mrefu, kiasi kwamba shughuli zao nyenginezo ambazo wahusika walikuwa wazifanye hawakuzifanya kwa wakati ule. Vilevile, kwa kuwa kazi hiyo ya mahojiano si ya siku moja, kwa hivyo fedha hizi kwa upande mmoja zilikuwa kama ni motisha na ahsante kwa walengwa wa utafiti, kwa hivyo ahsante hiyo ilizidisha mashirikiano na utashi kila zilipokuwa zikitolewa na kupatikana kile kilichokusudiwa.

3.5 Nadharia ya Uhalisia

Nadharia hii inabeba maana ya uwakilishi wa uhalisia wa mambo katika kazi ya fasihi. Nadharia hii iliibuka katika karne ya kumi na tisa kwa lengo la kupinga utanashati wenye maringo/mikogo/dharau/ kedi. Plato (427-347 KK) na Aristottle (384-322 KK) wanaona kwamba mhalisia huamini katika matokeo ya mambo ya ukweli au anazingatia ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa kwa tajiriba. Kwa hivyo, uhalisia hujikita katika mambo yaliyopo, tukio mahsusi na matukio yanayozuweza hasada za kijamii zilizopo. Mhakiki anayezingatia nadharia hii ya uhalisia huchunguza namna mtunzi anavyodhihirisha uhalisi wa mambo kupitia maudhui aliyoyazingatia, pamoja na wahusika alowasawiri katika kuwabebesha matukio na matendo yanayowakilisha jamii. Kwenye utafiti huu nadharia hii imemsaidia mtafiti kujua uhalisia wa maneno hayo ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu katika kuyaangalia undani wake.

SURA YA NNE

4.0 MBINU NA NJIA ZA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti anaonesha mbinu na njia tafauti alizozitumia wakati alipokuwa akikusanya na kuchambua data. Njia ni namna ya taratibu zinazotakiwa kufanywa na mtafiti ili kupata muradi anaoutaka. Mbinu ni njia za kupitia katika kufanya utafiti na kuweza kupata data na taarifa. Mbinu na njia mbalimbali zilitumika kwa nia na lengo la kukamilisha kazi ya utafiti huu. Sura hii imebainisha pia mfuatano wa matokeo, uteuzi wa walengwa wa utafiti, pahala pa utafiti, utaratibu wa ukusanyaji wa data jinsi ulivyokuwa na vifaa vilivyotumika katika utafiti.

4.2 Mbinu ya Maktabani

Mbinu hii ilimuwezesha mtafiti kupitia na kusoma vitabu, tasnifu na majarida mbalimbali yanayohusiana na mada na nyanja za utafiti wenyewe. Mtafiti alisoma tasnifu, vitabu majarida na wavupepe. Kwa mujibu wa maumbile ya utafiti huu, mtafiti alitumia mbinu ya maktabani ili kuweza kusoma maandiko na machapisho mbalimbali na kupata kazitangulizi, kupitia magazeti na majarida mbalimbali. Kwa ujumla hayo yote yalimsaidia mtafiti kufikia lengo lake alilolikusudia.

4.3 Mbinu ya Mahojiano

Katika utafiti huu, mbinu hii ya mahojiano ilitumika ili kupata data na taarifa za moja kwa moja zilizowezesha kupatikana kwa data sahihi kutoka kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu na hatimaye data hizi ziliwekwa katika maandishi.

Mbinu hii kwa kuwa ilitumia hojaji/dodoso ilimwezesha mtafiti kukutana na walimu. Mtafiti alitumia njia ya mahojiano kwa kuwauliza maswali walengwa kwa kupitia kwenye dodoso (angalia kiambatanisho A), ilitumika njia hii ili kupata ufafanuzi na kukusanya maelezo yaliyotolewa na baadaye kuhakiki maelezo hayo kwa umakini ili kupata data halisi na sahihi kutoka kwa walengwa. Njia hii ilimsaidia sana mtafiti kupata mawazo na fikra zenye kufaa kutoka kwa watafitiwa walengwa.

4.4 Mbinu ya Kutumia Maswali ya Ana kwa Ana

Mtafiti alitumia Mbinu ya maswali ya ana kwa ana, na walengwa walijibu kwa uwezo mkubwa na kwa uwazi na uhuru zaidi. Mbinu hii ilitumika kwa walimu, watu maarufu na weledi wa Kiswahili. Mbinu hii ilitumika ili kupata data za uhakika, na kwa kuzingatia kwamba nafasi na hadhi ya watafiti hao kuwa ni walimu wa vyo vikiu na watu mashuhuri weledi wa Kiswahili (angalia kiambatanisho B). Mbinu hii pia ilitumika mitaani katika kuwahoji wahusika ambao Mtafiti alihisi kwamba wanaweza kutoa mchango mzuri na muhimu katika kufanikisha utafiti huu. Kwa kiasi kikubwa, mtafiti anaona hii ni moja kati ya mbinu za kuaminika na kuwa na sifa ya uhakika. Mtafiti alirikodi maelezo yaliyotokana na maswali ya ana kwa ana kutoka kwa watafitiwa.

4.5 Uteuzi wa Watafitiwa

Katika kuufanya Utafti huu, Mtafiti aliteua watafitiwa wa aina mbali mbali. Kwanza kundi la watafitiwa ambao ni walimu wenye uelewa na upeo mpana katika lugha za Kiswahili, Kiarabu na Kiingereza. Kundi jengine la pili ni watu wenye sifa ya weledi katika lugha ya Kiswahili. Kundi la tatu ni wanafunzi Chuo Kikuu wa viwang vya

Stashahada ya Lugha Mwaka wa Pili na Shahada ya Elimu na Lugha Mwaka wa Pili na wa Tatu.

4.6 Ukusanyaji wa Data

Kwa mujibu wa utaratibu aliouibua mtafiti ndivyo data zilivyokusanywa. Mtafi alionana na wanafunzi wa Chuo Kikuu kimoja ndani ya Zanzibar wakiwa ni watafitiwa na pia kukutana na watafitiwa wengine akiwa na vifaa vyake baada ya kujitambulisha kwa wakuu wahusika wa Chuoni na walimu/wahadhiri wahusika.

4.7 ifaa vya UtafitiV

Mtafiti alitumia, katika utafiti huu, karatasi za maswali ya hojaji/dodoso, kalamu, kinasasauti cha elektroniki kwa lengo la kurikodi mahojiano pamoja na kompyuta, karatasi na kalamu. Vifaa hivi kwa kiasi kikubwa sana vilimsaidia vyema mtafiti katika hatua ya kuchambua data.

4.8 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa Data zilizokusanywa katika utafiti huu, ulifuata hatua mbalimbali kama ifuatavyo :

Mosi, kuzisoma taarifa zote zilizokusanywa, kuzichambua dodoso za wanafunzi na walimu kwa kutumia mbinu ya kiwango au ustahilifu na mbinu ya ujumla. Pili, kutoa tafsiri ya maelezo ya watafitiwa wengine kiuchambuzi na kwa mjibu wa mikabala yake. Tatu, kuyaaanisha maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu ambayo yanapatikana

katika nyaja za Kijamii, Kidini na Kibiashara (Kiuchumi) n.k. Katika kufanikisha kazi hii, Mtafiti alitumia mfumo wa nambari katika kufanikisha kazi hii.

Nne, uchambuzi, uanishaji na ufafanuzi wa mabadiliko ya kifonolojia, kimofolojia na kisemantiki kwenye maneno hayo yaliyokusanywa katika nyanja hizo.

4.9 Nadharia ya Uchambuzi wa Data

Katika Uchambuzi wa Data, Mtafiti kwa njia ambayo si ya moja kwa moja alitumia Nadharia ya Bango Kitita. Waasisi wa Nadharia hii ni Miles, M. & Huberman, M. 1994.

Nadharia hii imejikita kwenye sifa muhimu tatu nazo ni: Mosi, Upunguzaji data ambao ni mchakato wa uchaguzi, Ulengaji, Usahilishaji, Ufupishaji na Ufanyaji mabadiliko ya data zinazojitokeza kimaandishi. Pili, Uaridhishaji wa data; kijumla, huu ni mpangilio katika ufupisho wa uunganishaji wa taarifa zinazoruhusu kufikia hitimisho na uchukuaji wa hatua. Uaridhishaji unasaidia kufahamu nini kinachoendelea au kutokea na pia kufanya jambo ama kuchambua zaidi au kuchukua hatua kwa mujibu wa ufahamu. Tatu, Ufikiaji wa Hitimisho na Uthibitishaji katika mkondo wa tatu wa harakati za uchambuzi ni ufikiaji wa kutoa hitimisho na uthibitishaji. Mwanzo wa ukusanyaji wa data, mtafiti kama mchambuzi stahilifu alianza kwa kuamua mambo ya maana au yaliyokusudia kiini cha mamabo hayo, alionesha ukawaida, sampuli, maelezo, mpango unaowezekana na mitiririko ya sababu na mawazo.

SURA YA TANO

5.0 UCHAMBUZI WA DATA.

5.1 Utangulizi

Sura hii ya uchambuzi wa data, inajumuisha sehemu mbili za data zilizokusanywa, data zilizokusanywa kwa kupitia utafiti wa maktabani na zile data zilizopatikana uwandani. Katika data za maktabani, Mtafiti alikusanya maneno mbalimbali ya Kiswahili amabayo yana asili ya Kiarabu. Kwa kupitia utafiti wa maktabani, Mtafiti aliyagawa maneno hayo katika makundi manane. Makundi hayo ni: maneno ya kibiashara, maneno ya kiutawala/kisiasa, maneno ya kidini, maneno ya kitaaluma, maneno ya kijamii, maneno ya kifedha/kibiashara, maneno ya kibaharia/usafiri na maneno ya ujenzi na vifaa vyake. Katika uchambuzi wa data hizi, Mtafiti alitumia Nadharia ya Bangokitita hasa kwenye data za uwandani kama ilivyoelezwa hapo kabla.

5.2 Uchambuzi wa Data za Maktabani

5.2.1 Maneno ya Kibiashara

Jina la Kundi	Idadi ya maneno	Asilimia %
1. Kibiashara/ kiuchumi	14	04.844

Jadweli Na.4 Maneno ya Kibiashara/Kiuchumi.

Ardhia أرضية: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo kidakatonge 2 na irabu fupi a chini na kufuatiwa na kimadende ufizi r na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi d chenye ghuna na irabu fupi i mbele juu na kiyeyusho j (y') kaakaa gumu chenye mkazo na irabu fupi a chini na kipasuo meno ufizi t kisicho na ghuna na kuishia kwa irabu fupi u nyuma juu na nazali ufizi n yenye ghuna. Kwa kawaida katika Kiarabu, kimatamshi neno

halimaliziwi kwa irabu. Hii *un* ya mwisho ni irabu (tanwinu). Kwa hivyo neno hilo kwenye Kiarabu, muundo wake wa msingi ni /^ʔ*arḏijah*/.

Kwa upande wa maana katika Kiarabu neno hili linamaanisha “kiwanja, ghorofa, ardhi; ada ya uwekaji.” BAALBAKI (2003:).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa irabu fupi *a* chini nyuma na kimadende ufizi *r* na kumalizikia kwa kikwamizi meno *ḏ* chenye ghuna na irabu fupi *i* mbele juu na irabu fupi *a* nyuma chini. Neno hilo muundo wake wa ni /*arḏia*/.

Kwa upande wa maana katika Kiswahili, neno hilo linamaanisha “ada ya kuegesha chombo bandarini au uwanja wa ndege yaani *anchorage* kwa Kiingereza.” BAKIZA (2010:11).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwishakuingia katika Kiswahili, kwanza kuna ubadili konsonanti uliotokea mwanzo wa neno hili kutokana na kuwa katika lugha lengwa haina sauti /^ʔ/, kwa hivyo badili ya sauti hiyo ni /*a*/ . Hiyo ni tafauti ndogo ya kimatamshi kati ya Kiswahili na Kiarabu. Pili, kuna ufinyu semantiki katika neno hilo. Kwa upande wa maana, kwenye lugha ya Kiswahili lina ufinyu wa maana limejikita kwenye ada ya uegeshaji wa chombo bandarini au uwanja wa ndege tu.

Bandari بندري: Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na nazali ufizi *n* yenye ghuna na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Kimatamshi neno halimaliziwi kwa irabu, kwa hivyo muundo wake wa msingi ni /*bandar*/.

Kwa upande wa maana, neno hilo kwenye lugha hiyo ya Kiarabu linamaanisha “mahali inapotia nanga meli kwenye upwa; mji wa pwani; makao ya wafanyabiashara katika mji.” El-Jar (1973 : 251).

Kwenye Kiswahili, neno hilo vilevile linaanzia kwa kipasuo midomo *b* na irabu fupi mbele chini *a* na kufatiwa na nazali ufizi *n* yenye ghuna na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia kwa kimadende *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo katika lugha hiyo muundo wake wa msingi ni /bandari/.

Kwa upande wa maana kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, linamaanisha “pahali ambapo vyombo vya baharini hutia nanga kwa ajili ya kupakua na kupakia mizigo na abiria, diko, forodha; zawadi anayotoa tajiri kwa baharia wake baada ya kurudi safari ndefu.” Bakiza (2010:19).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna tafauti ndogo ya matamshi kwenye neno hilo, tafauti hiyo imekuja kutokana na ubadili irabu ambapo katika muundo wa msingi wa neno hilo katika Kiarabu lina irabu /u/ mwisho. Kwa hivyo kwenye lugha lengwa imebadilika na kuwa irabu hiyo ni /i/. Pili, kuna dhana ya neno hili ambayo ina pande mbili kwenye maana; upande wa kwanza kuna ufinyu semantiki ambapo maana hiyo imejifinya zaidi katika maana ya pahali ambapo vyombo vya majini hutia nanga na kupakia na kupakua mizigo. Upande wa pili wa maana ya neno hili kuna upanuzi semantiki ambapo kuna maana ya ziada ambayo kwenye lugha chanzi haikuweco. Maana hiyo ni zawadi atoayo tajiri kwa baharia wake baada ya kurudi kutoka safari ndefu.

Bei : Kwenye Kiarabu, neno hilo linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye irabu fupi mbele chini *a* na kiyeyushi *j* kaakaa gumu kufuatiwa na kikwamizi koromeo ^ʿ chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n* yenye ghuna. Kimatamshi kwenye Kiarabu, neno halimaliziwi au halisimamiwi kwa irabu, ile *un* iliyoko mwisho wa neno ni irabu. Kwa hivyo muundo wake wa msingi neno hilo ni /*bajʿ*/.

Neno hilo katika lugha hiyo ya Kiarabu lina maana ya “mauzo, uuzaji.” El-Jar (1973 : 259).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye irabu fupi mbele kati *ε* na kumalizikia kwa irabu fupi mbele juu *i*. Kwenye Kiswahili neno hilo muundo wake msingi ni [*bei*].

Kwa upande wa maana, neno hilo linamaanisha “kima cha fedha chenye thamani ya kuuzia au kununulia kitu.” BAKIZA (2010:24), KKS (2004:25 Ch.II).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna tafauti ya matamshi; tafauti hiyo imekuja kutokana na ubadili irabu ambapo katika muundo wa msingi wa neno hilo katika Kiarabu lina irabu /u/ mwisho. Kwa hivyo kwenye lugha lengwa badili ya irabu hiyo ni irabu /i/. Vilevile kwenye neno hilo, kuna uimarishi irabu ambao ni mchakato wa kifonolojia unaojijhusisha na kuinua irabu ya kati chini /a/ kwenda kwenye irabu ya kati juu /ε/ kwenye neno hilo katika Kiswahili. Pili, kuna ufinyu semantiki; maana imejifinya zaidi katika dhana ambayo kimaana imeegemea zaidi kwenye idadi ya fedha ya kununulia au kuuzia jambo au kitu.

Biashara **بيع شراء**: Neneo hili ni moja katika Kiswahili, lakini asili yake kwenye Kiarabu ni maneno mawili. Neno la kwanza ni /baj:^ʕun/, ambapo neno hili linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kiyeyushi kaakaa gumu *j* na kikwamizi koromeo ^ʕ chenye ghuna na kumalizia kwa irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Kutokana na kuwa neno halimaliziwi au halisimamiwi kwa irabu, kwa hivyo neno hilo muundo wake wa msingi ni /baj:^ʕ / kwani mwisho lina lina irabu *un* ambayoni tanwini.

Kama lilivyokwisha oneshwa hapo juu, neno hili lina maana ya “ ununzi, ununuaji; uuzaji, mauzo.” Mandhour (--:23Juz. viii), BAALBAKI (2003:256).

Neno la pili ambalo linaanzia kwa kikwamizi kaakaa ufizi *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele *i* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu ndefu chini *a*: na kumalizikia kwa kipasuo kidakatonge ^ʔ na irabu fupi nyuma *u* na nazali ufizi *n* yenye ghuna, un hiyo ni irabu. kuwa neno halimaliziwi au halisimamiwi kwa irabu, kwa hivyo muundo wa msingi wa neno hilo ni

/fira:^ʔ/.

Neno hili lina maana ya “ununuzi, uuzaji; thamani ya ununuaji, ununuzi.” Mandhour (--:427 Juz. xiv), El-Jar (1973:704).

Maneno haya yalisharabiwa katika Kiswahili kama neno moja. Neno hilo moja, linaanzia kwa sauti kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele *i* na kufuatiwa na irabu fupi chini kati *a* na kikwamizi kaakaa ufizi *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi kati *a* na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi kati *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /biafara/.

Katika Kiswahili zimechukuliwa dhana zile zile mbili za asili katika Kiarabu na kupata maana ambayo ni “ununuzi na uuzaji; uchuuzi.” BAKIZA (2010:26).

Mabadiliko yaliyotokea baada ya kusharabiwa katika Kiswahili kwanza, kwenye neno hili ndani ya muundo wake, kwa kuliangalia lile neno la kwanza katika lugha chanzi, kumetokea uimarishi irabu ambao ni mchakato wa kifonolojia unaojijusisha na kuinua irabu ya kati chini /a/ kwenda kwenye irabu ya kati juu /ε/ kwenye neno hilo katika Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu ambapo kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna mfumo wa Konsonanti Konsonanti Irabu (KKI), irabu hiyo ni /u/ ambayo iko mwisho. Kwa hivyo kwenye lugha lengwa imebadilika irabu hiyo na kuwa /i/ mwisho. Tatu, kwenye lile neno la pili, katika lugha chanzi, katika Kiswahili kumetokea badiliko la ufupishi irabu ili kwenda sambamba katika mfumo wa irabu za Kiswahili.

Faida فائدة: Neno hili kwenye Kiarabu, linaanzia kwa sauti kikwamizi meno mdomo wa chini *f* kisicho cha ghuna chenye irabu refu chini *a*: na kufuatiwa na kipasuo koo [?] chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n* yenye ghuna, Muundo wa msingi wa neno hilo ni /fa:ʔidah/, mwisho wa neno hili kuna *taau* ya kufunga yenye irabu *un* ambayo ni tanwini, kimatamshi inatamkwa kama *hau* ili kuepuka kusimamia irabu

Kwa upande wa maana katika Kiarabu lina maana ya “fedha au mali thabiti kwa njia sahihi; jambo linalotoa manufaa k.v. elimu au mali; pato la fedha au mali katika wakati maalumu na kwa bei maalumu.” El-Jar (1973:795).

Kwa upande wa Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na irabu fupi mbele juu *i* na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Muundo wake wa msingi neno hilo ni [*faida*].

Katika Kiswahili lina maana ya “pato linalobakia baada ya kutoa gharama zote hasa kwenye biashara; pato katika chumo; jambo au kitu chenye maana; manufaa, neema.” BAKIZA (2010:79).

Kwa upande wa mabadiliko baada ya neno hilo baada ya kusharabiwa kwenye Kiswahili, kwanza, kumetokea ufupishi irabu, ambapo kwenye lugha chanzi, neno hilo lina irabu ndefu ambayo kwenye lugha lengwa imefupishwa ili kukubaliana na mfumo wa irabu kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu ambapo katika muundo wa msingi wa neno hilo kwenye Kiarabu linaishia /h/ ambayo kimsingi taau ya kufunga yenye irabu *un* imebadilika na kuwa irabu /a/ katika lugha lengwa.

Ghala غالى : Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini *y* chenye ghuna na irabu refu chini *a:* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu refu chini *a:*. Muundo wa msingi wa neno hilo ni /*ya:la:*/.

Neno hilo kwenye lugha hiyo, lina dhana ya kitenzi. Kwa muktadha wa maana, linamaanisha “zidisha mno; eleza kupita kiasi; zidi mno; kuza; pitiliza mipaka; pandisha bei; taka bei kubwa ya jambo, toza ada kubwa kwa.” El-jar (1973 : 868).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini *y* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi *a*. Muundo wake wa msingi ni [*yala*].

Kwa muktadha wa maana, neno hilo lina dhana ya nomino ambayo inamaanisha “jengo la kuwekea na kuhifadhia bidhaa, bohari, stoo.” BAKIZA (2010:97).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu; irabu ya mwanzo na ya pili katika neno hilo zimekuwa fupi ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Pili, kuna ufinyu semantiki; neno hilo limechukua maana finyu zaidi kuliko ile maana asilia katika lugha chanzi. Kwenye neno hilo inaonekana kuwa maana imejifinya na kujikita zaidi katika jengo la kuhifadhia.

Hakimiliki *حَقِّ مَلِكِي*: Katika Kiarabu, neno hilo linatokana na maneno mawili, la kwanza ni lile ambalo linaanzia kwa kikwamizi koromeo h kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge q kisicho cha ghuna chenye mkazo na irabu fupi nyuma juu u . Muundo wa msingi wa neno hilo ni */ħaqu/*. Lina maana ya wajibu, ukweli, uthibitifu, nguvu ya umiliki. Mandhour (--:49 Juz. x). Neno la pili linaanzia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kitambaza ufizi l kisicho cha ghuna na kumalizikia kwa kipasuo kaakaa laini k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i na kiyeyushi kaakaa j na irabu fupi nyuma juu u . Muundo wa msingi wa neno hilo ni */milkij/*. Lina maana ya jambo linalomilikiwa; maji, kisima, kimilikiwa, umiliki. Mandhour (--:491Juz.x). Maneno mawili hayo, *ħaqu* na *milkiju*, kwa pamoja yameunda mjengeko */haqu milkij/*.

Kwa upande wa maana, mjengeko huo unamaanisha “umilisi, uwezo wa kumiliki.”

Kwenye Kiswahili, neno hilo linanzia kwa kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi

mbele juu i , na kufuatiwa na nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kitambaza ufizi l kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i na kujiwa na kipasuo kidakatonge k isicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i . Katika lugha hiyo ya Kiswahili, muundo wake wa msingi neno hili ni */hakimiliki/*.

Kwa upande wa maana, neno hilo linamaanisha “haki ya kisheria anayopewa mtu au shirika ya kumiliki bidhaa aliyozalisha pamoja na kazi, sanaa na maandishi.” BAKIZA (2010:).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; ambapo irabu */u/* katika lugha chanzi imebadilika na kuwa */i/* kwenye lugha lengwa. Pili kuna upanuzi semantiki; hapa neno hili limezidi upeo wa maana. Dhana ya neno hili inabeba uwezo wa kisheria ndani yake na maana iliyojikita katika umiliki wa jambo. Tatu, neno linajitokeza kama nomino.

Hakishiriki* *حَقِّ مَشَارِكَة : Katika Kiarabu, neno hilo linatokana na maneno mawili, la kwanza, kama ilivyo elezwa hapo juu, ni lile ambalo linaanzia kwa kikwamizi koromeo \hbar kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini a na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge q kisicho cha ghuna chenye mkazo na irabu fupi nyuma juu u . Muundo wa msingi wa neno hilo ni */haqu/*. Neno la pili ambalo linaanzia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na kufuatiwa na kikwamizi kaakaa gumu f kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu chini a ; na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi mbele chini a na kumalizikia kwa kipasuo kidaka tonge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele a na kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i na

nazali ufizi *n* yenye ghuna. Muundo wa msingi wa neno hilo ni /*muḥa:rakah*/. Mwisho wa neno hili kuna *taau* ya kufunga, yenye irabu *in* ambayo ni tanwini, kimatamshi inatamkwa kama *hau* ili kuepuka kusimamia irabu.

Neno hilo lina maana ya hali ya kuwa pamoja; uchanganyaji wa nasabu. Mandhour (--: 448 Juz.x). Maneno mawili hayo ambayo yanaunda mjengeko wa neno moja *haqumuḥa:rakah* kama kijalizo (adjunct) na kimilikishi (genitive).

Kwa upande wa maana, katika lugha ya Kiarabu maneno hayo kwa pamoja yanamaanisha “umilisi, umiliki; uwezo wa kushiriki.”

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kikwamizi kaakaagumu *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele *i*. Neno hilo katika lugha hiyo ya Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*hakiḥiriki*/.

Kwa upande wa maana, neno hilo katika Kiswahili linamaanisha “haki ya kisheria anayopewa mtu baada ya kushiriki katika kukamilisha au kuendeleza kazi ya mtu mwengine.” Bakiza (2010:109).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu ambapo irabu /u/ imebadilika na kuwa irabu /i/ katika lugha lengwa. Pili, kuna udondoshi konsonati, *m* na irabu *u* katika ile sehemu ya neno la pili katika muundo wa msingi wa neno ambalo ni kimilikishi kwenye lugha chanzi. Tatu, neno linajitokeza kama nomino. Nne, kuna upanuzi semantiki; neno hili lina ziada ya upeo wa maana. Dhana ya

neni hili inabeba uwezo wa kisheria ndani yake na ni maana iliyojikita katika ushiriki wa kazi au jambo.

Hasara *خسارة*: Kwenye Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo kisicho cha ghuna x chenye irabu fupi chini a na kufuatiwa na kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna chenye irabu refu chini a : na kumalizikia kwa kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi chini a na kuishia kwa kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazli ufizi n yenye ghuna. Muundo wa msingi wa neno hilo ni */xasa:rah/*. Mwisho wa neno hili kuna *taau* ya kufunga, yenye irabu *in* ambayo ni tanwini, kimatamshi inatamkwa kama *hau* ili kuepuka kusimamia irabu.

Kwa upande wa maana katika Kiarabu ni “dhara au kinyume cha faida, upotevu; angamio.” BAALBAKI (2003:510).

Kwenye Kiswahili linaanzia kwa kikwamizi koo h chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kikwamizi ufizi kisicho cha ghuna s na irabu fupi kati na kumalizikia kwa kimadende ufizi r na irabu fupi kati a ; neno hili muundo wake wa msingi ni */hasara/*.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “hali ya kupungukiwa au kuharibika mali katika biashara; kinyume cha faida; uharibifu, upotevu, madhara.” KKS (1981: 76).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu ambapo irabu */un/* mwisho kwenye lugha chanzi, kimsingi imebadilika na kuwa irabu */a/* katika lugha lengwa. Pili, kuna ufupishi irabu; irabu a : imefupishwa ili kwenda

sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Kwa upande wa maana hakuna badiliko lolote la kimaana baina ya lugha mbili hizi.

Mali *مال*: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa nazali midomo miwili m yenye ghuna na irabu refu chini a : na kufuatiwa na kitambaza ufizi l na kumalizikia irabu fupi nyuma juu u na nazali ufizi n yenye ghuna. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, muundo wa msingi wa neno hili ni $/ma:l/$.

Kwa upande wa maana, katika Kiarabu neno hili lina maana ya “fedha; neema; vitu au mambo yote yanayomilikiwa, bidhaa; utajiri.” BAALBAKI (2003:939).

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kwa nazali midomo m na irabu fupi chini a na kitambaza ufizi l na irabu fupi juu mbele i . Neno hili kwenye Kiswahili muundo wake wa ni $/mali/$.

Kwenye Kiswahili katika upande wa maana, neno hili linamaanisha “bidhaa au mambo yote yenye thamani yanayomilikiwa na mtu; vitu vyenye thamani kubwa alivyonavyo mtu, kitu cha thamani kubwa.” KKS (2004:219 Ch.II).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu; irabu a : imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu ambapo irabu $/u/$ kwenye lugha chanzi imebadilika na kuwa irabu $/i/$ katika lugha lengwa. Tatu, kuna ufinyu semantiki. Neno hili limechukua maana finyu, ambapo maana imejikita zaidi kwenye vitu vinavyomilikiwa.

Tijara *تجارة*: Katika Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele i juu na kufuatiwa na kikwamizi kaakaa gumu ufizi $dʒ$ na

irabu ndefu chini a : na kumalizikia kwa kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi chini a na kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali ufizi n . Muundo wa msingi wa neno hilo ni /tidʒa:rah/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hili lina maana ya “uuzaji na ununuzi kwa lengo la kupata faida, biashara, uchumi, bidhaa.” BAALBAKI (2003:275).

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kwa kipasuo ufizi kisicho cha ghuna t chenye irabu fupi chini a na kufuatiwa na kikwamizi kizuio kaakaa gumu J na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi chini a , muundo wake wa msingi ni /tijara/.

Katika Kiswahili, neno hili lina maana ya “ziada inayopatikana katika kazi au biashara, faida.” KKS (2004:405 Ch.II).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili: kwanza, kuna ufupishi irabu; irabu a : imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Pili, kuna ufinyu semantiki; neno hilo limechukua maana finyu zaidi. Kimaana, neno hilo limejikita katika faida inayotokana na biashara.

Mshitiri مشتري: Kwenye Kiarabu neno hili, linaanzia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na kufuatiwa na kikwamizi kaakaa ufizi f kisicho cha ghuna na kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kiyeyushi kaakaa j na kuishia kwa irabu fupi nyuma juu u . Kwa kawaida, kwenye Kiarabu katika usemaji, neno halisimamiwi kwa irabu mwisho wake. Kwa hivyo muundo wa msingi wa neno hilo ni /muftarij /.

Katika Kiarabu neno hili lina maana ya “mnunuzi.” Ibnu- Ebad (-- : 177 Juz.II).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa nazali midomo m na kikwamizi kaakaa ufizi f kisicho cha ghuna na kipasuo ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi juu mbele i na kumalizikia kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i . Neno hili muundo wake wa msingi ni ni /*mfitiri*/.

Kwenye Kiswahili neno hili lina maana hiyo hiyo ya “mnunujaji au mnunuzi.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi irabu; kuna irabu u mwanzoni mwa neno hilo katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu, irabu hiyo imedondoshwa baada ya neno hilokusharabiwa kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu ambapo irabu / u / kwenye lugha chanzi imebadilika na kwa irabu / i / katika lugha lengwa. Kimaana hakuna badiliko lolote, kuna usawa katika maana baina ya Kiswahili na Kiarabu.

Soko سوق: Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu nyuma juu u : na kumalizikia kwa kipasuo kidakatonge kisicho cha ghuna q chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali ufizi n . Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, Muundo wa msingi wa neno hilo ni /*su:q*/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hili lina maana ya “muundi; mahali panapo fanywa shughuli za kibiashara.” Ibnu- Ebad (-- :490 Juz.I)

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna chenye irabu fupi kati nyuma ɔ na kumalizikia kwa kipasuo kaakaa laini kisicho cha ghuna k chenye irabu fupi kati nyuma ɔ . Neno hili, muundo wake wa msingi ni ni [*sɔkɔ*].

Katika Kiswahili neno hilo lina maana ya “sehemu maalumu iliyojengwa kwa ajili ya kuuzia na kununulia bidhaa mbali mbali, mahali pa kudumu wafanya biasha wanapouza bidhaa mbali mbali.” BAKIZA (2010:373).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kusharabiwa kwenye Kiswahili: kwanza, kuna ufupishi irabu ambapo irabu ndefu nyuma juu /u:/ kwenye muundo wa msingi wa neno hilo kwenye lugha chanzi imefupika na kuwa fupi kati nyuma /ɔ/ kwenye lugha lengwa. Pili, kuna badiliko la ufinyu semantiki, neno hili limechukua ufinyu wa maana kwenye Kiswahili, ufinyu huo wa maana umejikita kwenye sehemu maalumu iliyojengwa kwa ajili ya kuuzia na kununulia bidhaa.

Tajiri *تاجر* : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna na irabu ndefu chini *a:* na kufuatiwa na kikwamizi kaakaa gumu *dʒ* na irabu fupi juu mbele *i* na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Ile *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, basi muundo wa msingi wa neno hilo ni /*ta:dʒir*/.

Katika Kiarabu neno hili lina maana ya “mfanyabiashara wa aina yoyote awe mkubwa au mdogo, muuza ulevi.” El-Jawhari (1987:600).

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi kizuiio kaakaa gumu *J* na irabu fupi juu mbele *i* na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi juu mbele *i*. Neno hili, muundo wake wa kifonetiki ni /*tajiri*/.

Kwenye Kiswahili neno hilo linamaanisha “mtu mwenye hali nzuri kiuchumi na mwenye fedha nyingi.” BAKIZA (2010:384).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili. Kwanza kuna ufupishi irabu ambapo irabu ndefu chini /a:/ kwenye muundo wa msingi wa neno hilo katika lugha chanzi, irabu hiyo imefupika na kuwa irabu fupi nyuma /a/ kwenye lugha lengwa. Pili kuna ufinyu semantiki, neno hili limechukua maana finyu zaidi ambayo imejikita katika mtu mwenye mali nyingi, mtu anayeajiri wafanyakazi.

5.2.2 Maneno ya Kisiasa/ Kiutawala

Jina la Kundi	Idadi ya maneno	Asilimia %
1. Kiutawala/kisiasa	17	05.882

Jadwali Na.5 Maneno ya Kisiasa/ Kiutawala .

Amirijeshi أميرجيش: Katika Kiarabu neno hili linajitokeza kama maneno mawili ambayo ni ²ami:jrun na *dʒajfun*. Neno la kwanza katika Kiarabu linaanzia kwa kipasuo koo ² chenye ghuna na irabu fupi *a* mbele chini na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu ndefu *i*: mbele juu na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazli ufizi *n*. hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasilimii irabu mwisho wa neno, basi muundo wa msingi wa neno hilo ni /²ami:r/ na linamaanisha kiongozi, mfalme, mtoto wa kifalme, mshauri. El-Jar (1973:166). Na neno la pili linaanzia kwa kikwamizi kaakaa *dʒ* chenye ghuna na irabu fupi *a* mbele chini na kiyeyushi *j* kaakaa gumu na kikwamizi kaakaa *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Vivyohivyo muundo wa msingi wa ni /*dʒajf*/. Lina maana

ya askari, kundi la watu waendao vitani, kundi la jambo lolote. El-Jar (1973:416).
Maneno hayo yanapojitokeza kama neno moja, muundo wake wa msingi ni /[?]ami:rudʒajf
/.

Neno hilo kwenye Kiarabu linamaanisha “kiongozi mkuu wa jeshi.”

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa irabu fupi *a* chini na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi *i* mbele juu na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi *i* mbele juu na kumalizikia kwa kikwamizi kizuio kaakaa *J* chenye ghuna na irabu fupi kati *ε* na kikwamizi kaakaa ufizi *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi *i* mbele juu. Neno hili muundo wake wa msingi ni [*amiriJεfi*].

Kwa upande wa maana katika lugha ya Kiswahili, linamaanisha “mkuu wa jeshi.”
BAKIZA (2010:8).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; mwanzo wa neno hilo kwenye Kiarabu limeanza kwa sauti[?] ambayo ni konsonanti katika neno hili. Kwa hivyo neno hilo la Kiarabu lilipoingia kwenye Kiswahili, konsonanti hiyo ilidondoshwa na kubakia sauti irabu /a/ ambayo iko mwanzoni mwa neno hilo. Pili, kuna ubadili irabu, neno hilo kwenye Kiarabu lina irabu pacha /aj/. Lilipoingia kwenye Kiswahili irabu hiyo ilifupika na kuwa ya kati mbele /ε/. Tatu, ufinyu semantiki; neno hili limechukua maana finyu katika Kiswahili kuliko ile ya Kiarabu. Inaonekana wazi kuwa maana hiyo ya Kiswahili imejifinya na kujikita zaidi kwenye jeshi tu.

Awamu ^{أعوام}: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo koo ^ʔ chenye ghuna na irabu fupi *a* mbele chini na kufuatiwa na kikwamizi koromeo ^ʕ na kumalizikia kwa kiyeyushi midomo *w* na irabu ndefu *a:* mbele chini na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno. Neno hili katika Kiarabu muundo wake wa asili ni /^ʔa^ʕwa:mu/.

Neno hili liko katika wingi, umoja wake ni /^ʕa:m/ lenye maana ya “mwaka mmoja; mchana.” Katika lugha hiyo ya Kiarabu neno hili lina maana ya “miaka mingi.” El-Jar (1973:807).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa irabu fupi *a* chini mbele na kufuatiwa na kiyeyushi midomo *w* na irabu fupi *a* mbele chini na kumalizikia kwa nazali midomo *m* na irabu fupi *u* nyuma juu. Neno hilo katika Kiswahili muundo wake ni /awamu/.

Neno hili kwa upande wa maana, katika Kiswahili lina maanisha “kipindi ambacho jambo maalumu limepangwa kutekelezwa k.m. muda wote wa rais katika kuongoza nchi.” BAKIZA (2010:13).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti, mwanzo wa neno hilo kwenye Kiarabu katika muundo wake wa msingi limeanza kwa sauti konsonanti ^ʔ. Kwa hivyo konsonati hiyo ilidondoshwa katika Kiswahili na kubakia /a/. Vilevile, neno hili lina sauti konsonanti ^ʕ ambayo imedondoshwa na ikabakia irabu /a/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna ufupishi irabu, irabu ndefu /a: / iliyoko kwenye neno hili katika Kiarabu, imefupishwa ili kwenda sambamba

na mfumo wa Kiswahili. Tatu, kuna semantiki hamishi; kuna uhamishi kamili wa maana asilia ya kwenye Kiarabu. Neno hilo limepata maana mpya katika Kiswahili, ingawa kwa kiasi kidogo ina uhusiano hata kama si wa moja kwa moja.

Baraza برز: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu fupi a mbele chini na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi a mbele chini na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi z chenye ghuna na irabu fupi a mbele chini. kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, Neno hili muundo wake wa msingi ni /baraz/.

Katika lugha ya Kiarabu, neno hilo kwa upande wa maana, lina dhana ya kitenzi na linamaanisha “tokeza, gandamia; enda haja ” El-Jar (1973:228).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu fupi a mbele chini na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi z chenye ghuna na irabu fupi a chini, neno hilo kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni [baraza].

Kwa upande wa maana, katika lugha hiyo ya Kiswahili neno hilo lina dhana ya nomino, linamaanisha “sehemu iliyoinuka aghalabu hugandana na ukuta nje au ndani ya nyumba ambayo sehemu hiyo watu hukaa kupumzika au kukaribishia wageni; maskani; kikundi cha watu aghalabu wenye mnasaba na shughuli maalumu na walioteuliwa kusimamia shughuli iliyo katika jamii ” BAKIZA (2010:21).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza kuna badiliko la upanuzi semantiki ambapo maana ya neno hili, imekuwa jumuishi zaidi kuliko maana

yake katika lugha chanzi. Katika Kiswahili, neno hili linaonekana kuongezeka upeo wa maana na limeegemea zaidi kwenye mahali wanapokaa watu kwa mazungumzo, kundi la wateuliwa kwa ajili ya mnasaba na kusimamia shughuli katika jamii.

Desturi دستور: Neno hili asili yake ni la Kiajemi. Lilisharibiwa kwenye Kiarabu, katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo meno ufizi d chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na kufuatiwa na kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna na kujiwa na kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu nyuma juu u : na kumalizikia kimadende r chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u . Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo muundo wa msingi wa neno hilo ni $/dustu:r/$.

Kwenye Kiarabu, maana ya neno hili ni “utaratibu fulani unaofuatwa na kufanyiwa kazi; daftari maalumu linaloandikwa majina ya askari na vipato vyao; daftari maalumu linalokusanya sheria na kanuni za mfalme; katiba ” El-Jar (1973:532).

Katika Kiswahili, linaanzia kwa kipasuo meno ufizi d chenye ghuna na irabu fupi nyuma kati ε na kufuatiwa na kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna na kujiwa na kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na kumalizikia kimadende r chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i . Muundo wake wa msingi ni $/desturi/$.

Katika Kiswahili neno hili lina maana ya “mwenendo au tabia ya mtu; utaratibu wa jambo, kawaida ” BAKIZA (2010:63).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika lugha chanzi, kuna irabu ndefu $/u:/$. Irabu hiyo, imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika

Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hilo mwisho lina irabu fupi /u/. Irabu hiyo imebadilika na kuwa /i/ kwenye lugha lengwa. Tatu, kuna ufinyu semantiki, kutoka kwenye Kiarabu kwenda kwenye Kiswahili, neno limechukua maana finyu zaidi ikilinganishwa na ile maana ya Kiarabu. Hapa inajitokeza kuwa, maana ya neno imejifinya kwa kujikita kwenye mwenendo na kawaida.

Diwani ديوان : Neno hili liliingia katika Kiarabu kutoka kwenye Kifursi / Kiajemi. Kwenye Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu ndefu mbele *i*: na kufuatiwa na kiyeyushi midomo *w* na irabu ndefu chini *a*: na kumalizilikia kwa nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo muundo wake wa msingi ni /di:wa:n/.

Katika Kiarabu lina maana ya “daftari la majina ya askari na wale watu wanaopewa chochote k.m fedha n.k.; makusanyo ya mashairi ya mshairi fulani; kitabu; maandishi; sehemu ambayo hushughulikia mambo ya nchi na kusimamia mambo ya uongozi, afisi”. El-Jar (1973:550).

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele *i* na kumalizilikia kwa kiyeyushi midimo *w* na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa nazali meno ufizi *n* na irabu fupi mbele *i*. Katika Kiswahili, neno hili muundo wake ni /diwani/.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “kiongozi wa Wadi katika Jimbo ambaye huchaguliwa na wananchi kwa kura” BAKIZA (2010:69).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili, mwanzo na kati kuna irabu ndefu /i:/ na /a:/. Irabu hizo zimefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Pili, kuna ufinyu semantiki, katika Kiswahili limechukua maana finyu ikilinganishwa na ile maana kongwe ya Kiarabu. Huo ni upeo mpana wa tafauti ya maana kati ya Kiarabu na Kiswahili kwenye neno hili.

Hakimu **حكيم** : Katika Kiarabu, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kipasuo kaaka laini *k* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu mbele juu *i*: na kumalizikia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini juu *u* nazali ufizi *n* yenye ghuna. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo kwenye lugha hiyo ya Kiarabu neno hilo muundo wake wa msingi ni /*haki:m*/.

Kwa upande wa maana, katika Kiarabu neno hilo linamaanisha “mwenye busara, mwenye akili; mwenye ujuzi wa kisheria; mwanafalsafa; daktari.” El-Jar (1973:550).

Katika Kiswahili neno hilo, linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*.

Katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni /*hakimu*/.

Kwa muktadha wa kimaana, katika Kiswahili neno hilo lina maana ya “mtaalamu wa sheria anayetarajiwa kusikiliza mashtaka kortini, jaji; mwamuzi baina ya pande mbili au zaidi katika mgogoro.” KKS (1981:73).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti, kutokana na sauti konsonanti \hbar ya neno hilo la Kiarabu kutokwepo kwenye Kiswahili, kwa hivyo sauti hiyo ilibadilishwa na kuwa konsonanti h kwenye Kiswahili. Pili, kuna ufinyu semantiki, maana ya neno hili imejifinya. Dhana iliyopo katika maana kwenye neno inaonekana wazi kuwa imejifunga zaidi katika sheria na uamuzi.

Halifa **خليفة**: Neno hili kwenye Kiarabu, linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini x kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini a na kufuatiwa na kitambaza ufizi l kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu mbele juu i : na kumalizikia kwa kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini a na kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali ufizi n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo katika lugha hiyo ya Kiarabu, neno hilo muundo wake wa msingi ni $/xali:fah/$.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hili linamaanisha “yule ajaye baada ya kuondoka wa mwanzo; kiongozi.” BAALBAKI (2003:523).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi mbele chini a na kufuatiwa na kitambaza ufizi l kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i na kumalizikia kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini a . Katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa kifonetiki ni $/halifa/$.

Kwa upande wa maana, neno hilo kwenye lugha hiyo ya Kiswahili linamaanisha “kiongozi wa Waislamu; kiongozi wa tarika za dhikiri; kiongozi wa baadhi ya ngoma”. KKS (2004:107).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti, kutokana na sauti konsonati x ya neno hilo la Kiarabu kutokuwepo kwenye Kiswahili, kwa hivyo ilibadilishwa kwa konsonanti h kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hilo katika Kiarabu limeishia kwa irabu /u/, kwa hivyo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili ilibadilika na kuwa irabu /a/ ambayo iko mwisho wa neno hilo. Tatu, kuna ufinyu semantiki ambapo maana yake imejifinya. Neno hilo linajitokeza kama nomino inayobeba dhana ya uongozi.

Halmashauri أهل مشورة: Katika Kiarabu neno hili linatokana na mjengeko wa maneno mawili, la kwanza ni ²ahlu ambalo linaanzia kwa kipasuo koo ² chenye ghuna na irabu fupi mbele chini a na kufuatiwa na kipasuo koo h chenye ghuna na kitambaza ufizi l kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u . Muundo wa msingi wa neno hilo ni /²ahlu/. Neno la pili ni mafwara ambalo linaanzia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kikwamizi kaakaa gumu f kisicho cha ghuna na kiyeyushi midomo w chenye irabu fupi mbele chini a na kumalizikia kwa kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi mbele chini a na kuishia kwa kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna. Muundo wa msingi wa neno hili ni /mafwarah/. Kwa hivyo maneno hayo yanajitokeza katika mjengeko wa neno moja ahlu mafwarah kama kijalizo (adjunct) na kimilikishi (genitive).

Kwa hivyo neno hilo, kwenye Kiarabu, kwanza neno *ahlu* lina maana ya “jamaa; familia, watu wanaohusiana kindugu; wakaazi wa mahali; raia; memba wa kundi au kazi fulani; wafuasi.” BAALBAKI (2003:204). Neno *mashwara* lina maana ya “ushauri, mapendekezo; rai; maoni.” BAALBAKI (2003:1050). Kwa muktadha wa mjengeko wa maneno hayo kwa pamoja unamaana ya “watu wanaotoa ushauri, mawazo na rai.”

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kikwamizi kaakaagumu *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini *a*, na kumalizikia irabu fupi nyuma juu *u* na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Katika Kiswahili, neno hilo muundo wake ni [*halmashauri*].

Kwa upande wa maana, neno hilo katika Kiswahili linamaanisha “kikundi cha watu wanaosimamia jambo; taasisi ya utawala katika ngazi ya Wilaya na Miji.” BAKIZA (2010:109).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi wa kotonanti na irabu */ʔa/* mwanzo wa neno hilo kwenye Kiarabu, sehemu iliyobakia baada ya udondoshi huo, ina mkusanyiko wa konsonanti */hl/* imeongezwa irabu *a* ili kuondoa mkusanyiko huo lakini pia sehemu hiyo ina irabu */u/* mwisho kwa hivyo imebadilika na kuwa irabu */a/*. Pili, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu limeishia kwa irabu */a/*, kwa hivyo baada ya kwishakuingia katika Kiswahili kulitokea badiliko la irabu na kuwa */i/* ambayo iko mwisho wa neno hilo. Tatu, kuna semantiki imarishi, neno limepata maana mpya ambayo kwa kiasi fulani

imepata mwelekeo ulio kinyume na maana kongwe ile ya Kiarabu. Inaonekana kwamba dhana hiyo mpya imeegemea zaidi kwenye usimamizi wa mambo na utawala katika ngazi ya Wilaya au Mji. Neno hilo linajitokeza kama nomino inayojitegemea.

Hatamu **ختم** : Neno hili kwenye Kiarabu linaanzia kwa kikwamizi kaakaa lani x kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kumalizikia kwa nazali midomo miwili m na irabu fupi nyuma juu u na nazali ufizi n, un ya mwisho wa neno hii ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo muundo wa msingi wa neno hilo ni */xatam/*.

Katika Kiarabu neno hili lina maana ya “tundutundu za sega la nyuki; asali; mhuri rasmi unaopigwa juu ya waraka na kuthibitika kisheria; zuio; mwisho” Mandhour (-- :163 Juz.xii).

Katika Kiswahili linaanzia kwa kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kipasuo ufizi kisicho cha ghuna t chenye irabu fupi chini a na nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u . Neno hili muundo wake wa msingi ni */hatamu/*.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “ugwe wa kamba au ngozi unaofungiwa lijamu ya kumwongozea farasi au punda; madaraka ya uongozi.” BAKIZA (2010:113)

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Sauti $[x]$ iliyomo kwenye neno hilo la Kiarabu, ni sauti ambayo inajitokeza kama konsonati. Katika mfumo wa sauti za Kiswahili, sauti hiyo haimo, kwa hivyo,

umetokea ubadili wa konsonani /x/ kwa konsonanti /h/. Pili, kuna semantiki hamishi, neno hilo limechukua maana nyengine mpya tafauti na ile maana ya awali katika Kiarabu. Inaonekana hapa, dhana hiyo ya kwenye Kiswahili imejikita zaidi kwenye kifaa kinachotumika katika uongozaji mnyama hasa punda na farasi. Vilevile katika Kiswahili tunasema “kushika hatamu” yaani kushika madaraka, au kuongoza.

Katiba كتيبة: Kwenye Kiarabu neno hili, linaanzia kwa sauti kipasuo kaakaa laini *k* isiyo ya ghuna yenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu mbele juu *i*; na kumalizikia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*; *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, hivyo muundo wa msingi wa neno hili ni /*kati:bah*/. Kwa upande wa maana, neno hili kwenye Kiarabu lina mnasaba wa kijeshi kwa maana ya “jeshi, kikosi kikubwa cha jeshi chenye majumba, askari au wanamgambo.” Moustafa (-- : 775 Juz. II).

Katika Kiswahili vilevile, linaanzia kipasuo kaakaa laini *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi chini nyuma *a*. Muundo wake wa msingi ni [*katiba*].

Katika Kiswahili, neno hili lina maana ya “utaratibu au sheriamama iliyowekwa kwa maandishi au bila ya maandishi katika kuongoza nchi.” BAKIZA (2010:148).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu kwenye muundo huo wa msingi wa neno hilo katika lugha chanzi, mwisho lina irabu fupi /u/. Irabu hiyo imebadilika na kuwa /a/ mwisho kwenye lugha lengwa. Pili, ufupishi irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kuna irabu ndefu mbele juu /i:/, katika Kiswahili irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu wa lugha hiyo ya Kiswahili. Tatu, kuna semantiki hamishi, neno hili limepata uhamishi kamili wa maana na kupata maana mpya, ambayo haina uhusiano na maana kongwe katika lugha chanzi.

Mfawidhi **مَفْوَض** : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma *u* na kufuatiwa na kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kiyeyushi mdomo *w* chenye mkazo na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo ufizi meno *d* chenye ghuna na irabu fupi chini juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo muundo wa msingi wa neno hilo ni /*mufawad*ʔ/.

Kwenye Kiarabu, maana ya neno hili ni “mwenye kupewa uwezo au mamlaka juu ya jambo ; kiongozi, mwamuzi.” Mandhour (-- :290 Juz.vii).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia vilevile kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na kufuatiwa na kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kiyeyushi mdomo *w* na irabu fupi mbele juu *i* na kikwamizi meno *ð* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Muundo wa msingi wa neno hilo ni /*mfawidhi*/.

Katika Kiswahili neno hili lina maana ya “mtu aliyepewa mamlaka ya kuongoza idara au kituo.” BAKIZA (2010:241).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu ambapo irabu fupi nyuma juu /u/ kwenye muundo wa msingi wa neno hilo kwenye lugha chanzi imebadilika na kuwa /i/ kwenye lugha lengwa. Pili, kuna ubadili konsonanti, sauti kipasuo *ḍ* imebadilika na kuwa kikwamizi *ḍ*. Tatu, kuna ufinyu semantiki, hapa neno hili lina ufinyu wa maana kidogo kwani maana imeelekea na imejikita kwenye mtu aliyepewa uwezo wa uongozi wa kituo au idra.

Mratibu مرتب: Neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye mkazo na irabu fupi chini *a* na kumalizia kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu nyuma juu *u* nazali n. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, hivyo neno hili katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*muratab*/.

Maana ya neno hili katika Kiarabu ni “yenye kupangwa katika mpangilio mzuri, yenye kufanywa vizuri; cheo; malipo ya mfanyakazi kila mwezi, mshahara.” BAALBAKI (2003:1016).

Katika Kiswahili neno hili, linaanzia vilevile kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na kufuatiwa na kimadende *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizia kwa kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele *i* na kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*mratibu*/.

Kwenye Kiswahili lina maana ya mtu mwenye madaraka ya kupanga, kuunganisha na kusimamia shughuli za watu mbalimbali. KKS (1981:186).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi irabu, irabu ya mwanzo kwenye neno hili /a/ imedondoshwa. Pili, kuna udondoshi konsonanti, kwenye muundo wa msingi wa neno hili, katikati kuna konsonanti radidi/kariri /tt/, kwa hivyo moja kati ya hizo imedondoshwa. Tatu, kuna semantiki hamishi, kwa kiasi kikubwa neno hili limechukua maana mpya, lakini kidogo kuna uhusiano na maana ya awali kwenye Kiarabu.

Ratiba رَتَبَة: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kimadende *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye mkazo na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo muundo wa msingi wa neno hilo ni /*ratab*/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu linamaanisha “tulua, -to ondoka; -wa thabiti, andaa, tayarisha, panga; toa, zalisha.” Mandhour (-- 409: Juz.I), BAALBAKI (2003:576).

Kwenye Kiswahili, linaanzia kwa kimadende *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna, na irabu fupi chini *a*. Katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*ratiba*/.

Katika Kiswahili lina maana ya “mpango wa mfululizo wa mambo yanayofanyika au yatakayofanyika katika uendeshaji wa shughuli fulani kulingana na wakati uliopangwa.” BAKIZA (2010:344).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti, katikati ya neno hili kwenye muundo wake wa msingi kuna kosonanti radidi / kariri, kwa hivyo moja kati ya konsonanti hizo imedondohswa kwenye Kiswahili. Pili, kuna upanuzi semantiki, neno hili limezidi upeo wa maana iliyoendea zaidi kwenye mpango wa matukio katika shughuli kwa mujibu wa wakati uliopangwa.

Sera *سيرة*: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu mbele juu *i*: na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuan na irabu fupi chini *a*, na kumalizikia kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo muundo wa msingi wa neno hilo ni /*si:rah*/.

Kwa upande wa maana, neno hili kwenye Kiarabu linamaanisha “mwendo; njia, mwenendo; tabia ya mtu aliyonayo; maandiko kwa ukamilifu juu ya maisha, kazi na mambo maarufu ya mtu.” BAALBAKI (2003: 554).

Kwenye Kiswahili vilevile, linaanzia kwa kikwamizi ufizi *s* kicho cha ghuna chenye irabu refu mbele kati *ε*: na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* na kumalizikia kwa irabu fupi chini *a*, katika Kiswahili muundo wa msingi wa neno hili ni [*sera*].

Kwenye Kiswahili neno hili hususan kwa muktadha wa siasa na uongozi, lina maana ya “utaratibu wa kuendesha jambo ili kukidhi haja za serikali, chama, dini au shirika; namna au mpango wa utekelezaji wa mambo ya nchi, taasisi n.k.” BAKIZA (2010:359).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna uimarishi irabu chini, katika muundo wake wa msingi kwenye lugha chanzi kuna irabu ndefu mbele juu /i:/ ambayo imefupika na kuwa irabu fupi kati mbele /ε/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna semantiki hamishi ambapo neno hilo limepoteza mwelekeo wa maana ya zamani katika lugha chanzi.

Sheha *شيخة*: Katika Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kikwamizi ufizi kaakaa *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kiyeyushi kaakaa gumu *j* na kikwamizi kakaa laini *x* na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kipasuo ufizi meno *t* na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo muundo wake wa msingi ni /*fajxah*/.

Maana ya neno hili kwa Kiarabu ni “mwanamke ambaye umri wa ujana wake umemaliza na kuingia umri wa utu uzima wake; hali ya kike ya neno shaykhu.”

Kwenye Kiswahili, linaanzia kwa kikwamizi ufizi kaakaa *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele kati *ε* na kumalizikia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa kifonetiki ni [*fεha*].

Hapo zamani, katika utawala wa vijiji Visiwani Zanzibar, mkuu wa kijiji alikuwa mwanamke, lakini shughuli zake zote za nje zilikuwa zikifanywa na mumewe. Kwa hivyo neno hili lilitokea huko. (Prof. Lodhi 2016)

Katika Kiswahili lina maana ya “kiongozi wa Serikali katika ngazi ya Kijiji.” BAKIZA (2010 :363).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna uimarishi irabu, katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno hili kuna irabu pacha /aj/ ambayo imeinuliwa na kuwa irabu ya kati /ε/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili konsonanti, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kuna sauti konsonanti /x/ ambayo imebadilika na kuwa /h/ katika Kiswahili kutokana na kuwa katika Kiswahili sanifu sauti hiyo haimo. Tatu, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hilo katika Kiarabu limeishia kwa irabu /u/, kwa hivyo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili irabu hiyo ilibadilika na kuwa irabu /a/ ambayo iko mwisho wa neno hilo. Nne, kuna semantiki hamishi, neno hili limechukua maana mpya katika lugha lengwa, maana hiyo haina uhusiano kabisa na ile maana iliyotangulia kwenye Kiarabu.

Taratibu ترتیب: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kujiwa na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu mbele juu *i*: na kumalizikia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa

Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo muundo wa msingi wa neno hili ni /*tarti:b*/.

Kwa upande wa maana, neno hili katika Kiarabu linamaanisha “mpango, mpangilio, utaratibu.” El-Jar (1973:287).

Katika Kiswahili, linaanzia vilevile kwa kipasuo ufizi *t* na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele *i* na kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi nyuma *u*. Muundo wake wa msingi ni /*taratibu*/.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “kanuni, njia au mpango unaotumika katika kufanya jambo fulani; kaida; pasi na haraka; pole pole, asteaste.” BAKIZA (2010:389).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna uongezaji sauti. Kwenye muundo wa msingi wa neno hili, kuna mkusanyiko wa konsonanti /*rt*/, katika Kiswahili kwenye mkusanyiko huo imeongezwa irabu /*a*/ ili kuepusha mkusanyiko huo. Pili, kuna ufupishi irabu, kwenye neno hili kuna irabu ndefu mbele juu /*i*/, irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Tatu, kuna upanuzi semantiki, maana imekuwa jumuishi zaidi na kuzidi upeo kuliko ule muundo wa maana ya mwanzo kwenye lugha chanzi.

5.2.3 Maneno ya Kidini

Jina la Kundi	Idadi ya maneno	Asilimia %
1. Kidini	19	06.574

Jadweli Na.6 Maneno ya Kidini.

Adhana *أذنا*: Katika Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kipasuo koo ² chenye ghuna na irabu fupi chini mbele *a* na kufuatiwa na kikwamizi meno *ð* chenye ghuna na irabu ndefu mbele chini *a*: na kumalizikia kwa nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, Katika lugha hiyo ya Kiarabu muundo wake wa msingi ni /²aða:n/.

Kwa upande wa maana, neno hili linamaanisha “wito;wito wa sala”. Mandhour (-- :9 Juz. Xiii), El-jar (1973:52).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa irabu fupi chini mbele *a* na kufuatiwa na kikwamizi meno *ð* chenye ghuna na irabu fupi chini mbele *a* na kumalizikia kwa nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi chini mbele *a*. Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msngi ni /*adhana*/.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “matamshi maalumu ya Kiarabu yenye madhumuni ya kuwajuilisha Waislamu kuwa wakati wa sala umewadia”. BAKIZA (2010:2).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti, mwanzo wa neno hili kwenye Kiarabu limeanza kwa sauti konsonanti ² katika neno hili. Kwa hivyo, konsonanti hiyo ilibadilika na kuwa /a/ ambayo iko mwanzoni mwa neno hilo. Pili, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu chini /a:/

ambayo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Kwa upande wa maana hakuna badiliko lolote, kwani neno hilo linabeba dhana sawa kati ya Kiarabu na Kiswahili.

Adhuhuri **ظهر** : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi meno mtandazo *ž* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi koo *h* chenye ghuna na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, Neno hilo, katika lugha hiyo ya Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*žuhr*/. Kwenye Kiarabu neno hilo pia huchukua alama ya umaalumu (definite article) mwanzo, yaani *al* ambayo huungana na /*žuhr*/ kuwa /*ažžuhr*/.

Kwa upande wa maana, neno hili katika Kiarabu linamaanisha “nusu au katikati ya mchana.” El-Jar (1973:800).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa irabu fupi chini mbele *a* na kufuatiwa na kikwamizi meno *đ* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Muundo wake wa msingi ni /*adhuhuri*/.

Kwa upande wa maana katika Kiswahili, linamaanisha “sala ya faradhi inayosaliwa na waislamu katika wakati wa mchana; kipindi baina ya saa sita mchana mpaka saa tisa.” BAKIZA (2010:2).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna uingizaji sauti, kwenye muundo wake wa msingi neno hili lina mkusanyiko wa

konsonanti /hr/, imeongezwa sauti irabu *u* ili kuondosha mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu, kuna irabu /u/ mwisho wa neno kwenye Kiarabu, katika hali hiyo neno hilo lilipoingia kwenye Kiswahili, irabu hiyo ilibadilika na kuwa irabu /i/ mwisho. Pili, kuna upanuzi semantiki, neno hilo limepata maana jumuishi kuliko muundo wake wa awali wa maana kwenye Kiarabu. Hii ni kusema kwamba neno hilo limezidi upeo wa maana.

Ajinabi **أجنيبي**: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo koo ² chenye ghuna na irabu fupi chini mbele *a* na kufuatiwa na kikwamizi kaakaa gumu *ǰ* kisicho cha ghuna na nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi chini mbele *a* na kiyeyushi kaakaa *j* chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno. Kwa hivyo kwenye lugha hiyo ya Kiarabu, neno hilo muundo wake wa msingi ni /²*adǰnabij*/.

Katika lugha hiyo, neno hili linamaanisha “-geni, sio ya kawaida; mgeni, mtu asiye mwenyeji.” El-jar (2010:27).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa irabu fupi chini mbele *a* na kufuatiwa na kikwamizi kizuio kaakaa gumu *J* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni /*ajinabi*/.

Kwenye lugha hiyo, neno hilo lina maana ya “mtu asiyekuwa ndugu wa damu; mtu unayeweza kufunga naye ndoa.” BAKIZA (2010:4).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti, mwanzo wa neno hilo kwenye Kiarabu limeanza kwa sauti [?] ambayo ni konsonanti katika neno hili. Kwa hivyo neno hilo la Kiarabu lilipoingia kwenye Kiswahili, konsonanti hiyo ilidondoshwa na ikabakia sauti /a/ ambayo iko mwanzoni mwa neno hilo. Pili, kuna uongezaji sauti. Kwenye neno hili kuna mkusanyiko wa konsonanti Jn kwenye muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu, kutokana na hali hiyo baada ya neno kuingia kwenye Kiswahili liliongezewa sauti /i/. Tatu, kuna semantiki hamishi. Neno hili limepata maana iliyo kinyume na ile maana ya kwenye Kiarabu, hii ni kusema kuwa limepoteza mwelekeo wa maana baada ya kuingia kwenye Kiswahili. Kwenye dhana hiyo ya Kiswahili limeegemea zaidi umbali wa mtu anayeweza kuoa au kuolewa, dhana hiyo imeegemezwa hivyo kidini zaidi.

Baraka *بركة*: Kwenye Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kimadende *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, hivyo neno hili katika Kiarabu, muundo wake wa msingi ni */barakah/*.

Neno hili katika Kiarabu lina maana ya “uongezekaji wa ziada; furaha; neema; kheri inayoendelea;wingi wa kila jambo au kitu chenye kheri;”. Mandhour (-- 390 Juz. Xiii), El-Jar 1973:231). Katika mkabala wa kidini ni “wema wa jambo.”

Katika Kiswahili linaanzia kwa kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kimadende r chenye ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kipasuo kidakatonge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini. Katika Kiswahili, neno hili muundo wake wa msingi ni /*Baraka*/.

Katika Kiswahili neno hili linamaanisha “mambo mema kwa jumla, mafanikio neema, heri; wingi wa kitu.” BAKIZA (2010:20).

Badiliko la neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, badiliko pekee ni ile dhana iliyoko kwenye muktadha wa kidini inayopatikana katika neno hili.

Dhambi **ذنب**: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi meno δ chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na nazali ufizi n yenye ghuna, na kujiwa na kipasuo midomo b chenye ghuna na kuishia irabu fupi nyuma juu u na nazali ufizi n . Sauti nazali ufizi n imefuatiwa na sauti kipasuo midomo b kutokana na ujio huo imepatikana sauti nazali midomo m , ($n + b \rightarrow /m$). Kwa hivyo neno hili muundo wake wa msingi ni /*ḍamb*/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu lina maana ya “ ufanyaji wa jambo kinyume na sharia, kosa.” Moustafa (---) :316 Juz.II.

Katika Kiswahili linaanzia kwa kikwamizi meno δ chenye ghuna na irabu fupi chini a kumalizikia kwa nazali midomo m na kipasuo midomo b na irabu fupi mbele juu i ; muundo wake wa msingi ni /*dhambi*/.

Kwenye Kiswahili, neno hili lina maana ya “kosa linalovunja amri au sheria ya dini; maasi au uhalifu wa dini; malipo ya kitendo kinachokwenda kinyume na sheria ya dini.” TUKI (1981 :44).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wake wa msingi neno hili lina mkusanyiko wa konsonanti na irabu /u/ mwisho kwenye Kiarabu, katika hali hiyo neno hilo lilipoingia kwenye Kiswahili lilipata kabadala irabu /i/ mwisho wa neno. Pili, kuna semantiki upanuzi, neno hili baada ya kuingia kwenye Kiswahili limepata maana jumuishi kuliko ile maana ya Kiarabu, hii ni kusema kuwa neno limezidi upeo wa maana.

Dua دعاء: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi koromeo ^ʿ chenye ghuna na irabu ndefu chini *a*: na kumalizikia kwa kipasuo koo ^ʔ kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, hivyo neno hili muundo wake wa msingi ni /du^ʿa:ʔ/.

Kwa upande wa maana, kwenyenye Kiarabu lina maana ya “ombi au lile analoombewa yeyote liwe jema au baya; mwaliko” Moustafa (--- :286 Juz.I.

Katika Kiswahili, vilevile neno hili linaanzia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kumalizikia kwa irabu ya kati *a* katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*dua*/.

Kwenye Kiswahili, kwa upande wa maana lina maana ya “ombi la mja kwa Mola wake” BAKIZA (2010:72); neno hili ni katika jumla ya istilahi za dini hasa ya Kiislamu.

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwishakuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, lina irabu ndefu. Baada ya kuingia kwenye Kiswahili, irabu hiyo ilifupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu ulivyo katika Kiswahili. Pili, kuna udondoshi konsonanti pamoja na irabu /[?]*u*/. Tatu, kuna ufinyu semantiki, kwa upande wa maana, neno limechukua maana finyu katika Kiswahili.

Fatiha *فاتحة* : Kwenye Kiarabu neno hili lianaanzia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu chini *a*: na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kikwamizi koromeo *h* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno. Kwa hivyo kwenye Kiarabu, neno hili muundo wake wa msingi ni /*fa:tiħah*/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu linamaanisha “-enye kufungua, sura ya kwanza katika mpangilio wa msahafu; ufunguzi wa jambo, mwanzo wake muktadha huu ni usomaji wa *suratu-l-fatiha* kwa ajili ya kutaka kuomba dua.” Moustafa (--- : 671 Juz.II).

Katika Kiswahili linaanzia kwa kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kufuatiwa na kipasuo ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i na kumalizia kwa kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi chini a . Kwenye Kiswahili, neno hili muundo wake wa msingi ni

/fatiha/.

Kwa upande wa Kiswahili, lina maana ya “dua inayoanzia kwa kusomwa *alhamdu* na kumaliziwa kwa dua yenyewe iliyokusudiwa.” BAKIZA (2019:82).

Neno hili nalo linajitokeza katika Kiswahili kama ni istilahi ya kidini.

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu, katika muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, mwanzoni lina irabu ndefu. Baada ya kuingia kwenye Kiswahili, irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu za Kiswahili ulivyo. Pili, kuna Ubadili konsonanti, ubadili huo umetokea kwenye konsonanti $/h/$ katika neno hilo katika upande wa Kiarabu. Kwa kuwa sauti hiyo kwenye Kiswahili haipo, hivyo ilipata mbadala wa konsonanti $/h/$. Tatu, kuna upanuzi semantiki, neno hili baada ya kuingia kwenye Kiswahili limepata maana jumuishi kuliko ile maana ya Kiarabu, hii ni kusema kuwa neno limezidi upeo wa maana.

Futari **فطور**: Neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa sauti kikwamizi meno mdomo f isiyo ya ghuna yenye irabu fupi chini a na kufuatiwa na kipasuo meno mtandazo t na irabu ndefu nyuma juu u : na kuishia kwa kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali ufizi n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu,

kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno. Kwa hivyo kwenye lugha hiyo ya Kiarabu neno hilo muundo wake wa msingi ni /*faṭu:r*/.

Kwa upande wa maana, katika Kiarabu neno hili linamaanisha “chakula kinacholiwa mwanzo kama kifungua kinywa.” El-Jar (1973)

Kwenye Kiswahili linaanzia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kimadende *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Muundo wake wa msingi ni /*futari*/.

Katika Kiswahili neno hili lina maana ya “chakula kinacholiwa baada ya jua kutua katika mwezi wa ramadhani; chakula kama muhogo, viazi, ndizi, kunde n.k.” KKS (2004:90).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu, kwenye muundo wa msingi, neno hili lina irabu ndefu *u*:. Irabu hii imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika lugha hiyo. Pili, kuna ubadili irabu, neno hili mwisho lina irabu /*u*/ kwenye muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu. Irabu hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa /*i*/ . Tatu, kuna semantiki hamishi, kwenye neno hili umetokea uhamishaji kamili wa maana inayopendeza katika Kiswahili, maana hiyo mpya ina uhusiano na maana iliyotangulia. Dhana inayobeba maana ya neno hili imegemea kwenye muktadh wa kidini.

Halali *حلال* : Kwenye Kiarabu neno hilo, linaanzia kwa kikwamizi koromeo *ḥ* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu mbele chini *a*: , na kumalizikia kitambaza ufizi *l* chenye irabu

fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno. Kwa hivyo Katika lugha hiyo ya Kiarabu neno hilo muundo wake wa msingi ni */ħala:l/*.

Kwa upande wa maana, neno hilo kwenye Kiarabu linamaanisha “kitu au jambo lenye kuruhusiwa, isiyo katazwa; ya kisheria; yenye kukubalika kwa mujibu wa sheria ya nchi; yenye kuruhusiwa kwa mujibu wa dini ya Kislamu.” El-Jar (1973).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia kwa kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili neno hilo muundo wake wa kmsingi ni */halali /*.

Kwenye Kiswahili, neno hilo lina maana ya “kitu au jambo lenye kukubalika kwa mujibu wa sheria ya nchi; yenye kuruhusiwa kwa mujibu wa dini ya Kiislamu.” BAKIZA (2010: 109).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti, ubadili huo umetokea kwenye konsonanti */ħ/* kwenye neno hilo katika upande wa Kiarabu. Kwa kuwa sauti hiyo kwenye Kiswahili haipo, hivyo ilipata mbadala wa konsonanti */h/*. Pili, kuna ufupishi irabu, katika muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, katikati neno hili lina irabu ndefu. Baada ya kuingia kwenye Kiswahili, irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu za Kiswahili ulivyo.

Tatu, kuna ufinyu semantiki, kwa upande wa maana neno limechukua maana finyu katika Kiswahili kuliko ile maana ya Kiarabu.

Halafu **خلف**: Kwenye Kiarabu, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini x chenye ghuna na irabu fupi mbele chini a na kufuatiwa na kitambaza ufizi l kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini a na kumalizikia kwa kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini a . Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, neno hilo katika lugha hiyo ya Kiarabu muundo wake wa msingi ni */xalaf/*.

Kwa upande wa maana, neno hilo linamaanisha “kuwa mrithi, fuatia baada ya, kuja baada ya; chukua nafasi au pahali pa; kuwa badili ya.” Ibnu Mandhour (-- : 82 Juz.ix), El-Jar (1973).

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi mbele chini a na kufuatiwa na kitambaza ufizi l kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini a na kumalizikia kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u . Katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni *[halifu]*.

Kwa upande wa maana, neno hilo linamaanisha “kitendo cha mtu kufa kabla ya mrithiwa; tenda kinyume cha kanuni au sheria, vunja sheria, kataa kutii, asi.” BAKIZA (2010: 109).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti, ubadili huo umetokea kwenye konsonanti $/x/$ katika neno hilo kwenye upande wa Kiarabu. Kwa kuwa sauti hiyo kwenye Kiswahili haipo, hivyo ilipata mbadala

wa konsonanti /h/. Pili, kuna upanuzi semantiki, neno hili limepata maana jumuiishi kuliko maana ya mwanzo, neno hili limezidi upeo wa maana. Linajitokeza kama kitenzi kinachobeba dhana ya kufa mrathi kwanza kabla ya mrithiwa na dhana ya kutotii na kuvunja sheria.

Hitima خاتمة : Neno hili katika Kiarabu, linaanzia kwa kikwamizi kidakatonge x na irabu refu nyuma a : na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi t chenye irabu fupi mbele juu i na kumalizikia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi chini a na kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali ufizi n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo kwenye Kiarabu, neno hili muundo wake wa msingi ni / $xa:timah$ /.

Kwa upande wa maana, neno hili katika Kiarabu lina maana ya “umalizaji wa jambo; jambo linalomaliziwa kwenye kitabu; umwagiliaji maji wa mazao; mwisho wa jambo au kitu chochote.” Katika muktadha wa kidini ni “kumaliza k.m. kuandika au kusoma kitabu k.v. Kuraani n.k.” El-Jar (1973), Ibnu Mandhour (-- : 163 Juz. xii).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi koo h chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i na kumalizikia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi chini a . Kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni / $hitima$ /.

kwenye Kiswahili linamaanisha “usomaji wa Kuraani pamoja na dua nyenginezo kwa ajili ya kumuomba maiti afikishiwe thawabu za kisomo hicho.” BAKIZA (2010: 117).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu. Kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, konsonanti ya pili kutoka mwanzo ina irabu ndefu /a:/, baada ya kuingia kwenye Kiswahili neno hili, irabu hiyo imefupishwa na kuwa fupi /a/ ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu za Kiswahili ulivyo na pia ikabadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Pili, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili limemalizikia kwa irabu /u/, lilipoingia kwenye Kiswahili irabu hiyo ilibadilika na kuwa /a/ mwisho. Tatu, kuna ufinyu semantiki, kwa upande wa maana neno hili limechukua maana finyu katika Kiswahili kuliko ile maana ya Kiarabu. Maana hiyo ya Kiswahili katika ufinyu wake, imejikita zaidi kwenye usomaji wa Kuraan na kumuombea maiti kwa muktadha wa kidini.

Juzuu جزء : Neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa sauti kikwamizi kaakaa gumu *dz* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na kumalizikia kwa kipasuo koo² na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo kwenye Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*dzuz*²/.

Kwa upande wa maana, katika Kiarabu linamaanisha kuwa ni “sehemu ya jambo au kitu; kipande.” Ibnu Mandhour (-- : 45 Juz. ii).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi kizuio kaakaa gumu *J* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na kumalizikia kwa irabu ndefu nyuma juu *u*: Kwenye Kiswahili, neno hili muundo wake wa msingi ni /*juzuu* /.

Kwenye Kiswahili lina maana ya sehemu moja kati ya thalathini zilizomo katika msahafu; sehemu moja ya kitabu kilichogawanywa katika sehemu nyingi.” BAKIZA (2010: 136).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti, sauti konsonanti /²/ katika neno hilo kwenye Kiarabu, kwa kuwa sauti hiyo kwenye Kiswahili haipo, hivyo ilidondoshwa na kubakia irabu /u/. Pili, kuna ufinyu semantiki, kwa upande wa maana neno hili limechukua maana finyu katika Kiswahili kuliko ile maana ya Kiarabu. Maana hiyo ya Kiswahili katika ufinyu wake, imejikita zaidi kwenye sehemu ya maandiko na muktadha wa kidini.

Kuzaini *كزين*: Kwenye Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kiyeyushi kaakaa gumu *j* na kumalizikia kwa nazali ufizi *n* yenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /zajn/.

Maana ya neno hili kwa Kiarabu ni “jambo au kitu kinachotumika katika kupamba, pambo; -zuri,-ipendezayo.” Ibnu Mandhour (-- :201 Juz. I).

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa nazali ufizi yenye ghuna *n* na irabu fupi mbele juu *i*. Kwenye Kiswahili, muundo wake wa msingi ni /kuzaini/.

Katika Kiswahili neno hili lina maana ya “kushawishiwa na shetani ili ufanye jambo baya na kupata dhambi.” BAKIZA (2010: 463), KKS (2004:466).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kungia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu, neno hili kwenye muundo wake wa msingi, limejitokeza kama nomino yenye mkusanyiko wa konsonanti mwisho *jn* na kumalizikia irabu /u/. Kwa hivyo lilipoingia kwenye Kiswahili lilipata badili ya irabu /i/ mwisho wa neno hili. Pili, kuna semantiki hamishi, kwenye neno hili umetokea uhamishaji kamili wa maana inayopendeza katika Kiswahili. Dhana inayobeba maana ya neno hili imeegemea zaidi kwenye muktadha wa kidini.

Maghufira مغفرة: Katika Kiarabu, neno hili linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *y* chenye ghuna na kumalizikia kwa kikwamizi meno *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele *i* na kimadende *r* chenye irabu fupi chini *a* na kipasuo meno *t* ufizi kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo kwenye Kiarabu, neno hili muundo wake wa msingi ni /*mayfirah* /.

Maana ya neno hili katika Kiarabu ni “msamaha, kusitiri, kufunika”; katika mkabala wa kidini ni “kusamehewa makosa aliyoyafanya mja kwa Mola wake.” El-Jar 1973:), Ibnu Mandhour (-- : 25 Juz. v).

Katika Kiswahili linaanzia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kikwamizi koromeo y chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na kumalizikia kwa kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele i na kimadende r chenye ghuna na irabu fupi chini a . Katika Kiswahili neno hili muundo wake wa msingi ni [*mayufira*].

Kwenye Kiswahili liliingia kidini, kwa hivyo maana yake iko kwenye kidini zaidi kama ilivyokwisha elezwa.

Mabadiliko ya neno hili baadaya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna uongezaji sauti, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu kuna konsonanti mkusanyiko yf , kwa hivyo lilipoingia kwenye Kiswahili sauti irabu /u/ iliongezwa ili kuondoa mkusanyiko huo. Pili, kuna ufinyu semantiki, kwa upande wa maana neno hili limechukua maana finyu katika Kiswahili kuliko ile maana ya Kiarabu. Maana hiyo ya Kiswahili katika ufinyu wake, imejikita zaidi kwenye msamaha kwa muktadha wa kidini.

Maulidi مولد : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kiyeyushi mdomo w na kitambaza ufizi l kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi d chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali ufizi n . Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*mawlid* /.

Kwa upande wa maana, neno hili kwenye Kiarabu lina maana ya “uzawa wa mtu; mzazi, muda au wakati wa kuzaliwa.” BAALBAKI (2003:1143).

Kwenye Kiswahili linaanzia vilevile kwa nazali midomo *m* na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na irabu fupi nyuma juu *u* na kumalizikia kwa kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*maulidi*/.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “maelezo ya maisha ya Nabii Muhammad (s.a.w) yaliyo katika sura ya ushairi; kisomo cha maelezo hayo; sherehe ya kuadhimisha kuzaliwa Nabii Muhammad (s.a.w).” BAKIZA (2010:227)

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu, neno hili kwenye muundo wake wa msingi, linajitokeza kama nomino yenye mkusanyiko wa konsonanti mwisho na kumalizikia kwa irabu /u/. Kwa hivyo lilipoingia kwenye Kiswahili lilipata irabu hiyo iliyobadilika na kuwa /i/ mwisho wa neno hili. Pili, kuna semantiki imarishi, neno hili limepata maana jumuishi chanya inayopendeza. Dhana inayochukua hiyo maana jumuishi chanya inayopendeza kwenye Kiswahili iko kidini zaidi.

***Mсахafu* مصحف**: Katika Kiarabu neno hili, linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi mtandazo *ş* kisicho cha ghuna na kikwamizi koromeo *h* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna na irabu fupi nyuma juu una nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa

Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo kwenye Kiarabu neno hili, muundo wake wa msingi ni /muṣḥaf/.

Kwenye muktadha wa maana, neno hili katika Kiarabu linamaanisha “kitabu kitukufu cha Kur-ani cha Waislamu; kitabu chenye kurasa zenye maandishi.” BAALBAKI (2003:1052), El-Jar (1973: 1121).

Kwenye Kiswahili vilevile, linaanzia kwa nazali midomo *m* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi juu nyuma *u*. Kwenye Kiswahili, neno hili muundo wake wa msingi ni / *msahafu* /.

Katika Kiswahili limeingia kwenye muktadha wa kidini kwa maana kitabu cha Kur-ani. BAKIZA (2010:270).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, irabu /u/ ya mwazo imedondoshwa. Pili, kuna uongezaji sauti; katikati ya neno hili kwenye muundo wake wa msingi, kuna konsonanti mkusanyiko *ṣḥ*, umeongezewa sauti irabu /a/ kati ili kuondoa mkusanyiko huo. Kwenye neno hili hakuna mabadiliko ya dhana na kimaana.

Sala صلاة: Neno hili kwenye Kiarabu linaanzia kwa kikwamizi ufizi mtandazo *ṣ* kisicho cha ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* chenye irabu ndefu chini *a*: na kumalizikia kwa kipasuomeno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu,

kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hili muundo wake wa msingi ni /*ṣala:h*/.

Maana ya neno hili katika Kiarabu, kimsingi ni “ombi au dua; rehema; msamaha, maghufira”, lakini katika muktadha wa kidini hasa kwa mwislamu ni “harakati anazozifanya baada ya kuhirimia ikiwemo kurukuu, kusujudu pamoja na matendo na visomo vyote katika shughuli hiyo.” Ibnu Mandhour (---:464 Juz.xiv), El-Jar (1973: 748).

Katika Kiswahili, linaanzia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kitambaza ufizi *l* chenye irabu fupi chini *a*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*sala*/.

Katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hili lina maana ya “vitendo vinavyofanywa kuanzia kuhirimia hadi kutoa salamu.” BAKIZA (2010: 353).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, mwishoni mwa neno kuna irabu ndefu. Baada ya kuingia kwenye Kiswahili, irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu za Kiswahili ulivyo. Pili, kuna ubadili irabu, kuna irabu /u/ mwisho kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, katika hali hiyo neno hilo lilipoingia kwenye Kiswahili lilipata mbadala wa irabu /a/ mwisho. Tatu, kuna ufinyu semantiki, kwa upande wa maana, neno limechukua maana finyu katika Kiswahili kuliko ile maana ya Kiarabu.

Shekhe شَيْخ: Katika Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kikwamizi ufizi kaakaa *f* kisicho cha ghuna na irabu irabu fupi chini *a* ikifuatiwa na kiyeyushi kaakaa gumu *j* na

kikwamizi kakaa laini x na kumalizikia irabu fupi numa juu na nazali ufizi n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo muundo wake wa msingi ni $/fajx/$.

Maana ya neno hili kwa Kiarabu ni “mtu ambaye umri wa ujana wake umemaliza na kuingia umri wa utu uzima wake ; kiongozi wa watu hata kama umri wake si mkubwa. Mwalimu mkubwa ambaye watu hupata elimu kutoka kwake.” El-Jar (1973: 728-729), Ibnu Mandhour (--:39 Juz.iii).

Kwenye Kiswahili linaanzia kwa kikwamizi ufizi kaakaa f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele kati ε na kumalizikia kwa kikwamizi kaakaa laini x chenye ghuna na irabu fupi mbele kati ε , neno hilo muundo wake wa msingi ni $/shekhe/$.

Katika Kiswahili lina maana ya “mwanachuoni mwenye kiwango cha juu cha elimu ya dini ya kiislamu.” BAKIZA (2010:363).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna uimarishi irabu, katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno hili kuna irabu pacha $/aj/$ ambayo imeinuliwa na kuwa irabu ya kati fupi $/\varepsilon/$ kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hilo katika Kiarabu limeishia kwa irabu $/u/$, kwa hivyo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili irabu hiyo ilibadilika na kuwa irabu ya kati fupi $/\varepsilon/$ ambayo iko mwisho wa neno hilo. Tatu, kuna semantiki imarishi, neno hili limechukua maana mpya katika muktadha wa kidini.

Thawabu ثواب : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi meno θ isiyo ya ghuna yenye irabu ndefu chini a : na kufuatiwa na kiyeyushi mdomo w na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali ufizi n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, hivyo kwenye Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/\theta awa:b/$.

Kwa upande wa maana katika Kiarabu, neno hili linakusudiwa “malipo kutokana na kufanya jambo jema; kipawa, tunuku”, kidini ni “malipo anayoandikiwa mtu na Mwenyezi Mungu kwa kufanya jambo au amali njema.” El-Jar (1973: 369).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi meno θ kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kufuatiwa na kiyeyushi mdomo w na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u , kwenye Kiswahili neno hili muundo wake wa msingi ni $/thawabu/$.

Neno hili liliingia kwa mintarafu ya kidini lenye maana ya “malipo anayoandikiwa mtu na Mwenyezi Mungu kwa kufanya jambo au amali njema.” BAKIZA (2010: 395).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu katikati ya neno hili kuna irabu ndefu, baada ya kuingia kwenye Kiswahili, irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu za Kiswahili ulivyo. Pili, kuna ufinyu semantiki, kwa upande wa maana neno hili limechukua maana finyu katika Kiswahili kuliko ile maana ya Kiarabu. Maana hiyo imejikita kwenye malipo ya Mwenyezi Mungu kwa wajawake tu.

Uradi **ورد** : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kiyeyushi mdomo *w* chenye irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kimadende *r* chenye ghuna na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hili katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */wird/* na wingi wake ni *awra:d*.

Katika jumla ya maana za neno hili katika Kiarabu, mojawapo ni sehemu ya Kuraani tukufu inayosomwa kila usiku; katika mkabala wa kidini ni Kuraani pamoja na baadhi ya dua zinazosomwa kwa mnasaba maalumu kwa mujibu wa mapokezi ya hadithi za Mtume (S.A.W). El-Jar (1973:1281), BAALBAKI (2003:1228-1229), Ibnu Mandhour (--:456 Juz.iii). .

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kwa irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kimadende *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni */uradi/*.

Kwa upande wa Kiswahili liliingia kidini na maana yake ni hiyo hiyo iliyoelezwa kidini kwenye Kiarabu. BAKIZA (2010: 437), KKS (2004:440).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwishakuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu. Kabla ya konsonanti ya mwisho kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu kuna irabu ndefu */a:/*, baada ya kuingia kwenye Kiswahili, irabu hiyo imefupishwa na kuwa */a/* ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu za Kiswahili ulivyo. Pili, kuna ubadili irabu,

kwenye muundo wake wa msingi neno hili lina irabu /u/ mwisho kwenye Kiarabu, katika hali hiyo neno hilo lilipoingia kwenye Kiswahili irabu hiyo ilibadilika na kuwa /i/ mwisho. Kwa upande wa maana neno hili limebakia na maana ile ile ya mwanzo katika Kiarabu pamoja na mwelekeo wa kidini.

5.2.4 Maneno ya Kitaaluma

Jina la Kundi	Idadi ya maneno	Asilimia %
1. Kitaaluma	26	08.996

Jadweli Na.7 Maneno ya Kitaaluma.

Daftari دفتر: Katika Kiarabu, neno hilo linaanzia kwa kipasuo meno ufizi d chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna na kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a , na kumalizikia kwa kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */daftar/*.

Neno hili kwenye lugha hiyo ya Kiarabu linamaanisha “kitabu kinachoandikiwa hesabu na mambo mengine yanayohitaji kuhifadhiwa na kutunzwa; karatasi zilizowekwa / kukusanywa pamoja” El-Jar (1973:535), Ibnu Mandhour (-- : 289 Juz. iv).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kipasuo ufizi d chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna na kipasuo ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kimadende ufizi r chenye

ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni /*daftari*/.

Neno hilo kwenye Kiswahili lina maana ya “kitabu cha kutunzia kumbukumbu; buku la kuandikia.” KKS (2004:56), BAKIZA (2010:60).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; badiliko hilo linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu ambalo lina irabu fupi nyuma juu /*u*/ mwisho wa neno hilo, irabu hiyo kwenye Kiswahili imepata badili, nayo ni irabu fupi mbele juu /*i*/. Pili, kuna ufinyu semantiki, huu ni mchakato wa mbano wa maana uliotokea kwenye neno hili ambalo limepata maana finyu zaidi.

***Dahalia* داخلية**: Katika Kiarabu, neno hilo linaanzia kwa kipasuo meno ufizi *d* na irabu ndefu mbele chini *a*: na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *x* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kiyeyushi kaakaa gumu *j* chenye irabu fupi mbele chini *a*, na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo kwenye Kiarabu, neno hili muundo wake wa msingi ni /*da:xiliyah*/.

Katika lugha hiyo ya Kiarabu, neno hilo lina maana ya “mwanafunzi anayeishi, kula na kulala skuli, mwanafunzi wa skuli ya bweni.” El-Jar (1973:518).

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kipasuo koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia kwa kitambaza ufizi *l* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kuishia irabu fupi *a*. Neno hilo katika lugha ya Kiswahili muundo wake wa msingi ni */dahalia/*.

Neno hilo lina maana ya “mahali wanapoishi wanafunzi kwa shughuli za kimasomo; nyumba maalumu wanayolala wanafunzi wasiorudi majumbani mwao baada ya masomo, bweni la wanafunzi.” BAKIZA (2010:61).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu chini */a:/* mwanzo wa neno hilo, kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu. Irabu hiyo katika Kiswahili imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili konsonanti. Kwenye muundo wa msingi wa neno hili katikati kuna konsonanti *x* ambayo ni sauti kikwamizi koromeo. Sauti hiyo [x] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imebadilishwa kwa konsonanti */h/* kwenye Kiswahili. Tatu, kuna udondoshi konsonanti; badiliko hili ni la udondoshi wa konsonanti radidi */yy/* zilizopo mwisho wa neno hili. Udondoshi huu ni kwa lengo la kuondosha mkusanyiko huo uliopo katika neno hili la Kiswahili. Nne, kuna ubadili irabu; badiliko hilo linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu ambalo lina irabu fupi chini juu */u/* mwisho wa neno hilo, irabu hiyo kwenye Kiswahili imepata badili nayo ni irabu fupi mbele juu */a/*. Tano, kuna upanuzi semantiki, neno hili limepata maana ambayo ni jumuishi kuliko ile ya muundo wa maana ya mwanzo kwenye Kiarabu, maana hiyo ya Kiswahili ni pana zaidi

na yenye upeo wenye dhana ya mahali wanapoishi wanafunzi wasiorudi majumbani kwao kwa ajili ya masomo.

Darasa *درس*: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kimadende *r* chenye ghuna na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hili katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */dars/*.

Kwa muktadha wa maana neno hili kwenye Kiarabu linamaanisha “jambo linalosomeshwa ambalo limo katika kitabu, somo.” El-Jar (1973:530).

Katika Kiswahili neno hili, linaanzia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna na irabu fupi chini *a*. Kwenye Kiswahili neno hili muundo wake wa msingi ni */darasa/*.

Katika Kiswahili lina maana ya “sehemu au chumba kinachotumika kwa kusomeshea wanafunzi.” BAKIZA (2010:63).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu, badiliko hilo linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu, kuna mkusanyiko wa konsonanti */rs/* na irabu fupi nyuma juu */u/* mwisho wa neno. Irabu hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi chini */a/*. Pili, kuna uongezaji sauti irabu */a/* ili kuondosha mkusanyiko wa konsonanti uliopo. Tatu, kuna

semantiki hamishi, neno hili limepata maana yenye kinyume kidogo na ile maana asili ya Kiarabu. Maana hiyo ni mpya, imejikita zaidi katika chumba au sehemu ya kufundishia wanafunzi.

Durusu درس : Neno hilo katika Kiarabu, linaanzia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika lugha hiyo ya Kiarabu muundo wake wa msingi ni */daras/*.

Kwa muktadha wa maana ya neno hilo kwenye lugha hiyo, linamaanisha “fukuza, achisha; soma na hifadhi; pitiwa na muda; ingilia,jamii; ingia kwenye hedhi” Fairouzabadi (--- :206 Juz.i), El-Jar (1973:530).

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hilo katika lugha hiyo ya Kiswahili muundo wake wa msingi ni */durusu/*.

kwa upande wa maana, neno hili katika Kiswahili lina maana ya “kitendo cha kurudia k.v. somo au kitabu, pitia maandishi, talii.” BAKIZA (2010:74), KKS 2004:70).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna badiliko la irabu juu. Kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, irabu zote tatu za neno hili ni fupi chini */a/*. Katika Kiswahili irabu zote hizo ni fupi zimekuwa za nyuma juu */u/*. Pili, kuna semantiki hamishi, badiliko lililolifanya neno hili kupata maana

mpya yenye kinyume na ile maana asili ya Kiarabu, na pia hakuna uhusiano wowote na maana hiyo mpya.

Falaki **فلك**: Kwenye Kiarabu neno hili, linaanzia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo ufizi *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo katika lugha hiyo ya Kiarabu, neno hilo muundo wake wa msingi ni */falak/*.

Kwa muktadha wa maana, katika lugha hiyo ya Kiarabu linamaanisha “njia za mzuguuko wa nyota angani; kitu au jambo lolote la duara.” El-Jar (1973:917).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi meno *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo katika lugha ya Kiswahili muundo wake wa msingi ni */falaki/*.

Kwa muktadha wa maana katika lugha hiyo ya Kiswahili lina maana ya “taaluma ya kufahamu nyota na kazi zake, unajimu; maarifa ya kubashiri matukio kwa kutumia elimu ya nyota; njia dhahania inayopita sayari.” BAKIZA (2010:80), KKS 2004:76).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu, badiliko hilo linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu ambalo lina irabu fupi chini juu */u/* mwisho wa neno hilo, irabu hiyo kwenye

Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Pili, kuna semantiki imarishi, neno hili limepata maana jumuishi chanya katika Kiswahili, hali hiyo ni mwendelezo mzuri katika maana hiyo ya neno.

Fasili *فصل*: kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *ṣ* mtandazo kisicho cha ghuna na kujiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo katika lugha hiyo ya Kiarabu, neno hilo muundo wake wa msingi ni /*faṣl* /.

Kwa muktadha wa maana, neno hilo kwenye lugha hiyo lina maana ya “kizuizi baina ya mambo mawili; makutano ya mifupa miwili mwilini; tawi; sura katika kitabu; sehemu moja kati ya sehemu nne za mwaka; moja kati ya sehemu za igizo; hukmu baina ya haki na batili; ukuta mdogo chini ya kiwango cha ngome.” Ibnu Mandhour (-- :520 Juz.xi), El-Jar (1973:910).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kujiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*fasili*/.

Kwa upande wa maana, neno hili lina maana ya “maelezo yanayofafanua maana ya neno fulani; upambanuzi wa maandishi katika kitabu kwa kuyagawa katika sehemu; tumbo katika jamii lenye sifa nzuri, ukoo unaojulikana; kitendo cha kueleza waziwazi, fafanua; kitendo cha kueleza maana au tafsiri ya istilahi; kitendo cha kukatakata kitambaa kwa

mujibu wa vipimo kabla hakijashonwa nguo; kitendo cha kupambanua jambo ili liwe wazi.” BAKIZA (2010:82).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu, badiliko hilo linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu. Kuna mkusanyiko wa konsonanti /s/ na irabu fupi chini juu /u/ mwisho wa neno, irabu hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Pili, kuna uongezaji sauti irabu /i/ ili kuondosha mkusanyiko wa konsonanti uliopo. Tatu, kuna semantiki hamishi, neno hili limepata uhamishi kamili wa maana ambayo ni kinyume na maana ile ya Kiarabu, kwa kiasi kidogo neno hilo limepoteza mwelekeo wa maana iliyotangulia au kwa maneno mengine limechukua maana mpya.

Ghuna غنة: Katika Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *y* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kumalizikia kwa nazali meno ufizi *n* yenye mkazo na ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hili katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*yu'nah*/.

Kwa upande wa maana, neno hili kwa Kiarabu ni “sauti inayotokea kwenye kaaka laini na pua.” El-Jar (1973:887), Ibnu Mandhour (-- :315 Juz.xiii).

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *y* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hili, kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni

/yuna /.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “sauti ya mngurumo inayotoka kwenye koromeo.” Masamba, na wenziwe (2004:33-34).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu, badiliko hilo linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi. Kwenye Kiarabu kuna mkusanyiko wa konsonanti /nn/ na irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno, irabu hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /a/. Pili, kuna udondoshi konsonanti radidi /nn/ japo kwamba konsonanti radidi hizo haziko mwisho wa neno, moja kati ya hizo imedondoshwa kwa lengo la kuondosha mkusanyiko huo uliopo. Tatu, kuna semantiki hamishi, badiliko lililolifanya neno hili kupata maana mpya yenye kinyume kidogo na ile maana asili ya Kiarabu, lakini kuna uhusiano wa maana hiyo mpya. Uhusiano uliopo kwenye maana hiyo ni kule kujikita kwa maana mbili hizo kwenye sauti. Kinyume kilichopo baina ya maana hizo mbili ni pale mahali pa matokeo ya sauti hizo.

Hadhira *حاضرة* : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi *ḍ* chenye ghuna na irabu ndefu mbele juu *i:* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo katika lugha hiyo ya Kiarabu, neno hilo muundo wake wa msingi ni /*hādī:rah*/.

Kwa muktadha wa kimaana, neno hili katika lugha hiyo ya Kiarabu linamaanisha “mahali panapowekewa tende; kikundi cha watu wanne mpaka wanane.” BAALBAKI (2003 :446), El-Jar (1973:452), Ibnu Mandhour (-- :196 Juz.iv).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na sauti kikwamizi meno ulimi *ḍ* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hili kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*hadhira*/.

Kwa upande wa maana, neno hilo katika Kiswahili lina maana ya “msomaji, mtazamaji au msikilizaji wa kazi ya fasihi.” BAKIZA (2010:107), KKS (2004:104).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu mwisho lina irabu fupi nyuma juu /*u*/. Irabu hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi chini /*a*/. Pili, kuna ufupishi irabu, kwenye muundo wa msingi neno hili katikati lina irabu ndefu mbele juu *i*:. Irabu hiyo kwenye Kiswahili imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu wa lugha hiyo ya Kiswahili. Tatu, kuna ufinyu semantiki, huu ni mchakato wa mbano wa maana uliotokea kwenye neno hili ambalo limepata maana finyu zaidi. Neno hili limejikita katika muktadha wa kifasihi unaowahusisha watu wanaoishghulikia kazi ya fasihi kwa kuisoma, kuitazama au kuisikiliza.

***Ikisiri* قصر**: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo kidakatonge *q* na irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi kaakaa gumu *ṣ* mtandazo kisicho cha ghuna na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*.

Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hili kwenye Kiarabu muundo wake wa msingi ni /qiʃr/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu linamaanisha “uchache wa urefu, ufup; -fupi.” El-Jar (1973: 953), Ibnu Mandhour (-- : 95 Juz.vi).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kimadende ufizi *r* chenye irabu fupi mbele juu *i*.

Kwa upande wa Kiswahili muundo wake wa msini ni / ikisiri/, neno hili lina maana ya “maelezo mafupi kuhusu kitabu au makala.” BAKIZA (2010:123).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna uongezaji sauti irabu. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, katikati ya neno hili kuna mkusanyiko wa konsonanti *ʃr*, kwa hivyo kwenye Kiswahili mkusanyiko huo uliongezewa sauti irabu /i/ ili kuondosha mkusanyiko konsonanti huo. Vilevile neno hili limeongezewa irabu /i/ mwanzo. Pili, kuna ubadili irabu, badiliko hilo linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu. Kwenye muundo huo kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno, irabu hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Tatu, upanuzi semantiki, neno hili limepata maana ambayo ni jumuishi kuliko muundo wa maana ya mwanzo kwenye Kiarabu, maana hiyo ya Kiswahili ni pana zaidi na yenye upeo.

Isimu اسم : Kwenye Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kipasuo koo ^ʔ kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbelu juu *i* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kumalizikia kwa nazali meno ufizi *n* yenye ghuna. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /^ʔism/.

Kwa upande wa maana, neno hili katika Kiarabu linamaanisha “jina la mtu, kitu au jambo.” El-Jar (2010: 96),

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kwa irabu fupi mbele juu *i* ikifuatiwa na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Muundo wake wa msingi ni [*isimu*].

Kwenye Kiswahili neno hili lina maana ya “taaluma ya uchambuzi wa lugha kwa njia ya kisayansi, sayansi ya lugha, lughawiya, tamko linalosisitiza jambo.” BAKIZA (2010 :123).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna uongezaji sauti irabu /i/ ili kuondosha mkusanyiko wa konsonanti uliopo mwanzoni mwa neno hili. Pili, kuna udondoshi konsonanti, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, kuna sauti konsonanti kipasuo koo /^ʔ/ sauti hiyo imedodoshwa kwenye Kiswahili. Tatu, kuna Semantiki hamishi; badiliko lililolifanya neno hili kupata maana mpya yenye kinyume na ile maana asili ya Kiarabu, na pia hakuna uhusiano wowote na maana hiyo mpya. Badiliko hilo limejikita zaidi kwenye sayansi ya lugha.

Kuakisi عكس : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi koromeo ζ yenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a . Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, muundo wake wa msingi ni /^ʕakas/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hili linamaanisha “kugeza mwanzo mwisho na mwisho mwanzo; vutia chini kisha kandamiza na angusha chini; vuta na binya kwa nguvu; fungua ngamia shingo kwenye mguu wake mmoja hali ya kuwa kalala.” El-Jar (1973:846), Ibnu Mandhour (-- :144 Juz. xi). Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa kipasuo kidakatonge k kisicho ghuna chenye irabu fupi mbele juu i na kufuatiwa na irabu fupi chini a na kipasuo kidakatonge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i . Kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni /kuakisi/.

Katika Kiswahili lina maana ya “kurudisha nyuma mwanga au mionzi; kuashiria au kuonesha jambo fulani k.v kwa kupitia kwenye uandishi n.k.” BAKIZA (2010:5).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Kwenye muundo wa msingi wa neno hili mwanzo kabisa kuna konsonanti ^ʕ ambayo ni sauti kikwamizi koromeo. Sauti hiyo [^ʕ] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imepata badili /a/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu, katika muundo wa msingi kwenye Kiarabu kuna irabu katikati na mwisho wa neno ambazo ni fupi chini /a/. Irabu hizo zote mbili katika Kiswahili kwenye neno hili zimebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Tatu, kuna semantiki hamishi, kwenye neno hili umetokea

uhamishaji kamili wa maana inayopendeza katika Kiswahili, maana hiyo mpya kwa kiasi ina uhusiano na maana iliyotangulia.

Kufasiri *فيسر*: Katika Kiarabu, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi meno f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kujiwa na kimadende ufuzi r chenye ghuna na irabu fupi chini a . Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwenye lugha hiyo ya Kiarabu, kwa hivyo neno hilo muundo wake wa msingi ni */fasar/*.

Kwa muktadha wa maana, neno hilo lina maana ya “fafanua na bainisha; funua kilichofunikwa; chunguza k.m ili kujua maradhi aliyonayo mhusika .” El-Jar (1973:908), Ibnu Mandhour (-- :55 Juz.v).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kipasuo kidakatonge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na kiwamizi f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i na kujiwa na kimadende ufuzi r chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i . Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni */fasiri/*.

Kwa muktadha wa maana, neno hilo kwa lugha ya Kiswahili linamaanisha “kitendo cha kuhamisha maana ya matini ya lugha moja na kuipeleka kwenye lugha nyengine, tarjumi.” BAKIZA (2010:82), KKS (2004:78).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu kwenye muundo wa msingi wa neno hili kuna irabu tatu fupi chini */a/* zinazojenga neno hilo. Irabu mbili, ya pili na ya tatu kwenye Kiswahili zimebadilika na kuwa fupi

mbele juu /i/. Pili, kuna semantiki hamishi, neno hili limepata maana yenye kinyume kidogo. Maana imejikita katika uhamishaji wa maana kutoka lugha moja kwenda lugha nyengine.

Kuhakiki حَقَّقَ : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini mbele *a* na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge *q* kisicho cha ghuna chenye mkazo na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa tena na kipasuo kidakatonge *q* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini mbele *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*haqqaq*/.

Kwa muktadha wa kimaana katika lugha hiyo ya Kiarabu, neno hilo linamaanisha “tekeleza, timiza, pata, fanya; toa, zalisha; timiza; jibu, itikia; thibitisha, hakikisha; sadikisha.” BAALBAKI (2003:481), El-Jar (1973: 457).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge *k* isicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele mbele juu *i* na kufuatiwa tena na kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. Neno hili kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*kuhakiki*/.

Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, katika muktadha wa kimaana, linamaanisha “kitendo cha kuchambua maandishi hasa kazi za fasihi; kitendo cha kuthibitisha uhalisi wa kitu.” BAKIZA (2010:108).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti, kwenye muundo wa msingi wa neno hili mwanzo kabisa kuna konsonanti \hbar ambayo ni sauti kikwamizi koromeo. Sauti hiyo $[\hbar]$ haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imebadilika na kuwa konsonanti /h/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna udondoshi konsonanti, badiliko hili ni la udondoshi wa konsonanti radidi /qq/ zilizopo katikati ya neno kwenye muundo wake wa msingi. Udondoshi huu ni kwa lengo la kuondosha mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Tatu, kuna semantiki imarishi, neno hili limepata maana jumuishi chanya katika Kiswahili, hali hiyo ni mwendelezo mzuri katika maana hiyo ya neno. Neno limejikita katika uchambuzi wa kazi za maandishi na ithibati ya uhalisia wa kitu.

Lughawiya لغويات : Katika Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kitambaza ufizi l kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na kufuatiwa na kikwamizi kidaka tonge y chenye ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kiyeyushi midimo w chenye irabu fupi mbele juu i na kiyeyushi kaakaa gumu j chenye mkazo na kuishia kwa irabu ndefu chini a : na kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali ufizi n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*luyawija:t*/.

Kwa upande wa maana, neno hili katika Kiarabu lina maana ya “taaluma au sayansi ya lugha.” BAALBAKI (2003:922).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa kitambaza ufizi l na irabu fupi nyuma juu u na kufuatiwa na kikwamizi kaakaa laini y chenye ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia

kwa kiyeyushi midomo w na irabu fupi mbele juu i na kiyeyushi kaakaa gumu j na irabu fupi chini a . Kwenye Kiswahili neno hilo muundo wake wa msingi ni /*luɣawija*/

Neno hili limeingizwa Katika Kiswahili likiwa na maana ya taaluma inayoangalia kiuchambuzi kwenye lugha katika nyanja tafauti. BAKIZA (2010 :212).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti, katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, karibu na mwisho wa neno hili kuna konsonanti radidi/kariri /*yy*/, kwa hivyo konsonanti moja kati ya hizo imedondoshwa katika Kiswahili. Pili, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu chini /*a*:/ mwishoni mwa neno hilo kwenye muundo wa msingi wa neno hilo katika Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Hakuna mabadiliko kwa upande wa maana, ni maana ileile ya Kiarabu.

Mahafali محفل: Katika Kiarabu neno hili, lianaanzia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kikwamizi koromeo h kisicho cha ghuna na kufuatiwa na kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i na kumalizia kwa kitambaza meno ufizi l kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*mahfil*/.

Katika muktadha wa maana, neno hili kwenye Kiarabu linamaanisha “baraza, mkusanyiko wa watu.” BAALBAKI (2003: 992).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kikwanizi meno ufizi f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kitambaza ufizi l kisicho cha ghuna chenye irabu fupi juu mbele i . Kwenye Kiswahili neno hili muundo wake wa msingi ni /mahafali/.

Kwenye Kiswahili neno hili; lina maana ya “mkusanyiko mkubwa wa watu kwa ajili ya sherehe fulani; sherehe ya kutunuku vyeti, stashahada au shahada.” BAKIZA (2010 : 216).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu kuna mkusanyiko wa konsonanti. Katika mkusanyiko huo mna sauti [h] ambayo haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imebadilika na kuwa /h/. Pili, kuna ubadili irabu, neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu, mwisho kuna irabu fupi nyuma juu /u/ ambayo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Tatu, kuna upanuzi semantiki, neno hili limepata maana mpya ambayo imekuwa jumuishi kuliko maana ya mwanzo kwenye Kiarabu. Maana hii mpya katika Kiswahili ni pana na imezidi upeo kimaana. Upeo huo ni ule utunukiaji tunuku za kitaaluma.

Mdahalo مدخل : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi d chenye ghuna na kumalizikia kwa kikwamizi kaakaa laini x kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini na kitambaza ufizi l kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali ufizi n . Hii

un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*madxal*/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hili lina maana ya “uingiaji; mahali pa kuingilia; mwenendo mzuri.” El-Jar (1973: 1056), Ibnu Mandhour (-- : 239 Juz.xi).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa nazali midom *m* yenye ghuna na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabi fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi kati na kati *o*. Neno hili katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*mdahal*o/.

Katika Kiswahili lina maana ya “majadiliano baina ya watu wengi juu ya jambo moja maalumu; mjadala, kongamano.” KKS (2004:236), BAKIZA (2010:238)

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi irabu; katika muundo wa asili wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo baada ya konsonanti kuna irabu fupi chini /*a*/. Katika Kiswahili irabu hiyo imedondoshwa. Pili, kuna ubadili konsonanti. Kwenye muundo wa msingi wa neno hili kuna mkusanyiko wa konsonanti. Katika mkusanyiko huo kuna sauti [x] ambayo haimo katika Kiswahili, kwa hivyo sauti konsonanti hiyo imepata badili /*h*/. Tatu, kuna badiliko la upanuzi semantiki, neno hili limepata maana mpya ambayo imekuwa jumuishi kuliko maana ya mwanzo katika Kiarabu. Maana hii mpya katika Kiswahili ni pana na imezidi upeo kimaana. Upeo huo ni ile dhana ya mjadala baina ya watu wengi juu ya jambo.

Mhariri محرر : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti nazali m midomo yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na kufuatiwa na kikwamizi koromeo h kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kimadende ufizi r chenye mkazo na ghuna na kifuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kumalizikia kimadende r na irabu fupi nyuma u na zazli n yenye ghuna. Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /muħariru/.

Kwa upande wa maana, neno hili kwenye Kiarabu lina maana ya “mpigania uhuru, mkombozi; mwandishi, katibu, karani.” BAALBAKI (2003:988).

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kwa nazali m midomo yenye ghuna na kufuatiwa na kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kimadende ufizi r hicho hicho chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i . Kwenye lugha ya Kiswahili neno hili muundo wake wa msingi ni /mhariri/.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “mpitiaji wa maandishi kwa njia ya kuyasoma, kuyasahihisha, kuyaweka sawa vile yanavyotakiwa yajitokeze au kuyasanifisha na kuwa katika sura ya kitabu, jarida n.k.; mtu mwenye dhamana ya maandishi yote katika kitabu au gazeti.” BAKIZA (2010:246).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi irabu, katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo baada ya konsonanti kuna irabu fupi /u/, irabu hiyo imedondoshwa katika Kiswahili. Pili, kuna

udondoshi konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, katikati ya neno hili kuna konsonanti radidi/kariri /rr/, kwa hivyo konsonanti moja kati ya hizo imedondoshwa katika neno la Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu, neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu, mwisho kuna irabu fupi nyuma juu /u/ ambayo imefupika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/ katika Kiswahili. Nne, kuna ufinyu semantiki, neno hili limepata ufinyu wa maana kwenye Kiswahili. Ufinyu huo ni kule kujikita maana ya neno hili katika kusoma, kusahihisha, kuweka sawa na dhamana ya maandishi ya kitabu n.k.

Mkalimani **مكلم**: Katika Kiarabu, neno hili linaanzia kwa sauti nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kipasuo kidaka tonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye mkazo na irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*mukalim*/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hili lina maana ya “msemaji, mzungumzaji.” BAALBAKI (2003:1041).

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kwa sauti nazali midomo *m* na kufuatiwa na kipasuo kaakaa laini *k* chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*mkalimani*/.

Kwenye Kiswahili neno hili, lina maana ya “mfasiri wa lugha moja kwenda lugha nyengine papo kwa papo, mtapta.” KKS (2004:250), BAKIZA (2010:250).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi irabu, katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo baada ya konsonanti kuna irabu fupi /u/, irabu hiyo imedondoshwa katika Kiswahili. Pili, kuna udondoshi konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, karibu na mwisho wa neno hili kuna konsonanti radidi/kariri /ll/, kwa hivyo konsonanti moja kati ya hizo imedondoshwa katika neno la Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu; neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu mwisho kuna irabu fupi nyuma juu /u/ ambayo imebadilika na kuwa fupi chini /a/ na kufuatiwa na irabu fupi mbele juu /i/ baada ya nazali kwenye Kiswahili. Nne, kuna upanuzi semantiki, neno hili limepata maana mpya ambayo imekuwa jumuishi kuliko maana ya mwanzo katika Kiarabu. Maana hii mpya katika Kiswahili ni pana na imezidi upeo kimaana. Upeo huo ni ule ufasiri / utapta wa papo kwa papo kutoka lugha moja kwenda lugha nyengine.

Msamiati مساميات : Katika Kiarabu, neno hili linaanzia kwa sauti nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na nazali midomo *m̄* yenye ghuna na mkazo yenye irabu fupi chini *a*, na kumalizikia kwa kikwamizi kaakaa gumu *y* na irabu ndefu chini *a*: na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu

hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*musamaya:t*/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hili kimsingi linatokana na neno *ismu kwa hivyo* lina maana ya “majina ya watu, vitu na mambo mengineyo.” Ibnu Mandhour (-- 397 Juz. xiv),

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma *a* na kumalizikia kwa nazali midomo *m* yenye irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na irabu fupi kati *ə* na kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi juu mbele *i*. Kwenye Kiswahili neno hili muundo wake wa msingi ni /*msamiəti*/.

Kwenye Kiswahili linamaanisha “jumla ya maneno katika lugha.” KKS (2004:272).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi irabu, katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo baada ya konsonanti kuna irabu fupi /u/, irabu hiyo imedondoshwa katika Kiswahili. Pili, kuna udondoshi konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, katikati ya neno hili kuna konsonanti radidi/kariri /mm/, kwa hivyo konsonanti moja kati ya hizo imedondoshwa kwenye neno la Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu, katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu mwisho kuna irabu fupi nyuma juu /u/ ambayo imefupika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/ katika Kiswahili. Nne, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu chini /a:/ mwishoni mwa neno hilo. Katika muundo wa msingi wa neno hilo katika Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika

Kiswahili. Tano, kuna badiliko la semantiki imarishi, neno hili limepata maana jumuiishi chanya katika Kiswahili, hali hiyo ni mwendelezo mzuri katika maana ya neno.

Msanifu مصنف : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti nazali m midomo yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na kifuatiwa na kikwamizi ufizi kaaka gumu ς kisicho na ghuna chenye irabu fupi chini a na kujiwa na nazali ufizi n yenye ghuna na mkazo na irabu fupi mbele juu i , na kumalizikia kwa kikwamizi meno ya juu mdomo f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali ufizi n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */muṣānif/*.

Kwa muktadha wa maana, neno hili katika Kiarabu linamaanisha “mwandishi, mtunzi au mkusanyaji wa kazi zinazotaalaki na uandishi na utunzi.” El-Jar (1973:1124).

Katika Kiswahili linaanzia kwa nazali midomo m yenye ghuna na kufuatiwa na kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kufuatiwa na nazali ufizi n yenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kumalizikia kwa kikwamizi meno ya juu na mdomo wa chini f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u . Kwenye Kiswahili, neno hili muundo wake wa msingi ni */msanifu/*.

Neno hili lina maana ya “mtu mwenye mazowea au ujuzi wa kupanga au kuweka vitu katika hali nzuri k.v. kwenye majengo au maandishi.” Bakiza (2010: 270).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi irabu, katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo baada ya konsonanti kuna irabu fupi /u/, irabu hiyo imedondoshwa katika Kiswahili. Pili, kuna

udondoshi konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, katikati ya neno kuna konsonanti radidi/kariri /nn/, kwa hivyo konsonanti moja kati ya hizo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu, katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu, mwisho kuna irabu fupi nyuma juu /u/ ambayo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Nne, kuna upanuzi semantiki, neno hili limepata maana mpya ambayo imekuwa jumuishi kuliko maana ya mwanzo katika Kiarabu. Maana hii mpya katika Kiswahili ni pana na imezidi upeo kimaana. Upeo huo ni “ule uwezo wa kupanga na kuweka hali nzuri ya vitu na majengo.”

Nahau نحو: Katika Kiarabu, neno hili linaanzia kwa nazali meno ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *h* kisicho cha ghuna na kumalizikia kwa kiyeyushi midomo *w* chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*nahw*/.

Kwa upande wa maana, neno hili kwenye Kiarabu lina maana ya “kusudio, upande, njia, kiasi, mfano; taaluma inayoelezea kwayo taratibu na kaida ya lugha ya Waarabu.” El-Jar (1973:1196).

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia vilevile kwa nazali ufizi *n* na irabu fupi chini *a* kufuatiwa na kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hilo, katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*nahau*/.

Kwenye Kiswahili, lina maana ya “misemo mifupi mifupi yenye maana iliyojificha.”
BAKIZA (2010: 298).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu. Badiliko hilo linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu ambako kuna mkusanyiko wa konsonanti /ħw/ na irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno hilo. Irabu hiyo kwenye Kiswahili imebakia kama ilivyo nayo ni fupi nyuma juu /u/. Pili, kuna uongezaji sauti irabu /a/ ili kuondosha mkusanyiko wa konsonanti /ħw/ uliopo. Tatu, kuna semantiki hamishi, badiliko lililolifanya neno hili kupata maana mpya yenye kinyume na ile maana asili ya Kiarabu, na pia hakuna uhusiano wowote wa maana hiyo mpya. Badiliko hilo limejikita zaidi kwenye misemo mifupi.

Shahada شهادة : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi kaaka gumu ufizi] kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi kidakatonge *h* chenye ghuna na irabu ndefu chini *a:* na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*aha:dah* /.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu linamaanisha “utoaji wa maelezo ya mtu juu ya yale aliyoyaona au kuyasikia; maelezo yanayotolewa mbele ya mahakama, kiapo, cheti

kinachothibitisha kwamba mhusika aliye nacho kamaliza kiwango fulani cha elimu au mafunzo.” El-Jar (1973: 725)

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kikwamizi kaakaa gumu \int kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kufuatiwa na kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kipasuo ufizi d chenye ghuna na irabu fupi chini a . Kwenye Kiswahili neno hili muundo wake wa msingi ni $/\int ahada/$.

Kwa upande wa Kiswahili, neno hili lina maana ya “kiwango cha elimu ya Chuo Kikuu.” BAKIZA (2010:360),KKS (2004: 364).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu chini $/a:/$ katikati yake, katika muundo wa msingi wa neno hilo katika Kiarabu. Irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu, badiliko hilo linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu ambalo lina irabu fupi nyuma juu $/u/$ mwisho wa neno hilo, irabu hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi chini $/a/$. Tatu, kuna semantiki imarishi, neno hili limepata maana jumuishi chanya katika Kiswahili, hali hiyo ni mwendelezo mzuri katika maana hiyo ya neno.

Stashahada *استشهاد* : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo koo $?$ chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i , na kufuatiwa na kikwamizi ufizi kisicho cha ghuna s na kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kikwamizi kaakaa gumu ufizi \int kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kikwamizi koo h chenye irabu ndefu chini a : na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi d chenye

ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /[?]isti]ha:d/.

Katika Kiarabu neno hili lina maana ya “kuomba kutoa ushadidi; kutegemea jambo kwa ushahidi.” El-Jar (1973 :82).

Kwenye Kiswahili linaanzia kwa kikwamizi ufizi kisicho cha ghuna *s* na kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi kaakaa gumu ufizi] kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kikwamizi koromeo *h* chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni /sta]ahada/.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “kiwango cha elimu baina ya sekondari na elimu ya shahada ya kwanza, diploma.” BAKIZA (2010 : 376).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti. Kwenye muundo wa msingi wa neno hili mwanzo kabisa kuna konsonanti [?] ambayo ni sauti kipasuo koo. Sauti hiyo [[?]] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imedondoshwa pamoja na irabu yake kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu, irabu ya pili kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu ambayo ni irabu fupi mbele juu /i/, kwenye Kiswahili imekuwa irabu fupi chini /a/. Tatu, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu chini /a:/ katikati ya neno hilo, katika muundo wa msingi wa neno hilo kwenye Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Nne, kuna uongezaji sauti irabu /a/ ili

kuondosha mkusanyiko wa konsonanti uliopo mwishoni mwa muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu. Tano, kuna ubadili irabu, badiliko hilo linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu ambalo lina irabu fupi chini juu /u/ mwisho wa neno hilo, irabu hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi chini /a/. Sita, kuna semantiki imarishi; neno hili limepata maana jumuishi chanya katika Kiswahili, hali hiyo ni mwendelezo mzuri katika maana hiyo ya neno.

Sanaa صناعة : Neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa kikwamizi ufizi kaakaa gumu ʃ mtandazo kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i na kufuatiwa na nazali meno ufizi n yenye irabu ndefu chini a : na kumalizikia kwa kikwamizi koromeo ʕ chenye ghuna na irabu fupi chini a na kuishia kwa kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/\text{ʃina}:\text{ʕah}/$.

Maana ya neno hili kwa upande wa Kiarabu ni “kazi; ujuzi au amali yoyote anayoifanya mtu akawa mahiri wa amali hiyo na ikawa ndiyo kazi yake, uwezo wa kutengeneza vitu kutokana na mali ghafi; kazi au amali ya mtu aifanyayo Fairozabadi (1302 H : 51).”

Kwa upande wa Kiswahili neno hili linaanzia vilevile kwa kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kufuatiwa na nazali ufizi n yenye ghuna na irabu ndefu chini a : Kwenye Kiswahili, neno hili muundo wake wa msingi ni $/sana:/$.

Kwenye Kiswahili neno hili maana yake ni “ufundi wa kuwasilisha hisia na mawazo ya binadamu kwa maandishi, michoro au uchongaji; zao linalotokana na ufundi huo.” KKS (1981:249).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Kwenye muundo wa msingi wa neno hili mwanzo kabisa kuna konsonanti ς ambayo ni sauti kikwamizi kaakaa gumu. Sauti hiyo [ς] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imebadilika na kuwa /s/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu baada ya konsonanti ya kwanza kuna irabu fupi mbele juu /i/ ambayo imebadilika na kuwa irabu fupi chini /a/ katika Kiswahili. Tatu, kuna semantiki hamishi; kwenye neno hili umetokea uhamishaji kamili wa maana inayopendeza katika Kiswahili, maana hiyo mpya ina uhusiano na maana iliyotangulia.

Sanifu **صنف**: Kwenye Kiarabu, neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi kaakaa gumu mtandazo ς isiyo ya ghuna yenye irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na nazali meno ufizi *n* yenye ghuna na kufuatia kikwamizi meno *f* chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni / ς inf/.

Kwa upande wa maana kwenye Kiarabu, neno hili linamaanisha “aina, sifa, kundi.” BAALBAKI (2003:702).

Kwa upande wa Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kikwamizi meno ya juu mdomo *f* chenye irabu fupi nyuma juu *u*. Kwenye Kiswahili neno hili muundo wake wa msingi ni /sanifu/.

Katika Kiswahili neno hilo lina maana ya “ya kupendeza; yenye kufuata taratibu au kanuni zilizokubaliwa.” BAKIZA (2010: 355).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Kwenye muundo wa msingi wa neno hili mwanzo kabisa kuna konsonanti ς ambayo ni sauti kikwamizi kaakaa gumu. Sauti hiyo [ʃ] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imebadilika na kuwa /s/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu, badiliko hili linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu. Baada ya konsonanti ya kwanza, kuna irabu fupi mbele juu /i/ ambayo imebadilika na kuwa irabu fupi nyuma juu /u/ katika Kiswahili. Tatu, kuna badiliko la semantiki hamishi, kwenye neno hili umetokea uhamishaji kamili wa maana inayopendeza katika Kiswahili, maana hiyo mpya ina uhusiano na maana iliyotangulia.

Taaluma **تعلم**: Neno hili katika Kiarabu, linaanzia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kikwamizi koromeo ʕ chenye ghuna na irabu fupi nyuma *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye mkazo na irabu fupi nyuma juu *u* na kuishia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*taʕallum*/.

Kwa upande wa maana, neno hili katika Kiarabu lina maana ya “ujifunzaji wa aina za maarifa mbalimbali pamoja na kupata ujuzi.” El-Jar (2010: 312).

Katika Kiswahili, linanzia vilevile kwa kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu chini *a*: na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi juu *u* na kumalizikia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*ta:luma*/.

Katika Kiswahili neno hili lina maana ya “ujuzi, elimu katika fani yoyote.” KKS (2004:388), BAKIZA (2010:381).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu, badiliko hilo linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu ambako kuna mkusanyiko wa konsonanti //l/ na irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno hilo, irabu hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi chini /a/. Pili, kuna udondoshi konsonanti. Kwenye muundo wa msingi wa neno hili mwanzo kabisa kuna konsonanti ^ʃ ambayo ni sauti kikwamizi koromeo. Sauti hiyo [ʃ] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imedondoshwa na kubakia irabu /a/ kwenye Kiswahili. Vilevile, kuna udondoshi konsonanti radidi //l/ japo kwamba konsonanti radidi hizo haziko mwisho wa neno, udondoshi huo ni kwa lengo la kuondosha mkusanyiko huo uliopo katika neno hili kwenye Kiswahili. Tatu, kuna upanuzi semantiki, neno hili limepata maana ambayo ni jumuishi kuliko muundo wa maana ya mwanzo kwenye Kiarabu, maana hiyo ya Kiswahili ni pana zaidi na yenye upeo.

Tasnifu تصنيف: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *ʃ* kisicho cha ghuna na kufuatiwa na nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu ndefu mbele juu *i*: na kikwamizi meno

mdomo f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/taʃni:f/$.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hili lina maana ya “kuweka kwa mpango na utaratibu maalumu, kupangilia; kitabu chenye fani mbali mbali.” El-Jar (1973:302).

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kipasuo ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kufuatiwa na kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna na kumalizikia kwa nazali ufizi n yenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u . Katika Kiswahili neno hili muundo wake wa msingi ni $/tasnifu/$.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “maandiko ya kitaaluma yanayochanganua mada maalumu aghalabu kwa ajili ya kupata shahada ya juu.” BAKIZA (2010:390).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, uwekaji wa konsonanti mkusanyiko, neno hili limekubali mchakato huu wa kuwekwa mkusanyiko wa konsonanti sn . Pili, kuna upanuzi semantiki, neno hili limepata maana mpya ambayo imekuwa jumuishii kuliko maana ya mwanzo ya Kiarabu. Maana hii mpya katika Kiswahili ni pana na imezidi upeo kimaana.

5.2.5 Maneco ya Kijamii

Jina la Kundi	Idadi ya maneno	Asilimia %
1. Kijamii	150	65.439

Jadweli Na.8 Maneno ya Kijamii.

Abyadhi أبيض: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo koo $ʔ$ chenye ghuna na irabu fupi nyuma chini a na kufuatiwa na kipasuo midomo b chenye ghuna na kiyeyushi kaakaa j chenye irabu fupi chini mbele a na kumalizikia kipasuo meno ufizi $ḍ$ chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/ʔabijaḍ/$.

Katika lugha hiyo ya Kiarabu, kwa upande wa maana neno hilo linamaanisha “-eupe; -tupu, -siyo na alama au kitu; -enye kung’ara; hana kosa, hana lawama.” BAALBAKI (2003:26-27).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa irabu fupi chini mbele a na kufuatiwa na kipasuo midomo b chenye ghuna na kiyeyushi kaakaa j chenye irabu fupi mbele chini a na kumalizikia kwa kikwamizi meno $ḍ$ chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i . Neno hili kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni $/abijaḍi/$.

Neno hilo linamaanisha “upande wa dhumna usio na vidoto.” BAKIZA (2010:1).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno hili kuna konsonanti $/ʔ/$ sauti hiyo $[ʔ]$ haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imebadilika na kuwa $/a/$ kwenye neno hilo la Kiswahili. Pili, kuna badiliko la uongezaji sauti. Kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna mkusanyiko wa konsonanti $/by/$. Ili kuepuka mkuasnyiko huo kwenye Kiswahili, imeongezwa sauti irabu fupi $/i/$. Tatu, kuna ubadili irabu, neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye

Kiarabu, mwisho kuna irabu fupi nyuma juu /u/ ambayo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/ mwisho kwenye neno hili la Kiswahili. Nne, kuna badiliko la ufinyu semantiki, neno hili limepata ufinyu wa maana kwenye Kiswahili. Ufinyu huo ni kule kujikita maana ya neno hili katika upande wa dhumna usio na vidoto.

Ada ^{عادة} : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo ^ʕ chenye ghuna na irabu ndefu chini *a*: na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na *nazali n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /^ʕ*a:dah*/.

Kwa upande wa maana, katika lugha hiyo ya Kiarabu linamaanisha “matumizi; ufanyaji wa jambo; mazoea.” El-Jar (1973:803).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hilo katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*ada*/.

Kwa upande wa maana katika lugha hiyo ya Kiswahili, linamaanisha “kawaida au tabia iliyozeleka katika kufanya jambo; malipo kwa ajili ya huduma k.v. ya tiba .” BAKIZA (2010:2).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno kuna konsonanti /^ʕ/, sauti hiyo [^ʕ] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo

imebadilika na kuwa /a/ kwenye neno hilo la Kiswahili. Pili, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu chini /a:/ mwanzoni katika muundo wa msingi wa neno hilo katika Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu, badiliko hili linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu, mwisho kuna irabu fupi nyuma juu /u/ ambayo imebadilika na kuwa irabu fupi chini /a/ mwisho kwenye neno hili la Kiswahili. Nne, kuna semantiki imarishi, neno hili limepata maana jumuishiki chanya katika Kiswahili, hali hiyo ni mwendelezo mzuri katika maana ya neno. Maana hiyo ina uhusiano na maana ya Kiarabu.

Adimu عدم : Neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa kikwamizi koromeo ^ʃ chenye ghuna na irabu fupi chini mbele *a* na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /^ʃ*adim*/.

Katika lugha hiyo ya Kiarabu, kwa upande wa maana linamaanisha “kukosekana, kuto kuwepo; kuwa na haja, hitajia.” BAALBAKI (2003:754).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa irabu fupi chini mbele *a* na kufuatiwa na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele *i* na kumalizikia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni /*adimu*/.

Katika Kiswahili, neno hilo linamaanisha “yenye kupatikana kwa uchache au shida.” BAKIZA (2010:2).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno kuna konsonanti /^ʕ/sauti hiyo [ʕ] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imebadilika na kuwa /a/ kwenye neno hilo la Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu, badiliko hili limetokea mwishoni mwa neno hili la Kiswahili kwa kuwa na irabu fupi nyuma juu /u/. Tatu, kuna badiliko la semantiki hamishi, maana ya neno hili katika Kiswahili ina uhusiano na ile maana ya Kiarabu lakini pia ina dhana ya kivumishi.

Afriti عفریت : Neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa kikwamizi koromeo ^ʕ chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kikwamizi meno *f* kisicho cha ghuna na kujiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu ndefu mbele juu *i*: na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na na zali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /^ʕ*ifri:t*/.

Kwa upande wa maana, katika Kiarabu linamaanisha “shetani, kibwengo; mjanja; habithi; jeki ya kuinulia gari.” BAALBAKI (2003:767).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi meno *f* kisicho cha ghuna na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* . Neno hilo katika Kiswahili, muundo wake wa msingi ni /*afriti* /.

Katika lugha hiyo linamaanisha “mtu mwenye vitendo viovu.” BAKIZA (2010:3).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno kuna konsonanti /ʕ/ sauti hiyo [ʕ] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imebadilika na kuwa /a/ kwenye neno hilo la Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu, badiliko hili linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu, mwisho kuna irabu fupi nyuma juu /u/ ambayo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Tatu, kuna ufinyu semantiki, neno hili limepata ufinyu katika maana kwenye Kiswahili. Ufinyu huo ni kule kujikita maana ya neno hili katika mtu mwenye sifa ya vitendo viovu tu.

Ahsante *أحسنت*: Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo koo ^ʔ chenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *ħ* kisicho cha ghuna na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa nazali *meno* ufizi *n* yenye ghuna na kuishia kwa kipasuo *meno* ufizi *t* kisicho cha ghuna na irabu fupi chini *a* au irabu fupi mbele juu *i*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /^ʔ*ahsant* /.

Neno hilo katika Kiarabu linamaanisha “umefanya vyema; vyema!”

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa irabu fupi chini *a*, na kikwamizi koromeo *h* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa nazali ufizi *n* na kuishia kwa kipasuo ufizi *t* chenye irabu fupi mbele kati *ε*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*ahsante*/, linamaanisha “kuonesha ridhaa na

furaha kwa aliyetendewa jambo; kitu apewacho mtu kama ni shukurani.” BAKIZA (2010:4).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kipasuo koo /ʔ/. Sauti hiyo imedondoshwa katika Kiswahili. Pili, kuna uimarishi irabu; kwenye muundo wa msingi neno hili lina irabu fupi chini /a/. Kutokana na mchakato wa kifonolojia, irabu hiyo imeinuliwa na kuwa ya kati juu /ε/. Tatu kuna uongezaji sauti irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili mwanzoni kuna konsonanti mkusanyiko /ħs/. Irabu fupi chini /a/ imeongezwa ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Nne, kuna upanuzi semantiki; neno limepata maana jumuishii kuliko ile maana iliyo kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana ya ridhaa na furaha.

Ajali *أجل*: Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kipasuo koo ^ʔ chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi kaakaa gumu *ǧ* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a*, na kumalizikia kwa kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /^ʔ*adǧal*/.

Katika lugha hiyo ya Kiarabu neno hili linamaanisha “muda,wakati,wakati maalumu uliopangwa; muda wa mwisho, mwisho wa muda; mwisho wa wakati wa mauti; kufikia muda wa deni; muda wa kitu au jambo” El-Mandhour(-- : 32).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa irabu fupi chini mbele *a* na kufuatiwa na kikwamizi kizuio kaakaa gumu *J* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini mbele *a* na kumalizikia kwa kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /aʃali/.

Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo lina maana ya “tukio la ghafla lisilotarajiwa ambalo aghalabu husababisha madhara au hatari; ahadi.” BAKIZA (2010:4).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwishakuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno kuna konsonanti /ʔ/ sauti hiyo [ʔ] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imebadilika na kuwa /a/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu, badiliko hili linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu, mwisho kuna irabu fupi nyuma juu /u/ ambayo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Tatu, kuna semantiki hamishi, kwenye neno hili umetokea uhamishaji kamili wa maana, maana ya neno hili katika Kiswahili haina uhusiano na ile ya Kiarabu lakini pia ina dhana ya tukio lisilotazamiwa mara nyingi linakuwa na hatari na madhara.

Ajemi عجمي : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo ^ʃ chenye ghuna na irabu fupi chini mbele *a* na kufuatiwa na kikwamizi kaakaa gumu *ʃ* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini mbele *a* na kufuatiwa na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi juu mbele *i* na kiyeyushi kaakaa *j* chenye irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hilo muundo wake wa msingi /^ʃadʒamij/.

Kwa upande wa maana katika lugha hiyo ya Kiarabu, neno hili linamaanisha “mtu asiyekuwa Mwarabu; Mwaajemi, Mfursi, Mfarsi.” BAALBAKI (2003:752).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi kizuiu kaakaa gumu *J* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele kati *ε* na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni /aʃemi/.

Katika lugha hiyo ya Kiswahili neno hilo lina maana ya “tunda la mti wa mchenza lenye umbo la mvingo katika jamii ya chungwa lenye ganda nene lenye utufyuu.”

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno kuna konsonanti /ʃ/ sauti hiyo [ʃ] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imebadilika na kuwa /a/ kwenye neno hilo la Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu, badiliko hili linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu, mwisho kuna irabu fupi nyuma juu /u/ ambayo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Tatu, kuna uimarishi irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, irabu ya pili kutoka mwanzo wa neno ni irabu ya chini kati /a/; kutokana na mchakato wa kifonolojia, imeongezewa nguvu na kuwa ya kati juu /ε/ kwenye Kiswahili. Nne, kuna semantiki hamishi, kwenye neno hili umetokea uhamishaji kamili wa maana. Maana ya neno hili inayopatikana kwenye Kiswahili, imepoteza mwelekeo kabisa wa ile maana ya mwanzo katika Kiarabu, kwani neno hilo lina dhana mpya ambayo imejikita katika tunda la jamii ya chungwa.

Ajizi عجز : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo ^ʕ chenye ghuna na irabu fupi chini mbele *a* na kufuatiwa na kikwamizi kaakaa gumu *dʒ* kisicho cha ghuna na kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /^ʕ*adʒz*/.

Kwa upande wa maana katika lugha hiyo ya Kiarabu, linamaanisha “udhaifu, ulegevu, ugoigoi, kutokuwa na uwezo; upungufu, kutokuwa na kitu, kuhitaji.” BAALBAKI (2003:751).

Neno hilo katika Kiswahili linaanzia kwa irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi kizuo kaakaa gumu *J* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni /*aJizi*/

Katika Kiswahili, neno hili linamaanisha “usiri katika kufanya jambo.” BAKIZA (2010:5).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno kuna konsonanti /^ʕ/ sauti hiyo [ʕ] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imebadilika na kuwa /a/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna uongezaji sauti. Kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna mkusanyiko wa konsonti /*dʒz*/ . Ili kuepuka mkuasanyiko huo kwenye Kiswahili, imeongezwa sauti irabu fupi /i/. Tatu, kuna ubadili irabu, badiliko hili linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu, mwisho kuna irabu fupi nyuma juu /u/ ambayo imebadilika na kuwa irabu fupi

mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Nne kuna ufinyu semantiki, neno hili limepata ufinyu katika maana kwenye Kiswahili. Ufinyu huo ni kule kujikita maana ya neno hili katika uzohali wa kufanya jambo.

Alaka **علاقة** : Neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa kikwamizi koromeo ^ʕ chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu chini *a*: na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge *q* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo meno *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na *nazali n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /^ʕ*ala:qah*/.

Katika lugha hiyo ya Kiarabu, neno hilo linamaanisha “uhusiano, muunganiko, mawasiliano; uvumilivu.” BAALBAKI (2003:773-74).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa irabu fupi chini mbele *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. Neno hilo katika lugha hiyo ya Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*alaka*/.

Kwenye Kiswahili, neno hilo linamaanisha “mahusiano mema baina ya watu au mambo; matatizo yanayompata mtu kutokana na kitendo alichofanya au alichofanyiwa.” BAKIZA (2010 :6).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno

kuna konsonanti /ʃ/sauti hiyo [ʃ] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imebadilika na kuwa /a/ kwenye neno hilo la Kiswahili. Pili, kuna badiliko la ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu chini /a:/ katikati ya neno hilo katika muundo wa msingi kwenye Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa kwenye Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu, badiliko hili linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu, mwisho kuna irabu fupi nyuma juu /u/ ambayo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Nne, kuna upanuzi semantiki, neno hili limepata maana mpya ambayo imekuwa jumuishi kuliko maana ya mwanzo ya Kiarabu. Maana hii mpya katika Kiswahili ni pana na imezidi upeo kimaana. Maana ya pili ni kama kinyume cha ile maana ya kwanza huo ndio upana wa maana katika Kiswahili.

Alasiri العصر: Katika Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kipasuo koo ^ʔ chenye ghuna na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kicho cha ghuna na kujiwa na kikwamizi koromeo ^ʃ chenye ghuna na irabu fupi chini mbele *a* na kumalizikia kwa kikwamizi mtanadazo ufizi *ʃ* kisicho cha ghuna na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni ^ʔ*alʃaʃr/*.

Kwa upande wa maana, kwenye lugha hiyo ya Kiarabu neno hilo linamaanisha “kubinya, kuminya, kushindilia, kusindika; wakati wa baada ya jua kutenguka; zama, muda.” BAALBAKI (2003:764).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia kwa

kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingini /*alasiri*/.

Katika lugha hiyo ya Kiswahili neno hilo linamaanisha “sala ya faradhi inayosaliwa na Waislamu baina ya saa tisa na saa kumi na moja jioni; wakati baina ya saa tisa mchana na kabla ya kuanza kutua jua.” BAKIZA (2010:6).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno kuna konsonanti /ʔ/ sauti hiyo [ʔ] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imebadilika na kuwa /a/ kwenye neno hilo la Kiswahili. Pili, kuna ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, katikati ya neno kuna konsonanti / ʕ/ sauti hiyo [ʕ] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imebadilika na kuwa /a/ kwenye neno hilo la Kiswahili. Tatu kuna uongezaji sauti. Kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna mkusanyiko wa konsonti /*sr*/ . Ili kuepuka mkusanyiko huo kwenye Kiswahili, imeongezwa sauti irabu fupi /i/. Nne, kuna ubadili irabu, badiliko hili linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu, mwisho kuna irabu fupi nyuma juu /u/ ambayo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Tano, kuna semantiki hamishi, kwenye neno hili umetokea uhamishaji kamili wa maana. Maana ya neno hili iliyopatikana kwenye Kiswahili, ina uhusiano na ile maana ya mwanzo katika Kiarabu, kwani neno hilo lina dhana mpya ambayo imejikita katika sala inayosaliwa baina ya saa tisa na saa kumi na moja jioni; wakati baina ya saa tisa mchana na kabla ya kuanza kutua jua.

Alhasili *الحاصل*: Neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa kipasuo koo ^ʔ chenye ghuna na iarbu fupi chini nyuma *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna na kujiwa na kikwamizi koromeo *ħ* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu chini nyuma *a*: na kufuatiwa na kikwamizi ufizi mtandazo *ʃ* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kitambaza ufizi *l* chenye irabu fupi nyuma juu *u*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */ʔalħa:ʃiu/*.

Kwenye Kiarabu, neno hili linamaanisha “kwa ufupi, kwa muhtasari.” BAALBAKI (2003:445).

Katika Kiswahili neno hilo, linaanzia kwa irabu fupi chini *a* na kitambaza ulimi *l* kisicho cha ghuna na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini nyuma *a* na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. Katika Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi */alhasili/*

Katika Kiswahili, neno hilo lina maana inayoonesha “kuridhishwa na jambo; kwa kweli, kwa jumla.” BAKIZA (2010:6).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno kuna konsonanti */ʔ/* sauti hiyo *[ʔ]* haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imebadilika na kuwa */a/* kwenye neno hilo la Kiswahili. Pili, uwekaji wa konsonanti mkusanyiko, neno hili limekubali mchakato huu wa kuwekewa mkusanyiko wa konsonanti */lh/* mwanzoni mwa neno hili kwenye Kiswahili. Tatu, kuna badiliko la

semantiki hamishi, kwenye neno hili umetokea uhamishaji kamili wa maana. Maana ya neno hili inayopatikana kwenye Kiswahili, ina uhusiano na ile maana ya mwanzo katika Kiarabu, kwani neno hilo lina dhana mpya ambayo imejikita katika kuridhishwa, ukweli na hali ya ujumla.

Arusi عرس : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo ^s chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*, au fupi mbele juu *i*, na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /^surs /, /^sirs /.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hili lina maana ya “arusi/harusi au sherehe ya arusi kwa matamshi ya kwanza, na kwa matamshi ya pili lina maana ya harusu mwanamke au mwanamume.” Ejar (1973:823).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /arusi/.

Kwa upande wa Kiswahili lina maana hiyohiyo na pia linamaanisha “mhusika anayeolewa au anayeo, yaani biharusi na bwana harusu; pia maharusu; sherehe ya ndoa halali.” BAKIZA (2010:112), KKS (1981:76).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno kuna konsonantiki /ʕ/, sauti hiyo [ʕ] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imebadilika na kuwa /a/ kwenye neno hilo la Kiswahili. Pili, kuna uongezaji sauti, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu kuna mkusanyiko wa konsonti /rs/. Ili kuepuka mkuasnyiko huo kwenye Kiswahili, imeongezwa sauti irabu fupi /u/. Tatu, kuna ubadili irabu, neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu mwisho kuna irabu fupi nyuma juu /u/ ambayo imepata badili nayo ni irabu fupi mbele juu /i/ mwisho kwenye neno hili la Kiswahili.

Alimradi المراد: Neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa kipasup koo ^ʔ chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna na kujiwa na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu ndefu mbele chini *a*: na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /^ʔalmura:d/.

Kwenye Kiarabu neno hilo linamaanisha “lile jambo au kitu kitakiwacho, jambo litarajiwalo, -enye kukusudiwa.” BAALBAKI (2003:1013).

Katika Kiswahili neno hilo, linaanzia kwa irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na nazali midomo *m* yenye ghuna na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye irabu fupi *a* chini mbele na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fipi mbele juu *i*. Katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni /alimradi/.

Kwa upande wa maana, katika Kiswahili neno hilo linamaanisha “bora tu, bora ya kwamba.” BAKIZA (2010:7).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno kuna konsonanti /ʔ/ sauti hiyo [ʔ] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imebadilika na kuwa /a/ kwenye neno hilo la Kiswahili. Pili, kuna uongezaji sauti. Kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna mkusanyiko wa konsonanti /lm/. Ili kuepuka mkusanyiko huo kwenye Kiswahili, imeongezwa sauti irabu fupi /i/. Tatu, kuna uwekaji konsonanti mkusanyiko, neno hili limekubali mchakato huu wa kuwekwa mkusanyiko wa konsonanti /mr/ katikati ya neno hili kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu, badiliko hili linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu, mwisho kuna irabu fupi nyuma juu /u/ ambayo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Nne, kuna semantiki hamishi, kwenye neno hili umetokea uhamishaji kamili wa maana. Maana ya neno hili inayopatikana kwenye Kiswahili, ni kinyume na haina uhusiano na maana ya mwanzo katika Kiarabu.

Ami **عم** : Kwenye Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo ^ʕ chenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na nazali midomo *m* yenye ghuna na mkazo na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*ʕam* /.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hilo lina maana ya “ndugu wa kiume au kaka wa baba.”

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa irabu fupi chini *a* na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /ami/.

Kwenye Kiswahili, lina maana ya “ndugu wa kiume wa baba.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika neno hili kuna badiliko la sauti kikwamizi koromeo [ʔ] chenye ghuna, kwenye muundo wa msingi mwanzo wa neno kwenye Kiarabu; sauti hiyo imebadilika na kuwa [a]. Pili, kuna udondoshi konsonanti mwisho wa neno. Neno hili katika muundo wake wa msingi kuna mkusanyiko wa konsonanti radidi/kariri /mm/, moja kati ya hizi imedondoshwa. Tatu, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno hili. Irabu hiyo imebadilika na kuwa ya mbele juu /i/. Kwa upande wa maana hakuna badiliko lolote.

Amiri أمير: Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo koo ² chenye ghuna na irabu fupi *a* mbele chini na kufuatiwa na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu ndefu *i*: mbele juu na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /²ami:r/.

Kwa upande wa maana, neno hili katika Kiarabu linamaanisha “mwana wa mfalme; kiongozi, kamanda, bwanamkubwa.”

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa irabu fupi chini mbele *a* na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*amiri*/.

Katika Kiswahili neno hili linamaanisha “kiongozi wa kikundi au jumuiya ya watu.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno kuna konsonanti /ʔ/ sauti hiyo [ʔ] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imepata badili /a/ kwenye neno hilo la Kiswahili. Pili, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu mbele juu /i:/ katikati ya neno hilo katika muundo wa msingi wa neno hilo kwenye Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu, badiliko hili linatokana na neno hili katika muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu, mwisho kuna irabu fupi nyuma juu /u/ ambayo imepata badili nayo ni irabu fupi mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Nne, kuna badiliko la ufinyu semantiki, neno hili limepata ufinyu katika maana kwenye Kiswahili. Ufinyu huo ni kule kujikita maana ya neno hili katika uongozi kweye kikundi au jumuiya tu.

Anasa أنس : Neno hili kwenye Kiarabu linaanzia kwa kipasuo koo ʔ chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na nazali meno ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /ʔ*anisa*/, na linamaanisha “kufurahisha na kutuliza, kuvutia katika mazungumzo, hasa mwanamke.”

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hili muundo wake wa kifonetiki ni /*anasa*/, na lina maana ya “mambo au hali ya starehe na raha nyingi, kitu chenye thamani kubwa ambacho si muhimu.”

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili mwanzoni lina sauti konsonanti kipasuo koo /ʔ/, sauti hiyo imedondoshwa katika Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu katikati lina irabu fupi mbele juu /i/. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi chini /a/. Tatu, kuna upanuzi semantiki; neno hilo limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyoko kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana ya raha na starehe na thamani kubwa kwa jambo lisilo na umuhimu.

Ardhilhali عرض الحال : Kwenye Kiarabu neno hili linajitokeza katika maneno mawili, neno la kwanza katika maneno mawili hayo linaanzia kwa kikwamizi koromeo ^ʕ na irabu fupi *a* chini mbele na kufuatiwa na kimadende *r* chenye ghuna na kipasuo meno ufizi *ḍ* chenye ghuna na irabu fupi *u* nyuma juu. Neno la pili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *ḥ* kisicho cha ghuna na irabu ndefu *a*: mbele chini na kumalizikia kwa kitambaza ufizi *l* na irabu *i*, kwa pamoja katika Kiarabu maneno haya muundo wake wa msingi kama neno moja ni /^ʕ*ardul ḥa:l*/. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa

hivyo neno hilo katika Kiarabu liko katika sura kama hiyo kwenye muundo wake wa msingi.

Kwa upande wa maana neno hilo linamaanisha “kumbukumbu, ombi.”

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kwa irabu fupi *a* chini na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* na kikwamizi meno *ð* chenye ghuna na irabu fupi *i* mbele juu na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna na kumalizikia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi *a* mbele chini na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi *i* juu mbele. Neno hilo katika lugha hiyo ya Kiswahili muundo wake wa msingi ni /ardhilhali /.

Kwa upande wa maana, neno hilo katika lugha hiyo ya Kiswahili, “linamaanisha barua rasmi ya ombi.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno kuna konsonanti /ʕ/ sauti hiyo [ʕ] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imebadilika na kuwa /a/ kwenye neno hilo la Kiswahili. Pili, kuna uwekaji wa konsonanti mkusanyiko neno hili limekubali mchakato huu wa kuwekwa mkusanyiko wa konsonanti /rð/ na /lh/ katikati ya neno hili kwenye Kiswahili. Tatu, kuna badiliko la ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu mbele juu /i:/ mwisho wa neno hilo katika muundo wa msingi kwenye Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Nne, kuna semantiki hamishi, kwenye neno hili umetokea uhamishaji kamili wa maana. Maana ya neno hili iliyopatikana kwenye Kiswahili, ina tafauti ndogo lakini ina uhusiano na maana ya mwanzo katika Kiarabu.

Ashaakum حشى كم : Kwenye Kiarabu, haya ni maneno mawili. Neno la kwanza linaanzia kwa kikwamizi koromeo h kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kufuatiwa na kikwamizi kaakaa gumu f kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu mbele chini a ; neno hilo kwenye lugha hiyo ya Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/hafa:/$ neno hilo lina maana ya “sivyo hivyo”. Neno la pili nalo linaanzia kwa kipasuo kidakatonge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na kufuatiwa na nazali midomo m yenye ghuna. Katika lugha hiyo ya Kiarabu neno hilo muundo wake wa msingi ni $/kum/$; kwa kawaida neno hili haliji peke yake kama neno linalojitegemea bali linakuwa na neno jingine kabla yake. Kwa upande wa kimaana lina dhana ya kiwakilishi amabatano cha nafsi ya pili wingi.

Hivyo limekuja katika neno moja na muundo wake wa msingi ni $/hafa:kum/$.

Neno hili linamaanisha “sivyo hivyo jamani.”

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa irabu fupi mbele chini a na kufuatiwa na kikwamizi kaakaa gumu f kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu mbele chini a : na kumalizikia kwa kipasuo kidakatonge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na kuishia nazali midomo m yenye ghuna. Kwenye Kiswahili neno hilo muundo wake wa msingi ni $/asha:kum/$.

Kwa upande wa maana, neno hili katika Kiswahili linamaanisha “tamko la kuomba radhi kabla ya kusema neno la karaha.”

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno

kuna konsonanti /h/ sauti hiyo [h] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imepata badili ya sauti irabu /a/ kwenye neno hilo la Kiswahili. Pili, kuna upanuzi semantiki, neno hili limepata maana mpya ambayo imekuwa jumuishiki kuliko maana ya mwanzo ya Kiarabu. Maana hii mpya katika Kiswahili ni pana na imezidi upeo kimaana ambao ni ashirio la kuomba msamaha katika kutaja jambo la karaha au lisilopendeza.

Asilani أصلا: Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kipasuo koo ² kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chi *a*, na kufuatiwa na kikwamizi ufizi mtandazo ξ kisicho cha ghuna na kumalizikia kwa kitambaza meno ufizi *l* na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa nazali meno ufizi *n*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /²ašlan/.

Kwenye Kiarabu neno hili lina maana ya “msingi, chanzo.”

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*, na kumalizikia kwa kitambaza ufizi *l* chenye irabu fupi chini *a* na nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hili kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni /asilani/.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “kusisitiza katika kupinga au kukataa jambo; katu!, kamwe!, kabisa!, sini.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu. Neno hili mwanzo lina sauti konsonanti /²/; sauti hiyo imedondoshwa kwa kuwa haimo katika Kiswahili. Pili, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu neno hili lina sauti konsonanti kikwamizi ufizi /š/. Sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa

kikwamizi ufizi /s/. Tatu, kuna uongezaji sauti irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katikati kuna konsonanti mkusanyiko /sl/. Irabu fupi mbele juu /i/ imeongezwa ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Pia mwisho wa neno imeongezwa irabu fupi mbele juu /i/. Nne, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia nayo imejikita zaidi kwenye msisitizo wa kupinga.

Aula *أولى*: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo koromeo ^ʔ chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kiyeyushi midomo *w* na kumalizikia kwa kitambaza *l* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu chini *a:*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /^ʔau:la:/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hili linamaanisha “bora zaidi, yenye kufaa zaidi, ya kipaumbele.”

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kwa irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na irabu fupi nyuma juu *u* na kuishia kwa kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingii ni /*aula*/

Katika Kiswahili neno hili lina maana ya “kazi au mipango inayopewa umuhimu wa kwanza kushughulikiwa; kipaumbele.”

Mabadiliko ya neno hili baada kwisha kuingia katika Kiswahili, mosi, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu; neno hili lina sauti konsonanti /^ʔ/ ambayo imepata mbadala wa irabu /a/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu nyuma juu /u:/ na ndefu chini /a:/ kwenye muundo wake wa

msingi. Irabu hizo zimefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Tatu, kuna ufinyu semantiki, ufinyu huo wa maana katika Kiswahili; umejikita katika ile mipango inayopewa umuhimu wa kwanza katika kushughulikiwa.

Badani **بَدَانِي**: Kwenye Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi *a* mbele chini na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi *a* mbele chini na kumalizikia kwa nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi *u* juu nyuma na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */badan /*.

Katika Kiarabu neno hilo linamaanisha “mwili; mnyama k.v. mbuzi n.k; kiwiliwili.”

Katika Kiswahili linaanzia kwa kipasuo midomo chenye ghuna na irabu fupi *a* mbele chini na kufuatiwa na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi *a* mbele chini na kumalizikia kwa nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi *i* mbele juu. Neno hilo muundo wake wa msingi ni */badani /*.

Kwa upande wa maana, katika Kiswahili linamaanisha “sehemu ya nguo ambayo si mikono au ukosi hasa ya shati, kanzu, juba, koti au joho; sehemu ya kifua na mgongo.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu kuna irabu fupi nyuma */u/* mwisho wa neno hili, kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu */i/*. Pili, Semantiki hamishi, kwenye neno hili umetokea uhamishaji kamili wa maana. Maana

ya neno hili inayopatikana kwenye Kiswahili, ni kinyume kabisa na maana ya Kiarabu iliyotangulia na pia imepoteza mwelekeo wa maana hiyo tangulizi na haina uhusiano na maana ya mwanzo katika Kiarabu.

Batara بطار: Kwenye Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi *a* mbele chini na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi *t* mtandazo kisicho cha ghuna chenye irabu fupi *a* mbele chini na kuishia kwa kimadende ufizi *r* na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n* yenye ghuna. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*baṭar* /.

Kwa upande wa maana katika Kiarabu, neno hilio linamaanisha “kutokuwa na shukurani, kutotosheka, kutozingatia huruma, kukosa huruma (rahma) moyoni; majivuno.”

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi *a* mbele chini na kufuatiwa na kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi *a* mbele chini na kuishia kwa kimadende ufizi *r* na irabu fupi *a* mbele chini. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*batara*/.

Neno hilo linamaanisha “hali ya mtu kufanya jeuri kutokana na ufanisi alioupata, kiburi.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno kuna konsonanti /*t̤*/ sauti hiyo [*t̤*] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti /*t̤*/ imepata konsonanti badili /*t*/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu kuna irabu fupi nyuma juu /*u*/ mwisho wa neno

hili, kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi chini /a/. Tatu, semantiki hamishi, kwenye neno hili umetokea uhamishaji kamili wa maana. Maana ya neno hili inayopatikana kwenye Kiswahili, ni tafauti kidogo na maana ya Kiarabu iliyotangulia lakini ina mwelekeo na uhusiano wa maana hiyo tangulizi. Kimaana neno limejikita kwenye jeuri ya kipato au ufanisi wa jambo tu.

Batini *باطن*: Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi *a* mbele chini na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi mtandazo *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kuishia kwa nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*batin*/.

Kwa upande wa maana kwenye Kiarabu, neno hilo linamaanisha “kutia laini nguo; jaza, tia kitu ndani ya kitu.”

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hili katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*batini*/.

Kwa upande wa maana, neno hilo linamaanisha “kitendo cha kutia kitambaa chengine ndani ya nguo inayoshonwa.”

Mabadiliko makubwa katika neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, katikati ya neno kuna konsonanti /*t*/; sauti hiyo [*t*] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo

konsonanti /t/ imepata konsonanti badili /t/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna ufinyu semantiki; neno hili limepata ufinyu katika maana kwenye Kiswahili. Ufinyu huo ni kule kujikita maana ya neno hili katika kutia kitambaa chengine kwa ndani kwenye nguo inayoshonwa tu.

Bazazi بَزَازِ: Kwenye Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na mkazo na irabu ndefu mbele chini *a*: na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /baʒa:z/.

Kwa upande wa maana katika lugha hiyo ya Kiarabu neno hilo linamanisha “muuza vitambaa; mfanyabiashara wa bidhaa kavu; mshughulikiaji katika utengenzaji wa nyuzi za kutengenezea vitambaa.”

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kipasuo midomo *b* na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kikwamizi *z* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni /bazazi/.

Kwa upande wa maana katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo linamaanisha “mtu anayetumia ujanja wa maneno au vitendo ili kupata kitu kutoka kwa mwengine, tapeli.”

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu refu chini /a:/ katikati katika muundo wa msingi

kwenye Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Pili, kuna udondoshi konsonanti, katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, katikati ya neno hili kuna konsonanti radidi/kariri /zz/, kwa hivyo konsonanti moja kati ya hizo imedondoshwa katika Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno hili, kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Nne, kuna badiliko la semantiki punguzi; neno hili limepata maana jumuiiko hasi kwa maana ya kuwa neno hili halipendezi.

Bado بادو: Neno hili kwenye Kiarabu linaanzia kwa sauti kipasuo midomo *b* yenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi koromeo ^ʿ chenye ghuna na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /ba^ʿd/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hilo linabeba dhana ya kielezi; kwanza katika kumaanisha “hali ya baadaye kintiririko pale neno hili linapoegemezwa na jambo, pili kielezi cha wakati na mahali, pia linamaanisha “pamoja na, hivi sasa.”

Katika Kiswahili neno hilo, linanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi kati nyuma *o*. katika lugha hiyo ya Kiswahili muundo wake wa msingi ni /bado/.

Kwa upande wa maana, linabeba dhana ya “hali ya kutofika muda na linamaanisha kabla ya wakati uliotajwa.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, udondoshi konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, katikati ya neno kuna konsonanti /s/ sauti hiyo [ʃ] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo sauti konsonanti hiyo kwenye neno hili imedondoshwa kwenye Kiswahili. Pili, kuna Ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno hili, kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi kati nyuma /ɔ/. Tatu, kuna ufinyu semantiki, neno hili limepata ufinyu wa maana kwenye Kiswahili. ufinyu huo ni kule kujikita katika hali ya kutofika muda na kumaanisha kabla ya wakati uliotajwa.

Baki بقى: Kwenye Kiarabu, neno hilo linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kipasuo kaakaa laini *q* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kuishia kwa kiyeyushi kaa kaa gumu *j* na irabu fupi mbele chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /baqij/.

Katika Kiarabu, Kwa upande wa maana, linamaanisha “kudumu kwa muda mrefu, kuto malizika au kutokwisha; kuthibiti.”

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi kidaka tonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. Neno hili katika lugha hiyo ya Kiswahili muundo wake wa msingi ni /baki/.

Kwa upande wa maana kwenye Kiswahili, neno hilo linamaanisha “kitendo cha kuwapo pahali kwa kitambo fulani; kitendo cha kuendelea kuwapo pahali baada ya kumalizika

jambo; kitendo cha jambo kukosa kumalizika; sehemu ya hesabu iliyobakia baada ya kugawanya au kutolewa kiasi fulani.”

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, katikati ya neno kuna konsonanti /q/; sauti hiyo [q] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti /q/ imepata konsonanti badili /k/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna udondoshi konsonanti na irabu katika silabi ya mwisho /ya/ [ja]. Tatu, kuna upanuzi semantiki, neno hili limepata maana mpya ambayo imekuwa jumuishi kuliko maana ya mwanzo ya Kiarabu. Maana hii mpya katika Kiswahili ni pana na imezidi upeo kimaana.

Baka **بقة**: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kipasuo kaakaa laini *q* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi koromeo *ç* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /baqaç/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hilo linamaanisha “rangi yenye mng’aro mweupe na mweusi mwilini mwa wanyama k.v. mbwa na ndege.”

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi kidaka tonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini *a*. Kwenye Kiswahili neno hilo muundo wake wa msingi ni /baka/

Kwa upande wa maana, neno hili katika lugha hiyo ya Kiswahili lina maana ya “rangi iliyotafauti katika manyoya au ngozi ya mnyama, ndege au ukuta, paku, doto.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, katikati ya neno kuna konsonanti /q/; sauti hiyo [q] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti /q/ imepata konsonanti badili /k/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna udondoshi wa konsonanti /ʕ/ mwisho wa neno. Tatu, kuna upanuzi semantiki, neno hili limepata maana mpya ambayo imekuwa jumuishiki kuliko maana ya mwanzo ya Kiarabu. Maana hii mpya katika Kiswahili ni pana na imezidi upeo kimaana.

Bara *بَرَا*: Neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye mkazo na ghuna pamoja na irabu fupi chini mbele *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasilimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*bar*ʔ/.

Kwa upande wa maana, neno hilo katika Kiarabu lina maana ya “kusadikisha kwa kiapo; mwenye kusadikisha kwa yamini; mwenye kuwatii na kuwatendea wema wazazi wake; moja kati ya majina matukufu ya Mwenyezi Mungu; ardhi au nchi kavu.”

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a*. Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni /*bara*/.

Katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo linamaanisha “sehemu kubwa sana ya nchi kavu inayopakana na bahari kuu, kontinenti.”

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu kwenye muundo huo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, ambalo mwisho lina irabu fupi /u/ iliyopata irabu badili /a/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna udondoshi konsonanti, neno hili lina konsonanti radidi/kariri /rr/ mwisho kwenye muundo wa msingi, kwa hivyo moja kati ya hizo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ufinyu semantiki, neno hili kwenye Kiswahili limechukua maana finyu zaidi kuliko kwenye Kiarabu, ufinyu huo kimaana umejikita zaidi kwenye ardhi au nchi kavu.

Baradhuli *با رذيل* : Neno hilo asili yake katika Kiarabu ni maneno mawili, la kwanza ni *ba:* ambalo linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu ndefu mbele chini *a:*. Neno hilo lina maana ya “mwenye, baba wa”. Neno la pili ni *radijli* ambalo linaanzia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi meno *ḍ* chenye ghuna na irabu ndefu mbele juu *i:* na kuishia kwa kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *I* na nazali *n*, neno hilo lina maana ya “duni, ya hali ya chini.” Katika Kiarabu maneno hayo yanajitokeza kwenye muundo wa msingi */ba:radijl/*. Kutikana na kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu, muundo wake wa msingi umekuwa katika hali hiyo. Neno hilo, kwenye Kiarabu lina maana ya “mtu duni wa hali ya chini.”

Kwenye Kiswahili neno hilo linajitokeza kama neno moja, linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kikwamizi meno *ḍ* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kumalizikia kwa kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu

fupi mbele juu *i*. Katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni /baraḍuli/.

Katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo lina maana ya “mwanamume anayelawitiwa, hanithi, msenge.”

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu mbele juu /a:/ mwanzoni mwa neno katika muundo wa msingi kwenye Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Pili, kuna ufupishi irabu kwenye muundo wa msingi wa neno hili katikati kwenye Kiarabu, kuna irabu ndefu mbele juu /i:/ nayo kwenye Kiswahili imefupishwa na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Tatu, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno hili, kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Nne, kuna badiliko la semantiki punguzi, neno hili limepata maana jumuishi hasi haipendezi, maana hiyo imejikita katika sifa mbovu ya mwanamume anayetendewa tendo la kijinsia.

Barafu **برافو** : Neno hili asili yake ni kiajemi, liliingia kwenye Kiarabu. Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /barad/.

Kwenye lugha hiyo ya Kiarabu, neno hili lina maana ya “maji yaliyoganda yanayoanguka kutoka mawinguni katika sura ya mawe, theluji.”

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /barafu/.

Neno hilo katika Kiswahili, lina maana ya “maji yaliyoganda au kugandishwa kwenye chombo kutokana na baridi kali.”

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika neno hili kuna badiliko la sauti, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu kabla ya irabu ya mwisho kuna sauti kipasuo [d] yenye ghuna. Katika Kiswahili sauti kipasuo hiyo imebadilika na kuwa sauti kikwamizi [f] isiyo ya ghuna. Pili, kuna badiliko la semantiki hamishi. Neno hili limepata uhamishi wa maana kutoka kwenye Kiarabu, maana hiyo imepata tafauti ndogo sana ya kimaana ambapo bado maana hiyo ina uhusiano na ile maana ya Kiarabu. Dhana ya neno hili kwenye Kiswahili imesimamia zaidi kwenye maji yaliyogandishwa katika chombo kwa baridi kali.

Barizi *بريزي*: Asili ya neno hili ni kiajemi /baraza:n/. Katika Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /baraz/.

Kwenye Kiarabu, neno hili linamaanisha “jitokeza, dhihiri, onekana; enda haja kubwa.”

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*, katika lugha hiyo ya Kiswahili neno hili muundo wake wa msingi ni /barizi/.

Neno hili katika lugha hiyo ya Kiswahili lina maana ya “kitendo cha kujumuika pamoja katika mzungumzo ya barazani au kikaoni.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna badiliko la irabu. Kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, irabu zote tatu ni fupi mbele chini /a/ lakini kwenye muundo wa neno hili katika Kiswahili irabu mbili, ya katikati na ya mwisho, ni fupi mbele juu /i/. Pili, kuna badiliko la semantiki hamishi, neno hili limepata uhamishi kamili wa maana iliyo kinyume na ile ya mwanzo katika Kiarabu. Neno hili limechukua maana mpya, maana inayojikita kwenye muktadha wa kujitia katika kikao cha mazungumzo.

Baruti **بروت** : Asili ya neno hili ni kiajemi kutoka Kituruki /barud/. Liliingia Kwenye Kiarabu, linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu ndefu nyuma juu *u*: na kumalizikia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *n*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /baru:d/.

Neno hilo kwenye Kiarabu, lina maana ya “mada inayotokana na mchanganyiko wa natroni, kibiritiupele na makaa hutumika kutengenezea risasi na vitu vya miripuko.”

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kumalizikia kwa kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. Katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni /baruti/.

Kwa muktadha wa maana, katika Kiswahili linamaanisha “ungaunga unaotumika kwa ajili ya kuripulia vitu k.v. miamba.”

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu nyuma juu /u:/ mwishoni katika muundo wa msingi kwenye Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Pili, kuna ubadili konsonanti. Katika neno hili kuna badiliko la sauti, kwenye muundo wa msingi wa neno hilo katika Kiarabu kabla ya irabu ya mwisho kuna sauti kipasuo [d] yenye ghuna sauti hiyo imebadilika na kuwa kipasuo [t] kisicho cha ghuna. Tatu, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu kuna irabu fupi chini mbele /u/ mwisho wa neno hili, kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Hakuna badiliko kubwa la kisemantiki kwani dhana ya neno hili takriban ni ileile katika Kiarabu na Kiswahili, nayo ni ungaunga wa kuripulia vitu.

Bedui *بدي* : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kiyeyushi kaakaa laini *w* kikifuatiwa na irabu fupi mbele *i* na kumalizikia

kwa kiyeyushi kaakaa gumu j chenye mkazo na irabu fupi nyuma juu u na nazali ufizi n yenye ghuna. Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */badawij/*.

Neno hili linamaanisha “mtu mwanamume mzaliwa na mkaazi wa shamba kijijini.”

Kwa upande wa Kiswahili, neno hili linaanzia kwa sauti kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu fupi kati mbele ε ikifuatiwa na kipasuo ufizi d chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u , na kumalizikia kwa irabu fupi juu mbele i . Neno hilo muundo wake wa msingi ni */bedui/*.

Neno hili lina maana ya “mtu katili matata.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu irabu ya kwanza ni fupi chini */a/*. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi kati mbele */ε/*. Irabu ya pili imekuwa vilevile fupi nyuma juu */u/*. Pili, udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu, neno hili mwisho lina sauti konsonanti kiyeyushi chenye mkazo */j/*. Katika Kiswahili sauti hiyo imedondoshwa. Tatu, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu limeishia kwa irabu fupi nyuma juu */u/*, irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu */i/*. Nne, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili ambayo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia, pia imejikita zaidi kwenye sifa ya kutokuwa na huruma kwa maana ya ukatili na umatata.

Bilauri بلور : Katika Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi *a* mbele chini na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi *a* mbele chini na kufuatiwa na kiyeyushi midomo *w* na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi *u* nyuma juuna nazali *n* yenye ghuna. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */balawr /*.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hilo lina maana ya “chombo cha kigae.” Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi *i* mbele juu na kufuatiwa na kitambaza *l* na irabu fupi mbele chini *a* na irabu fupi nyuma juu *u* na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo katika lugha hii ya Kiswahili muundo wake wa msingi ni */bilauri/*.

Katika upande wa maana, neno hili linamaanisha “gilasi ya kigae inayonywewa maji.”

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwishoni mwa neno kuna konsonanti kiyeyushi midomo */w/*. Sauti hiyo [w] imepata badili */u/* kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu kuna irabu fupi nyuma juu */u/* mwisho wa neno, kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu */i/*. Tatu, kuna upanuzi semantiki, neno hili limepata maana mpya ambayo imekuwa jumuishi kuliko maana ya mwanzo ya Kiarabu. Maana hii mpya katika Kiswahili ni pana na imezidi upeo kimaana kwa kujikita kwenye chombo cha kigae cha kunywea maji basi.

Bitana *بِطَانَة*: Kwenye Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu mbele chini *a*: na kumalizikia kwa nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n* yenye ghuna. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */biṭa:nah/*.

Kwa upande wa maana, neno hilo kwenye Kiarabu, linamaanisha “kitambaa cha ndani ya nguo, sehemu ya ndani ya kitu.”

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi *i* mbele juu na kufuatiwa na kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia kwa nazali ufizi yenye ghuna *n* na irabu fupi mbele chini *a*. Katika Kiswahili neno hili muundo wake wa msingi ni */bitana/*.

Kwa upande wa maana katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hili linamaanisha “kitambaa laini kinachoshonewa ndani ya nguo.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna badiliko la ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu chini */a:/* mwanzoni mwa neno katika muundo wa msingi kwenye Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Pili, kuna ubadili konsonanti. Katika neno hili kuna badiliko la sauti, kwenye muundo wa msingi wa neno hilo katika Kiarabu konsonanti ya pili kutoka mwanzo ni sauti kipasuo *[t]* isiyo ya ghuna, katika Kiswahili imebadilika na kuwa */t/*. Tatu, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno

hili kwenye Kiarabu kuna irabu fupi nyuma /u/ mwisho wa neno hili, kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi mbele chini /a/. Nne, kuna badiliko la ufinyu semantiki; neno hili kwenye Kiswahili limechukua maana finyu zaidi kuliko kwenye Kiarabu, ufinyu huo kimaana umejikita zaidi kwenye kitambaa laini cha ndani kishonewacho ndani ya nguo.

Busati *بساط*: Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghunu na irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu chini *a*: na kuishia kwa kipasuo ufizi meno mtandazo *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n* yenye ghuna. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*bisa:t*/.

Katika Kiarabu neno hili lina maana ya “ardhi tambarare iliyo sawasawa; ardhi pana; - pana..”

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*busati*/.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “jamvi lililotengenezwa aghlabu kwa mabua ya mpunga au nganu.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu mwanzoni kuna irabu fupi

mbele juu /i/. Irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi nyuma juu *u* katika Kiswahili. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu chini /a:/ katikati kwenye muundo wake wa msingi. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Tatu, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili lina sauti konsonanti /t/ mwisho wa neno, sauti konsonanti hiyo imepata mbadala wa sauti konsonanti /t/ kwenye Kiswahili. Nne, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu limeishia kwa irabu /u/, irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa /i/. Tano, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya kwa kiasi haina mwelekeo wala uhusiano wa maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita kwenye jamvi la mabua ya nganu au mpunga.

Busara بصيرة : Katika Kiarabu, neno hili linaanzia kwa sauti kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi nyuma chini *a*, na kikwamizi ufizi ξ mtandazo kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu mbele juu *i*: na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n* yenye ghuna. Neno hili muundo wake wa msingi ni /baʃi:rah/.

Neno hili kwenye Kiarabu lina maana ya “nguvu za utambuzi; akili; bayana; hoja; ushahidi.”

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*, na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hili kwenye Kiswahili, muundo wake wa msingi ni /busara/.

Kwenye Kiswahili linamaanisha “akili au werevu wa kuweza kufikiria na kuamua kutenda jambo linalofaa; hekima; falsafa; utaratibu wa kutumia akili na maarifa katika kukabiliana na jambo au kutatua tatizo/mzozo.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu lina irabu fupi chini /a/ mwanzo wake. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi nyuma juu /u/. Vilevile neno hili kwenye muundo wake wa msingi, katikati lina irabu ndefu mbele juu /i:/. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi chini /a/. Pia kwenye muundo wake wa msingi, mwisho lina irabu fupi nyuma juu /u/; kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi chini /a/. Pili, kuna ubadili konsonanti, kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu; neno hili lina sauti konsonanti kikwamizi ufizi mtandazo /ʃ/. Sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi ufizi /s/. Tatu, kuna upanuzi semantiki; neno limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyo kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana, kutokana na kujumuisha dhana ya uwezo wa kiakili katika kukabiliana na jambo pamoja na uwezo wa kufikiri.

Buruji **برج**: Neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na kumalizikia kwa kikwamizi kaakaa *dʒ* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*burdʒ* /.

Kwa muktadha wa maana, neno hili katika Kiarabu, lina maanisha “jumba kubwa au kasri yenye ngome; nyumba iliyojengwa juu ya ukuta wa mji au juu ya ukuta wa ngome; moja katika maumbo dhahania kumi na mbili ya falaki nayo ni kondoo, dume la ng’ombe, jawzaau, saratani, simba, shuke, mizani, nge, upinde, mbuzi, ndoo na nyangumi.”

Kwenye Kiswahili neno hili, linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kumalizikia kwa kikwamizi kizuio kaakaa gumu *J* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni */buruJi/*.

Kwa muktadha wa maana, neno hili kwenye Kiswahili linamaanisha “ngome yenye kuta zenye mapengo sehemu ya juu, sera; mnara; tarumbeta ndogo ya askari ya kuashiria tukio kambini; uwazi maalumu katika uzio ambao nyuma yake huwekwa mtego wa kunasia samaki; pahali ambapo panadhaniwa nyota hubaki kwa muda wa siku moja kabla ya kuendelea na safari yake.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna uongezaji irabu; kwenye muundo wa misngi kwenye Kiarabu neno hili katikati lina mkusanyiko wa konsonanto */rdʒ/*, kwa hivyo kwenye Kiswahili imeongezwa irabu */u/* ili kuondoa mkusanyiko huo. Pili, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu kuna irabu fupi nyuma juu */u/* mwisho wa neno hili, kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu */i/*. Tatu, kuna badiliko la semantiki imarishi, neno hili limepata maana jumuishi chanya katika Kiswahili, hali hiyo ni

mwendelezo mzuri katika maana ya neno. Maana hiyo ina uhusiano na ile maana ya Kiarabu.

Bwana *بوان* : Asili ya neno hili ni Kiajemi /ba:na/ kwa maana ya “mkuu, mwenye/mwinyi”. Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kipasuo midomo *b* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kiyeyushi *w* midomo na irabu ndefu chini *a*: na kumalizikia kwa nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi juu nyuma *u*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /buwa:n/.

Kwenye Kiarabu neno hilo lina maana ya “nguzo inayosimamishiwa hema linapojengwa.”

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna pamoja na kiyeyushi *w* midomo na irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia kwa nazali *n* yenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a*. Katika Kiswahili neno hili muundo wake wa msingi ni /bwana/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiswahili neno hilo lina maana ya “lakabu ya heshima ya mwanamume; lakabu ya heshima ya mume wa mtu; tamko linalomfanya mtu asikilize.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna badiliko la udondoshi irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili, baada ya konsonanti ya kwanza, lina irabu fupi nyuma juu /u/. Irabu hiyo imedondoshwa. Pili, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu nyuma chini /a:/ katikati kwenye muundo

wake wa msingi katika Kiarabu. Irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno hili. Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Tatu, kuna semantiki hamishi, neno hili limepata uhamishi kamili wa maana tafauti na ile ya Kiarabu. Neno hili limechukua maana mpya inayojikita katika lakabu ya heshima ya mwanamume; lakabu ya heshima ya mume wa mtu; tamko linalomfanya mtu asikilize.

Dafina **دَفِينَة** : Neno hili kwenye Kiarabu, linaanzia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a*, na kufatiwa na kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu mbele juu *i*: na kufuatiwa na nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi nyuma chini *a* na kuishia kwa kipasuo meno ufizi kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*dafi:nah*/.

Kwa muktadha wa kimaana, neno hilo kwenye Kiarabu, linamaanisha “jambo au kitu kilichozikwa, mali iliyozikwa ardhini, kanzi.”

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a*, na kufuatiwa na kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a*, kwenye Kiswahili neno hilo muundo wake wa msingini /*dafina*/.

Kwa upande wa maana kwenye Kiswahili, neno hili linamaanisha “vitu vya thamani vilivyofichwa ardhini zama za kale, kanzi, kasiki.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu mbele juu /i:/ katikati kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu. Irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno hili. Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele chini /a/. Kwa upande wa kisemantiki, dhana ya neno hili takriban ni ile ile ya Kiarabu kwa maana ya “vitu vya thamani vilivyohifadhiwa ardhini kwa muda mrefu.”

Dhihaka **ضحك**: Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo meno ufizi \ddot{d} chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kufuatiwa na kikwamizi koromeo \dot{h} kisicho cha ghuna na kuishia kwa kipasuo kaakaa laini k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/\ddot{d}\dot{h}k/$.

Neno hilo linamaanisha “kucheka, uchekeji; tundu/tobo nyeupe; asali; ukarara wa mtende unapopasuka; ajabu.” El-Jar (1973), Ibn Mandhour (...:459 Juz. x).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi meno \ddot{d} chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kufuatiwa na kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi chini a na kuishia kwa kipasuo kidakatonge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a . Neno hilo kweye lugha hiyo ya Kiswahili muundo wake wa msingi ni $/dhihaka/$.

Neno hili kwenye Kiswahili lina maana ya “maneno au vitendo vya mzaha; utani, masihara.” BAKIZA (2010).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti, mwanzo wa neno hili kuna konsonanti sauti kipasuo meno ufizi chenye ghuna [d̥] katika muundo wa msingi kwenye Kiarabu. Sauti hiyo imebadilika na kuwa kikwamizi meno chenye ghuna [ð] kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wake wa msingi wa neno hili kuna irabu fupi chini juu /u/ mwisho wa neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi chini /a/ kwenye Kiswahili. Tatu, kuna semantiki hamishi; neno hilo limepata maana mpya kwenye Kiswahili ambayo ina mwelekeo na uhusiano wa maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita na kuegemea zaidi kwenye utani na mzaha.

Dhoruba ضربة : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo meno ufizi d̥ chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na kuishia kwa kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu fupi a na kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali n. Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /darba/.

Kwenye Kiarabu neno hilo lina maana ya “kipigo, upigaji, ugongaji; janga; msiba; balaa; makubaliano”. El-Jar (1973), Ibn Mandhour (... :548 juz. i).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi meno ð chenye ghuna na irabu fupi kati nyuma juu ɔ na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi

nyuma juu *u* na kuishia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /ɔruba/.

Katika Kiswahili neno hili lina maana ya “upepo mkali wenye nguvu na mawimbi makubwa baharini, tufani, kimbunga.”

Mabadiliko ya neno hili baada kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti, mwanzo wa neno hili kuna konsonanti sauti kipasuo meno ufizi chenye ghuna [ɖ] kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu. Sauti hiyo imebadilika na kuwa kikwamizi meno chenye ghuna [ð] kwenye Kiswahili. Pili, kuna uongezaji sauti irabu /u/ kwenye konsonanti mkusanyiko /rb/ ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wake wa msingi wa neno hili kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi chini /a/ kwenye Kiswahili. Nne, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo wala uhusiano wa maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita kwenye hali ya upepo mkali wenye nguvu.

Duru نور: Neno hilo kwenye Kiarabu linaanzia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kiyeyushi midomo *w* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /dawr/.

Kwa upande wa maana, neno hilo katika Kiarabu lina maana ya “kurudi kitu kama kilivyokuwa; muda mdogo; mwendo; tabaka ya kitu chenye mzunguuko juu yake; mzunguuko, kuzunguuka.” Ibn Mandhour (... :395 Juz. iv), El-Jar (1973).

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*.

Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni */duru/*.

Kwa upande wa maana, neno hilo linamaanisha “mzunguko; kitendo cha kwenda kwa mzunguko; kitendo cha kuzunguka kwa zamu.” BAKIZA (2010).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu lina irabu fupi nyuma chini */a/* mwanzo. Kwenye Kiswahili, irabu hiyo ya mwanzo imebadilika na kuwa irabu fupi nyuma juu */u/*. Vilevile kiyeyushi midomo */w/* kilichopo katikati ya neno hili kwa upande wa Kiarabu, kwenye Kiswahili kimedondoshwa moja kwa moja. Pili, kuna ufinyu semantiki, neno hili kwenye Kiswahili limechukua maana finyu zaidi kuliko kwenye Kiarabu. Maana imejifinya, ufinyu huo kimaana umejikita zaidi kwenye mzunguuko.

Dumuzi دعوص : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kikwamizi koromeo ^ʿ na kufuatiwa na nazali midomo *m* yenye ghuna na chenye ghuna na irabu ndefu nyuma juu *u*: na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi *ʃ* mtandazo kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu

hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /du^ʕmu:ʃ/.

Kwa muktadha wa maana kwenye lugha hiyo, linamaanisha “funza anayekuwa kwenye kidimbwi pale kinapokauka maji; umbo la mpito la baadhi ya wadudu baada ya kutotolewa na kabla ya kukua na kukamilika umbo lao.” El-Jar (1973:534).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, neno hili muundo wake wa msingi ni /dumuʒi/.

Kwa muktadha wa maana, neno hilo katika Kiswahili lina maana ya “mdudu anayetoboa nafaka kavu.” Bakiza (2010:73).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi wa sauti konsonanti [ʕ] kwenye Kiswahili. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu nyuma juu /u:/ katikati kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu. Irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Tatu, kuna ubadili konsonanti. Katika neno hili kuna badiliko la sauti, kwenye muundo wa msingi wa neno hilo katika Kiarabu konsonanti ya mwisho ni sauti kikwamizi mtandazo ufizi [ʃ] isiyo ya ghuna. Kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi ufizi /z/ chenye ghuna. Nne, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu kuna irabu fupi nyuma juu /u/. Kwenye Kiswahili, irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Tano, kuna ufinyu semantiki, neno hili kwenye Kiswahili

limechukua maana finyu zaidi kuliko kwenye Kiarabu; ufinyu huo kimaana ni kule kujiegemeza zaidi kwenye funza anayetoboa nafaka kavu tu.

Dunia **دنيا**: Neno hilo katika Kiarabu linaanzia kwa kipasu meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na nazali ufizi *n* na kiyeyushi kaakaa gumu *j* na kujiwa na irabu ndefu chini *a*: Kwenye lugha hiyo ya Kiarabu, neno hilo muundo wake wa msingi ni */dun-ja:/*.

Kwa upande wa maana katika lugha hiyo, lina maana ya “ulimwengu; maisha ya duniani hivi sasa; kinyume cha akhera; wa nasabu, wa karibu kinasabu; ulimwengu, maisha.” Moustafa (-- :298 Juz. i), El-Jar (1973:544).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kuishia kwa irabu fupi chini *a*. Neno hilo katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni */dunia/*

Kwa upande wa maana, neno hili katika lugha hiyo ya Kiswahili linamaanisha “sayari tunayoishi ndani yake; mwenendo wa maisha.” BAKIZA (2010:74).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna uongezaji sauti; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katikati kuna mkusanyiko wa sauti konsonant *[nj]*, imeongezwa sauti irabu */i/* baina ya mkusanyiko ili kwenye Kiswahili kuepuka mkusanyiko huo. Pili, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu chini mbele */a:/* mwishoni kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu. Irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Tatu, kuna

ufinyu semantiki; neno hili kwenye Kiswahili limechukua maana finyu kidogo kuliko kwenye Kiarabu. Ufinyu huo kimaana ni kule kujiegemeza zaidi kwenye sayari na mwenendo wa maisha.

Duni دُنْيَا : Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kikwamizi meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma mbele *a* na kufuatiwa na nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu ndefu mbele juu *i*: na kumalizikia kwa kipasuo koo [?] chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*dani*:[?] /.

Kwa muktadha wa maana neno hilo kwenye Kiarabu linamaanisha “ya chini, isiyo na thamani, yenye hali ya chini; hahe hohe.” Moustafa (-- :298 Juz. i).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni /*duni*/.

Kwa upande wa maana, neno hili kwenye Kiswahili linamaanisha “isiyo na thamani; ubao unaotandikwa ndani ya ngarawa kwa ajili ya kuwekea samaki.” BAKIZA (2010:74).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu lina irabu fupi nyuma mbele /*a*/. Kwenye Kiswahili, irabu hiyo ya mwanzo imebadilika na kuwa irabu fupi nyuma juu /*u*/. Pili, kuna badiliko la ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu mbele

juu /i:/ mwishoni kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu. Irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Tatu, kuna udondoshi sauti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu kuna sauti [ʔ]. Sauti hiyo imedondoshwa hususan ilivyokuwa haimo ndani ya mfumo wa sauti za Kiswahili. Nne, ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu kuna irabu fupi nyuma /u/ mwisho wa neno hili. Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Tano, kuna semantiki imarishi; neno hili lina uvumishi wa kitu au mtu, na nomino yenye maana iliyojikita zaidi kwenye ubao wa kuelekea samaki katika ngarawa. neno hili limepata maana jumuishi chanya katika Kiswahili, hali hiyo ni mwendelezo mzuri katika maana ya neno. Maana hiyo ina uhusiano na maana ya Kiarabu.

Ewaa! إي والله : Katika Kiarabu, neno hilo linatokana na muundo wa maneno matatu, la kwanza linaanzia kwa kipasuo koo ^ʔ chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kiyeyushi kaakaa gumu *j*, neno hilo muundo wake wa msingi ni /^ʔij/, la pili linaanzia kwa kiyeyushi midomo *w* chenye irabu fupi chini *a*. Muundo wake wa msingi ni /wa/; na neno la tatu linaanzia kwa kitambaza meno ufizi *l* chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kipasuo koo *h*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /lah/. Muundo wote mzima unaojitokeza kama neno moja ambalo muundo wake wa msingi ni /^ʔij walah/.

Kwa muktadha wa maana, neno hilo kwenye lugha hiyo ya Kiarabu linamaanisha “naam, ndiyo.” El-Jar (1973:203).

Katika Kiswahili, neno hili linaanza kwa irabu fupi kati chini ε na kufuatiwa na kiyeyushi midomo w na irabu ndefu chini a :. Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili neno hilo muundo wake wa msingi ni /*ewa*:/.

Kwa muktadha wa maana, neno hili linamaanisha “tamko la kuonesha hisia ya kukubali au kuridhika na kitu, jambo au maelezo.” BAKIZA (2010: 78).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna uimarishi irabu; irabu ya chini kati /*a*/ imeinuliwa na kuwa irabu ya kati juu /*\varepsilon*/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna udondoshi konsonanti. Neno hili lina konsonanti /*ʔ*/ mwanzo wa neno kwenye muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu, kwa hivyo konsonanti hiyo imedondoshwa katika Kiswahili; vilevile konsonanti /*l*/ na /*h*/ nazo hizi zimedondoshwa kwenye Kiswahili. Tatu, kuna upanuzi semantiki; neno hili limepata maana mpya ambayo imekuwa jumuiishi kuliko maana ya mwanzo kwenye Kiarabu. Maana hii mpya katika Kiswahili ni pana na imezidi upeo kimaana kwa kujikita kwenye kuonesha hisia ya kukubali au kuridhika na kitu, jambo au maelezo.

Enzi عَزَى : Katika Kiarabu neno hili, linaanzia kwa kwa kikwamizi koromeo ʕ chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi z chenye ghuna na mkazo na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni

/[*ʕiz*]/.

Neno hilo lina maana ya “utukufu, kinyume cha udhalili; mvua kubwa; nguvu.” El-Jar (1973:827). Ibnu Mandhour (..... : 274 juz. v)

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa irabu fupi chini kati ϵ na kufuatiwa na nazali ufizi n yenye ghuna na kuishia kwa kikwamizi ufizi z chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i . Neno hilo kwenye lugha hiyo ya Kiswahili muundo wake wa msingi ni /enzi /.

Neno hilo kwenye Kiswahili lina maana ya “zama; hadhi; kitendo cha kuonesha kudhihirisha utukufu wa Mwenyezi Mungu.” BAKIZA (2010:78).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti, kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu; mwanzo wa neno hili kuna sauti konsonanti / ζ / ambayo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu; baada ya kudondoshwa konsonanti ya mwanzo, kuna irabu fupi mbele juu / i /; irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi chini kati ϵ katika Kiswahili. Tatu, imeongezwa sauti konsonanti nazali n . Nne, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu limeishia kwa irabu ya nyuma juu / u /. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa ya mbele juu / i /. Tano, kuna upanuzi semantiki, neno limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyo kwenye Kiarabu; pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana ya utukufu wa kidini hasa kwa Mwenyezi Mungu.

Fadhaa **فزع**: Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kikwamizi ufizi z chenye ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kikwamizi koromeo ζ chenye ghuna na irabu fupi

chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /faza^ʕ /.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu linamaanisha “tisha, ogopesha; kimbilia kwa, - enda kwa; vundumka kwa kuogopa; ghabbika mno, shitadi hasira; enda mbali.” Moustafa (--):687 Juz. II; El-Jar (1973:907).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi meno *ð* chenye ghuna na irabu ndefu chini *a*: . Neno hili kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni /fadhaa /.

Kwa upande wa maana, neno hilo kwenye lugha hiyo ya Kiswahili lina maana ya “hali ya mtu kupatwa na mbabaiko kutokana na jambo la kushitua, ubabaikaji, ubabaifu, jakamoyo.” BAKIZA (2010:79).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; katika muundo wake wa msingi wa neno hili kuna sauti kikwamizi ufizi *z* sauti hiyo imebadilika na kuwa kikwamizi meno *ð*. Pili, kuna udondoshi konsonanti, mwisho wa neno hili kuna konsonanti sauti koromeo [ʕ], sauti hiyo imedondoshwa na kubaki irabu *a*. Tatu, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya na kwa kiasi kidogo ina uhusiano na ile ya awali kwenye Kiarabu. Maana hiyo mpya ina mwelekeo wa maana iliyotangulia. Maana ya kwenye Kiswahili imeegemea zaidi kwenye mbabaiko unaosababishwa na jambo la kushitua.

Fahuwa **فهو** : Katika Kiarabu neno hilo lina kiambishi awali ambacho kinaanzia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. Katika lugha

hiyo ya Kiarabu kiambishi hicho muundo wake wa msingi ni *fa* chenye kazi ya uunganishi (chenye maana ya mpangilio), kiunganishi cha jawabu shurutia, hunasibisha kitenzi cha wakati uliopo kwa kiambishi *an* kilichoachwa kiwajibu, mwendelezo unaokata maana iliyotangulia, hakikisho la maneno; kiambishi hicho kinakuwa katika kiarifu. Neno linalofuata baada ya kiambishi hicho, linaanzia kikwamizi koo *h* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kumalizikia kwa kiyeyushi midomo *w* chenye irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni */huwa/* kwa kawaida huja pamoja katika sentensi shurutia ambayo jawabu yake inaonesha uhakika na kuwa muundo wa msingi wa neno hilo ni */fahuwa/*.

Kwa upande wa maana katika lugha hiyo linamaanisha “basi ndio hilo.” El-Jar (1973:890).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kumalizikia kwa kiyeyushi midomo *w* na irabu fupi chini *a*. Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili neno hilo muundo wake wa msingi ni */fahuwa/*.

Kwa upande wa maana, neno hilo katika Kiswahili linamaanisha “basi ni jambo zuri; ni vyema; ni sawa.” BAKIZA (2010:79).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna semantiki hamishi, neno limepata maana mpya na kwa kiasi kidogo ina uhusiano na ile ya awali kwenye Kiarabu. Maana hiyo mpya ina mwelekeo wa maana iliyotangulia. Maana ya kwenye Kiswahili imeegemea zaidi kwenye kueleza hali ndiyo ya jambo na liko sawa.

Faka فاك: Kwenye Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu chini *a*: na kufuatiwa na kipasuo koromeo *q* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /fa:q/.

Kwa muktadha wa kimaana, neno hili linamaanisha “kuwa na mpasuko juu; kuwa, pandia juu yake; zidi kwa fadhila; vunja juu yake; -wa -zuri wakati wa kufa.” Moustafa (--):49,707 Juz. I,II; El-Jar (1973:894).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili neno hilo muundo wake wa msingi ni /faka/.

Kwa upande wa maana neno hilo lina maana ya “uwezo wa kiuchumi wa kufanya jambo; nafasi ya kufanya jambo.” BAKIZA (2010:80).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu chini /a:/ katikati kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo ya Kiswahili. Pili, kuna ubadili konsonanti; katika muundo wa msingi wa neno hili kuna sauti kipasuo koromeo *q* sauti hiyo imebadilika na kuwa kipasuo kidakatonge *k*. Tatu, kuna semantiki hamishi, neno limepata maana mpya na kwa kiasi kidogo ina uhusiano na ile ya awali kwenye Kiarabu. Maana hiyo mpya ina mwelekeo wa maana iliyotangulia. Maana ya kwenye Kiswahili imeegemea zaidi kwenye uwezo wa kufanya jambo kifedha, na wasaa au nafasi ya kufanya jambo.

Fataki **فتق** : Kwenye Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kikwamizi meno f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kipasuo ufizi meno t kisicho cha ghuna na kujiwa na kipasuo koromeo q kisicho cha ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */fatq/*.

Kwa upande wa maana, neno hili kwenye lugha hiyo ya Kiarabu linamaanisha “upasukaji, uchanikaji; asubuhi; mahali papana au palipotandawaa; mahali palipokuwa hapajanyeshewa na mvua ambapo sehemu nyenginezo zinazoizunguuka sehemu hiyo zimenyeshewa; janga kubwa; kutoka kwa kiungo au sehemu ya ndani ambayo kiungo hicho kinapatikana.” El-Jar (1973:896).

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kikwamizi f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a , kinafuatiwa na kipasuo ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kujiwa na kipasuo kidakatonge k kisicho cha ghuna na irabu fupi mbele juu i . Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni */fataki/*.

Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo lina maana ya kipande cha moyo wa ubegu wa muhogo au aina ya mbegu ambazo watoto hutia kwenye mdungudungu na kuzisukuma ili zilie kama risasi”. BAKIZA (2010 : 82)

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna badiliko la uongezaji irabu */a/* kwenye mkusanyiko konsonanti */tq/* mwishoni mwa neno hili kwa lengo la kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu;

kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Tatu, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya na kwa kiasi kidogo ina uhusiano na ile ya awali kwenye Kiarabu. Maana hiyo mpya ina mwelekeo wa maana iliyotangulia. Maana ya kwenye Kiswahili imeegemea zaidi kwenye kifaa cha mchezo wa watoto kitoacho sauti.

Faradhi فرض: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi meno *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kimadende ufuzi *r* chenye ghuna na kujiwa na kipasuo meno ufuzi *ḍ* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*farad̥*/.

Kwa upande wa maana, neno hilo linamaanisha “sehemu ndogo ya mapato n.k inayotolewa; jambo ambalo ameliwajibisha Mwenyezi Mungu kwa waja wake; sala isiyo ya suna; jambo ambalo mtu amejilazimishia mwenyewe kwa nafsi yake; wazo au fikra inayochukuliwa kuwa ni hoja juu ya jambo au kadhia fulani; sharti ya sala na mfumo wake; fedha ambazo si za mapato, kodi wala faini anazozikamilisha kuzipata Kamishna wa mapato; vipewa na mambo mengineyo ya askari”. El-jar (1973:904).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi meno *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kimadende ufuzi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* kujiwa na kikwamizi meno *ḍ* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Kwenye lugha hiyo, neno hili muundo wake wa msingi ni /*farad̥i*/.

Kwa upande wa maana, neno hili kwenye Kiswahili lina maana ya “jambo ambalo mtu analazimika kulitekeleza, wajibu; kiasi cha chakula kinachomtosheleza mtu kushiba; mauti.” BAKIZA (2010:81).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; katika muundo wa msingi wa neno hili kuna sauti kipasuo meno ufizi *ḍ* sauti hiyo imebadilika na kuwa kikwamizi meno. Pili, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Tatu, kuna badiliko la semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya ina mwelekeo wa maana iliyotangulia kwa kiasi fulani. Maana ya kwenye Kiswahili imeegemea zaidi kwenye, utoshelevu wa chakula unaoplekea shibe ya mtu, wajibu.

Faragha فرغ: Neno hili kwenye Kiarabu linaanzia kwa sauti kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenya irabu fupi chini *a* na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kikwamizi koromeo *y* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*faray*/.

Kwa muktadha wa maana, kwenye Kiarabu neno hili linamaanisha “kuwa -tupu, mimina, mwaga, maliza, kamilisha. -fa.” El-Jar (1973:904), Ibnu Mandhour (.....: 444 juz. viii).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kikwamizi kidakatonge *y* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*faraya*/.

Katika Kiswahili neno lina maana ya “sehemu ambayo watu wengine hawatakiwi kuifahamu; mazungumzo ya watu ambayo wengine hawatakiwi kuyajua; mahali au nafasi ya kufanyia jambo kwa siri.” BAKIZA (2010:81).

Badiliko la neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya ina mwelekeo wa maana iliyotangulia kwa kiasi fulani. Maana ya kwenye Kiswahili imeegemea zaidi kwenye sehemu ya siri, mazungumzo ya siri ya watu maalumu na mahali penye nafasi ya kutosha jambo mbali na watu wengine.

***Fatani* فتنان**: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi *t'* kisicho cha ghuna chenye mkazo na irabu ndefu chini *a*: na kumalizikia kwa nazali meno ufizi *n* na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*fata:n*/.

Neno hili lina maana ya “mwingi wa fitina; mwenye kuvutia na kushangaza; shetani.” El-jar (1973:895).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabau fupi chini *a* na kumalizikia kwa nazali ufizi *n* yenye irabu fupi mbele juu *i*. Muundo wake wa msingi ni */fatani/*.

Neno hili linamaanisha “mtu mchonganishi, dhabidhabina.” BAKIZA (2010:82), KKS (2004:78).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili katikati lina sauti konsonanti */t/* yenye mkazo inayoashiria kuwa ni konsonanti radidi/kariri */tt/*. Moja kati ya hizo kwenye Kiswahili imedondoshwa. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi, katikati lina irabu ndefu chini */a:/*. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Tatu, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu limeishia kwa irabu fupi nyuma juu */u/*, irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu */i/*. Nne, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili umejikita zaidi kwenye mtu mchonganishi, dhabidhabina.

***Fedheha* فضيحة** : Neno hili kwenye Kiarabu linaanzia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kipasuo meno ufizi *ḏ* kisicho cha ghuna chenye irabu irabu ndefu juu mbele *i*: na kuishia kikwamizi koromeo *h* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa

kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /fadi:hah/.

Kwa muktadha wa kimaana, neno hilo kwenye Kiarabu lina maana ya “kashfa, kuonesha mabaya ya mtu aliyonayo.” El-Jar (1973:912).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi kati juu *ε* na kikwamizi meno *ð* chenye ghuna na irabu fupi kati juu *ε* na kuishia kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /fedheha/.

Kwenye Kiswahili neno hilo lina maana ya “naza, izara, aibu.” BAKIZA (2010: 83).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuinga katika Kiswahili, mosi, kuna uimarishi irabu; kuna irabu fupi chini kati /a/ imeimarishwa kwa kuinuliwa na kuwa ya kati juu/ε/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna irabuchini; irabu ndefu mbele juu /i:/ kwenye muundo wake wa msingi katikati ya neno hili, imefupishwa na kuwa fupi mbele kati /ε/ kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wake wa msingi wa neno, kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi chini /a/ kwenye Kiswahili. Nne, kuna ufinyu semantiki; maana ya Kiswahili imejikita zaidi kwenye aibu.

Fisadi **فسد**: Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi meno *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kuishia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna

na irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*fasid*/.

Katika Kiarabu neno hilo lina maana ya “oza, haribika; tetemeka au yumbayumba na ona udhaifu wake.” El-Jar (1973:908), El-Jawhari (1978 : 519 Juz.ii).

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*fisadi*/.

Katika Kiswahili lina maana ya “mharibifu, muovu; mwenye kutumia jambo au kitu kwa njia mbaya; mgomvi, mfitinishi.” BAKIZA (2010 : 85), KKS (2004: 82).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, mosi, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili lina irabu fupi chini /*a*/ mwanzo. Irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /*i*/ kwenye Kiswahili; vilevile kuna irabu fupi mbele juu/*i*/. Irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi chini katika Kiswahili. Kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu limeishia irabu /*a*/; irabu hiyo imebadilika na kuwa /*i*/ katika Kiswahili. Pili, kuna upanuzi semantiki; neno limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyo kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana kujikita kwenye tabia mbovu.

***Furaha* فَرَح** : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kimadende ufizi *r* chenye ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye irabu fupi nyuma juu

u na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*faraħu*/.

Kwa muktadha wa kimaana, kwenye Kiarabu lina maana ya “furaha; sherehe ya arusi; kinyume cha huzuni; kufurahisha; majivuno, batara”. El-Jar (1973:901), Ibnu Mandhour (... :549 Juz.ii)

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia vilevile kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*furaha*/ . Katika Kiswahili, neno hili lina maana ya “hali ya kuwa mchangamfu, furaha.” El-Jar (1973:91).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu. Kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi chini mbele /*a*/ mwanzo wa neno hili. Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi nyuma juu /*u*/; vilevile, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi nyuma juu /*u*/ mwisho wa neno hili. Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi chini /*a*/ . Pili, kuna ubadili konsonanti. Katika neno hili kuna badiliko la sauti kikwamizi koromeo [*ħ*] kisicho cha ghuna, kwenye muundo wa msingi mwisho wa neno kwenye Kiarabu. Katika Kiswahili sauti hiyo imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo /*h*/ chenye ghuna. Tatu, kuna ufinyu semantiki, neno hili kwenye Kiswahili limechukua maana finyu zaidi kuliko kwenye Kiarabu, ufinyu huo kimaana ni kule kujiegemeza zaidi kwenye furaha basi.

Ghafla غفلة : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo y chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna na kujiwa na kitambaza ufizi l kisicho cha ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kipasuo ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*yaflah*/.

Kwa muktadha wa kimaana, neno hilo katika lugha hiyo ya Kiarabu lina maana ya “usahaulifu, kisahau, kutokumbuka; bila ya kukusudia; bila ya hadhari; dharau.” BAALBAK (2003 : 802).

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo y chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna na kujiwa na kitambaza l kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a , na muundo wake wa msingi ni /*ghafla*/

Neno hilo kwenye Kiswahili linamaanisha “bila ya kutarajiwa, mara tu.” KKS (2004: 95).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu limeishia kwa irabu fupi nyuma / u / . Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwafupi chini / a / . Pili, kuna uwekaji konsonanti mkusanyiko kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu; mwisho wa neno hili kuna konsonanti mkusanyiko / fl / . Mkuasnyiko huo,

vilevile kwenye Kiswahili umewekwa. Tatu, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili umejikita zaidi kwenye hali ya kutotazamiwa na kwa mshtukizo wa jambo.

Ghaibu غيب : Kwenye Kiarabu neno hili, linaanzia kwa kikwamizi koromeo y chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na irabu ndefu mbele juu i : na kujiwa na kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/yai:b/$.

Neno hili kwenye Kiarabu lina maana ya “kuto kuhudhuria; kutokuonekana.” El-Zubaydi (---: 830 :2).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini y chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na irabu fupi mbele juu i na kujiwa na kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u , muundo wake wa msingi ni $/ghaibu/$.

Kwa upande wa maana, neno hilo katika Kiswahili lina maana ya “hali ya kutojulikana au kutoonekana bayana jambo au kitu.” BAKIZA (2010: 97).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, mosi, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu mbele juu $/i:/$ mwanzoni kwenye muundo wake wa msingi. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Pili, kuna upanuzi semantiki, neno limepata maana jumuishi

kuliko ile maana iliyo kwenye Kiarabu, pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana ya kutojikana, kutoonekana.

Ghairi غير: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini *y* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na irabu ndefu *i*: na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*yai:r*/.

Katika Kiarabu neno hilo lina maana ya “-engine kuliko, tafauti na, si sawa, sio; sio sawa; isipokuwa; lakini; -engine.” El-Jar (1973:888).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kidakatonge *y* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Kwenye Kiswahili, neno hili muundo wake wa msingi ni /*ghairi*/

Neno hilo lina maana ya “kitendo cha kukataa jambo ambalo awali mhusika alikubali kulitenda.” BAKIZA (2010: 97).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu mbele juu /*i*/ katikati ya muundo wake wa msingi. Irabu hiyo imefupishwa kwenye Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu limeishia irabu /*u*/. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa /*i*/. Tatu, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili umejikita zaidi kwenye hali ya kukataa tu .

Ghashashi عَشَّاش : Kwenye Kiarabu, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini y chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kikwamizi kaakaa gumu f kisicho cha ghuna chenye mkazo na irabu ndefu chini a : na kumalizikia tena kwa kikwamizi kaakaa gumu f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/yafa:f/$.

Kwenye Kiarabu neno hili lina maana ya “mdanganyifu, laghai, sio mwaminifu; mpotoshaji; haraka; chache; -sio safi”. Mandhuri (---:323: Juz. vi).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi kidakatonge y chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kiwamizi kaakaa gumu f chenye irabu fupi chini a na kumalizikia vilevile kwa kikwamizi kaakaa gumu f kisicho cha ghua na irabu fupi mbele juu i . Kwenye Kiswahili, neno hili muundo wake wa msingi ni $/ghashashi/$.

Kwa upande wa maana, neno hili katika Kiswahili, lina maana ya “mtu mwenye tabia ya kufanya ghibiba katika biashara; mtu aliyezoweza kuwadanganya watu ili apate mali au fedha.” BAKIZA (2010: 98).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu, neno hili lina sauti kikwamizi konsonanti $/f/$ yenye mkazo. Mkazo huo unaashiria uradidi/ukariri konsonanti $/ff/$, kwa hivyo moja kati ya sauti konsonanti hizo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu chini $/a:/$ katikati ya muundo wake wa

msingi. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Tatu, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu limeishia kwa irabu /u/. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa /i/. Nne, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili, umejikita zaidi kwenye sifa ya udanganyifu aliyonayo mtu katika bishara pia mtu mwenye mazoea ya kudanganya ili apate mali.

Gharadhi غرض : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini y chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi \dot{d} chenye ghuna na irabu fupi chini u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni / $yara\dot{d}$ /.

Neno hilo katika Kiarabu linamaanisha “lengo, madhumuni, kusudio, shabaha; ashiki,-wa na hamu. penda.” El- Jawhari (1987: Juz.iii).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi kidakatonge y chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kikwamizi meno \dot{d} chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i , na muundo wake wa msingi ni / $gharadhi$ /.

Neno hilo katika Kiswahili linamaanisha “hoja zinazotolewa ili kupinga jambo; hoja ya mtu au tendo la kujipendekeza ili kujipatia kitu kwa mtu mwingine.” BAKIZA 2010: 98).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu, neno hili lina sauti kipasuo konsonanti /d̥/ mwisho wa neno. Sauti konsonanti hiyo imepata mbadala wa sauti kikwamizi konsonanti /ð/ kwenye Kiswahili. Pili, ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu limeishia kwa irabu fupi nyuma /u/. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele /i/. Tatu, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya kwa kiasi haina mwelekeo wala uhusiano wa maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita zaidi kwenye hoja ya kupinga jambo.

Ghamidha غمض : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini *y* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi mbele *i* na kujiwa na kipasuo ufizi d̥ chenye ghuna na irabu fupi *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni Neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /yamad̥/.

Neno hilo kwenye Kiarabu linamaanisha “-isio eleweka , kutofahamika, kuwa -enye.” El-Jar (1973:885).

Katika Kiswahili neno hilo, linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini *y* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kuishia kwa kikwamizi meno ð chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hili kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni /ghamidha/.

Kwa upande wa maana, neno hilo katika Kiswahili linamaanisha “hali ya kulifanya jambo dogo kuwa kubwa; utata.” BAKIZA (2010: 98).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu katikati lina irabu fupi chini /a/. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu /i/. Pili, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya kwa kiasi haina mwelekeo wala uhusiano wa maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita zaidi kwenye kukuza jambo.

Ghamu غَم : Kwenye Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini y chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na nazali midomo *m* yenye mkazo na ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali n. Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*yam*/.

Kwa muktadha wa maana, neno hili kwenye Kiarabu lina maana ya “huzuni, simanzi, msongo wa mawazo, wasiwasi, maumivu ya moyoni; janga; jambo lisilofahamika ” Razi (2014).

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kikwamizi kidakatonge y chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na nzali midomo m yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u, muundo wake wa msingi ni /*ghamu*/.

Kwa upande wa maana, neno hilo katika Kiswahili lina maana ya “majonzi.” BAKIZA (2010: 98).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu, neno hili lina sauti nazali konsonanti /*m̄*/ yenye mkazo unaoashiria kuwa ni konsonanti radidi/kariri /*mm*/; moja kati ya konsonanti hizo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Pili, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili, umejikita zaidi kwenye majonzi basi.

Ghanima غنيمة: Katika Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kikwamizi kaaka laini *y* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu ndefu mbele juu *i*: na kumalizikia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasilimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*yani:mah*/.

Neno hili kwenye Kiarabu linamaanisha “uporaji, unyang’anyi; zawadi; pato, faida, manufaa; maliinayotekwa katika vita;ujira, thawabu, malipo.” Ibnu Mandhour (... : 445 Juz.xii), BAALBAKI (2003: 806).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi kidakatonge *y* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kuishia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hilo katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*ghanima*/.

Neno hilo katika Kiswahili limeingiza maana zote za kiarabu katika fasili moja, na lina maana ya “neema inayopatikana hasa baada ya ushindi katika vita; ngawira.” BAKIZA (2010: 98).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu mbele juu /i:/ katikati ya muundo wake wa msingi. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Pili, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu limeishia kwa irabu fupi nyuma juu /u/. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi chini /a/. Tatu, kuna upanuzi semantiki; neno limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyo kwenye Kiarabu; pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana ya neema ya mali inayopatikana baada ya ushindi kwenye vita.

Gharika غرق : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini y chenye ghuna na irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kipasuo koromeo q kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /yaraq/.

Neno hilo linamaanisha “kuzama, kufa maji; uzamaji kwenye maji” Razi (2014), Ibnu Mamdhour (.... : 445 Juz.xii),

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kikwamizi kidakatonge y chenye ghuna na irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kumalizikia kwa kipasuo kidakatonge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a . Neno hili kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni /gharika/, na linamaanisha “maangamizi yanayotokana na janga la kimaumbile k.v. mafuriko au tufani, nakama.” BAKIZA (2010: 98).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadiliirabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu katikati lina irabu fupi chini /a/. Irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi mbele juu /i/. Vilevile kwenye Kiarabu limeishia irabu fupi nyuma juu /u/ kwenye muundo wake wa msingi; irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi chini /a/. Pili, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili lina sauti kipasuo koromeo konsonanti /q/ mwisho. Sauti konsonanti hiyo imepata mbadala wa sauti konsonanti /k/ kwenye Kiswahili. Tatu, kuna upanuzi semantiki; neno limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyo kwenye Kiarabu, pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana ya nomino ambayo kimaana imejikita kwenye nakama pamoja na maangamizi yanayosababishwa na janga la kimaumbile.

Gharama غرامة : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini y chenye ghuna na irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu ndefu chini a : na kumalizikia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi chini a na kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na

nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*yara:mah*/. Neno hilo linamaanisha “adhabu, fedha za adhabu, faini; jambo linalolazimika kutekelezwa” Razi (2014).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kidakatonge *y* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*gharama*/, na linamaanisha “malipo ya huduma iliyotolewa.” BAKIZA (2010:98).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu chini /*a*:/ katikati ya muundo wake wa msingi. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu mwisho lina irabu fupi nyuma juu /*u*/, kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa fupi chini /*a*/. Tatu, kuna semantiki hamishi, neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia na imejikita zaidi kwenye malipo ya jambo.

Ghashi غَشِي : Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini *y* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *ʃ* kisicho cha ghuna chenye mkazo na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni

tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /yif/.

Katika Kiarabu neno hilo linamaanisha “udanganyifu, ulaghai; ujanja; kinyume, hiana.” El-Jar (1973: 878).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kidakatonge y chenye ghuna na irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kikwamizi ufizi \int kisicho cha ghuna na irabu fupi mbele juu i . Neno hilo muundo wake wa msingi ni /ghashi/.

Neno hilo lina maana ya “uchafu unaotoka au kuchuruzika kwenye kijaraha; udanganyifu wa kuigiza kitu halisi.” BAKIZA (2010 : 98).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili lina sauti kikwamizi konsonanti /ʃ/. Sauti yenye mkazo inayoashiria kuwa ni konsonanti radidi/kariri /ʃʃ/, moja kati ya konsonanti hizo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu mwanzo lina irabu fupi mbele juu /i/. Kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa fupi chini /a/. Vilevile kwenye Kiarabu limeishia kwa irabu fupi nyuma juu /u/, irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu /i/. Tatu, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya kwa kiasi ina mwelekeo na uhusiano na maana iliyotangulia nayo imejikita zaidi katika udanganyifu na maji yanayotoka kwenye kidonda.

Ghera غيرة : Kwenye Kiarabu, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini y chenye ghuna na irabu ndefu mbele juu i : na kufuatiwa na kimadende r chenye ghuna na irabu fupi chini na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /yajrah/.

Neno hili kwenye Kiarabu linamaanisha “wivu; hisia za heshima, hali ya kujali; kivumishi cha utenguaji Razi (2014).”

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kikwamizi kidakatonge y chenye ghuna na irabu fupi mbele kati ϵ na kumazikia kwa kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi chini a . Neno hili muundo wake wa msingi ni /ghera /

Neno hilo linamaanisha “moyo wa kufanya jambo kwa kuogopa aibu iwapo halitafanywa au litashindikana, hisia za kutenda jambo kuepa aibu au hatari.” BAKIZA (2010 : 98).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu mwanzo lina irabu ndefu mbele juu /i:/. Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi mbele kati /ε/. Vilevile kwenye Kiarabu limeishia kwa irabu fupi nyuma juu /u/; irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi chini /a/. Pili, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili nayo kwa kiasi ina mwelekeo na uhusiano na maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita zaidi katika moyo wa kuchelea kufanya jambo ili kuepuka aibu endapo kama halitafanyika au kushindikana.

Ghuba غَبَّة : Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini *y* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kipasuo midomo *b* chenye ghuna na mkazo na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /yubah/.

Katika Kiarabu linamaanisha “chakula kisichotosha wala hakibaki.” El-Jar (1973: 249).

Katika Kiswahili neno hilo, linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini *y* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, neno hili muundo wake wa msingi ni /ghuba/.

Neno hilo lina maana ya “sehemu ya mwambao wa bahari iliyoingia ndani kwa upande wa nchi kavu, hori, komeo.” KKS (2004 96)

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu, neno hili mwisho lina sauti konsonanti /b/. Sauti yenye mkazo inayoashiria kuwa ni konsonanti radidi/kariri /bb/; moja kati ya konsonanti hizo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu neno hili limeishia kwa irabu fupi nyuma juu /u/. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi chini /a/. Tatu, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili ambayo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita zaidi katika sehemu ya mwambao wa bahari ulioingia ndani kwenye nchi kavu.

Ghubari غبار : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini y chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na kufuatiwa na kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu ndefu chini a : na kumalizikia kwa kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/yuba:r/$.

Kwa upande wa maana kwenye lugha hiyo ya Kiarabu, linamaanisha “vumbi, mvumbimvumbi; mfano wa vumbi” Razi (2014).

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kikwamizi kidakatonge y chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u , na kufuatiwa na kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kimadende r chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i . Neno hilo muundo wake wa msingi ni $/ghubari/$.

Kwa muktadha wa kimaana, neno hilo linamaanisha “wingu linaloambatana na upepo mkali; vumbi zito lililotanda hewani.” BAKIZA (2010: 98)

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu chini $/a:/$ kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu. Irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi nyuma juu $/u/$ mwisho wa neno hili. Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu $/i/$. Tatu, kuna badiliko la upanuzi semantiki; neno hili limepata maana mpya ambayo imekuwa jumuishiki kuliko maana ya

mwanzo ya Kiarabu. Maana hii mpya katika Kiswahili ni pana na imezidi upeo kimaana kwa kujikita kwenye wingu linalokuwa na upepo wenye nguvu kubwa.

Ghadhabu **غضب** : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo y chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi δ chenye ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni / $yad\delta ab$ /.

Kwa muktadha wa maana, neno hili linamaanisha “hali ya chuki yenye utashi wa kutaka kulipiza kisasi, hasira, hamaki; waka sana; chemka au pwaga sana.” El-Jar (1973: 879), Fairouzabadi (... : 154 Juz. i).

Katika Kiswahili neno hilo, linaanzia kwa kikwamizi koromeo y chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kikwamizi meno δ chenye ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u . Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, neno hili muundo wake wa msingi ni / $ghad\delta abu$ /.

Kwa muktadha wa maana kwenye lugha hiyo, neno hilo linamaanisha “hasira nyingi zinazosababishwa na maudhi, hamaki.” BAKIZA (2010:97).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuinga katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; katika muundo wake wa msingi wa neno hili lina sauti kipasuo meno ufizi δ , sauti hiyo imebadilika na kuwa kikwamizi meno δ . Pili, kuna ufinyu semantiki; neno hili

kwenye Kiswahili limechukua maana finyu zaidi ambayo imejikita katika hasira kubwa zinazosababishwa na kero na maudhi.

Ghulamu غلام : Asili ya neno hili ni Kiajemi /yola:m/ lenye maana ya mtumwa wa Mungu, Nabii. Katika Kiarabu, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini y chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na kufuatiwa na kitambaza ufizi l kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu chini a: na kumalizikia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali n. Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /yula:m/.

Kwa upande wa maana, neno hilo lina maana ya “mtoto mwanamume, kijana, barobaro; mtumishi; mtumwa.” El-Jar (1973: 882).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kidakatonge y chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u, na kufuatiwa na kitambaza ufizi l kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kumalizikia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u. Katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni /ghulamu/.

Kwa upande wa kimaana, neno hilo lina maana ya “mtoto wa kiume anayefikia hadi umri wa miaka kumi na nne; karata yenye alama ya J ambayo ni Mzungu wa Tatu na Q ni Mzungu wa Pili.” BAKIZA (2010:98).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu chini /a:/ katikati kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu. Irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu

katika Kiswahili. Pili, kuna semantiki hamishi, neno hili limepata uhamishi kamili wa maana tafauti na ile ya Kiarabu lakini maana hiyo ina uhusiano na ile ya mwanzo kwenye Kiarabu. Neno hili limechukua maana mpya ambayo imejifinya na kujikita katika kijana mwanamume wa umri wa miaka kumi na nane na kwenye mchezo wa karata alama ya J Mzungu wa tatu au Q Mzungu wa Pili.

Haba ﺣﺒﺎ : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi koromeo \hbar chenye ghuna na irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kipasuo midomo b chenye mkazo na ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/\hbar ab/$.

Kwenye Kiarabu neno hili lina maana ya “punje ya nafaka; sehemu moja juu ya kumi na sita ($1/16$) ya dinari.” El-Jar (1973: 427).

Katika Kiswahili linaanzia kwa kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu fupi chini a . Neno hilo muundo wake wa msingi ni $/haba /$.

Katika Kiswahili neno hilo lina maana ya “kidogo, chache, kisichotosha.” KKS (2004 :104).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu neno hili lina sauti konsonanti kikwamizi koromeo $/\hbar/$. Sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo $/h/$. Pili kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu,

neni hili mwisho lina sauti konsonanti kijasuo /b/ yenye mkazo inayoashiria kuwa ni konsonanti radidi / kariri /bb/. Moja kati ya hizo imedondoshwa. Tatu, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu mwisho lina irabu fupi nyuma juu /u/. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi chini /a/. Nne, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili ambayo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia nayo imejikita zaidi kwenye maana ya hali ya kuto tosha au uchache.

Habithi **خبِيث**: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi kidakatonge x kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a , na kijasuo midomo b chenye ghuna na irabu ndefu mbele juu i : pamoja na kuishia kwa kikwamizi meno \emptyset kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /xabi:ø/.

Kwa muktadha wa maana, kwenye Kiarabu neno hilo lina maana ya “-chafu, -baya, haramu.” El-Jar (1973: 471).

Kwenye Kiswahili linaanzia kwa kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi a na kijasuo midomo b chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i , na kuishia kwa kikwamizi meno \emptyset kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i . Neno hili muundo wake wa msingi ni /habithi/.

Kwenye Kiswahili, lina maana ya “mtu muovu; fisadi; mtu mjanja; mtu asiyejali utu wa mwengine.” KKS (2004:106),Bakiza (2010: 107).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, mosi, kuna ubadili konsonanti. Katika neno hili kuna sauti kikwamizi koromeo [x] kisicho cha ghuna, kwenye muundo wa msingi mwanzo wa neno hili kwenye Kiarabu; sauti hiyo imebadilishwa kwa sauti kikwamizi koromeo [h]. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu mbele juu /i:/ katikati kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye Kiswahili. Tatu, kuna upanuzi semantiki; neno hili limepata maana mpya ambayo imekuwa jumuishi. Maana hii mpya katika Kiswahili ni pana na imezidi upeo kimaana kwa kujikita kwenye sifa ya mtu muovu, fisadi na mjanja.

Hadhara *حاضرة* : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *ħ* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kipasuo meno ufizi *ḏ* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */ħaḏarah/*.

Neno hili katika Kiarabu lina maana ya “uhudhuriaji, ufikaji; mahali palipohudhuriwa; uimbaji; karibu; nyenzo na vifaa vya ujenzi.” El-Jar (1973: 452).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi meno *ḏ* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna kikiwa na irabu fupi chini *a*. Neno hili muundo wake wa msingi ni */hadhara/*.

Kwenye Kiswahili, neno hilo lina maana ya “mkusanyiko wa watu wengi kwa ajili ya jambo maalumu.” BAKIZA (2010: 107).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kuna sauti kikwamizi koromeo [ħ] mwanzo wa neno. Sauti hiyo imebadilika na kuwa /h/. Vilevile katikati ya neno hili kuna sauti kipasuo meno ufizi [ǎ]; sauti hiyo imebadilika na kuwa kipasuo ufizi [Ǿ]. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wake wa msingi, neno hili lina irabu fupi chini /u/ mwisho wake, irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi chini /a/ kwenye Kiswahili. Tatu, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo na uhusiano wa maana iliyotangulia. Maana hiyo kwenye Kiswahili imeegemea zaidi kwenye mkusanyiko wa watu wengi kwa ajili ya jambo maalumu.

Hadhi **هذ**: Kwenye Kiarabu, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo ħ kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi mtandazo meno ulimi *ž* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /ħaž /.

Kwa upande wa maana, neno hilo kwenye Kiarabu lina maana ya “bahati, fursa; bahati nzuri; heshima; fungu, sehemu; wasaa, utajiri.” El-Jar (1973: 453).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi meno ulimi *ð* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni /hadhi/.

Kwa upande wa maana neno hilo lina maana ya “hishima ya mtu katika utukufu wa jamii, darja, enzi.” BAKIZA (2010 :107).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu; kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno. Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Pili, kuna ubadili konsonanti. Katika neno hili kuna badiliko la sauti kikwamizi koromeo [ħ] kisicho cha ghuna, kwenye muundo wa msingi mwanzo wa neno kwenye Kiarabu. Katika Kiswahili sauti hiyo imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo /h/ chenye ghuna. Tatu, kuna ufinyu semantiki, neno hili kwenye Kiswahili limechukua maana finyu zaidi kuliko kwenye Kiarabu; ufinyu huo kimaana ni kule kujiegemeza maana katika hishima ya mtu inayoandamana na utukufu wake kijamii.

Haiba هيبة : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi koo *h* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kiyeyushi *j* kaakaa na kufuatiwa na kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*hajba*/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hilo lina maana ya “woga, hofu; heshima; hadhi.” BAALBAKI (2003:1214).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na irabu fupi mbele juu *i* na kumlizikia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*haiba*/ pia /*heba*/.

Katika Kiswahili, neno hilo lina maana ya ‘utambulisho wa mtu, jambo au kitu; mvuto wa sura/sifa nzuri ya mtu.’ BAKIZA (2010: 108).

Mabadiliko ya neno hilo baada kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, irabu fupi nyuma juu /*u*/ mwisho wa neno, imebadilika na kuwa irabu fupi chini /*a*/. Pili, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana iliyokinyume na ile ya awali kwenye Kiarabu. Maana hiyo mpya imepoteza mwelekeo wa maana iliyotangulia. Maana ya kwenye Kiswahili imeegemea zaidi kwenye utambulisho wa mtu au jambo.

Haki *حق* : Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kikwamizi koo *h* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na Kipasuo kidakatonge *q* kisicho cha ghuna chenye mkazo na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*haq*/.

Kwa upande wa maana katika Kiarabu, linamaanisha “mali, milki, umilisi; ukweli, yakini; sahihi, ndio.” BAALBAKI (2003:480).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi

mbele juu *i*. Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni /haki/.

Kwa upande wa maana neno hilo kwenye Kiswahili linamaanisha “jambo linalomstahikia mtu.” BAKIZA (2010:108).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika neno hili kuna badiliko la sauti kikwamizi koromeo [ħ] kisicho cha ghuna, kwenye muundo wa msingi mwanzo wa neno kwenye Kiarabu. Katika Kiswahili sauti hiyo imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo /h/ chenye ghuna; vilevile mwisho kuna sauti kipasuo kidakatonge /q/ kisicho cha ghuna, kwenye Kiswahili kimebadilika na kuwa /k/. Pili, kuna ubadili irabu kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno hili. Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Tatu, kuna ufinyu semantiki; neno hili kwenye Kiswahili limechukua maana finyu zaidi kuliko kwenye Kiarabu, ufinyu huo kimaana umejikita kwenye jambo mwajibikia mtu, na si vyenginevyo.

Hakika حقيقة: Neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa kikwamizi koromeo ħ kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini mbele *a* na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge *q* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu mbele juu *i*: na kipasuo kidakatonge *q* chenye irabu fupi chini *a*, na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna na kuishia kwa irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /ħaqi:qah/.

Kwa upande wa maana kwenye lugha hiyo ya Kiarabu, linamaanisha “ukweli; hali halisi.” BAALBAKI (2003:482).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na na kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa tena na kipasuo kidakatonge *k* isicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. Neno hili kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*hakika*/.

Kwa upande wa maana, neno hili katika Kiswahili, lina maanisha “ukweli wa jambo; bila ya shaka.” BAKIZA (2010:108).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika neno hili kuna sauti kikwamizi koromeo [*ħ*] kisicho cha ghuna, kwenye muundo wa msingi mwanzo katika Kiarabu. Katika Kiswahili sauti hiyo imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo /*h*/ chenye ghuna. Pili, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu mbele juu /*i*:/ katikati kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu. Tatu, kuna ubadili irabu kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi nyuma juu /*u*/ mwisho wa neno hili. Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi chini /*a*/. Nne kuna ufinyu semantiki, kwenye Kiswahili limechukua maana finyu zaidi kuliko kwenye Kiarabu, ufinyu huo kimaana ni kule kujiegemeza zaidi kwenye ukweli.

Hakiri حفير : Kwenye Kiarabu, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo *ħ* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge *q* kisicho

cha ghuna chenye irabu ndefu mbele juu *i*: na kumalizikia kwa kimadende *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*ħaqi:r*/.

Kwa upande wa maana, neno hilo kwenye Kiarabu linamaanisha “ya chini, duni,-dogo; ya kudharaulika, isiyo na thamani.” Ibn Mandhour (... : 207 Juz. iv), BAALBAKI (2003:482).

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni /*hakiri*/.

Kwa upande wa maana, neno hilo ndani ya Kiswahili, linamaanisha “mnyonge, dhalili.” KKS (2004:106).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika neno hili kuna sauti kikwamizi koromeo [*ħ*] kisicho cha ghuna, kwenye muundo wa msingi mwanzo wa neno kwenye Kiarabu. Katika Kiswahili sauti hiyo imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo /*h*/ chenye ghuna; vilevile katikati kuna sauti kipasuo kidakatonge /*q*/ kisicho cha ghuna, kwenye Kiswahili kimebadilika na kuwa /*k*/. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu mbele juu /*i*:/ katikati kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu; kuna irabu fupi nyuma juu /*u*/

mwisho wa neno hili. Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Nne, ufinyu semantiki; neno hili kwenye Kiswahili limechukua maana finyu zaidi kuliko kwenye Kiarabu, ufinyu huo kimaana ni kule kujiegemeza zaidi kwenye unyonge.

Halaiki *خلاق*: Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo x kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini a na kufuatiwa na kitambaza ufizi l kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu mbele chini a : na kipasuo koo 2 chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kumalizika kwa kipasuo kidakatonge q chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni / *xalqun*/.

Katika lugha hiyo ya Kiarabu neno hilo linamaanisha “maumbile; uumbaji; viumbe; kitu chochote kilichowekwa sawa.” El-Jar (1973:505).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi mbele chini a na kitambaza ufizi l kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini a na kufuatiwa na irabu fupi mbele juu i na kipasuo kaakaa laini k kisicho cha ghuna na irabu fupi mbele juu i . Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, neno hili muundo wake wa msingi ni /*halaiki*/.

Kwa upande wa maana, neno hili kwenye Kiswahili linamaanisha “idadi kubwa ya mkusanyiko wa watu, umati; sanaa ya mkusanyiko inayochezwa na watu wengi.” BAKIZA (2010:109).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika neno hili kuna sauti kikwamizi kaaka laini [x] kisicho cha ghuna, kwenye muundo wa msingi mwanzo wa neno kwenye Kiarabu. Kwenye Kiswahili sauti hiyo imebadilika na kuwa [h]. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu chini /a:/ katikati kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye Kiswahili. Vilevile katikati kuna sauti kipasuo koo /ʔ/ chenye ghuna; kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Pili, kuna ubadili irabu, neno hili mwisho lina irabu fupi nyuma juu /u/ kwenye Kiarabu, irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Tatu, kuna kuna badiliko la upanuzi semantiki, neno hili limepata maana mpya ambayo imekuwa jumuishi. Maana hii mpya katika Kiswahili ni pana na imezidi upeo kimaana kwa kujikita kwenye mkusanyiko wa watu wengi pamoja na sanaa inayochezwa na watu.

Halafu **خلاف**: Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kidaka tonge *x* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu mbele chini *a*: na kumalizikia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /xila:f/.

Katikika lugha hiyo ya Kiarabu, neno hili lina maana ya “mzozo, ugomvi, kutofahamiana, mgongano, tafauti; kinyume, vyenginevyo; tafauti na; kinyume cha, pamoja na; sivyo; na mengineyo, n.k.; ujaji wa mtu baada ya.” El-Jar (1973:503).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hili katika lugha hiyo ya Kiswahili, muundo wake wa msingi ni [*halafu*].

Kwa upande wa maana, kwenye Kiswahili neno hilo linamaanisha “baada ya, kesho, baadaye.” BAKIZA (2010:109), KKS (2004:106)

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Kwenye neno hili kuna sauti kikwamizi kaakaa laini [*x*] kisicho cha ghuna, katika muundo wa msingi mwanzo wa neno kwenye Kiarabu, imebadilika na kuwa [*h*]. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu chini /*a*:/ katikati kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo ya Kiswahili. Tatu, kuna ufinyu semantiki; neno hili kwenye Kiswahili limechukua maana finyu zaidi kuliko kwenye Kiarabu, ufinyu huo kimaana ni kule kujiegemeza zaidi kwenye maana za neno hili zinaonekana kubeba dhana moja tu nayo ni baadaye .

Halahala *الله الله*: Kwenye Kiarabu, neno hilo linaanzia kwa kipasuo koo ² chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi mbenuo *l* chenye irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia tena kwa kipasuo koo ² chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi mbenuo *l* na irabu fupi mbele chini *a* na

kikwamizi koromeo *h* . Katika lugha hiyo ya Kiarabu, neno hili muundo wake wa msingi ni /^ʔ*alaʔalah* /.

Kwa upande wa maana, neno ^ʔ*ala* hilo lina maana ya “jina ladhati yenye wajibu/ lazima ya kuwepo yaani Mwenyezi Mungu mwenyekuabudiwa.” El-Jar (1973:155). Linapojitokeza katika sura hii ya kujirudia inaonesha hali nzima ya kutilia nguvu jambo. Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia kwa kujirudia tena kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a*. Kwenye Lugha hiyo ya Kiswahili neno hilo muundo wake wa msingi ni /*halahala*/.

Kwa upande wa maana, neno hili katika lugha hiyo ya Kiswahili linamaanisha “tamko la kumsisitiza mtu asisahau jambo au kufanya jambo.” BAKIZA (2010:109)

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadilikonsonanti. Katika neno hili kuna sauti kipasuo koo [ʔ] chenye ghuna, kwenye muundo wa msingi mwanzo wa neno kwenye Kiarabu; sauti hiyo imebadilika na kuwa [h] katika Kiswahili. Pili, kuna ubadili semantiki; dhana ya neno hili kimaana ni “himizo kwa lengo la kusesitiza mhusika wa jambo kutosahau.”

Halbadiri *أهل بدر*: Katika Kiarabu neno hili linatokana na mjengeko wa maneno mawili, la kwanza ni ^ʔ*ahlu* ambalo linaanzia kwa kipasuo koo ^ʔ chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kipasuo koo *h* chenye ghuna na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hilo lina maana ya “jamaa, watu wa mtu wa

karibu; wahusika wa” Ibnu Mandhour (... : 28 Juz.xi). Neno la pili ni *badri* ambalo linaanzia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kipasuo ufizi meno *d*, chenye ghuna na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Lina maana ya “kisima cha mtu aliyejulikana kwa jina la badru, tukio la vita vilivyotokea hapo”. Ibnu Mandhour (... : 48 Juz.iv). Kwa hivyo maneno hayo yanajitokeza katika mjengeko wa neno moja *ahlubadri* kama kijalizo (adjunct) na kimilikishi (genitive). Mjengeko wa msingi wa neno hili ni */ahlubadr/*.

Neno hilo kwenye lugha hiyo ya Kiarabu, lina maana ya “watu mahsusi aliowasifu na kuwaridhia Mwenyezi Mungu ambao walishiriki katika vita vya mwanzo baina ya washirikina wa kikureish na Waislamu mahali paitwapo Badri.”

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna na kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni */halbadi/*.

Kwa upande wa maana, neno hilo linamaanisha “kisomo kinachoaminiwa kuwa humdhuru mkosa anayesomewa kwa uovu alioufanya.” BAKIZA (2010: 109).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika neno hili kuna sauti kipasuo koo [ʔ] chenye ghuna, kwenye muundo wa msingi mwanzo wa neno kwenye Kiarabu; sauti hiyo imebadilika na kuwa [h]. Pili, kuna uwekaji konsonanti mkusanyiko; neno hili limekubali kuwepo mkusanyiko

konsonanti /lb/ katikati ya neno hilo. Tatu, kuna uongezaji irabu /i/ ili kuondoa mkusanyiko wa konsonanti /dr/ mwisho wa neno hili. Nne, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata uhamishi kamili wa maana tafauti na ile ya Kiarabu. Neno hili limechukua maana hiyo mpya inayojikita katika kisomo chenye kuleta madhara kwa anayenuiliwa kutokana na uovu alioutenda.

Hali *حالي* : Kwenye Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h̄* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu mbele chini *a*: na kumalizikia kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna na irabu fupi nuima juu *u na nazali n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*h̄a:l*/.

Neno hilo katika lugha hiyo ya Kiarabu, linamaanisha “namna sifa na umbo la jambo lilivyo; jinsi vile mtu alivyo iwe vizuri au vibaya; wakati uliopo hivi sasa; dongo laini, jivu moto; kigari kinachotumiwa kumfundishia mtoto kwenda; namna ya kasi ya uondokaji k.m. wa baridi, joto, ukavu au mnyevu; nafasi; mtatuzi wa tatizo.” El-Jar (1973:424).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. neno hili muundo wake wa msingi ni / *hali*/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiswahili neno hilo linamaanisha, “kadiri ya mambo yanavyoonekana; dhati ya kiafya; uwezo wa kiuchumi; tamko linaloonesha uwiano wa hali mbili za jambo.” BAKIZA (2010:109).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika neno hili kuna badiliko la sauti kikwamizi koromeo [ħ] kisicho cha ghuna, kwenye muundo wa msingi mwanzo wa neno kwenye Kiarabu; sauti hiyo imebadilika na kuwa [h]. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu nyuma chini /a:/ katikati kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu; irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu; kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno. Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Nne, kuna ufinyu semantiki; neno hili kwenye Kiswahili limechukua maana finyu zaidi kuliko kwenye Kiarabu. Ufinyu huo kimaana ni kule kujiegemeza zaidi kwenye dhana ya uwiano wa hali mbili za jambo pamoja na dhati ya kiafya tu.

Haluwa *حلاوة* : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo ħ kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kitamabaza ufizi *l* kisicho cha ghuna na irabu ndefu chini *a*: na kiyeyushi midomo *w* na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na *nazali n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */ħala:wah/*.

Kwa upande wa maana, katika Kiarabu neno hilo lina maana ya “utamu, kinyume cha uchungu; uzuri; furaha.” El-Jar (1973:462), Ibnu Mandhour (... :191 Juz. xiv).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi *a* na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kuishia kiyeyushi midomo *w* chenye irabu fupi *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni */haluwa/*.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “chakula kinachotokana na uwanga, samli, sukari na viungo vyenginevyo.” BAKIZA (2010:109), KKS (2004:107).

Mabadiliko ya neno hili baada kwisha kuingaia katika Kiarabu, kwanza, kuna ubadili konsonanti; mwanzo wa neno hili kuna konsonanti sauti kikwamizi koromeo kisicho cha ghuna [*ħ*] kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, sauti hiyo imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo chenye ghuna [*h*] kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wake wa msingi wa neno hili kuna irabu fupi nyuma juu */u/* mwisho wa neno; irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi chini */a/* kwenye Kiswahili. Tatu, kuna semantiki hamishi, neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili ambayo ina mwelekeo na uhusiano wa maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita katika chakula maalumu cha mchanganyiko wa uanga, sukari, samli na viungo vyenginevyo.

Haraka *حركة*: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *ħ* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na *nazali n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu

mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*ḥarakah*/.

Neno hilo lina maana ya “ kinyume cha kutulia, mwendo, mwendo wa kitu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine.” Ibnu Mandhour (....: 140 Juz. x), El-jar (1973:441).

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*haraka*/.

Neno hili lina maana ya “upesi, chapuchapu, hima, halan.” KKS (2004:109), bakiza (2010:111).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kikwamizi koromeo /*ḥ*/ . Sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo /*h*/ . Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu mwisho lina irabu /*u*/ . Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi chini /*a*/ . Tatu, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili ambayo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita zaidi kwenye kasi.

***Harakati* حركات** : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi koromeo *ḥ* isiyo ya ghuna yenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na

irabu fupi chini *a*, na kujiwa na kipasuo kidakaonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu chini *a*: na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* pamoja na nazi ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*haraka:t*/.

Katika Kiarabu neno hili lina maana ya “miondoko au myendo ya kitu kutoka kilipo na kusogea pengine.” El-jar (1973:441).

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kipasuo kidaka tonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*harakati*/.

Kwenye Kiswahili neno hili lina maana ya “juhudi zinazofanywa na watu kwa ajili ya kufikia lengo fulani, pirikapirika pamoja na shughuli za jambo fulani; mapambano; shughuli za kazi za nchi, serikaki n.k.” KKS (2004:109), BAKIZA (2010:111).

Mbadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kikwamizi koromeo /*ħ*/ . Sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo /*h*/ . Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi katikati lina irabu ndefu chini /*a*/ . Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Tatu, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu, mwisho lina irabu fupi nyuma juu /*u*/ . Irabu hiyo katika

Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu /i/. Nne, kuna upanuzi semantiki, neno limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyo kwenye Kiarabu; pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana ya bidii, pirika za mambo pamoja na shughuli za nchi.

Hiari **خياري** : Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa sauti kikwamizi kaakaa laini *x* isiyo ya ghuna yenye irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kiyeyushi kaakaa gumu *y* chenye irabu ndefu chini *a*: na kuishia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*xiya:r*/.

Katika Kiarabu neno hilo lina maana ya “kuchagua; haki ya kuchagua; uhuru wa kuchagua; jambo bora; tango.” El-Jar (1973:513).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa sauti kikwamizi koromeo *h* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hili muundo wake wa msingi /*hiari*/.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “kukubali bila ya kulazimishwa, ridhia, fanya ridhaa; uchaguzi wa kutenda bila ya kulazimishwa, ridhaa.” KKS (2004:114).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti, mwanzo wa neno hili kuna konsonanti sauti kaakaa laini isiyo na ghuna [x] kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu; sauti hiyo imebadilika na kuwa sauti kikwamizi koromeo chenye ghuna [h] na kiyeyushi kaakaa /y/ kimebadilika na kuwa

irabu fupi chini /a/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu chini /a:/ katikati kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo ya Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wake wa msingi wa neno hili kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno; irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Nne, kuna upanuzi semantiki; neno limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyo kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu, pia neno hili limezidi upeo wa maana.

Hijabu **حجاب** : Neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nbele juu *i* na kufuatiwa na kikwamizi kaakaa gumu *ǧ* chenye ghuna na irabu ndefu chini *a*: na kumalizikia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */hidʒa:b/*.

Katika Kiarabu neno hili lina maana ya “pazia, kizuizi; nchani, pembeni; chochote kile kinachokaa na kuzuia baina ya vitu viwili; sehemu ya mlima iliyojitokeza; hirizi ivaliwayo kama kinga dhidi ya ubaya au silaha.” Ibnu Mandhour (... : 298: juz. i), El-Jar (1973:432).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi juu mbele *i* na kufuatiwa na kikwamizi kizuiio kaakaa gumu *ʃ* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kipasuo midomo chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hili muundo wake wa msingi ni */hijabu/*.

Katika Kiswahili, neno hili lina maana ya “ugonjwa wa kichwa unaoandamana na maumivu; vazi la wanawake lenye stara ya mwili; kitambaa kinachofunika kichwa na mabega huvaliwa na wanawake.” KKS (1973:114).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; mwanzo wa neno hili kuna konsonanti sauti kikwamizi kisicho cha ghuna [ħ]. Sauti hiyo imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo chenye ghuna [h] kwenye Kiswahili. Vilevile, sauti kikwamizi kaakaa gumu katikati ya neno hili [ʔ] imebadilika na kuwa kikwamizi kizuio kaakaa [ʃ]. Pili, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu chini /a:/ katikati kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu; irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo ya Kiswahili. Tatu, kuna upanuzi semantiki; neno limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyo kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu, pia neno hili limezidi upeo wa maana inayojikita kwenye ugonjwa wa kichwa; kitambaa kinachofunika kichwa na mabega kivaliwacho na wanawake.

Hima ^{هيماء} : Neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa kikwamizi koo *h* chenye ghuna na irabu fupi juu *i* na nazali midomo *m* yenye mkazo na ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*himah*/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hili linamaanisha “jambo lenye kutia ari ya kutendwa; matamano, utashi; azma; juhudi, bidii; ukakamavu, nguvu; kusudio kubwa; mtu mzima au mzee anayemalizika.”El-Jar (1973:1258).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* na irabu fupi mbele juu *i* na nazali midomo *m* na irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*hima*/.

Kwa upande wa maana, linamaanisha “upes, haraka, mbio; bidii, ari, nguvu.” KKS (2004:115).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, mosi, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa /a/. Pili, kuna ufinyu semantiki, neno hili kwenye Kiswahili limechukua maana finyu zaidi kuliko ile ya kwenye Kiarabu.

Halan 𐎧𐎡𐎴: Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu mbele chini *a*., na kufuatiwa na kitambaza ulimi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia kwa nazali ufizi *n* yenye ghuna. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*ha:lan*/.

Neno hilo linamaanisha “sasa hivi,punde, ghafla, mara moja, moja kwa moja; palepale.” BAALBAKI (2003: 448).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a*, na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia kwa nazali ufizi *n* yenye ghuna. Neno hilo muundo wake

wa msingi ni [*halan*], na linamaanisha “mara moja; papo hapo; bila ya kukawia; sasa hivi; upesi, haraka.” KKS (2004:106), BAKIZA (2010:109).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu, neno hili mwanzo lina sauti konsonanti /ħ/. Sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa /h/. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu mbele juu /a:/ mwanzoni mwa muundo wake wa msingi. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Kisemantiki hakuna badiliko lolote; dhana inayobeba maana katika Kiswahili ni kama ileile iliyoko kwenye Kiarabu.

Hayati *حياة* : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo ħ kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kiyeyushi kaakaa gumu *j* na irabu ndefu chini *a*: na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /ħaja:h/.

Neno lina maana ya “harakati za viungo vya mwili wa kiumbe katika hali ya kufanya kazi na kukua; muda wa mtu baina ya kuzaliwa mpaka kufikia kufa, kinyume cha mauti.” El-Jar (1973:473).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kiyeyushi kaakaa gumu *j* na irabu fupi chini *a* na kuishia kipasuo ufizi *t*

kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni */hayati/*.

Neno hilo lina maana ya “mtu ambaye ameshafariki, marehemu.” BAKIZA (2010: 114) , KKS (2004: 112).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi, lina irabu refu chini */a:/* katikati. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu neno hili limeishia irabu fupi nyuma juu */u/*. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu */i/*. Tatu kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili ambayo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita zaidi katika mtu aliyekwisha fariki, lakini kwa kuzungumzia aliyonena au aliyotenda wakati wa uhai wake.

***Heshima* حشم** : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h̄* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kikwamizi kaakaa gumu ufizi *f* chenye mkazo kisicho cha ghuna chenye irabu fupi *a* na kuishia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */hafam/*.

Neno hilo kwenye Kiarabu linamaanisha “kutia haya; kuona haya na kujizuia; kuudhi na kutoa maneno mabaya.” Ibnu Mandhour (... :135: juz.xii), BAALBAKI (2003:473).

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi kati juu ε , na kufuatiwa na kikwamizi kaakaa gumu ufizi *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa nazali midomo yenye ghuna *m* na irabu fupi chini *a*. Neno hili muundo wake wa msingi ni */hefima/*, na lina maana ya “thamani ya utu; utukufu, darja ya juu; staha, adabu, nidhamu; kitu apewacho mtu kama alama ya kuthaminiwa kwake.” KKS (2004:114) , BAKIZA (1973:117).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kikwamizi koromeo */ħ/*. Sauti hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo */h/*. Pili, kuna uimarishi irabu; kwenye muundo wa msingi neno hili irabu yake ya mwanzo ni fupi chini */a/*. Katika Kiswahili irabu hiyo imeimarishwa na kuwa irabu ya kati juu */ε/*. Tatu, kuna udondoshi kononanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili katikati lina sauti konsonanti */ff/* yenye mkazo inayoashiria kuwa ni konsonanti radidi/kariri */fff/*; moja kati ya hizo imedondoshwa. Nne, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi, irabu ya pili ni fupi chini */a/*. Irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi juu */i/* katika Kiswahili. Tano, kuna upanuzi semantiki; neno hili limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyoko kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana pana zaidi ambayo imejikita katika kustahi, atia ya thamani na utukufu kwa mtu.

Hirizi *حريز* : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *ħ* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*, na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na kuishia kwa

kikwamizi ufizi z chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/hirz/$.

Neno hili lina maana ya “mahali penye ngome pasipofikika; kinga; fungu,sehemu.” El-Jar (1973:440).

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i , na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi z chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i . Neno hilo muundo wake wa msingi ni $/hirizi/$.

Neno hili lina maana ya aina ya “kinga inayotengenezwa kwa karatasi na kuandikwa maandishi maalumu ndani yake na kukunjwa vizuri na kushonewa kitambaa cheusi au ngozi, huvaliwa mwilini; azima; talasimu.” BAKIZA (2010:117), KKS (2004: 115).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu, neno hili mwanzo lina sauti konsonanti $/h/$. Sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa $/h/$. Pili, kuna uongezaji sauti irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katikati ya neno kuna konsonanti mkusanyiko $/rz/$. Irabu fupi mbele juu $/i/$ iliongezwa ili kuondoa mkusanyiko huo. Tatu, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu neno hili limeishia kwa irabu fupi nyuma juu $/u/$. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu $/i/$. Nne, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili, umejikita zaidi kwenye kinga ivaliwayo mwilini.

Hodhi حوض : Neno hili katika Kiarabu, linaanzia kwa kikwamizi koromeo \hbar kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kiyeyushi midomo w na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi \dot{d} chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/\hbar w \dot{d} n/$.

Neno hilo lina maana ya “mahali yanapokusanyika maji; sehemu ya ndani ya sikio yenye mkunjo; ukuta na kizuizi cha meli dhidi ya upepo na mchafuko wa bahari.” BAALBAKI (2003:494).

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi nyuma ɔ , na kufuatiwa na kikwamizi meno \dot{d} chenye ghuna na irabu fupi mbele i . Neno hili muundo wake wa msingi ni $/hodhi/$.

Neno lina maana ya “shimo lililochimbwa au kujengwa na kusakafiwa kwa ajili ya kuhifadhia maji; kitendo cha kukusanya na kumiliki kitu kwa wingi.” BAKIZA (2010 :118).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu. Neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kikwamizi koromeo $/\hbar/$; sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo $/h/$. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu lina irabu pacha $/aw/$. Kwenye Kiswahili irabu pacha hiyo imebadilika na kuwa fupi nyuma $/ɔ/$. Vilevile kwenye Kiarabu neno hili limeishia kwa irabu fupi nyuma juu $/u/$; irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu $/i/$. Tatu,

kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili mwisho lina sauti konsonanti kipasuo meno ufizi /d̄/; sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi meno /ð/. Nne, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili, umejikita zaidi kwenye shimo lililojengwa kwa ajili ya kuhifadhia maji na vilevile kukusanya na kumiliki kitu kwa wingi.

Ijazi /إجازة/: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo koo² kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kipasuo kaakaa gumu dz chenye ghuna na irabu ndefu *a*: na kuishia kwa kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na *nazali n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /²ija:zah/.

Katika Kiarabu neno hilo lina maana ya “ruhusa au idhini kwa maandishi au kwa maneno, ruhusa ya kufanya biashara ya aina ya bidhaa zilizokuwa si huru; Shahada ya Chuo Kikuu atunukiwayo mhusika baada ya kukamilisha masomo.” El-Jar (1973:22).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kikwamizi kizuio kaakaa gumu J chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni [ijazi].

Kwenye Kiswahili, neno hili lina maana ya “maji maalumu ya sheikh au mwalimu wa dini ya Kiislamu anayompa mwanafunzi wake na kumruhusu asomeshe; idhini ya kutenda jambo lililo na dhima hususan katika dini, ufafanuzi wa kutumia jambo kwa radhi ya mwenye kujua.” KKS (2004 :122)

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, mosi, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu; neno hili lina sauti konsonanti /ʔ/. Sauti konsonanti hiyo imepata mbadala wa irabu /a/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu chini /a:/ kwenye muundo wake wa msingi. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Tatu, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Nne, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya ina mwelekeo na uhusiano kwa kiasi fulani na maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita zaidi kwenye maji maalumu ya sheikh au mwalimu wa dini ya Kiislamu anayompa mwanafunzi wake na kumruhusu asomeshe; idhini ya kutenda jambo lililo na dhima hususan katika dini.

Itikadi **عقائد** /: Kwenye Kiarabu neno hili, linaanzia kwa kipasuo koo ^ʔ chenye irabu fupi mbele juu *i* na sauti kikwamizi koromeo ^ʕ yenye ghuna na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kipasuo kidakatonge *q* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu chini *a:* na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /ʔiʕtiqa:d/.

Kwa mukatdha wa maana, kwenye Kiarabu neno hilo lina maana ya “imani au fikra juu ya jambo, mawazo; maamuzi.” BAALBAKI (2003:129).

Katatika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa irabu fupi mbele juu *i* na kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*, na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /itikadi/.

Katika Kiswahili lina maana ya “imani; mawazo fulani ambayo ni misingi ya nadharia za mila, mfumo wa kisiasa au kiuchumi.” KKS (2004 :125).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika neno hili kuna sauti kipasuo koo [ʔ] chenye ghuna, kwenye muundo wa msingi mwanzo wa neno hili kwenye Kiarabu; sauti hiyo imebadilika na kuwa [i]. Pili, kuna udondoshi konsonanti; sauti kikwamizi koromeo [ʕ] iliyoko mwanzoni mwa neno hili imedondoshwa. Tatu, kuna ubadili irabu kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno hili, irabu hiyo imebadilika na kuwa mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Nne, kuna upanuzi semantiki. Neno hilo limeongezeka wigo wake wa maana kwa kubeba zaidi dhana za mfumo wa kisiasa na kiuchumi.

Jasiri *جَسَار* : Kwenye Kiarabu neno hilo linaanzia kwa sauti kikwamizi kaakaagumu *ǰ* yenye ghuna na irabu fupi *a* na kikwamizi kaakaa ufizi *ʕ* chenye mkazo kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu chini *a*: na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /ǰaʕa:r/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hili lina maana ya “shujaa mwenye nguvu ya kukabili jambo gumu au zito.” BAALBAKI (2003 :423).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kizuio kaakaa gumu *J* chenye ghuna na irabu fupi nyuma *a* na kikwamizi kaakaa *s* kisicho cha ghuna na kuishia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi juu mbele *i*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*jasiri*/.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “mtu mwenye moyo wa kishujaa.” KKS BAKIZA (2010 :129), KKS (2004 :129).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; katika muundo wake wa msingi neno hili lina sauti mkazo ambayo ni konsonanti kariri/radidi /*ss*/, moja kati ya hizi imedondoshwa. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu ndefu chini /*a*/ katikati ya neno; irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi juu /*i*/. Vilevile kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi chini /*u*/ mwisho wa neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa /*i*/. Tatu, kisemantiki kuna tafauti ndogo sana ya kimaana nayo ni nguvu ya kukabili jambo.

Jazba *جَبَّة*: Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kaakaa gumu *dʒ* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi meno *ð* chenye ghuna na kuishia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kipasuo *t* ufizi kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na *nazali n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini

ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*jaḍbah*/.

Kwenye Kiarabu neno hili linamaanisha “mvuto; masafa marefu; kipande cha kitu.” El-Jar (1973:384).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kizuio kaaka gumu *J* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi kaaka ufizi *z* chenye ghuna na kuishia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*jazba*/.

Neno hili lina maana ya “madadi au mori unaomsababisha mtu kutenda jambo bila ya kufikiri au kujali matokeo yake.” BAKIZA (2010 :127).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu; neno hili lina sauti konsonanti kikwamizi /*ḍ*/ sauti konsonanti hiyo imebadilika na kuwaa /*z*/ kwenye Kiswahili; vilevile kuna tafauti ndogo ya matamshi kama ilivyoainishwa hapo juu. Pili, kuna uwekaji konsonanti mkusanyiko; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, kuna konsonanti mkusanyiko /*ḍb*/ katikati. Mkusanyiko huo umebakia katika Kiswahili ukiwa na konsonanti /*z*/ . Tatu, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wake wa msingi wa neno hili kuna irabu fupi nyuma juu /*u*/ mwisho wa neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele chini /*a*/ kwenye Kiswahili. Nne, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita zaidi kwenye mori na mdadi bila kuzingatia matokeo yake.

Karibu **قرب**: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo koromeo *q* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juum *u*, na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na kumalizikia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kuishia kwa nazali meno ufizi *n* yenye ghuna. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*qurb*.

Kwenye Kiarabu neno hili linamaanisha “kinyume cha mbali, karibu; nyonga, kiuno.” El-Jar (1973:971).

Kwenye Kiswahili linaanzia kwa kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kuishia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*karibu*/ na linamaanisha “siyo mbali kwa wakati au mahali; iliyo karibia; nusura; kiasi cha kukadiria; neno litumiwalo kumwitikia mtu aliyebisha hodi; neno linalotumiwa kumuaga mtu anayeondoka.” KKS (2004 :146), BAKIZA (2010 :146).

Mbadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kipasuo koo /*q*/. Sauti hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa kipasuo kidakatonge /*k*/. Pili, kuna uongezaji sauti irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili mwisho kuna konsonanti mkusanyiko /*rb*/. Irabu fupi mbele juu /*i*/ imeongezwa kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Tatu kuna upanuzi semantiki; neno hili limepata

maana jumuishi kuliko ile maana iliyoko kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana pana zaidi kimaana ambayo imejikita katika hali ya kutokuwa mbali kwa wakati au mahali, nusura, ukadiriaji, jawabu ya mwitiko wa ubishaji hodi, uagaji kwa aondokaye.

Karama كرامة: Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo kidaka tonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu ndefu chini *a*: na kufuatiwa na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /kara:mah/.

Kwa muktadha wa maana, kwenye Kiarabu lina maana ya “hadhi, heshima, ubora wa darja; miujiza.” El-Jar (1973:991).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia vilevile kwa kipasuo kaakaa laini *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /karama/.

Kwenye Kiswahili, neno hili lina maana ya “mambo makubwa ayatendayo mtu kinyume na kawaida.” KKS (2004 :145), BAKIZA (2010 :145).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, mosi, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu mbele chini /a:/ katikati kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno hili. Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele chini /a/. Tatu kuna semantiki hamishi; neno hili limepata uhamishi kamili wa maana tafauti na ile ya Kiarabu, neno hili limechukua maana hiyo mpya yenye mfumbato uliojikita katika ufanywaji wa mambo kinyume na kawaida.

Kikataa *قطعة*: Neno hili kwenye Kiarabu linaanzia kwa sauti kipasuo koromeo *q* isiyo ya ghuna yenye irabu fupi fupi juu mbele *i* na kipasuo meno ufizi mtandazo *t* kisicho cha ghuna na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *ç* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*qitçah*/.

Kwa muktadha wa maana, katika Kiarabu neno hilo lina maana ya “kipande cha kitu chochote.” El-Jar (1973:958).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu chini *a*:. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*kikataa*/.

Katika Kiswahili, neno hilo lina maana ya “sehemu au kijipande cha ardhi kinachomilikiwa chenye miti.” BAKIZA (2010:166).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; katika muundo wake wa msingi neno hili lina sauti kipasuo koromeo *q* sauti hiyo imebadilika na kuwa kipasuo kidakatonge *k* kwenye Kiswahili. Pili, kuna uongezaji sauti, kabla ya mkusanyiko wa konsonanti /tʃ/ zimeongezwa sauti [k] na [i] kwenye Kiswahili. Vilevile baina ya mkusanyiko huo wa konsonanti imetiwa sauti irabu [a] ili kuondoa mkusanyiko huo. Tatu, udondoshi konsonanti; mwisho wa neno hili kuna konsonanti sauti koromeo [ʔ], sauti hiyo imedondoshwa na kubaki irabu *a* kwenye Kiswahili. Nne, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya ina mwelekeo wa maana iliyotangulia. Maana ya kwenye Kiswahili imeegemea zaidi kwenye kipande cha ardhi kilichomilikiwachenye miti.

Kuduhushi دهش: Katika Kiarabu, neno hilo linaanzia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi kaakaa gumu *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. Kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /dahaf/.

Kwa upande wa maana katika lugha hiyo ya Kiarabu, lina maana ya “shangaza, rusha akili, emewa, dwaa”. El-Jar (1973), Ibn Mandhour (... :303 Juz. vi).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi

nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kumalizikia kwa kikwamizi kaakaa gumu *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni */duhufi/*.

Kwenye Kiswahili, neno hilo lina maana ya “peleleza; kitendo cha kutunza kitu au mtu.” BAKIZA (2010).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu lina irabu fupi nyuma chini */a/* zote tatu. Kwenye Kiswahili, irabu mbili za mwanzo zimebadilika na kuwa irabu fupi nyuma juu */u/* na ile ya mwisho imekuwa fupi mbele juu */i/*. Pili, kuna semantiki hamishi, neno hili limepata uhamishi kamili wa maana ambayo ni tafauti na ile ya Kiarabu. Neno hili limechukua maana mpya ambayo imejikita kwenye kupeleleza na kutunza.

***Kukashifu* كشف** : Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa sauti kipasuo kidaka tonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kikwamizi ufizi kaakaa *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */kaʃaf/*.

Katika upande wa maana, neno hilo kwenye Kiarabu linamaanisha “onesha kilichokuwa kimejificha, ondoa.” El-Jar (1973:1000).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye

irabu fupi chini *a* na kikwamizi ufizi kaakaa *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kuishia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni */kukashifu/*.

Katika Kiswahili, neno hilo lina maana ya “kitendo cha kumtendea mambo ya jinsia mtoto ambaye hajabaleghe; kuambia maneno mabaya yasiyopendeza.” BAKIZA (2010:147), KKS (2004:147).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi chini */a/* katikati ya neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa ya juu mbele */i/* kwenye Kiswahili. Vilevile kuna irabu fupi chini */a/* mwisho wa neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi nyuma juu */u/* kwenye Kiswahili. Pili, kuna semantiki hamishi, neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo wa maana iliyotangulia. Maana hiyo ya kwenye Kiswahili imeegemea zaidi kwenye kumtendea mtoto asiye baleghe mambo ya kijinsia na kuambia maneno yasiyopendeza.

***Kukinai* قنع**: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo kidakatonge *q* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kikwamizi koromeo ^ʿ chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */qana^ʿ/*.

Neno hilo kwenye Kiarabu lina maana ya “omba na kuwa mnyonge; elekea, enda kwenye makao ya; zuia na nyima lile alitakalo; kuto tarajia na kuto taka lile asilokuwa nalo mhusika, tosheka.” El-Jar (1973: 971).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kipasuo kaakaa laini *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*kukinai*/.

Kwenye Kiswahili, neno hilo lina maana ya “kutosheka au kuridhika na kitu ulichonacho; kukosa hamu ya kufanya zaidi jambo fulani baada ya kulifanya au kukila chakula fulani mara nyingi cha kutosha.” BAKIZA (2010:172).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuinga katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti, kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu; neno hili lina sauti konsonanti /q/ mwanzo wa neno, sauti konsonanti hiyo imepata mbadala wa sauti konsonanti /k/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kuna irabu fupi chini /a/ mwanzo wa neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Vilevile mwisho wa neno hili kwenye Kiarabu lina irabu fupi chini /a/, irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi mbele juu /i/ katika Kiswahili. Tatu, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili umejikita katika kutosheka na kukosa hamu ya jambo baada ya kulitenda kwa wingi.

Kopo كوب: Neno hili kiasili, sio la Kiarabu. Limeingia kwenye Kiarabu kutoka kwenye Kifursi. Kwa hivyo neno hilo, kwenye Kiarabu linaanzia kwa kipasuo kaakaa laini *k*

kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kiyeyushi midomo *w* na kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*kawb*/.

Neno hili kwenye Kiarabu lina maana ya “gilasi isiyo kuwa na mkono wa kukamatia.” El-Jar (1973: 1013).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kipasuo kidaka tonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi kati nyuma juu *ɔ* na kufuatiwa na kipasuo midomo *p* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi kati nyuma juu *ɔ*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*kopo*/.

Kwenye Kiswahili, neno hilo lina maana ya “chombo cha bati au plastiki kinachochotewa au kutiliwa maji n.k..” BAKIZA (2010 :196),KKS (2004:195).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wake wa msingi mwanzo wa neno hili, kuna irabu pacha /*aw*/, irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi kati nyuma juu /*ɔ*/ kwenye Kiswahili. Vilevile, mwisho kuna irabu fupi nyuma juu /*u*/; irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi kati nyuma juu /*ɔ*/.

Pili, kuna ubadili konsonanti; mwisho wa neno hili kuna konsonanti sauti kipasuo chenye ghuna [*b*]. Sauti hiyo imebadilika na kuwa kipasuo kisicho cha ghuna /*p*/ kwenye Kiswahili. Tatu, kuna semantiki hamishi, neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili ambayo ina mwelekeo na uhusiano wa maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita kwenye chombo kilichotengenezwa kwa bati au plastiki kwa ajili ya kuchotea au kutilia maji.

***Kuasisi* أَسَس**: Neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa kipasuo koo ^ʔ chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *ś* chenye mkazo kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /^ʔaśas/.

Kwenye lugha hiyo ya Kiarabu, neno hilo lina maana ya “anzisha, anza; weka msingi, jenga, unda; panga, fanya.”

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na irabu fupi mbele chini *a* na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni /kuasisi/.

Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo lina maana ya “kitendo cha kuanzisha kitu au jambo la kudumu.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna badiliko la ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno kuna konsonanti /^ʔ/ sauti hiyo [^ʔ] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imepata badili /a/ kwenye neno hilo la Kiswahili. Pili, kuna udondoshi konsonanti, katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno hili kuna konsonanti radidi/kariri /ss/, kwa hivyo konsonanti moja kati ya hizo imedondoshwa katika Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa

neni hili kwenye Kiarabu kuna irabu fupi chini mbele /a/, kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Nne, kuna semantiki hamishi, kwenye neno hili umetokea uhamishaji kamili wa maana. Maana ya neno hili inayopatikana kwenye Kiswahili, ina tafauti ndogo lakini ina uhusiano na maana ya mwanzo katika Kiarabu.

***Kuatili* عطل** : Neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa kikwamizi koromeo ^s chenye ghuna na irabu fupi *a* chini mbele na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi *i* mbele juu na kumalizikia kwa kitambaza ufizi *l* chenye irabu fupi *a* chini mbele. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /^satila/.

Kwa upande wa maana katika lugha ya Kiarabu, linamaanisha “kuto kuwa na kitu, taka, hitajia, kuwa na haja na; kaa bila ya kazi, kaa bure, zuia kwa muda; ingilia kati.”

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na irabu fupi *a* chini mbele na kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi *i* mbele juu na kumalizikia kwa kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi *i* mbele juu. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /kuatili/.

Kwa upande wa maana, neno hili katika Kiswahili, linamaanisha “kitendo cha kuharibu mtu, kitu au hali, kudhoofisha.”

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo wa neno kuna konsonanti /^ʔ/ sauti hiyo [^ʔ] haimo katika Kiswahili, kwa hivyo konsonanti hiyo imepata badili /a/ kwenye neno hilo la Kiswahili; na vilevile katikati ya neno hili kuna

konsonanti /t/ sauti hiyo nayo [t] haimo kwenye Kiswahili; kwa hivyo nayo imepata konsonanti badili /t/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kati na mwisho kwenye Kiarabu kuna irabu fupi chini mbele /a/, kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Tatu, kuna ufinyu semantiki, neno hili limepata ufinyu katika maana kwenye Kiswahili. Ufinyu huo ni kule kujikita maana ya neno hili katika kuharibu na kudhoofisha.

Kudabiri دَبِير : Asili ya neno hili ni Kiajemi /*dabir*/ kwa maana ya katibu, meneja. Kwenye Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kipasuo midomo *b* chenye ghuna na mkazo pamoja na irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*dabar*/.

Katika Kiarabu, neno hilo linamaanisha “fuata kwa nyuma ya; patwa na jambo la kuzingatia; andika; pokea hadithi kutoka kwa mtu baada kufa kwake.”

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kipasuo kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Katika lugha hiyo ya Kiswahili neno hili muundo wake wa msingi ni /*kudabiri*/.

Kwa upande wa maana katika Kiswahili, neno hilo linamaanisha “kitendo cha kufikiri juu ya jambo zito; chunguza.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti. Neno hili lina konsonanti radidi/kariri /bb/ katikati kwenye muundo wa msingi, kwa hivyo konsonanti moja kati ya hizo imedondoshwa katika Kiswahili. Pili, ubadili irabu; katika muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, kati na mwisho wa neno kuna irabu fupi mbele chini /a/. Kwenye Kiswahili, irabu hizo zimebadilika na kuwa za mbele juu /i/. Tatu, kuna ufinyu semantiki; neno hili kwenye Kiswahili limechukua maana finyu zaidi kuliko kwenye Kiarabu; ufinyu huo kimaana umejikita zaidi kwenye kufikiri na kuchunguza tu.

***Kudhili* ذحلي**: Neno hilo kwenye Kiarabu linaanzia kwa sauti kikwamizi meno *ḍ* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kitambaza meno ufizi *l* chenye mkazo na irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*ḍal*/.

Kwa upande wa maana, katika Kiarabu neno hilo lina maana ya “kudharau na kuona kuwa mtu au kitu ni duni kabisa,-wa -a hali ya chini; fanyia urafiki na upoe” El-Jar (1973), Ibn Mandhour (... :256 Juz. xi).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi meno *ḍ* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*dhili*/.

Kwenye Kiswahili, neno hilo lina maana ya “kupatiha tabu, kusumbua, kudhiki.” BAKZA (2010).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, mosi, kuna udondoshi konsonanti, katika muundo wake wa msingi wa neno hili kuna sauti mkazo ambayo ni konsonanti kariri/radidi /ll/ mwisho, moja kati ya silabi hizi imedondoshwa. Pili, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi chini /a/ mwisho wa neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi juu /i/. Tatu, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana iliyokinyume na ile ya awali kwenye Kiarabu. Maana hiyo mpya imepoteza mwelekeo wa maana iliyotangulia. Maana ya kwenye Kiswahili imeegemea zaidi kwenye dhiki, usumbufu na kupatisha taabu.

***Kudhihaki* ضحك**: Kwenye Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kipasuo meno ufizi \dot{d} chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kikwamizi koromeo \dot{h} kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i na kumalizikia kwa kipasuo kidaka tonge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a . Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/\dot{d}a\dot{h}ik/$.

Kwa upande wa maana, neno hilo kwenye Kiarabu lina maana ya “cheka; tania, fanyia mzaha; toa sauti hasa kima; mweka; ng’ara; staajabu.”

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kipasuo kidakatonge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na kufuatiwa na kikwamizi meno \dot{d} chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kufuatiwa na kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kipasuo kidakatoge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i . Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni $/kudhihaki/$.

Kwa muktadha wa maana, neno hilo katika Kiswahili lina maana ya “kitendo cha kumfanyia mtu mzaha, tania; kitendo cha kumdharau mtu.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika neno hili kuna badiliko la sauti, kwenye muundo wa msingi wa neno hilo katika Kiarabu konsonanti ya kwanza ni sauti kipasuo meno ufizi [d̥] yenye ghuna, katika Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi meno /ð/ chenye ghuna; vilevile kuna sauti kikwamizi koromeo [h̥] isiyo ya ghuna, nayo katika Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo /h/ chenye ghuna. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu kuna irabu fupi nyuma mbele /u/ mwisho wa neno hili. Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Tatu, kuna ufinyu semantiki, neno hili kwenye Kiswahili limechukua maana finyu zaidi kuliko kwenye Kiarabu, ufinyu huo kimaana umejikita zaidi kwenye utani na dharau.

Kufa *توفى*: Katika Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiw na kiyeyushi midomo *w* na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye mkazo na irabu ndefu chini *a*: Kwenye lugha hiyo ya Kiarabu neno hilo muundo wake wa msingi ni /*tawafa*:/.

Kwa upande wa maana, neno hili linamaanisha “fisha; chukua kikamilifu; kamilisha; andaa, tayarisha.” Moustafa (--):1047 Juz. II; El-Jar (1973:355).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi mdomo meno *f* kisicho cha ghuna na irabu fupi chini *a*. Kwenye lugha hiyo muundo wake wa msingi ni /*kufa*/.

Kwa upande wa maana, neno hilo linamaanisha “kitendo cha kutoka uhai; kitendo cha kukosa hisia.” BAKIZA (2010:79).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi wa silabi mbili za mwanzo kwenye Kiarabu *ta* na *wa*. Pili, kuna badiliko la udondoshi konsonanti. Neno hili lina konsonanti radidi/kariri /ff/ mwishoni kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu, kwa hivyo konsonanti moja kati ya hizo imedondoshwa katika Kiswahili. Neno hilo limechukua sura nyengine nayo ni ya silabi moja (Konsonanti Irabu-KI). Tatu kuna ufinyu semantiki, neno hili kwenye Kiswahili limechukua maana finyu zaidi kulikoile ya kwenye Kiarabu, ufinyu huo kimaana ni kule kujiegemeza zaidi kwenye hali ya kutokuwa hai na kukosa hisia.

***Kughafilika* غفل** : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *y* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini *a* na kujiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna na irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni Kwenye lugha ya Kiarabu, neno hilo muundo wake wa msingi ni /*yafal*/.

Katika Kiarabu linamaanisha “sahau; fanya jambo bila ya kukusudia, puuza, kuto kuwa na hadhari; acha kwa kutokukumbuka” El-Jawhariy (--: 22:2).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *y* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi

mbele juu *i* na kujiwa na kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*.

Kwenye Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni /*kughafilika*/.

Kwa muktadha wa maana, neno hilo katika Kiswahili lina maana ya “sahau, pitikiwa.”

BAKIZA (2010:97), KKS (2004: 95).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu katikati kuna irabu fupi chini /*a*/, irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu *i* katika Kiswahili. Vilevile mwisho wa neno hili kwenye Kiarabu kuna irabu fupi chini /*a*/, irabu hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /*i*/. Kuna ongezeko la kimofolojia nalo ni kipashio *ka* mwishoni mwa neno hilo kinachoonesha kauli ya kutendeka wenyewe katika Kiswahili. Pili, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili, umejikita katika kusahau tu.

***Kughani* غنى** : Katika Kiarabu, neno hili linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini *y* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na nazali ufizi *h* yenye mkazo na ghuna na irabu ndefu chini *a*: . Kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*yaña*:/.

Neno hilo linamaanisha “imba, tia irabu, irabisha; imba kwa kusifu, sifu; fanya awe tajiri, tajirisha.” El-Jar (1973:887).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi kidakatonge *y* chenye ghuna na irabu

fupi chini *a* na kufuatiwa na nzali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*ghani*/

Neno hilo katika Kiswahili lina maana ya “kitendo cha kuimba au kusoma kwa kutia madoido ya kurefusha sauti za vokali.” BAKIZA (2010:98).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu, neno hili lina sauti nazali konsonanti /*ḥ*/ yenye mkazo inayoashiria kuwa ni konsonanti radidi / kariri /*nn*/, moja kati ya konsonanti hizo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu mwisho lina irabu ndefu chini /*a*/. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa /*i*/. Tatu, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili, umejikita zaidi kwenye uimbaji na urefushaji hasa wa sauti za irabu.

***Kughasi* غَسَّ** : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini *y* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *ś* kisicho cha ghuna chenye mkazo na irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*yaś*/.

Katika Kiarabu linamaanisha “ingia kwenye mji; toa kasoro au aibu; funika; zamisha; tolea sauti ghis-ghis.” El-Jar (1973: 877) , Fairouzabadi (... : 723 Juz.i).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi kidakatonge *y* chenye ghuna na irabu

fupi chini *a*, na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. Kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni /ghasi/.

Katika Kiswahili neno hili linamaanisha “kera kwa kelele, zogo au maneno yasiyo na maana.” KKS (2004 : 95) , BAKIZA (2010 : 98).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti, kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu; neno hili lina sauti kikwamizi konsonanti /s/ yenye mkazo inayoashiria kuwa ni konsonanti radidi/kariri /ss/. Moja kati ya konsonanti hizo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu mwisho lina irabu fupi chini /a/. Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi mbele juu /i/. Tatu, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili maana ambayo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia, na imejikita zaidi kwenye kero la kelele. Wakati mwengine siku hizi pia linatumika kwa maana ya kuleta fujo.

Kujuzu *جَزْ* : Neno hili katika Kiarabu linatokana na mnyambuliko wa kitenzi *dʒa:za* , *yadʒu:zu*, *dʒawa:zan*, ndani ya mnyambuliko huu likachukuliwa neno *yadʒu: zu* ambalo ni kitenzi cha wakati uliopo; alama ya wakati uliopo ni kile kiambishi cha mwanzo wa neno baada ya kunyambuliwa. Lilipoingia kwenye Kiswahili, ile njeo (alama asilia ya wakati) katika Kiarabu ilidondoshwa na likabakia neno *ju:zu*. Pamoja na kuwa ndani ya Kiswahili Sanifu kama anavyodai Massamba na wenzake (2004:4) hujitokeza kwa kiasi fulani dhana ya irabu ndefu hasa yale maneno yenye irabu mbili za aina moja. Hali hiyo

ya irabu ndefu siyo ya matumizi makubwa na si kwa wingi, kwa hivyo irabu ndefu katika neno *ju:zu* ilifupika kama kawaida neno hilo likawa *juzu*.

Kwa hivyo neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa sauti kipasuo kaakaa gumu *dʒ* yenye ghuna na irabu ndefu chini *a*: kufuatiwa na kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */dʒa:z/*.

Katika Kiarabu linamaanisha “nenda katika; pitiliza, vuka kiwango; tekeleza; ruhusu.” El-Jar (1973 :373).

Kama ilivyo kwisha fafanuliwa hapo juu, kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi kizuio kaakaa guma *J* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni */kujuzu/*.

Kwenye Kiswahili, lina maana ya “pasa, faa, husu, lazimu.” BAKIZA (2010 :136), KKS (2004 :135).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu chini */a:/* katikati kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo ya Kiswahili. Pili, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo wala uhusiano wa maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita katika ufaaji, uhusianifu na ulazima.

Kufariji فَرَج : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi meno mdomo *f* isiyo ya ghuna yenye irabu fupi chini *a*, na kimadende ufizi *r* chenye mkazo na ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi kaakaa gumu *ǧ* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni ni /*fa'arǧ*/.

Katika Kiarabu neno hilo lina maana ya “kutanua, kupanua; kuondoa k.m. huzuni au mawazo”. El-jar (1973:901).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*, na kumalizikia kwa kikwamizi kizuiio kaakaa gumu *f* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*kufariji*/.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “kuliwaza, kupoza mwenzio baada ya kufikwa na msiba; burudisha.” KKS (204: 77).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kweye Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili katikati lina sauti konsonanti /*r*/ yenye mkazo inayoashiria kuwa ni konsonanti radidi/kariri /*rr*/; moja kati ya konsonanti hizo imedondoshwa. Pili, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu irabu ya pili na ya tatu zote hizo ni fupi chini /*a*/. Irabu hizo katika Kiswahili zimebadilika na kuwa fupi mbele juu /*i*/. Irabu ya tatu na ya mwisho imekuwa hivyo kutokana na neno hili limeishia irabu /*u*/ kwenye muundo wake wa msingi katika

Kiarabu. Tatu, takriban kisemantiki neno hili linabeba dhana ileile ya kuliwaza kutokana na masaibu yamfikayo mtu.

***Kugaragara* جر جر** : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi kaakaa gumu *dʒ* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na kufuatiwa tena na kikwamizi kaakaa gumu *dʒ* chenyenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni Neno hili muundo wake wa msingi ni /*dʒardʒar*/.

Katika lugha ya Kiarabu lina maana ya “tetemesha sauti kwenye koo, toa sauti kwenye koo baada ya kufikisha maji.” El-Jar (1973:387);

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na sauti kipasuo kidaka tonge *g* chenye ghuna na irabu fupi chi *a* na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa tena na kipasuo kidaka tonge *g* chenye ghuna na irabu fupi chi *a* na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hili muundo wake wa msingi /*kugaragara*/.

Katika Kiswahili linamaanisha “lala na biringitia juu ya kitu k.m. kitanda, mkeka au ardhini; geuka geuka mahali ulipolala”. BAKIZA (2010:95).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili lina sauti konsonanti /*dʒ*/ mwanzo na katikati ya neno. Sauti konsonanti hiyo imepata mbadala wa sauti konsonanti kipasuo /*g*/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna uongezaji sauti irabu kati chini /*a*/

kwenye konsonanti mkusanyiko /rdʒ/ ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Tatu, kuna semantiki hamishi, neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya kwa kiasi haina mwelekeo wala uhusiano wa maana iliyotangulia na imejikita kwenye kulala na kubiringitia au kugeukageuka mahali penyewe alioplala mhusika.

Kugharimu غرم : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini y chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i , na kumalizikia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi chini a . Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*yarima*/.

Katika Kiarabu neno hili linamaanisha “ lipa / toa faini, kula hasara, pata hasara.” BAALBAKI (2003: 797), El-Jar (1973: 876), Ibnu Mamdhour (... : 436 Juz.xii).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kipasuo kidakatonge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na kufuatiwa na kikwamizi kidakatonge y chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kumalizikia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi nyuma. Neno hilo kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*yarimu*/.

Neno hilo kwenye Kiswahili lina maana ya “kitendo cha kuhitaji kima fulani cha malipo.” BAKIZA (2010 :98).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu katikati lina irabu fupi chini a , kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu /i/. Vilevile kwenye Kiarabu limeishia kwa irabu fupi chini /a/; irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi nyuma juu /u/. Pili, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo wala uhusiano wa maana iliyotangulia nayo imejikita zaidi kwenye kuhitaji thamani kwa ajili ya jambo.

Kughariki غرق : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini y chenye ghuna na irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kumalizikia kwa kipasuo koromeo q kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a . Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni Neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*yariq*/.

Neno hilo linamaanisha “zama, kufa maji; zamakwenye maji Razi (2014).” Ibnu Mamdhour (... : 445 Juz.xii),

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kipasuo kidakatonge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na kufuatiwa na kikwamizi kidakatonge y chenye ghuna na irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kumalizikia kwa kipasuo kidakatonge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i . Neno hili kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*kughariki*/.

Katika Kiswahili lina maana ya “kitendo cha kuzama kutokana na mafuriko au tetemeko la ardhi.” BAKIZA (2010:98).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu mwisho lina irabu fupi chini /a/, kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu /i/. Neno lina dhana ya kitenzi ambacho kimaana kimejikita katika tendo la kuzama au kuangamia kwenye mafuriko au tetemeko. Hakuna badiliko kubwa la kisemantiki.

***Kughilibu* غلب** : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *y* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kitambaza meno ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kuishia kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /yalab/.

Katika muktadha wa maana, neno hili kwenye Kiarabu linamaanisha “kushinda katika jambo au tukio lolote, toza nguvu.” El-Jar (1973: 882).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *y* chenye ghuna na irabu fupi juu mbele *i* na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kuishia kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /yilibu/.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “kushawishi mtu kwa maneno mpaka akubali kufanya jambo.” BAKIZA (2010: 98).

Mabadiliko ya neno hilo baada kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi chini /a/ mwisho wa neno. Irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi nyuma juu /u/. Vilevile irabu ya kwanza na ya pili ambazo ni fupi chini /a/ zimebadilika na kuwa za juu mbele /i/. Pili, kuna semantiki hamishi, neno limepata maana mpya na kwa kiasi kidogo ina uhusiano na ile ya awali kwenye Kiarabu. Maana hiyo mpya ina mwelekeo wa maana iliyotangulia. Maana ya kwenye Kiswahili imeegemea zaidi kwenye kushawishi kwa kutumia maneno mpaka kufanikiwa kufanya jambo.

Kuhajiri هجر : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi koo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi kaakaa *dʒ* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /hadʒar/.

Kwa upande wa maana katika Kiarabu, neno hili linamaanisha “ondoka, acha; tengana na; toka; hamisha, fukuza; nyima makaazi.” El-Jar (1973: 1242), Ibn Mandhour (... : 250 Juz.v).

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi kizuio *ʃ* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Katika lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake msingi ni /hajiri/.

Kwa upande wa maana neno hili katika Kiswahili linamaanisha “kitendo cha mtu kuondoka pao na kuishi pengine; kitendo cha mtu kutengana na mwenzake, gura, hama.” BAKIZA (2010:108).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu; kuna irabu fupi chini /a/ mwanzo, kati na mwisho wa neno hili. Kwenye Kiswahili irabu hizo zimebadilika kati na mwisho na kuwa irabu fupi mbele juu /i/. Pili, kuna ufinyu semantiki; neno hili kwenye Kiswahili limechukua maana finyu zaidi kuliko kwenye Kiarabu, ufinyu huo kimaana ni kule kujiegemeza zaidi kwenye kuhama mahali na kuhamia pengine, mtu kuachana na mwenzake.

***Kuhani* كُهَانِي** : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi koo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na nazali meno ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi *a* na kuishia kwa kipasuo koo [?] chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /hana[?]/.

Kwa muktadha wa maana, neno hilo kwenye Kiarabu lina maana ya “ pata, -ja bila tabu au mashaka; toa hongera, pongeza; -pa.” Ibnu Mandhour (....: 184 Juz. i), El-jar (1973:1259).

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *h* na irabu fupi chini *a*, na nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi juu mbele *i*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /kuhani/.

Kwenye Kiswahili neno hili lina maana ya “toa pole kwa mfiwa, toa taazia.” BAKIZA (2010: 111) , KKS (2004:108).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti. Katika neno hili kuna sauti kipasuo koo [ʔ] chenye ghuna, kwenye muundo wa msingi mwisho wa neno hili kwenye Kiarabu; sauti hiyo imedondoshwa. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi chini /a/ mwisho wa neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa /i/ kwenye Kiswahili. Tatu, kuna semantiki hamishi. Neno limepata maana iliyokinyume na ile ya awali kwenye Kiarabu, maana hiyo mpya imepoteza mwelekeo wa maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita zaidi katika rambirambi.

***Kuhawili* حَوْل** : Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa sauti kikwamizi koromeo *h* isiyo ya ghuna yenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kiyeyushi mdomo *w* chenye mkazo na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*hawal*/.

Kwenye Kiarabu neno hilo lina maana ya “badili, geuza; punguza; hamisha, peleka.” El-Jar (1973: 472).

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kiyeyushi midomo *w* na irabu fupi mbele juu *i* na kuishia kwa

kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni */kuhawili/*.

Katika Kiswahili lina maana ya “kuhamisha kitu au mtu kutoka mahali pamoja kwenda pengine.” KKS (2004: 112), BAKIZA (2010:114).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; mwanzo wa neno hili kuna konsonanti sauti kikwamizi koromeo isiyo ya ghuna [*ħ*] kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu; sauti hiyo imebadilika na kuwa sauti kikwamizi koromeo chenye ghuna [*h*] kwenye Kiswahili. Pili, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu, neno hili lina sauti konsonanti */w/* yenye mkazo. Mkazo huo unaashiria uradidi/ukariri konsonanti */ww/*, kwa hivyo moja kati ya konsonti hizo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu. Kwenye muundo wa msingi wa neno hili kuna irabu fupi chini */a/* mwisho wa neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu */i/* kwenye Kiswahili; pia katikati ya neno kuna irabu fupi chini */a/*, imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu */i/*. Nne, kuna ufinyu semantiki. Ufinyu huo wa maana katika Kiswahili, umejikita katika tendo la kuhamisha mtu, jambo au kitu toka pahali pamoja kwenda pengine.

***Kulaghai* كَلَا**: Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *y* chenye ghuna na irabu ndefu chini *a*: Neno hilo muundo wake wa msingi ni */laya:/*.

Neno hili lina maana ya “sema maneno au jambo lolote lililokuwa halikuzoeleka na si la kwaida au maneno ya kipuuzi; sema ,ongea;apa bila ya kuamini; fanya kosa, kosea; sema mambo siyo.” Ibnu Mandhour (... :250 Juz.xv).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *y* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kiyeyushi kaakaa *j*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*kulaghai*/.

Neno hilo lina maana ya “kudanganya, kufanyia ujanja, kushawishi kwa hila; hali ya kudanganya watu, ” KKS (2004:205).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu neno hili limeishia irabu ndefu chini /a:/. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa kiyeyushi kaakaa /j/. Pili, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili ambayo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia. Imejikita zaidi katika mtu mwenye hila, ujanja na udanganyifu.

***Kusadifu* صدف** : Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kikwamizi ufizi ş mtandazo kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*şadaf*/.

Katika Kiarabu lina maana ya “ondoka; puuza; tumia; mili kwenye jambo.” Ibnu Mandhour (.....:187Juz. ix).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kuishia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*kusadifu*/

Kwenye Kiswahili lina maana ya “kitendo cha kutokea jambo au tukio kwa wakati mmoja na jengine bila ya kutarajia.” BAKIZA (2010:351).

Mabadiliko ya neno hili baada kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti, kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu; neno hili lina sauti konsonanti /*ʃ*/ ambayo imepata mbadala wa sauti konsonanti /*s*/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wake wa msingi neno hili lina irabu fupi chini /*a*/ katikati ya neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /*i*/ kwenye Kiswahili. Vilevile mwisho wa neno hili kwenye Kiarabu lina irabu fupi chini /*a*/, irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi nyuma juu /*u*/ katika Kiswahili. Tatu, kuna semantiki hamishi, neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia na imejikita zaidi katika kutokea kwa jambo moja na jengine wakati mmoja.

***Kusadiki* صدق** : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi ufizi ζ mtandazo kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi d chenye ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kipasuo koromeo q kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a . Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */ṣadaq/*.

Kwenye Kiarabu neno hilo lina maana ya “kuja katika ile hali halisi, timiza na fanya vyema; sema kweli.” El-Jar (1973: 740).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kipasuo kidakatonge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na kufuatiwa na kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kipasuo ufizi d chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kumalizikia kwa kipasuo kidakatonge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i . Neno hili muundo wake wa msingi ni */kusadiki/*, na lina maana ya “kukubali kwamba maneno au kitendo fulani ni kweli, kuamini.” KKS (2004:355).

Mabadiliko ya neno hili baada kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kikwamizi ufizi */s/* na mwisho sauti konsonanti kipasuo koromeo */q/*. Sauti hizo kwenye Kiswahili zimebadilika na kuwa kikwamizi ufizi */s/* na kipasuo kidakatonge */k/*. Pili, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu mwisho lina irabu fupi chini */a/*. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu */i/*. Tatu, kuna, ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili umejikita zaidi kwenye kuamini.

***Kusawijika* اسود** : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo koo ² chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i , na kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna na kiyeyushi midomo w

chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na mkazo na irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /ʔ is-wad/, na lina maana ya “kuwa nyeusi , kupiga weusi.” El-Jar (1973:98).

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na sauti kikwamizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kiyeyushi midomo *w* chenye irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kikwamizi kizuio kaakaa gumu *J* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kuishia kwa kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* . Neno hili muundo wake wa msingi ni /kusawiJika/, na lina maana ya “kubadilika hali na kuwa mbaya kutokana na shida, njaa au ugonjwa; kuonesha uso wa huzuni au hasira” BAKIZA (2010: 357), KKS (2004: 361).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kipasuo koo /ʔ/. Sauti hiyo kwenye Kiswahili imedondoshwa. Pili, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu, katikati na mwisho lina irabu fupi chini /a/. Irabu hizo katika Kiswahili zimebadilika na kuwa fupi mbele juu /i/. Tatu, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu neno hili mwisho lina sauti kipasuo meno ufizi konsonanti /d/. Sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi kizuio kaaka gumu *J* na kuunganika na kiambishi *ka* cha kauli ya kutendeka wenyewe. Nne, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia

ambayo imejikita zaidi kwenye kuonesha huzuni na ubadilikaji wa hali kuwa mbaya kwa sababu ya dhiki, maradhi na njaa.

Kusema *سقى* : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na nazali midomo *m* yenye ghuna na mkazo na irabu ndefu chini *a*:. Neno hili muundo wake wa msingi ni */saʔa/*.

Neno hilo kwenye Kiarabu lina maana ya “kutaja au kuita jina; teua.” BAALBAKI (2003: 643).

Kwenye Kiswahili linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi kati mbele *ε* na kufuatiwa na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni */kusema/*, na lina maana ya “kutamka maneno, kunena, kuamba, kueleza; kutolea maneno makali au ya nasaha; kusengenywa, kuteta.” KKS (2004: 362).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna uimarishi irabu; kwenye muundo wa msingi neno hili irabu yake ya mwanzo ni fupi chini *a*. Katika Kiswahili irabu hiyo imeimarishwa na kuwa irabu ya kati juu */ε/*. Pili, kuna udondoshi kononanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili katikati lina sauti konsonanti */m/* yenye mkazo inayoashiria kuwa ni konsonanti radidi/kariri */mm/*. Moja kati ya konsonanti hizo imedondoshwa. Tatu, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi mwisho lina irabu ndefu chini */a:/*. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Nne,

kuna upanuzi semantiki; neno limepata maana jumuiishi kuliko ile maana iliyoko kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana pana zaidi kimaana ambayo imejikita katika utamkaji maneno, utoaji maneno makali au ya nasaha pamoja na kusengenya.

Kushadidia شَدِيدٌ: Kwenye Kiarabu, neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi kaakaa gumu ufizi *f* isiyo ya ghuna yenye irabu fupi chini *a*, na kipasuo meno ufizi *d* chenye mkazo na ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo hicho hicho meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*faḍad*/.

Kwenye Kiarabu linamaanisha “kaza kwa nguvu, weka vizuri.” El-Jar (1973:703)

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na sauti kikwamizi *f* isiyo ya ghuna yenye irabu fupi chini *a*, na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na irabu fupi chini *a*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*kushadidia*/.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “kukung’ang’ania, kutilia nguvu au mkazo.” BAKIZA (2010:360).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu, neno hili katikati lina sauti konsonanti /*d*/ yenye mkazo inayoashiria kuwa ni konsonanti radidi/kariri /*dd*/.

Moja kati ya hizo imedondoshwa. Pili, kuna ubadili irabu; katika neno hili kwenye

Kiarabu irabu ya pili na ya tatu zote hizo ni fupi chini /a/. Irabu hizo katika Kiswahili zimebadilika na kuwa fupi mbele juu /i/. Vilevile, neno hili mwisho limeishia irabu /u/; kwenye Kiarabu, irabu hiyo imebadilika na kuwa /i/ katika Kiswahili. Tatu, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia tena imejikita zaidi kwenye ung'ang'anizi na ukazaniaji katika maneno au maelezo. Irabu ya mwisho ambayo ni /a/ inaonesha kwa kumaanisha kuwa neno hilo liko katika kauli ya kutendea.

Kunazii نزع: Neno hili kwenye Kiarabu linaanzia kwa sauti nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi koromeo ^ʿ chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /nza^ʿ/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu lina maana ya “ ng’oa, zua; toa kitu/jambo kwenye; -wa na shauku;malizana na; nyoosha;shabihiana na; chota kwa.tengeneza, fanya vizuri; kataza, zuia ;gombana” Fairozabad (... :85).

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu ndefu mbele juu *i*; neno hili muundo wake wa msingi ni /kunazii/.

Katika Kiswahili neno hili lina maana ya “jambo la aibu linaloadhirisha mtu na kuvunjia heshima yake / kushushia hadhi na kufedhehi.” BAKIZA (2010:300).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu, neno hili lina irabu tatu fupi chini /a / kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu, irabu ya pili imebadilika na kuwa fupi mbele juu i katika Kiswahili. Pili, kuna udondoshi konsonanti; mwisho wa neno hili kuna konsonanti sauti koromeo [ʔ], sauti hiyo kwenye Kiswahili imedondoshwa na kuwekwa irabu *i*. Tatu, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo wa maana iliyotangulia kwenye Kiarabu. Maana ya kwenye Kiswahili imeegemea zaidi kwenye kufedhehi, kuadhirisha na kuvunja heshima.

Kuwadi قَوَادٍ: Katika Kiarabu neno hili liko katika wingi *quwá:du* na umoja wake ni *qa:idun*. Pia linajitokeza katika sura nyengine nayo ni *qawdu*. Katika ile hali ya wingi, neno hili linaanzia kwa kipasuo kidakatonge *q* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kiyeyushi midomo *w* chenye mkazo na irabu ndefu chini *a*: na kuishia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */quwá:d/*. Katika ile sura nyengine, linaanzia vilevile kwa kipasuo kidakatonge *q* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kiyeyushi midomo *w* na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */qawd/*.

Kwenye Kiarabu neno hili lina maana ya “viongozi wa nchi au majeshi. Kwenye sura ya pili neno hilo kwenye Kiarabu lina maana ya “farasi aongozwaye na hapandiwi.” BAALBAKI (2003:840), Ibnu Mandhour (.... :370 Juz.iii).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kiyeyushi midomo *w* na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*kuwadi*/.

Kwenye Kiswahili, neno hilo lina maana ya “mtu anayepeleka habari za siri kutoka kwa mtu fulani kwenda kwa mwengine, hasa kati ya mwanamke na mwanamume.” KKS (2004: 202), BAKIZA 2010: 204).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti, mwanzo wa neno hili kuna konsonanti sauti kipasuo kidaka tonge kisicho cha ghuna [*q*] kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu; sauti hiyo imebadilika na kuwa kipasuo kidakatonge kisicho cha ghuna [*k*] kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wake wa msingi wa neno hili kuna irabu fupi nyuma juu /*u*/ mwisho wa neno; irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /*i*/ kwenye Kiswahili. Tatu, kuna semantiki hamishi; neno hilo limepata maana mpya kwenye Kiswahili ambayo haina mwelekeo wala uhusiano wa maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita kwenye mpelekaji wa habari za siri za ufuska au muwezesaji wa uzinzi baina ya watu wawili mwanamke na mwanamume.

Maalumu معلوم : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kikwamizi koromeo ^ʕ chenye ghuna na kitambaza meno ufizi *l* chenye irabu ndefu nyuma juu *u*: na kumalizikia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *una nazali n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /ma^ʕlu:m/, na linamaanisha “kitu au jambo lenye kueleweka au kujulikana.” El-Jar (1973:1134).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa nazali mido *m* yenye irabu ndefu chini *a*: na kumalizikia kwa kitambaza *l* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kuishia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna yenye irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hili muundo wake wa kifonetiki ni /ma:lumu/, na lina maana ya “yenye sifa au nafasi ya pekee miongoni mwa vitu vyengine; mahususi, hususan.” BAKIZA (2010:213).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi ndani ya Kiarabu. Neno hili katikati lina sauti konsonanti kikwamizi koromeo /ʕ/, sauti hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi chini /a/. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi kati lina irabu ndefu nyuma juu /u:/. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Tatu, kuna upanuzi semantiki; neno hili limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyoko kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana pana zaidi kimaana ambayo imejikita katika upekee wa jambo au kitu na umahsusi wake.

Madhali *ما زال*: Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu ndefu chini *a*: na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu ndefu chini *a*., na kuishia kwa kitambaza ufizi *l* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */ma:za:l/*. Neno hili kwenye Kiarabu lina maana ya “kutoacha kuwa.”

Kwenye Kiswahili linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi meno *ð* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kitambaza ufizi *l* chenye ghuna na irabu fupi *a*. Neno hili muundo wake wa msingi ni */madhali/*, linamaanisha “kwa kuwa, kwa sababu, maadamu.” KKS (2004: 214).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi mwanzo na kati lina irabu ndefu chini */a:/*. Irabu hizo zimefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Pili, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili ambayo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia nayo imejikita kwenye hali ya sababu.

Maadamu *ما دام*: Neno hili kwenye Kiarabu linaanzia kwa sauti nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu ndefu chini *a*., na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu ndefu chini *a*: na kumalizikia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo

katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*ma:da:m*/, na lina maana ya “kutoacha kuwa.”

Kwenye Kiswahili linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu ndefu chini *a*: na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*ma:damu*/, na lina maana ya “tamko la kuonesha sababu au hali ya kutendeka kwa jambo; kwa kuwa, kwa sababu.” KKS (2004: 212).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi kwenye Kiarabu katikati lina irabu ndefu chini /*a*/. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Pili, kuna Semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili ambayo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia nayo imejikita kwenye hali ya sababu ya kutendeka kwa jambo.

Maharimu *محرم*: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *h* kisicho cha ghuna na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*maħram*/.

Neno hili lina maana ya “jambo amabalo Mwenyezi Mungu amelikataza; yule ambaye hawezi kuoia au kuolewa na mwenziwe.” Ibnu Mandhour (... :119 Juz, xii), El-Jar (1973: 1077).

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kuishia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /maharimu/.

Neno hili lina maana ya “mtu ambaye huwezi kumuoa au hawezi kuolewa kutokana na uhusiano wa ubaba, umama n.k. katika mtiririko huo.” BAKIZA (2010:216), KKS (2004: 216).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili katikati lina sauti konsonanti kikwamizi koromeo /ħ/; sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo /h/. Pili, kuna uongezaji sauti irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katikati kuna konsonanti mkusanyiko /ħr/. Irabu fupi chini /a/ imeongezwa ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili, umejikita zaidi kwenye mtu ambaye hawezi kuoia au kuolewa kutokana na uhusiano wa ubaba au umama.

Makarama مكرّم : Katika Kiarabu neno hili, linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna

chenye irabu fupi nyuma *a*, na kujiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na mkazo na irabufupi chini *a* na kumalizikia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */muka'am/*.

Neno hili lina maana ya “mtu mwema mwenye kuheshimika au karimu kwa kila mtu.” El-Jar (1973: 1148).

Kwa upande wa Kiswahili, neno hili linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hili muundo wake wa msingi ni */makarama/*.

Neno hili lina maana ya “mambo yaliyokuwa si ya kawaida, maajabu aliyokuwa nayo mtu hasa mchamungu.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwishakuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu lina irabu fupi nyuma juu */u/*. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi chini */a/*; vilevile neno hili kwenye Kiarabu mwisho lina irabu fupi nyuma juu */u/*. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi chini */a/*. Pili, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu neno hili kabla ya konsonanti ya mwisho lina sauti konsonanti */r/* yenye mkazo inayoashiria kuwa ni konsonanti radidi/kariri */rr/*. Moja kati ya hizo imedondoshwa. Tatu, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili tena haina mwelekeo wala

uhusiano na maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita zaidi kwenye maajabu na mambo yasiyo ya kawaida yaliyofumbatwa ndani ya nafsi yenye sifa ya uchamungu.

***Maluuni* ملعون** : Neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa sauti nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna na kufuatiwa na kikwamizi koromeo ^ʿ chenye ghuna na irabu ndefu nyuma juu *u*: na kuishia kwa nazali meno ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /mal^ʿu:n/.

Kwa muktadha wa maana, neno hilo kwenye Kiarabu lina maana ya “mwenye kulaaniwa na kuwa mbali na rehema za Mwenyezi Mungu, mwenye kufukuzwa kwenye rehema za mw.mungu, mwenye kulaniwa na kila mtu; mwenye kutukanwa shetani; mwenye nuhusi.” El-Jar (1973:1036), Ibnu Madhour (... :387 Juz.xiii).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu nyuma juu *u*: na kuishia kwa nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /maluuni/.

Kwenye Kiswahili neno hilo lina maana ya “mtu anayefanya mambo kinyume na maadili.” BAKIZA (2010:220).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna uongezaji sauti; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kuna mkusanyiko wa konsonanti /l^ʿ/. Kwa hivyo sauti irabu /u/ imeongezwa ili kuondosha mkusanyiko huo.

Pili, kuna udondoshi konsonanti. Katika neno hili kuna sauti kikwamizi koromeo [ʕ] chenye ghuna kwenye muundo wa msingi mwisho wa neno kwenye Kiarabu; sauti hiyo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi chini /u/ mwisho wa neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi mbele juu /i/ katika Kiswahili. Nne, kuna semantiki hamishi, neno limepata maana iliyokinyume na ile ya awali kwenye Kiarabu. Maana hiyo mpya imepoteza mwelekeo wa maana iliyotangulia kwenye Kiarabu. Maana ya kwenye Kiswahili imeegemea zaidi kwa mtendaji wa mambo yasiyokuwa ya maadili.

Marahaba **مرحبا** : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *h* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi *a* chini na kumalizikia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa nazali meno ufizi *n* yenye ghuna. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*marħaba* /.

Kwenye Kiarabu lina maana ya “kuambia karibu; karibisha, ingiza kwenye furaha.” Ibnu Mandhour (... : 413 Juz. i).

Kwenye Kiswahili linaanzia vilevile kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kimadende ufuzi *r* na irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi *a*. Neno hilo katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*marahaba*/ na lina maana ya “kiitikio cha maamkizi ya mdogo kwa mkubwa aliyeambiwa shikamoo,

tamko la kukubaliana na maelezo yaliyotolewa; kweli.” KKS (2004:223), BAKIZA (2010 :223).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna uongezaji sauti irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katikati kuna konsonanti mkusanyiko /rħ/. Irabu fupi chini /a/ imeongezwa ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili katikati lina sauti konsonanti kikwamizi koromeo /ħ/. Sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo /h/. Tatu, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili, umejikita zaidi kwenye kiitikio cha maamkizi kwa mkubwa lakini. Pia tamko la kuthibitisha kuwa jambo ni la kweli na kukubaliana na maelezo yaliyotolewa.

Marufaa مرفع : Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* na kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi koromeo ^ʿ chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /mirfa^ʿ /.

Neno hili kwenye Kiarabu lina maana ya “kinyanyulio; kifaa cha kunyanyulia vitu vizito, krini.” El-Jar (1973: 1099).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na

kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu chini *a*:. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*marufa*:/.

Kwenye Kiswahili neno hilo lina maana ya “kikalio cha vitabu wakati wa kusoma kinachofanana na mbuzi ya kukunia nazi.” BAKIZA (2010:224).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kuna irabu fupi mbele juu /i/ mwanzo wa neno; irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi chini /a/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna uongezaji sauti irabu /u/ kwenye konsonanti mkusanyiko /*rf*/ ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Tatu, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu; neno hili lina sauti konsonanti /*s*/ sauti konsonanti hiyo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Nne, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi chini /a/ kwenye Kiswahili. Tano, kuna semantiki hamishi, neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili ambayo haina mwelekeo wala uhusiano wa maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita katika kikalio cha vitabu wakati wa kusoma.

Mastakimu مستقيم : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kipasuo koromeo *q* chenye irabu ndefu mbele juu *i*: na kuishia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa

kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */mustaqi:m/*.

Neno hili kwenye Kiarabu linamaanisha “yenye kunyooka pasi na mwinamo na mpindo; sehemu ya mwisho ya utumbo au chango kubwa; -zuri, -ema; -enye kubainisha haki na batili .” El-Jar (1973: 1108), Ibnu Mandhour (... 496 Juz. xii).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna na kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni */mastakimu/*.

Kwenye Kiswahili, neno hilo lina maana ya “mahali anapoishi au anapokaa mtu, makaazi.” BAKIZA (2010:223), KKS (2004:225).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwanzo wa neno; irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele chini /a/ kwenye Kiswahili. Pili, kuna uwekaji konsonanti mkusanyiko; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna konsonanti mkusanyiko /st/ katikati. Mkusanyiko huo umebakia katika Kiswahili. Tatu, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu mbele juu /i:/ katikati kwenye muundo wake wa msingi, irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Nne, kuna semantiki hamishi; neno

hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo wala uhusiano wa maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita katika mahali pa makaazi tu.

Mdadi **مداد** : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi *a* na kufuatiwa na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n* yenye ghuna. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*madad*/.

Neno hilo kwenye Kiarabu lina maana ya “msaada; jeshi, wasaidizi na wafuasi kwenye vita.” Ibnu Mandhour (... :396 Juz.iii).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa nazali midomo *m* na kufuatiwa na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*mdadi*/.

Katika Kiswahili, lina maana ya “nguvu za hisia zinazomfanya mtu kufanya jambo bila ya kujijua aghlabu kutokana na kulipenda sana jambo; hamasa au jazba aipatayo mtu hasa kwenye shughuli inayohusiana na kuimba.” KKS (2004:223), BAKIZA (2010 :233).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, mosi, kuna udondoshi irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, irabu ya mwanzo wa neno hili /*a*/ imedondoshwa kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wake wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu kuna irabu fupi nyuma juu /*u*/ mwisho wa neno. Irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /*i*/ kwenye Kiswahili. Tatu, kuna

semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita zaidi katika hisia / hamsa zisababishazo mhusika kutojitambua kutokana na kupenda mno jambo na pia jazba aipatayo mhusika kwenye kuimba.

Mhadimu **خادم** : Katika Kiarabu, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo x chenye ghuna na irabu ndefu chini a : na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi d chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kumalizikia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/xa:dim/$.

Kwa upande wa maana, neno hilo kwenye Kiarabu linamaanisha “mtumishi, mhudumu, mtumwa, kijakazi.” El-Jar (1973: 476), Ibnu Mandhour (... :166 Juz.xii).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa nazali midomo m yenye ghuna na kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kipasuo ufizi d chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kumalizikia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u . Neno hilo katika lugha hiyo ya Kiswahili muundo wake wa msingi ni $/mhadimu/$.

Kwa muktadha wa kimaana, neno hili kwenye Kiswahili lina maana ya “mtumishi.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika neno hili kuna sauti kikwamizi kaakaa laini $[x]$ kisicho cha ghuna, kwenye muundo wa msingi mwanzo wa neno kwenye Kiarabu; sauti hiyo

imebadilika na kuwa [h]. Pili, kuna uongezaji sauti nazali /m/ mwanzo wa neno hili. Tatu, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu chini /a:/ katikati kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye Kiswahili. Nne, kisemantiki, neno hili lina wiana na ile dhana iliyoko kwenye Kiarabu.

Mharuma *محرم*: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*, na kikwamizi koromeo *ħ* kisicho cha ghuna na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kuishia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*muħrim*/.

Neno hilo lina maana ya “Mwislamu aliyevaa nguo maalumu katika ibada ya hijja; mwenye kuingia kwenye ibada ya hijja.” BAALBAKI (2003:979), Ibnu Mandhour (... :119 Juz.xii).

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kimadende *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kuishia nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*mharuma*/.

Neno hili lina maana ya “kitambaa chembamba kirefu kinachotupiwa shingoni au begani.” KKS (2004:245).

Mabadiliko ya neno hili baada kwisha kuingaia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Irabu ya mwanzo wa neno hili fupi nyuma juu /u/ imedondoshwa kwenye Kiswahili. Pili, kuna uongezaji sauti irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katikati kuna konsonanti mkusanyiko /ħr/. Irabu fupi chini /a/ imeongezwa ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu kabla ya konsonanti ya mwisho lina irabu fupi mbele juu /i/. Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi nyuma juu /u/. Vilevile kwenye Kiarabu neno hili limeishia kwa irabu fupi nyuma juu /u/; irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi chini /a/. Nne, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili ambayo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita zaidi katika kitambaa kivaliwacho kwa kutupiwa mabegani au shingoni.

Medani **ميدان** : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kiyeyushi kaakaa gumu *j*, na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu ndefu chini *a*: na nazali meno ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /majda:n/.

Neno hilo linamaanisha “uwanja ulioandaliwa kwa ajili ya mashindano na michezo ya farasi n.k.” Ibnu Mandhour (... : 177 Juz. ii).

Kwenye Kiswahili linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi kati mbele *ε*, na kufuatiwa na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Na kumalizikia

kwa nazali ufizi n yenye ghuna na irabu fupi mbele juu i . Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*medani*/.

Neno hili lina maana ya “uwanja au mahali pa kupigania vita; uwanja wa kitaaluma au fani.” KKS (2004:238).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu mwanzo lina irabu fupi chini /*a*/ . Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi mbele kati /*ε*/ . Vilevile kwenye Kiarabu limeishia irabu fupi nyuma juu /*u*/ , irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu /*i*/ . Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi, katikati lina irabu ndefu chini /*a*:/ . Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Tatu, kuna upanuzi semantiki; neno limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyoko kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana ya kwenye taaluma.

Mharabu *مخرب* : Katika Kiarabu, neno hili linaanzia kwa sauti nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u ikifuatiwa na kikwamizi kidakatonge x chenye irabu fupi chini a , na kimadende ufizi r chenye mkazo na irabu fupi juu mbele i na kumalizikia kwa kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*muxarib*/.

Neno hili linamaanisha “mvunjaji, mharibifu; mwizi” Ibnu Mandhour (... : 347 Juz. i).

Kwenye Kiswahili, linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na kufuatiwa na kikwamizi korneo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kimadende ufizi *r* chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /mharabu/

Neno hili lina maana ya “mtu anayefanya vitendo vya kuharibu, kuwafuja wengine; mtundu (hasa mtoto).” BAKIZA (2010:246)

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, irabu ya mwanzo wa neno hili /u/ imedondoshwa kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili mwisho lina sauti kikwamizi kidakatonge /x/ chenye ghuna. Sauti hiyo imebadilika na kuwa sauti /h/ kwenye Kiswahili. Tatu, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu. Neno hili kabla ya konsonanti ya mwisho lina sauti konsonanti /r/ yenye mkazo inayoashiria kuwa ni konsonanti radidi/kariri /rr/; moja kati ya hizo imedondoshwa. Nne, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu lina irabu fupi mbele juu /i/. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi chini /a/. Tano, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili umejikita zaidi kwenye ufujaji, uharibifu na utundu.

Mila **آل**: Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye mkazo na irabu fupi chini *a* na kuishia kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u*

na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */milah/*.

Kwa upande wa maana, neno hilo kwenye Kiarabu lina maana ya “dini au utaratibu wa dini; mwenendo.” Ibnu Mandhour (... : 628 Juz. xi).

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni */mila/*.

Kwenye Kiswahili neno hilo lina maana ya “taratibu na nyenendo zikiwemo silka na kawaida za kiutamaduni zilizorithiwa kutoka kwa mababu wa mababu hadi kufikia vizazi vilivyopo hivi sasa.” KKS (2004:247).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti, katika muundo wa msingi wa neno hili kuna konsonanti kariri/radidi */ll/*, moja kati ya hizi imedondoshwa. Pili, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi nyuma juu */u/* mwisho wa neno hili, irabu hiyo imebadilika na kuwa */a/*. Tatu kuna semantiki hamishi, neno hili limepata uhamishi kamili wa maana tafauti na ile maana ya Kiarabu, neno hili limechukua maana hiyo mpya iliyojikita katika taratibu na nyenendo zikiwemo silka na kawaida za kiutamaduni zilizorithiwa kutoka kwa mababu wa mababu hadi kufikia vizazi vilivyopo hivi sasa.

Msiba مصيبة: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kikwamizi kaakaagumu ufizi ş mtandazo kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu mbele juu *i*: na kufuatiwa na kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /muṣi:bah/.

Kwa upande wa maana, neno hilo kwenye Kiarabu linamaanisha “janga, maafa makubwa.” El-Jar (1973:1124).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia vilevile kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na kikwamizi ufizi kaaka gumu *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi nyuma *a*. Neno hilo kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni /msiba/.

Katika Kiswahili neno hili lina maana ya “jambo linalosababisha huzuni kubwa.” BAKIZA (2010:273).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi irabu mwanzo wa neno hili katika muundo wake wa msingi. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu mbele juu /i:/ katikati kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu; irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno hili, irabu hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa /a/. Nne, kuna ufinyu semantiki, neno hili

kwenye Kiswahili limechukua maana finyu zaidi kuliko kwenye Kiarabu, ufinyu huo wa kimaana ni kule kujiegemeza zaidi kwenye dhana ya jambo la huzuni kubwa.

Mnada منادي: Neno hili kwenye Kiarabu linaanzia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u , na kufuatiwa na nazali meno ufizi n yenye ghuna na irabu ndefu chini a : na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi d chenye ghuna na irabu ndefu mbele juu i :. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /muna:di/.

Kwenye Kiarabu linamaanisha “mwitaji, mwenye kuita.” Ibnu Mandhour (... : 364 Juz. xv).

Katika Kiswahili, linaanzia kwa nazali midomo m na nazali ufizi n yenye ghuna na irabu fupi chini a , na kuishia kipasuo ufizi d chenye ghuna na irabu fupi chini a . Neno hilo muundo wake wa msingi ni /mnada/.

Kwenye Kiswahili neno hili lina maana ya “uuzaji wa bidhaa kwa njia ya kutaja bei na huku washitiri wakiongeza mpaka kufikia bei muwafaka na akabarikiwa mhusika aliyefika bei ile ya mwisho; mahali panapouzwa vitu kwa namna hiyo.” KKS (2004:262).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Irabu ya mwanzo wa neno hili ni /u/; irabu hiyo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi katikati lina irabu refu chini /a:/. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Tatu kuna, ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu limeishia irabu refu mbele juu

/i:/. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi chini /a/. Nne, kuna upanuzi semantiki; neno limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyo kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana ya uuzaji bidhaa kwa njia ya sauti na kuongeza bei mpaka kufikia ile iliyokubalika na kubarikiwa mhusika. Dhana ya pili ni mahali pale panapofanywa uuzaji huo.

Mradi مراد : Katika Kiarabu neno hili, linaanzia kwa sauti nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*, na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu ndefu chini *a*: na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /mura:d/.

Kwenye Kiarabu neno hili lina maana ya “jambo ambalo linatakiwa liwe au lipatikane.” BAALBAKI (2003 : 1013).

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kwa nazali midomi *m* yenye ghuna na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi juu mbele *i*. Katika Kiswahili neno hili muundo wake wa msingi ni /mradi/.

Katika Kiswahili neno hilo lina maana ya “shughuli au biashara fulani inayomuingizia mtu kipato; mpango fulani wa maendeleo k.v.ya nchi unaotarajiwa kutimizwa au uliokwisha anzwa.” KKS (2004:270).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Irabu ya mwanzo wa neno hili /u/ imedondoshwa kwenye Kiswahili. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi katikati lina irabu ndefu chini /a:/. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Tatu, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu mwisho lina irabu fupi nyuma juu /u/. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu /i/. Nne, kuna upanuzi semantiki; neno hili limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyo kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana ya biashara na mipango ya maendeleo inayotarajiwa kutimizwa au iliyokwisha anzishwa.

Mwajiri **موجر**: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*, na kipasuo koo[?] kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *ǧ* chenye ghuna na mkazo na irabu fupi chini *i* na kumalizikia kwa kimadende *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*muʔaǧir*/. Neno hilo kwenye Kiarabu linamaanisha “mkodishaji, mpangishaji.” Ibnu Mandhour (... :10 Juz. iv).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na imefuatiwa na irabu fupi nyuma juu *u* na irabu fupi chini *a* kwa hivyo irabu mbili hizo zinapokutana pamoja zinabadilika na kuwa kiyeyushi midomo *w* yaani $u + a \rightarrow w$, na kufuatiwa na irabu fupi chini *a* na kikwamizi kizuio kaakaa gumu *J* chenye ghuna na

irabu fupi mbele juu *i*, na kumalizikia kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni [*mwaJiri*] na neno hili lina maana ya “mtu, shirika au kampuni inayoandika mtu au watu kazi kwa malipo au mshahara.” KKS (2004:290)

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili katikati lina sauti konsonanti kipasuo koo /ʔ/. Sauti hiyo imedondoshwa katika Kiswahili. Vilevile kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu; neno hili katikati lina sauti konsonanti /dʒ/ yenye mkazo inayoashiria kuwa ni konsonanti radidi/kariri /dʒdʒ/. Moja kati ya sauti hizo imedondoshwa. Pili, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo limeishia irabu fupi nyuma juu /u/. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu /i/. Tatu, kuna upanuzi semantiki; neno limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyoko kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana ya mhusika wa uajiri.

Mzandiki *زنديق* : Neno lina hili asili ya Kiajemi. Katika Kiarabu linaanzia kwa kikwamizi meno ufizi *z* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na nazali ufizi *n* yenye ghuna na kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu ndefu mbele juu *i*: na kuishia kwa kipasuo kidakatonge mtandazo kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*zindi:q*/.

Kwenye Kiarabu lina maana ya “mtu ambaye hudhahirisha uumini au imani na kuificha kufuru yake aliyonayo; Yule ambye hamuamini mw.mungummoja na pia haamini akhera.” Ibnu Mandhour (... : 146 Juz. x).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa nazali midomo m yenye ghuna na kufuatiwa na kikwamizi ufizi z chenye ghuna na irabu fupi chini a na nazali ufizi n yenye ghuna na kumalizikia kwa kipasuo ufizi d chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kipasuo kidakatonge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i . Neno hili muundo wake wa msingi ni /*mzandiki*/.

Katika Kiswahili lina maana ya “mnafiki, mdanganyifu, muongo mkubwa.” KKS (2004:298).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, mosi, kuna uwekaji sauti konsonanti /*m*/ mwanzo kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiswahili. Pili, ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, mwisho kuna konsonanti q . Sauti hiyo imebadilika na kuwa k kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu juu /*i*/ katikati kwenye muundo wake wa msingi. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Nne, ubadili irabu, kwenye muundo wake wa msingi wa neno hili kuna irabu fupi nyuma juu /*u*/ mwisho wa neno; irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /*i*/ kwenye Kiswahili. Tano, kuna semantiki hamishi, neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya kwa kiasi ina mwelekeo na uhusiano wa maana iliyotangulia nayo imejikita kwenye sifa za uongo, udanganyifu na unafiki.

Nazaa نازاء: Neno hili kwenye Kiarabu linaanzia kwa sauti nazali ufizi n yenye ghuna na irabu ndefu chini a : na kikwamizi ufizi z chenye ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kikwamizi koromeo $ʕ$ chenye ghuna na irabu fupi chini a . Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/na:zaʕ/$.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu lina maana ya “kukaribia kukata/kutoka roho au kufa; kugombana; kuungana au kugusana.” El-Jar (1973:1182-1183).

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kwa nazali ufizi n yenye ghuna na irabu fupi chini a na kuishia kwa kikwamizi ufizi z chenye ghuna na irabu ndefu chini a .; neno hili muundo wake wa msingi ni $/nazaa/$.

Katika Kiswahili neno hili lina maana ya “jambo la aibu linalomuadhirisha mtu na kumvunjia heshima yake / linalomshushia mtu hadhi na kumfedhehesha.” BAKIZA (2010:300).

Mbadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu chini $/a:/$ mwanzo kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo ya Kiswahili. Pili, kuna udondoshi konsonanti; mwisho wa neno hili kuna konsonanti sauti koromeo $[ʕ]$, sauti hiyo imedondoshwa na kubaki irabu a . Tatu, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo wa maana iliyotangulia. Maana ya kwenye Kiswahili imeegemea zaidi kwenye kufedhehi, kuadhirisha na kuvunjia heshima.

Naam ناعم: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kikwamizi koromeo ^ʿ chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna. Neno hili kwenye Kiarabu muundo wake wa msingi ni /na^ʿam/.

Katika Kiarabu neno hili lina maana ya “kusadikisha jambo au tukio linapotokea, jawabu lioneshalo kuwa ni kweli baada ya kwisha kuulizwa.” El-Jar (1973:1213), Ibnu Mandhour (... : 579 Juz. xii).

Kwenye Kiswahili linaanzia kwa nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu ndefu chini *a*: na kumalizikia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna. Neno hilo katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni /naam/.

Katika Kiswahili lina maana ya “kuitikia wakati mtu anapoitwa; kuonesha kukubali; ndiyo; hasa; sawa; neno litumikalo ili kuonesha hamu ya kumtaka msemaji aendelee kueleza anachosema.” KKS (2004:300).

Mbadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu, neno hili katikati lina sauti konsonanti /ʿ/. Kwenye Kiswahili sauti hiyo imedondoshwa. Pili, kuna upanuzi semantiki; neno limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyo kwenye Kiarabu. Pia limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana ya kuashiria utashi wa anayesema/msikilizaji kwa msemaji kuendelea na anachokisema.

Nafasi **نفس**: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa nazali meno ufizi n yenye ghuna na irabu fupi chini a , na kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */nafas/*.

Kwenye Kiarabu neno hilo linamaanisha “upepo mwepesi na mwanana; hewa anayovuta kiumbe hai; adabu na tabia njema; fundu la maji; nafasi, wasaa.” Jar (1973: 1216).

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kwa nazali ufizi n yenye ghuna na irabu fupi chini a , na kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i . Neno hili muundo wake wa msingi ni [*nafasi*], na lina maana ya “mahali patupu ambapo panaweza kuwekwa kitu; muda; uwezekano wakufanya/kutenda jambo.” KKS (2004:300).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu limeishia irabu fupi nyuma juu $/u/$. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu $/i/$. Pili, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili umejikita zaidi kwenye mahali patupu na ambapo panaweza kuwekwa kitu; muda.

Neema **نعمة**: Kwenye Kiarabu neno hilo linaanzia kwa nazali meno ufizi n yenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kikwamizi koromeo $ʿ$ chenye ghuna na kufuatiwa na nazali

midomo m yenye ghuna na irabu fupi chini a na kuishia kwa kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */ni^hmah/*.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hilo lina maana ya “mali na mambo mengineyo aliyoyapata mtu au hali nzuri aliyokuwa nayo.” Ibnu Mandhour (... : 579 Juz. xii).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa nazali ufizi n yenye ghuna na irabu ndefu kati nyuma ε : na kuishia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi chini a . Neno hilo muundo wake wa msingi ni */neema/*

Kwenye Kiswahili lina maana ya “hali ya kuwepo kwa wingi mahitaji ya mtu na mambo mengineyo.” KKS (2004:304).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna uimarishi irabu, neno hili lina irabu fupi mbele juu */i/* mwanzo wa neno, irabu hiyo imeimarishwa na kuwa fupi kati mbele */ε/*. Pili, kuna ubadili konsonanti. Kwenye neno hili kuna sauti kikwamizi koromeo [^h] kisicho cha ghuna, katika muundo wa msingi mwanzo wa neno hili kwenye Kiarabu; sauti hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi kati mbele */ε/*. Tatu, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi nyuma juu */u/* mwisho wa neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa */a/*. Nne, kuna upanuzi semantiki, neno limepanuka kimaana kutokana na maana hiyo kujikita kwenye hali ya kuwepo kwa wingi mahitaji ya mtu na mambo mengineyo.

Nuhusi نَحْس: Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa nazali meno ufizi n yenye ghuna na irabu fupichi a na kikwamizi koromeo \hbar kisicho cha ghuna na kufuatiwa na kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/na\hbar s/$.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hilo lina maana ya “jambo lenye mkosi, bahati mbaya, mkosi; ugumu na dhara; jambo lenye kiza, vumbi, upepo wenye vumbi; tabu, dhara; kinyume cha furaha.” Ibnu Mandhour (...:227 Juz.vi).

Katika Kiswahili, vilevile neno hili linaanzia kwa nazali ufizi n yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na kufuatiwa na kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na kuishia kwa kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i . Neno hilo muundo wake wa msingi ni $/nuhusi/$.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “kisirani, mkosi, balaa.” KKS (2004:312).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi nyuma $/a/$ mwanzo wa neno hili, kwenye Kiswahili, irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi nyuma juu $/u/$. Pili, uongezaji irabu $/u/$ kwenye mkusanyiko konsonanti $/\hbar s/$ katikati ya neno hilo kwa lengo la kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi nyuma juu $/u/$ mwisho wa neno hili. Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu $/i/$. Nne, kuna ufinyu semantiki, neno hili kwenye Kiswahili limechukua maana

finyu zaidi kuliko kwenye Kiarabu, ufinyu huo wa kimaana ni kule kujiegemeza zaidi kwenye dhana ya mikosi na balaa.

Salaala **صلى الله عليه** : Kimsingi asili ya neno hili kwenye Kiarabu ni kishazi chenye maneno *sala llahu alayhi*. Neno la kwanza linaanzia kwa kikwamizi ufizi mtandazo ṣ kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kitambaza *l* chenye mkazo na irabu ndefu chini *a*: Neno hilo muundo wake wa msingi ni */sala:/*, lina maanisha “Sali; omba dua; choma, unguza; -wa wapili; pasha moto”. El-Jar (1973:750). Neno la pili linaanzia kwa kitambaza meno ufizi *l* mtandazo na irabu ndefu chini *a*: na kufuatiwa na kikwamizi koo *h* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. linamaanisha “Mw.Mungu”. Ibnu Mandhour (... :467 Juz.xiii). Neno hilo muundo wake wa msingi ni */a:h/*. Neno la tatu linaanzia kwa kikwamizi koromeo ^ʿ chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kitambaza meno ufizi *l* chenye irabu fupi chini *a*, pamoja na kiyeyushi kaakaa *j* na kumalizikia kikwamizi koo *h* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Muundo wake wa msingi ni */ʿalajh/*. Linamaanisha “kiambishi cha jar; nomino imaanishayo juu ya ; pamoja na” El-Jar (1973:851).

Kwenye Kiarabu kishazi hicho kinamaanisha “reheema za Mwenyezi Mungu ziwe pamoja naye/ juu yake.”

Kishazi hicho kimeingia katika Kiswahili kama neno moja linaloanzia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na, kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* chenye irabu ndefu chini *a*: na kumalizikia kwa kitambaza ufizi *l* chenye irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni */sala:la/*.

Kwenye Kiswahili neno hilo linamaanisha “tamko la kuonesha mshangao.” BAKIZA (2010:353).

Mabadiliko ya kishazi hiki yaliyotokea kwenye neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu neno hili lina sauti konsonanti kikwamizi ufizi mtandazo /ʃ/. Sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika kidogo na kuwa kikwamizi ufizi isiyo ya mtandazo /s/. Pili kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili mwanzo baada irabu ya kwanza lina sauti konsonanti /l/ yenye mkazo inayoashiria kuwa ni konsonanti radidi/kariri /ll/. Moja kati ya hizo imedondoshwa. Kuna konsonanti kitambaza kizito /h/ katikati ya kishazi hicho; kitambaza hicho kimefanywa chepesi kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ufupishi irabu; kishazi hiki kwenye muundo wake wa msingi, katikati kina irabu ndefu chini /a:/. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Nne, kuna semantiki hamishi; kishazi hiki kimepata maana mpya kwenye Kiswahili kama neno, maana hiyo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia. Pia imejikita zaidi kwenye hali ya kuonesha mshangao.

Salihina **صالحين** : Katika Kiarabu, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi ufizi mtandazo ʃ kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu chini a:, na kikwamizi koromeo ħ kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu mbele juu i: na kuishia kwa nazali ufizi n yenye ghuna na irabu

fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*ʃa:liħi:n*/.

Neno hili katika Kiarabu lina maana ya “watu wema wenye kutimiza wajibu wao na kutekeleza majukumu yao.” Ibnu Mandhour (... :516 Juz. ii).

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele *i*, na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kuishia nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*salihina*/.

Neno hili lina maana ya “mtu mwema; mtu mwenye kutekeleza ibada ya sala siku zote bila ya kuiacha.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu chini /*a*/ mwanzoni na irabu ndefu mbele juu /*i*/ mwishoni kwenye muundo wake wa msingi. Irabu hizo zimefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo ya Kiswahili. Pili, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana umejikita zaidi kwenye utu, wema na uchamungu wa mtu.

Sana *صنة* : Kwenye Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kikwamizi ufizi *ʃ* mtandazo kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na nazali meno ufizi *n* yenye ghuna na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *ʃ* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u*. Hii *un* ya

mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*san^hah*/.

Kwenye Kiarabu neno hilo lina maana ya “tendo la mara moja katika ufanyaji jambo; tendo au amali ya mfanyaji; tendo zuri” Fairozabadi (1302 H : 51).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*sana*/, na lina maana ya “ ilio zidi kawaida; zaidi, mno.” KKS (2004:358).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kikwamizi ufizi /*ʃ*/ mtandazo, sauti hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi ufizi /*s*/ isiyo ya mtandazo. Pili, kuna udondoshi kononanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili mwisho lina sauti konsonanti kikwamizi koromeo /*ʃ*/ pamoja irabu yake fupi chini *a*; sauti zote mbili hizo zimedondoshwa katika Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi, mwisho lina irabu fupi nyuma juu /*u*/. Irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi chini /*a*/ katika Kiswahili. Nne, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili nayo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia. Imejikita kwenye kuzidi ukawaida na mno.

Shaibu شيب : Katika Kiarabu neno hili, linaanzia kwa kikwamizi ufizi kaakaa f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kiyeyushi kaakaa j na kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/fajb/$. Neno hili lina maana ya “nywele nyeupe; mvi.” El-Jar (1973:727).

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kikwamizi ufizi kaakaa f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a , na kufuatiwa na irabu fupi mbele juu i na kumalizikia kwa kipasuo midomo chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u . Neno hili muundo wake wa msingi ni $/shaibu/$.

Neno hili lina maana ya “mzee, mtu mzima mkongwe mwanamume.” BAKIZA (2010:360).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu neno hili katikati lina kiyeyushi $/j/$. Kiyeyushi hicho katika Kiswahili kimebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu $i/$. Pili, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili ambayo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita zaidi katika mtu mzima mwanamume mkongwe.

Sharubati شربة : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi kaakaa-ufizi f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na kufuatiwa na kimadende r chenye ghuna na kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu fupi chini a na kuishia kipasuo ufizi t

kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali ufizi n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */furbah /*.

Kwenye Kiarabu neno hilo lina maana ya “kile kinywaji kinywewacho mara moja; wekundu k.m. wa kwenye uso.”El-Jar (1973:705).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kaakaa-ufizi f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma a na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na kuishia kwa kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu fupi chini a na kipasuo ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i . Neno hilo muundo wake wa msingi ni */sharubati/*.

Kwenye Kiswahili neno hilo lina maana ya “kinywaji kinachotengenezwa kwa maji, sukari na maziwa.” BAKIZA (2004:362).

Mabadiliko ya neno hili baada kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna uongezaji sauti irabu /u/ kwenye konsonanti mkusanyiko /rb/ ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wake wa msingi wa neno hili kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno; irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Tatu, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita katika kinywaji maalumu kilichotayarishwa kwa maji, sukari na maziwa.

Shauri شاور : Neno hili kwenye Kiarabu linaanzia kwa sauti kikwamizi kaakaa gumu ufizi f kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu chini a : na kufuatiwa na kiyeyushi midomo w chenye irabu fupi chini a na kumalizikia kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi chini a . Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/fa:war/$.

Katika muktadha wa maana, neno hilo kwenye Kiarabu lina maana ya “taka ushauri, omba nasaha, taka mawazo au rai.” El-Jar (1973:696).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kaakaa gumu f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kufuatiwa na irabu fupi nyuma juu u na kuishia kwa kimadende r chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i . Neno hilo muundo wake wa msingi ni $/shauri/$.

Katika Kiswahili lina maana ya “lalamiko dhidi ya mtu au jambo linalopelekwa mbele ya mahakama na kusikilizwa na hakimu; maelezo yanayokupa wewe rai ya kufanya au kutekeleza jambo; jambo aghalabu linalohitaji kuzungumzwa au kujadiliwa; maoni, rai, nasaha; toa maoni au nasaha.” KKS(2004:367), BAKIZA (2010:362).

Mabadiliko ya neno hili baada kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu chini $/a:/$ mwanzo kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo ya Kiswahili. Pili, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wake wa msingi wa neno kuna kiyeyushi $/w/$. Tatu, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kuna irabu fupi chini $/a/$ mwisho wa neno; irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi juu $/i/$ kwenye Kiswahili. Katikati ya neno, kiyeyushi

hicho kimebadilika na kuwa irabu fupi nyuma juu /u/ kwenye Kiswahili. Nne, upanuzi semantiki, neno hili limepata maana jumuishi kuliko ile maana ya Kiarabu. Maana hiyo ya Kiswahili imezidi upeo ambao umejitokeza zaidi kwenye lalamiko linalowasilishwa mahakamani na rai ya kufanya au kutekeleza jambo.

Sherehe شرح: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi ufizi kaakaa f kisicho cha ghuna chenye irabu fipi chini a , na kimadende ufizi r chenye ghuna na kufuatiwa na kikwamizi koromeo h kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali ufizi n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni / $farh$ /.

Neno hili katika Kiarabu lina maana ya “maelezo yenye ufafanuzi, tafsiri.” El-Jar (1973:705).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi ufizi kaakaa f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi kati mbele ε , na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi kati mbele ε na kumalizikia kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi kati mbele ε . Neno hilo muundo wake wa msingi ni / $shrehe$ /.

Neno hilo lina maana ya “vitendo vya furaha vinavyofanywa na mkusanyiko wa watu ili kufurahikia au kuadhimisha jambo fulani; shamrashamra; maelezo ya jambo kwa urefu.” KKS (2004:368).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu mwanzo lina irabu fupi

chini /a/. Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi mbele kati /ε/. Vilevile kwenye Kiarabu limeishia kwa irabu fupi nyuma juu /u/. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele kati /ε/. Pili, kuna uongezaji sauti irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katikati kuna konsonanti mkusanyiko /rħ/. Irabu fupi mbele kati /ε/ imeongezwa ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Tatu, kuna upanuzi semantiki; neno limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyo kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana ya vitendo vya furaha kwa lengo la kufurahikia au kuadhimisha jambo.

Shuka شُكَّة: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi kaakaa ufizi *f* kisicho cha ghuna chenye na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kipasuo kidakatonge *q* chenye ghuna na mkazo na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /fuqah/.

Kwenye Kiarabu neno hili lina maana ya “upande anaoendea msafiri; safari ya mbali; upande wa nguo au kitambaa;” El-Jar (1973:718).

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi kaakaa ufizi *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kipasuo kidaka tonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /shuka /.

Katika Kiswahili neno hili lina maana ya “nguo inayovaliwa hasa na wanaume kwa kujizonga nyongani na kufungwa; shiti.” BAKIZA (2010:367).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti, katikati ya neno hili kuna konsonanti sauti kipasuo kidakatonge chenye ghuna [q] kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu. Sauti hiyo imebadilika na kuwa kipasuo kidakatonge kisicho cha ghuna [k] kwenye Kiswahili. Pili, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili lina sauti konsonanti /q/ yenye mkazo. Mkazo huo unaashiria uradidi/ukariri konsonanti /qq/, kwa hivyo moja kati ya konsonti hizo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi chini /a/ kwenye Kiswahili. Nne, kuna ufinyu semantiki; neno hili kwenye Kiswahili limechukua maana finyu zaidi kuliko kwenye Kiarabu. Ufinyu huo wa kimaana ni kule kujiegemeza zaidi kwenye dhana ya upande wa nguo au kitambaa ambapo kwenye Kiswahili ni zaidi ya hapo pia kuna uvaaji unaomhusisha mwanamume.

Sehemu **سهمة**: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kikwamizi koo *h* chenye ghuna na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali ufizi *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /sahm/.

Katika Kiarabu neno hili lina maana ya “kikopo au gilasi inayochezewa kamari; sehemu, hisa; mshare.” El-Jar (1973: 682-84).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi kati mbele ε na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi kati mbele ε na kumalizikia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hili, kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni /*sehemu*/, na lina maana ya “kiasi fulani cha kitu au kundi la watu; upande wa mahali k.v. nchi au mji.” KKS (2004:362).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna uimarishi irabu; kwenye muundo wa msingi neno hili irabu yake ya mwanzo ni fupi chini /*a*/. Katika Kiswahili irabu hiyo imeimarishwa na kuwa irabu ya kati juu / ε /. Pili, kuna uongezaji sauti irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katikati lina konsonanti mkusanyiko /*hm*/. Irabu fupi kati juu / ε / imeongezwa ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Tatu, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili ambayo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia nayo imejikita kwenye upande wa nchi au eneo.

Silka **سلوك**: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*, na kitamabaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu nyuma juu *u*: na kumalizikia kwa kipasuo kidaka tonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*sulu:k*/, na linamaanisha “mwenendo wa mtu na tabia yake.” El-Jar (1973:674).

Kwenye Kiswahili linaanzia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*, na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna na kumalizikia kwa kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna na kuishia kwa irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni */silka/* na lina maana ya “mwenendo na utaratibu wa jamii ya watu waliourithi kutoka kwa mababu wa mababu zao; tabia za kuzaliwa alizo nazo mtu.” BAKIZA (2010: 369) , KKS (2004:375).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu, neno hili kwenye Kiarabu mwanzo lina irabu fupi nyuma juu */u/*; irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu */i/*. Vilevile mwisho wa neno hili kwenye Kiarabu limeishia irabu fupi nyuma juu */u/*. Kwenye Kiswahili irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi chini */a/*. Pili, kuna uwekaji wa konsonanti mkusanyiko; neno hili kwenye Kiswahili limewekewa konsonanti mkusanyiko */lk/* mwisho wake. Tatu, kuna upanuzi semantiki; neno limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyoko kwenye Kiarabu. Pa neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana ya mambo yaliyorithiwa kwenye jamii kutoka kwa mababu wa mababu.

Staftahi *استفتح*: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo koo [?] na irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *t* na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kikwamizi koromeo *h* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake

wa msingi ni /^ʔistaftah/, na lina maana ya “kuomba, kutaka kufungua k.m. mlango n.k.; kunusuru; anza kwa.” El-Jar (1973:85).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna na kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna na kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*stafthi*/, lina maana ya “chakula cha mwanzo kiliwacho hasa kwa wakati wa asubuhi, kifungua kinywa, chai ya asubuhi.” BAKIZA (2010 :376).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kipasuo koo /^ʔ/ yenye irabu fupi mbele juu /*i*/. Sauti hizo kwenye Kiswahili zimedondoshwa. Pili, kuna uwekaji konsonanti mkusanyiko; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kuna konsonanti mkusanyiko /*st*/ mwanzo wa neno. Kwenye Kiswahili mkusanyiko huo umewekwa mwanzo wa neno. Tatu, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu neno hili mwisho lina sauti konsonanti kikwamizi koromeo /*h*/. Sauti hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo /*h*/. Nne, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili nayo haina mwelekeo na maana ya Kiarabu. Uhusiano uliopo kimaana ni ule ufunguaji wa kinywa kwa ajili ya ulaji wa mwanzo hasa asubuhi.

Kustahi /استحيا/: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo koo ^ʔ na irabu fupi juu mbele *i*, na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi koromeo *ħ* kisicho cha ghuna na kuishia kiyeyushi kaakaa *j* na irabu ndefu chini *a*:. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*ʔistahja*:/, lina maana ya “kuacha hai; kuona haya, onea haya.” El-Jar (1973:79).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna na kufuatiwa na kipasuo ufizi *t* chenye irabu fupi chini *a*, na kumalizikia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*kustahi*/, na lina maana ya “kuwekea heshima, kuwekea adabu, **kuheshimu**.” KKS (2004:382).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu. Neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kipasuo koo /*ʔ*/ yenye irabu fupi mbele juu /*i*/. Sauti hizo kwenye Kiswahili zimedondoshwa. Pili, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu. Neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kikwamizi koromeo /*ħ*/. Sauti hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo /*h*/. Tatu, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi, mwisho lina irabu ndefu chini /*a*/. Irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi juu /*i*/ katika Kiswahili. Nne, kuna Semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili nayo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia. Imejikita kwenye kuheshimu.

Starehe استراحة: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti konsonanti kipasuo koo $ʔ$, na kufuatiwa na irabu fupi mbele juu i na kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna na kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu i , na kujiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu ndefu chini a : na kikwamizi koromeo h kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi t chenye irabu fupi nyuma juu u na *nazali* n . Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/ʔistira:hah/$, na lina maana ya “mahali maalumu palipotayarishwa kwa ajili ya kupunga upepo au mapumziko katika uwanja wa nyumba.” El-Jar (1973:80).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna na kipasuo ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi kati mbele ϵ na kumalizikia kwa kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi kati mbele ϵ . Neno hili muundo wake wa msingi ni $/starehe/$, na lina maana ya “hali ya kutokuweco shida au usumbufu, burudani; hali ya kuweco mambo ya anasa au furaha.” KKS (2004 :383).

Mabadiliko ya neno hili, baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kipasuo koo $/ʔ/$. Sauti hiyo kwenye Kiswahili imedondoshwa. Pili, kuna badiliko la irabu fupi chini kwenye muundo wa msingi wa neno hili. Kabla ya konsonanti ya mwisho kuna irabu ndefu chini $/a/$ na mwisho wa neno kuna irabu fupi chini; irabu

mbili hizi kwenye Kiswahili zimekuwa za kati chini mbele /ε/. Tatu, kuna upanuzi semantiki; neno limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyo kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana ya hali ya kutokuwepo usumbufu au shida, na hali ya furaha kwenye mambo ya anasa.

Somo سومي: Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufutiwa na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kiyeyushi kaakaa gumu *j*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /sami/. Katika Kiarabu neno hili linamaanisha “mtu mwenye jina sawa na la mwenziwe; mwenza.” El-Jar (1973:679).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna chenye irabu fupi kati juu *ɔ* na kufuatiwa na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi kati juu *ɔ*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /somo /, na linamaana ya “mtu wa jina moja na mwengine; mwalimu afundishaye mambo ya kunga unyagoni au kumbini; kungwi; mpango wa mafundisho ya elimu maalumu k.m. Hesabu, Kiswahili n.k.” BAKIZA (2010:374).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo lina irabu fupi chini /a/ na mwisho lina irabu ndefu mbele /i:/. Irabu hizo katika Kiswahili zimebadilika na kuwa fupi kati juu /ɔ/. Pili, kuna upanuzi semantiki; neno limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyo kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana pana zaidi

kimaana ambayo imejikita katika mafunzo ya mambo ya kunga unyagoni na ukumbini, mpango maalumu wa mafundisho katika elimu maalumu.

Tabia *طبيعة* : Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kipasuo meno ufizi t mtandazo kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu ndefu i : na kikwamizi koromeo ζ chenye ghuna na irabu fupi chini a na kuishia kwa kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u . Neno hili muundo wake wa msingi ni */t̤abi:çah/*.

Katika muktadha wa maana, neno hilo kwenye Kiarabu lina maana ya “maumbile au sifa.” El-Jar (1973:782).

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kipasuo ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kuishia kwa kipasuo midomo b chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na irabu fupi a . Neno hilo muundo wake wa msingi ni */tabia/*.

Kwenye Kiswahili neno lina maana ya “mwenendo na mazoea aliyojengeka nayo mtu kwa muda mrefu na kuwa ni sehemu ya maumbile yake.” BAKIZA (2010:382).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti. Katika neno hili kuna sauti kipasuo ufizi mtandazo $[t̤]$ kisicho cha ghuna, kwenye muundo wa msingi mwanzo wa neno hili kwenye Kiarabu; sauti hiyo imebadilika na kuwa kipasuo kisicho cha ghuna $[t]$. Pili, kuna ufupishi irabu, irabu ndefu $/i:/$ iliyopo katikati ya neno hili, irabu hiyo imefupishwa. Tatu, ubadili konsonanti. Katika neno hili kuna badiliko la sauti kikwamizi koromeo $[\zeta]$ chenye ghuna, kwenye muundo wa msingi mwanzo wa neno hili kwenye Kiarabu; sauti hiyo imebadilika na kuwa irabu

fupi chini /a/. Nne, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno, irabu hiyo imebadilika na kuwa /a/. Tano, kuna semantiki hamishi, neno hili limepata uhamishi kamili wa maana tafauti na ile maana ya Kiarabu, neno hili limechukua maana hiyo mpya iliyojikita katika mwenendo na mazoea aliyojengeka nayo mtu kwa muda mrefu na kuwa ni sehemu ya maumbile yake.

Tafadhali *تفضل*: Neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kipasuo meno ufizi *ḏ* chenye mkazo na ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kitamabaza meno ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*tafaḏal*/.

Kwenye Kiarabu neno hili linamaanisha “kupa au kutoa fadhila au ubora alionao mtu, kujidai ubora zaidi, kuvaa aina ya nguo ipitayo juu ya bega na chini ya kwapa hasa nyumbani.” El-Jar (1973:319).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi meno *ḏ* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni [*tafadhali*], na lina maana ya “neno la heshima la kumwomba mtu afanye jambo.” BAKIZA (2010:382).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kipasuo meno ufizi /d̄/. Sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi meno /ð/. Pili, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu, mwisho lina irabu fupi chini /a/. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu /i/. Tatu, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili, umejikita zaidi kwenye heshima wakati wa kutaka au kuomba jambo.

Takirima تكريم : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna, na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu ndefu mbele juu *i*: na kumalizikia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /takri:m/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu, neno hilo lina maana ya “kuheshimu, kukirimu, makaribisho ya heshima au ya ukarimu.” El-Jar (1973:329).

Katika Kiswahili, neno hilo vilevile, linaanzia kwa kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kipasuo kaakaa laini *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /takirima/.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “mapokezi mema ya kushughulikia mgeni, wema anaofanyiwa mgeni katika mapokezi na mwenyeji wake.” BAKIZA (2010:385).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu, neno hili lina irabu ndefu mbele juu /i:/ katikati kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu, irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno hili. Tatu, uongezaji irabu /i/ kwenye mkusanyiko konsonanti /kr/ katikati ya neno hilo kwa lengo la kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ufinyu semantiki; neno hili kwenye Kiswahili limechukua maana finyu zaidi kuliko kwenye Kiarabu, ufinyu huo wa kimaana ni kule kujiegemeza zaidi kwenye dhana ya kukirimiwa mgeni tu.

Tarika طريق : Kwenye Kiarabu neno hili kimatamshi linaanzia kwa sauti kipasuo meno ufizi *t* mtandazo kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma *a* na kimadende *r* ufizi chenye irabu ndefu juu *i*: na kumalizikia kwa kipasuo koromeo *q* na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*tari:q*/ .

Neno hilo lina maana ya “njia, barara kuu; namna; kundi fulani la wafuasi wa kisufi.”

Moustafa (-- : 556 Juz. II).

Katika Kiswahili neno hili, linaanzia kwa kipasuo ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kimadende r chenye irabu fupi juu i na kipasuo kidaka tonge k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a . Neno hili muundo wake wa msingi ni */tarikā/*.

Neno hili lina maana ya “kundi la watu wanaofuata mafunzo ya dini ya Kiislamu yanayotokana na uongozi wa shehe kutokana na njia za ufanyaji wa ibada hasa dhikiri.” KKS (2004:397).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu, neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kipasuo meno ufizi mtandazo */t/*. Sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa kipasuo ufizi */t/*. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi, katikati lina irabu ndefu mbele juu */i:/*. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Tatu, ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu limeishia irabu fupi nyuma juu */u/*. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi chini */a/*. Nne, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili, umejikita zaidi kwenye muktadha wa kidini pekee.

Taharuki *تحرّك*: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kipasuo meno ufizi t isiyo ya guhuna na irabu fupi chini a , na kikwamizi koromeo h kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye mkazo na irabu fupi nyuma juu u na kumalizikia kwa kipasuo kaakaa laini k kisicho cha ghuna chenye irabu fupi juu u na nzali n . Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu

hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */tahaʀuk/*.

Neno hili lina maana ya “hali ya kwenda kutoka mahali pamoja kwenda pengine; mwendo.” El-Jar (1973:386).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna na irabu fupi chini *a*, na kikwamizi koo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kimadende ufizi *r* chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kumalizikia kwa kipasuo kaakaa laini *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. Neno hili muundo wake wa msingi ni */tahaʀuki/*.

Neno hili lina maana ya “hali ya kutokuwa na utulivu na makini, wasiwasi, mbabaiko, mfazaiko wa nafsi; mshituko kutokana na tukio la jambo; hali ya kusubiri kujua kitakachotokea baadaye.” BAKIZA(2010: 383).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi kwenye Kiarabu, neno hili katikati lina sauti konsonanti kikwamizi koromeo */ħ/*. Sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo */h/*. Pili, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili katikati lina sauti konsonanti */r/* yenye mkazo inayoashiria kuwa ni konsonanti radidi/kariri */rr/*. Moja kati ya konsonanti hizo imedondoshwa. Tatu, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu limeishia kwa irabu fupi nyuma juu */u/*. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu */i/*. Nne, kuna upanuzi semantiki; neno limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyo kwenye Kiarabu, pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana ya hali ya nafsi kisaikolojia.

Tufani طوفان : Katika Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kipasuo meno ufizi t mtandazo kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu nyuma juu u : na kufuatiwa na kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu chini a : na kumazikia kwa nazali ufizi n yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u . Kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/tu:fa:n/$.

Katika Kiarabu neno hili lina maana ya “mafuriko makubwa, mafuriko; kiza kikubwa cha usiku; jambo au kitu chochote kingi; tukio linlofunika mambo mengine.” El-Jar (1973:794), Moustafa (-- : 760 Juz. II).

Kwenye Kiswahili linaanzia kwa kipasuo ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na kufuatiwa na kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kumalizikia kwa nazali ufizi n yenye ghuna na irabu fupi mbele juu i . Neno hili muundo wake wa msingi ni $/tufani/$.

Kwenye Kiswahili linamaanisha “upepo unaozunguka kwa nguvu sana aghalabu hutoka baharini kuelekea nchi kavu; kimbunga, dharuba.” BAKIZA (2010:403).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; mwanzo wa neno hili kuna konsonanti sauti kipasuo meno ufizi isiyo ya ghuna $[t]$ kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, sauti hiyo imebadilika na kuwa sauti kipasuo ufizi kisicho cha ghuna $[t]$ kwenye Kiswahili. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili lina irabu ndefu nyuma juu $/u:/$ mwanzo na irabu ndefu chini $/a:/$ kwenye muundo wake wa msingi katika Kiarabu, irabu hizo zimefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Tatu, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wake wa msingi wa neno hili kuna irabu fupi nyuma juu $/u/$ mwisho wa

neni; irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Nne, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo wala uhusiano wa maana iliyotangulia; tena imejikita kwenye upepo mkali wenye nguvu basi.

Tuhuma *تُهْمَة*: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kipasu koo *h* chenye ghuna na kujiwa na nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *t* na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */tuhmah/*.

Kwenye Kiarabu lina maana ya “shitaka, jambo au kosa linaloelekezwa kwa mtu au upande mwingine; dhana, shaka.” El-Jar (1973:18), Moustafa (-- : 6060 Juz.II) .

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kwa kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi nyuma *u* na kuishia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni */tuhuma/*.

Kwenye Kiswahili lina maana ya “kutilia shaka, kushuku, kudhani; shaka ya kudhania jambo baya.” BAKIZA (2010 :403).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna uongezaji sauti irabu /u/ kwenye konsonanti mkusanyiko */hm/* ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wake wa msingi wa

neni hili kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho wa neno; irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi chini /a/ kwenye Kiswahili. Tatu, kuna semantiki hamishi, neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya ina mwelekeo na uhusiano wa maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita kwenye kudhania zaidi hasa jambo baya.

Ufuska فسق : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi meno mdomo *f* isiyo ya ghuna yenye irabu fupi mbele juu *i* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi meno *s* kisicho cha ghuna na kumalizikia kwa kipasuo kidakakatonge mtandazo *q* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*fisq*/.

Kwenye Kiarabu neno hili lina maana ya “uasi; kutoka kwenye; kuchupa mipaka ya sheia.” El-Jar (1973:908), Moustafa (-- : 688 juz.II).

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kwa irabu fupi nyuma juu *u* na kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna na kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingii ni /*ufuska*/.

Katika Kiswahili, neno hilo lina maana ya “tabia ya uasharati na uzinzi.” BAKIZA (2010 :92).

Mabadiliko baada ya neno hili kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna uwekaji sauti irabu /u/; mwanzo kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu lina irabu

fupi chini /i/ mwanzo wa neno; irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi nyuma juu /u/ kwenye Kiswahili. Vilevile irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho kwenye muundo wa msingi wa neno imebadilika na kuwa irabu fupi chini /a/ katika Kiswahili. Tatu, kuna uwekaji konsonanti mkusanyiko; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu; kuna konsonanti mkusanyiko /sq/ katikati. Mkusanyiko huo umebakia katika Kiswahili baada ya sauti konsonanti *q* kubadilika na kuwa *k*. Nne, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia na imejikita zaidi katika tabia ovu ya uzinifu.

Uturi **عطر** : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi koromeo ^ʿ yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* ikifuatiwa na kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*ʕutr*/, na lina maana ya “manukato au uzuri; maji yenye harufu nzuri yaliyo katika seli za mimea.” El-Jar (1973:838), Moustafa (-- : 607 Juz.II).

Katika Kiswahili linaanzia kwa irabu fupi juu *u* na kipasuo ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi juu *u* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*uturi*/, na lina maana ya “mafuta mazuri, manukato.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu neno hili mwanzo lina

sauti kikwamizi konsonanti /ʃ/. Sauti hiyo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili konsonanti; sauti konsonanti *t* imebadilika na kuwa *t* katika Kiswahili. Tatu kuna uongezaji sauti irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili mwisho kuna konsonanti mkusanyiko /*tr*/. Irabu fupi mbele juu /*i*/ imeongezwa ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Nne, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu limeishia irabu fupi nyuma juu /*u*/. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu /*i*/. Tano, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili, umejikita zaidi kwenye mafuta mazuri ya kujitia mwilini au nguoni.

Wajibu **وَجِب** : Kwenye Kiarabu neno hilo linaanzia kwa kiyeyushi midomo *w* na kufuatiwa na irabu fupi chini *a* na kikwamizi kaaka gumu *ǧ* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*wadǧab*/.

Kwenye muktadha wa kimaana, katika Kiarabu neno hili linamaanisha “lazimika, pasa; anguka ardhini; tetemeka na piga haraka haraka hasa moyo; fariki, kufa; kula mlo mmoja kwa siku.” El-Jar (1973:1274).

Kwenye Kiswahili, neno hilo linaanzia vilevile kwa kiyeyushi midomo *w* na kufuatiwa na irabu fupi chini *a* na kikwamizi kizuio kaaka gumu *J* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* . Neno hili muundo wake wa msingi ni /*wajibu*/

Kwenye neno hilo, pia huongezeka kipashio *ka* mwishoni mwa neno kinachoonesha kauli ya kutendeka wenyewe katika Kiswahili.

Katika Kiswahili linamaanisha “si ya hiari, lazima;faradhi.” BAKIZA (2010:455).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu; mwisho kuna irabu mbili fupi chini /a/. Irabu hizo zimebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/ na kuunganika na kipashio cha kauli ya kutendeka mwisho wa neno kufuata mfumo wa Kiswahili wa kimofolojia. Pili, kuna ufinyu semantiki; badiliko hilo la maana limejifinya zaidi kwa kujikita katika kulazimika tu.

Waraka ورقة : Neno hili kwenye Kiarabu, linaanzia kwa kiyeyushi midomo *w* chenye irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo koromeo *q* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kuishia kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /waraqah/.

Kwa upande wa maana, kwenye Kiarabu neno hilo lina maana ya “jani la mmea au mti; karatasi ya kuandikia.” El-Jar (1973:1282).

Katika Kiswahili, neno hili linaanzia kwa kiyeyushi midomo *w* na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /waraka/.

Katika Kiswahili, neno hilo lina maana ya “maandishi rasmi yanayowasilishwa mkutanoni au mahali pengine yanayoelezea jambo au maudhui maalumu; ithibati ya ununuzi au umiliki wa jambo.” BAKIZA (2010 :457).

Mabadiliko ya neno hili baada kwisha kuingia katika Kiswahili, mosi, kuna ubadili konsonanti; katika muundo wake wa msingi neno hili lina sauti kipasuo koromeo [q] sauti hiyo imebadilika na kuwa kipasuo kidakatonge *k* kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi neno hili kuna irabu fupi nyuma juu /u/ mwisho, irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi chini /a/ kwenye Kiswahili. Tatu, kuna semantiki hamishi; neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili ambayo ina mwelekeo na uhusiano wa maana iliyotangulia kwa kiasi fulani. Maana kwenye Kiswahili imeegemea zaidi kwenye maandishi rasmi yanayoelezea maudhui maalumu na ithibati ya umiliki wa jambo.

Wasaa وسع : Kwenye Kiarabu neno hili linaazia kwa kiyeyushi midomo *w* pamoja na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna na kikwamizi koromeo *ç* chenye ghuna na irabu fupi nyuma *u na nazali n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /wusç/.

Neno hilo katika Kiarabu lina maana ya nguvu na uwezo. Moustafa (-- :1031 Juz.II).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kiyeyushi midomo *w* na irabu fupi chini *a* na kikwamizi ufizi kisicho cha ghuna na kufuatiwa na irabu ndefu chini *a*: . Muundo wake

wa msingi ni /wasaa/. Linamaanisha “ wakati alionao mtu kwa ajili ya kufanya jambo; uwezo wa kifedha.” BAKIZA (2010:457).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wake wa msingi mwanzo wa neno hili kuna irabu fupi nyuma juu /u/. Irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi chini /a/ kwenye Kiswahili. Vilevile, mwisho kuna irabu fupi nyuma juu /u/; irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi chini /a/. Tatu, udondoshi konsonanti, mwisho wa neno hili kuna konsonanti sauti koromeo [ʻ], sauti hiyo imedondoshwa. Nne, semantiki hamishi, neno limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo na uhusiano wa maana iliyotangulia. Kwenye Kiswahili maana hiyo, imeegemea zaidi kwenye nafasi ya kutenda jambo.

Zawadi زَوَادِي: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu fupi *a*, na kufuatiwa na kiyeyushi midomo *w* chenye mkazo na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /zawad/.

Katika Kiarabu neno hilo lina maana ya “kupa au kutoa chakula cha safarini.” El-Jar (1973:636).

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kiyeyushi midomo *w* chenye irabu fupi chini *a*, na kumalizikia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /zawadi/, na linamaanisha “kitu atunukiwacho mtu kuwa ni

ishara ya mapenzi, wema au kwa utendaji mzuri wa shughuli; atia.” BAKIZA (2010 :464).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi kononanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili katikati lina sauti konsonanti /w/ yenye mkazo inayoashiria kuwa ni konsonanti radidi/kariri /ww/; moja kati ya hizo imedondoshwa. Pili, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye Kiarabu mwanzo limeishia irabu fupi chini /a/. Irabu hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa fupi mbele juu /i/. Tatu, kuna upanuzi semantiki, neno limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyoko kwenye Kiarabu; pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana ya upewaji au utoaji wa kitu kwa wema na upendo kutokana na utendaji mzuri wa jambo.

5.2.6 Maneno ya Kiuhasibu / Kifedha

Jina la Kundi	Idadi ya maneno	Asilimia %
1. Kiuhasibu/kibiashara	09	03.114

Jadwali Na.9 Maneno ya Kiuhasibi/Kifedha.

Halasa خلاصة: Katika kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini x chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na kufuatiwa na kitambaza ufizi l kisicho cha ghuna chenye irabu ndefu mbele chini a : na kikwamizi ufizi \int kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chinina kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni

irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni

/xula:ʃah/. Neno hili linamaanisha “ufupisho, ikisiri; roho; kitu, jambo ; maji au juisi ya kitu.” El-Jar (1973:), BAALBAKI (2003:518).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi mbele chini *a* na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* kisicho cha guha chenye irabu fupi mbele chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele chini *a*.

Muundo wake wa msingini */halasa/*, na linamaanisha “ujira wa baharia baada ya kukatwa madeni kutoka kwenye hisa zao; mshahara wa wanamaji.” KKS (2004:106).

Mabadiliko ya neno hilo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kikwamizi koromeo */x/* kisicho cha ghuna; sauti hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo */h/*. Pili, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi mwanzo lina irabu fupi nyuma juu */u/*. Irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi chini */a/* katika Kiswahili. Tatu, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi katikati lina irabu ndefu chini */a:/*. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Nne, kuna ubadili irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi, mwisho lina irabu fupi nyuma juu */u/*. Irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi chini */a/* katika Kiswahili. Tano, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili ambayo haina

mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia kwenye Kiarabu. Imejikita kwenye fedha za malipo ya watu maalumu nao ni mabaharia na wanamaji.

Maduhuli *مدخل* : Katika Kiarabu neno hili linatokana na asili ya neno *daxlu* ambalo linaanzia kwa sauti kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi kaakaa laini *x* chenye ghuna na kumalizikia kwa kitambaza *l* kisicho cha ghuma na kuishia irabu fupi nyumajuu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */daxl/*, na linamaanisha “fedha anazozipata mtu kutokana na kazi aifanyayo; maradhi ya ndani kabisa katika mwili wa mtu; uovu, ubaya; kasoro, aibu; mti uliosokotana; watu fulani wanaojinasibisha na watu wengine ambao hawana nasaba nao.” El-Jar (1973:527).

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kwa nazali midomo *m* na irabu na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi juu *u*, na kumalizikia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi juu *u* na kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*.

Neno hili, katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni */maduhuli/*, na lina maana ya “mapato, mauzo; bidhaa ziingizwazo kutoka nchi za nje.” KKS 2004:214).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna uongezaji sauti nazali konsonanti */m/* mwanzo wa neno kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Irabu ya mwanzo wa neno hili */a/*, imebadilika kwenye Kiswahili na kuwa */u/*. Vilevile neno hili kwenye muundo wake

wa msingi, mwisho lina irabu fupi nyuma juu /u/. Irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi mbele juu /i/ katika Kiswahili. Tatu, kuna uongezaji sauti irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili mwisho kuna konsonanti mkusanyiko /x/. Irabu fupi nyuma juu /u/ imeongezwa ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Nne, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili mwisho lina sauti konsonanti kikwamizi kaaka laini /x/ kisicho cha ghuna; sauti hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo /h/ chenye ghuna. Tano, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili, umejikita zaidi kwenye mapato, mauzo na bidhaa zinazolingizwa kutoka nje ya nchi.

Masurufu **مصروف** : Katika Kiarabu, neno hili linaanzia kwa nazali midomo *m* na irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na sauti kikwamizi ufizi kaaaka gumu *ṣ* mtandazo isiyo na ghuna na kimadende ufizi *r* pamoja na irabu ndefu nyuma *u*: na kumalizikia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*maṣru:f*/. Lina maana ya matumizi; jambo au kitu chenye kutumiwa, gharama; fedha za matumizi; mwenye kuondolewa au kufukuzwa k.m kazini. BAALBAKI (2003:1053).

Kwenye Kiswahili, linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na sauti kikwamizi ufizi kaaaka gumu *s* isiyo ya ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* yenye ghuna na irabu fupi nyuma *u* na kuishia kwa kikwamizi meno *f* na irabu fupi nyuma juu *u*. Katika Kiswahili neno hilo

muundo wake wa msingi ni /*masurufu*/ na lina maana ya “fedha za matumizi ya safarini; chakula au matumizi ya njiani mtu anapokuwa safarini.”

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kikwamizi ufizi /*ʃ*/ mtandazo kisicho cha ghuna. Sauti hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi ufizi / *ʃ* / kisicho cha ghuna. Pili, kuna uongezaji sauti irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili mwisho kuna konsonanti mkusanyiko /*sr*/. Irabu fupi nyuma juu /*u*/ imeongezwa ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi. Katikati lina irabu ndefu nyuma juu /*u*:/; irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili. Nne, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili umejikita zaidi kwenye fedha, chakula au matumizi ya safarini.

Mhazini *خازن*: Neno hili kwenye Kiarabu linatokana na neno *xa:zin* ambalo linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini *x* chenye ghuna na irabu ndefu chini *a*.; na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*xa:zin*/. Lina maana ya “ulimi, lugha; mtu aliyepewa mamlaka ya kutunza fedha pamoja na namna ya matumizi yake.” El-Jar (1973: 476).

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kwa nazali midomo m yenye ghuna na kikwamizi koromeo h chenye ghuna irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kikwamizi ufizi z chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kumalizikia kwa nazali ufizi n yenye ghuna na irabu fupi mbele juu i . Neno hili muundo wake wa kifonetiki ni [mhazini], na lina maana ya “mshikafedha mkuu wa chama, ushirika, taasisi n.k.”. BAKIZA (2004).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna uongezaji sauti konsonanti [m]; mwanzo wa neno kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kikwamizi kaaka laini [x] kisicho cha ghuna; sauti hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo [h] chenye ghuna. Tatu, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi mwanzo lina irabu ndefu chini /a:/. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Nne, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Mwisho neno hili lina irabu fupi nyuma juu /u/; irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi mbele juu /i/ katika Kiswahili. Tano, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili, umejikita zaidi kwenye mtu mwenye kutunza fedha za ushirika, taasisi n.k.

Mizania ميزانية: Kwenye Kiarabu, neno hili linaanzia kwa nazali midomo m yenye ghuna na irabu ndefu mbele i : na kufuatiwa na kikwamizi ufizi z chenye ghuna na irabu ndefu chini a ;, na kumalizikia kwa nazali ufizi n yenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kiyeyushi kaaka gumu j na irabu fupi chini a na kumalizikia kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno

ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */mi:za:nijah/*. Neno hili lina maana ya “makadirio ya matumizi na mapato yanayopangwa na serekali, taasisi au watu binafsi kwa muda maalumu; mpango mahsusi unaoonesha muhtasari wa hesabu za fedha.” El-Jar (1973:1177), BAALBAKI (2003: 1145).

Katika Kiswahili, neno hilo linaanzia kwa nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*, na kufuatiwa na kikwamizi ufizi *z* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na irabu fupi kati na kati *ə*. Muundo wake wa msingi ni */mizania/*, na lina maana ya “hesabu za kuonesha usawa wa matumizi na mapato ya biashara ya shirika au nchi.” KKS (2004 :248).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi, mwanzo na katikati lina irabu ndefu juu */i:/* na chini */a:/*. Irabu hizo zimefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo. Pili, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu. Mwishoni kuna sauti kiyeyushi kaakaa */j/*. Sauti hiyo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Mwisho neno hili lina irabu fupi nyuma juu */u/*. Irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi kati */ə/* kwenye Kiswahili. Nne, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili umejikita zaidi kwenye usawa wa hesabu za matumizi na mapato.

Mrabaha *مرابهة*: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *r*, na kufuatiwa na kipasua midomo *b* chenye ghuna na

kumalizikia kwa kiwamizi koromeo \hbar kisicho na ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/rib\hbar u/$ na lina maana ya “chumo, jambo linalopatikana au linalochumwa; kitu cha ziada anachokilipa mdaiwa katika deni kwa mujibu wa shuruti maalumu; tafauti ya kinachopatikana baina ya fedha za kununulia na za kuuzia, faida; ongezeko katika biashara .” Ibnu Mandhour (... :443 Juz.ii)

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa sauti nazali midomo m yenye ghuna na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi chini a , na kumalizikia kwa kikwamizi koromeo h chenye ghuna na na irabu fupi chini a . Kwenye Kiswahili neno hili muundo wake wa msingi ni $/mrabaha/$, na lina maana ya “biashara inayofanywa na mtu na hali anampelekea mwenye mali kiasi fulani cha faida anayopata; faida au pato linalotokana na biashara; malipo anayopewa mwandishi au msanii na kampuni iliyotoa kazi yake kila baada ya kipindi fulani cha mauzo.” BAKIZA (2010: 268), KKS (1981 :185).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, mosi, kuna uongezaji sauti konsonanti $/m/$; mwanzo wa neno kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Irabu ya mwanzo wa neno hili $/i/$, imebadilika kwenye Kiswahili na kuwa $/a/$. Tatu, kuna uongezaji sauti irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili mwisho kuna konsonanti mkusanyiko $/b\hbar/$. Irabu fupi mbele juu $/i/$ imeongezwa ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Nne, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili mwisho lina

sauti konsonanti kikwamizi koromeo /h/ kisicho cha ghuna. Sauti hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo /h/ chenye ghuna. Tano, kuna upanuzi semantiki; neno hili limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyoko kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana pana zaidi kimaana, nayo imejikita zaidi kwenye sehemu ya faida ya bishara apelekewayo mwenye mali au pato la faida linalotokana na biashara.

Msarifu مصرف : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti nazali midomo m yenye ghuna na irabu fupi chini a , na kikwamizi ufizi kaakaa gumu mtandazo ς , na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kumalizikia kwa kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /maʃrif/. Linamaanisha “uondokaji; mahali pa matumizi; benki.” El-Jar (1973: 1121).

Katika Kiswahili linaanzia kwa sauti nazali midomo m yenye ghuna na kikwamizi ufizi s kisicho cha ghuna na kufuatiwa na irabu fupi chini a , na kumalizikia kwa kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kuishia kwa kikwamizi meno mdomo f kisicho ghuna na irabu fupi nyuma juu u . Neno hili katika Kiswahili muundo wake wa msingi ni /msarifu/.

Kwenye Kiswahili linamaanisha “mtu mwenye kusimamia na kuidhinisha matumizi mazuri ya fedha katika shirika, ofisi au kampuni; mtu mwenye kupanga na kuendesha mambo kwa utaratibu.” KKS (2004:273).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, irabu ya mwanzo wa neno hili ambayo ni fupi chini /a/. Irabu hiyo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kikwamizi ufizi mtandazo /ʃ/ kisicho cha ghuna. Sauti hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi ufizi /s/. Tatu, kuna uongezaji sauti irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili mwisho kuna konsonanti mkusanyiko /ʃr/. Irabu fupi mbele juu /i/ imeongezwa ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Nne, kuna upanuzi semantiki; neno hili limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyoko kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana pana zaidi, ambayo imejikita zaidi kwenye dhati ya mtu mwenye jukumu la kusimamia matumizi ya fedha vizuri au mpangaji na mwendeshiji mambo vyema.

Mshahara *مشاهدة*: Neno hili kimsingi linaanzia na nazali midomo *m* na irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na sauti kikwamizi ufizi kaakaa gumu ʃ isiyo ya ghuna na irabu ndefu chini *a*: na kumalizikia kwa kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kipasuo meno ufizi *t* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /muʃa:harah/.

Katika Kiarabu neno hili lina maana ya “kitu au jambo la kila mwezi, kitu au jambo lenye kutokea kila mwezi mara moja; malipo ya kila mwezi.” BAALBAKI (2003:680).

Katika Kiswahili neno hili linaanzia kwa nazali midomo m na kufuatiwa na sauti kikwamizi ufizi kaakaa gumu f isiyo ya ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kikwamizi korneo h chenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kimadende ufizi r na irabu fupi chini a . Katika Kiswahili, neno hili muundo wake wa msingi ni */mshahara/* na lina maana ya “fedha anazolipwa mtu kila mwezi kwa kazi aliyoajiriwa kufanya.” KKS (2004:273).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, mwazo kuna sauti irabu /u/. Sauti hiyo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi, mwanzoni lina irabu ndefu chini /a:/. Irabu hiyo imefupishwa katika Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu kwenye lugha hiyo ya Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, mwisho neno hili lina irabu fupi nyuma juu /u/. Irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi chini /a/ katika Kiswahili. Nne, kuna ufinyu semantiki, ufinyu huo wa maana katika Kiswahili, umejikita zaidi kwenye malipo ya kila mwisho wa mwezi.

Sarafu صرف: Kwenye Kiarabu neno hili lianaanzia kwa kikwamizi ufizi na kaakaa gumu ʃ kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na kumalizikia kwa kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */ʃarf/*.

Kwenye Kiarabu, neno hilo lina maana ya “ubadilishaji wa fedha za ndani ya nchi kwa fedha za kigeni; fedha ya nchini kimuundo na thamani yake.” El-Jar (1973: 743).

Kwenye Kiswahili, linaanzia kwa kikwamizi ufizi kaakaa gumu *s* kisicho cha ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kikwamizi meno mdomo *f* kisicho na ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hili kwenye Kiswahili muundo wake wa msingi ni /sarafu/.

Neno hili lina maana ya “vipande vya madini k.v. fedha, shaba au dhahabu vyenye thamani vinavyotumika kuwa ni pesa; chombo cha shaba kinachotumika kuwa ni pambo kwa wanawake ambacho huvaliwa shingoni au kichwani.”KKS (2004:360).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili mwanzo lina sauti konsonanti kikwamizi ufizi mtandazo /ʃ/ kisicho cha ghuna; sauti hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi ufizi /s/. Pili, kuna uongezaji sauti irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili mwisho kuna konsonanti mkusanyiko /ʃr/. Irabu fupi chini /i/ imeongezwa ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Tatu, kuna upanuzi semantiki; neno hili limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyoko kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana pana zaidi kimaana, nayo imejikita zaidi kwenye thamani na muundo wa fedha na pambo la shaba linalovaliwa na wanawake shingoni au kichwani.

5.2.7 Maneno ya Kibaharia / Usafiri

Jina la Kundi	Idadi ya maneno	Asilimia %
1. Kibaharia/ Usafiri	08	02.768

Jadwali Na. 10 Maneno ya Kibaharia/ Usafiri.

Abiria عابرين : Kwenye lugha Kiarabu, neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi koromeo ^ʕ yenye ghuna na irabu ndefu chini kati *a:*, na kufuatiwa na sauti kipasuo midomo *b* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu ndefu mbele juu *i*: na nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /^ʕ*a:birijn*/. Hivyo lilivyo liko kwenye wingi na umoja wake ni ^ʕ*a:bir*. Neno hili lina maana ya “wenye kupita au wenye kwenda, wenye kuangalia kitu au jambo; wapitao bila ya kusimama wala kukaa; mwenye kutoka machozi; mwenye kuzingatia jambo kwenye nafsi yake bila ya kusema; mwenye kueleza.” El-Jar (1973:), El-Jawhari (--- : 441 Juz.i).

Kwenye Kiswahili linaanzia kipasuo koromeo ^ʔ kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*, na kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kuishia irabu fupi chini kati *a*. Neno hili muundo wake wa msingi ni [^ʔ*abiriə*]. Lina maana ya “mtu anayesafiri kwa chombo chochote.” KKS (2004:1).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, mosi, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu, mwanzo kuna sauti kipasuo koo /^ʔ/. Sauti hiyo imedondoshwa kwenye Kiswahili; vilevile mwishoni mwa

neni hilo kwenye Kiarabu kuna kiyeyushi kaakaa j na nazali ufizi n hizi nazo zimedondoshwa. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi, mwanzo lina irabu ndefu chini /a:/. Irabu hiyo imefupishwa kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, mwisho wa neno hili kuna irabu fupi chini /a/. Irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi kati /ə / kwenye Kiswahili. Nne, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili umejikita zaidi kwenye msafiri wa chombo chochote.

Baharia بحري : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kipasuo midomo b yenye ghuna na irabu irabu fupi chini a , na kufuatiwa na kikwamizi koromeo h kisicho cha ghuna na kumalizikia kwa kimadende r chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na kuishia kwa kiyeyushi kaakaa j na irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /baħrij/.

Katika Kiarabu lina maana ya “-enye uhusiano na bahari, mfanyakazi wa chombo cha baharini.” BAALBAKI (2003: 226).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa sauti hiyo hiyo kipasuo midomo b yenye ghuna na irabu fupi chini a na kufuatiwa na kikwamizi koromeo h chenye ghuna na irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i na irabu fupi kati $ə$ mwisho wake. Neno hili muundo wake wa msingi ni [bahariə]. Neno hili lina maana ya “mfanyakazi mtu mzima katika jahazi au meli.” BAKIZA (2010:15).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili kati lina sauti konsonanti kikwamizi koromeo /ħ/ kisicho cha ghuna. Sauti hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi koromeo /h/ chenye ghuna. Pili, kuna uongezaji sauti irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katikati kuna konsonanti mkusanyiko /hr/. Irabu fupi chini /a/ imeongezwa ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye neno hilo katika Kiswahili. Tatu, kuna udondoshi konsonanti, kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu; mwishoni kuna sauti kiyeyushi kaakaa /j/. Sauti hiyo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Nne, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Mwisho wa neno hili kuna irabu fupi nyuma juu /u/; irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi fupi kati /ə / kwenye Kiswahili. Kisemantiki hakuna badiliko lolote; kwa upande wa maana katika Kiswahili haina tafauti na ile maana ya Kiarabu.

Gidamu *قيدام*: Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kipasuo koromeo *q* nzito isiyo ya ghuna yenye irabu fupi nyuma juu *u*; na kufuatiwa na sauti kipasuo meno na ufizi *d* yenye ghuna na mkazo na irabu ndefu chini kati *a*: na kumalizikia nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*quda:m*/. Neno hili lina maana ya “mbele, usoni; sehemuya mbele.” BAALBAKI (2003: 851).

Katika Kiswahili linaanzia kwa sauti kipasuo kidakatonge *g* yenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*, na kufuatiwa na kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia nazali midomo *m* yenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hili muundo

wake wa msingi ni /gidamu/, lina maana ya “sehemu ya mbele ya jahazi au mashua.” KKS (2004:96).

Mabadiliko ya neno hili baada kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili mwanzo lina sauti kipasuo koromeo nzito /q/ kisicho cha ghuna; sauti hiyo imebadilika na kuwa kipasuo kidakatonge /g/ chenye ghuna katika Kiswahili. Pili, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili katikati lina sauti konsonanti /d/ yenye mkazo inayoashiria kuwa ni konsonanti radidi/kariri /dd/. moja kati ya hizo imedondoshwa. Tatu, kuna ufupishi irabu, neno hili kwenye muundo wake wa msingi; katikati lina irabu ndefu chini /a:/. Irabu hiyo imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika Kiswahili. Nne, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili umejikita zaidi kwenye sehemu ya mbele ya jahazi au mashua.

Kuabiri *عبر* : Neno hili kwenye Kiarabu linaanzia kwa sauti kikwamizi koromeo ^ʿ yenye ghuna na irabu fupi chini fupi *a*, na kufuatiwa na sauti kipasuo midomo *b* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /^ʿabar/, na lina maana ya “kupita, kuvuka kutoka upande mmoja kwenda mwengine; kutoka machozi, kulia.” El-Jawhari (--- : 441 Juz.I).

Katika Kiswahili linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* na irabu

fupi mbele juu *i*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*kuabiri*/, lina maana ya “kuvuka kwa kutumia chombo cha majini kama vile meli, mashua n.k.” KKS (2004:1).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi wa neno hili kwenye Kiarabu, mwanzo kuna sauti kikwamizi koromeo /*ʕ*/. Sauti hiyo imedondoshwa kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu; kati na mwisho wa neno hili kuna irabu fupi chini /*a*/. Irabu hizo zimebadilika na kuwa fupi fupi mbele juu /*i*/ kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili, umejikita zaidi kwenye uvukaji kwa kutumia chombo cha majini.

***Kukisi* قاس:** Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kipasuo kidakatonge *q* isiyo ya ghuna yenye irabu refu chini *a:*, na kufuatiwa na sauti kikwamizi ufizi kaakaa gumu *s* isiyo ya ghuna yenye irabu fupi chini *a*. Kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*qa:s* /. Kwenye Kiarabu linamaanisha “pima masafa , pima wingi; geza.” Moustafa (-- :770 Juz.ii).

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na kufuatiwa naa kipasuo kaakaa laini *k* na irabu fupi mbele juu *i*, na kufuatiwa na kikwamizi ufizi kaakaa gumu *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele *i*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*kukisi*/. Neno hilo lina maana ya “kugeza tanga ili jahazi ielekee upande wenye upepo, maana hii hasa kwa matumizi ya watu wa pwani; kubahatisha.” BAKIZA (2010).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili mwanzo lina sauti kipasuo kidakatonge /q/ chenye ghuna; sauti hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa kipasuo kaakaa laini /k/ kisicho cha ghuna. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi, mwanzo lina irabu ndefu chini /a:/. Irabu hiyo imefupishwa kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, mwisho wa neno hili kuna irabu fupi chini /a/. Irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Nne, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili nayo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia. Imejikita kwenye dhana hasa ile ya matumizi ya watu wa pwani yaani kugeuza tanga la jahazi ili kufuata upepo.

Nahodha **ناهد**: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu ndefu chini *a:* na kufuatiwa na kikwamizi koo *h* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i* na kumalizikia kipasuo ufizi meno *ḏ* chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /na:hiḏ/.

Neno hili kwenye Kiarabu linamaanisha “watoto wa ndege waliokwisha kamilika mabawa yao na wanaweza kuruka; msuli wa juu kwenye sehemu ya juu ya mguu wa farasi; mwenye kusimama, msimamaji; mfanyakazi mkakamavu katika kazi.” El-jar (1973:1187), bin Ubad (--: 290 Juz.I).

Kwenye Kiswahili linaanzia nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na kikwamizi koromeo *h* chenye ghuna na irabu fupi nyuma kati *ɔ* na kumalizikia kikwamizi meno chenye ghuna *ð* na irabu fupi chini *a*. Neno hili muundo wake wa msingi ni */nahɔða/*, na lina maana ya “kiongozi mkuu anayeongoza na kukiendesha chombo cha angani au baharini.” BAKIZA (2010:298).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi mwanzo lina irabu ndefu chini */a:/*. Irabu hiyo imefupishwa kwenye Kiswahili. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Kati na mwisho wa neno hili kuna irabu fupi mbele juu */i/* na nyuma juu */u/*. Irabu hizo zimebadilika na kuwa fupi nyuma kati *ɔ* na fupi chini */a/* kwenye Kiswahili. Tatu, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili mwisho lina sauti kipasuo meno ufizi */d̥/* chenye ghuna. Sauti hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi meno */ð/* chenye ghuna. Nne, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Maana hiyo mpya haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia, nayo imejikita kwenye dhana ya ukuu, uongozi na uendeshaji wa chombo cha angani na baharini.

Nauli نَوَال: Neno hili katika Kiarabu linaanzia kwa nazali meno ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi *a* chini, na kufuatiwa na kiyeyushi mdomo *w* chenye mkazo na irabu ndefu chini *a:* na kumalizikia kwa kitambaza ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu

muundo wake wa msingi ni /*nawá:l*/. Neno hilo lina maana ya “kitu / jambo litolewalo; kweli.” El-jar (1973:1230), Bin Ubaad (-- : 457 Juz. ii).

Kwa upande wa Kiswahili, neno hili linaanzia kwa nazali ufizi *n* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kufuatiwa na irabu fupi nyuma juu *u* na kumalizikia kwa kitambaza meno ufizi *l* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni /*nauli*/, na lina maana ya “malipo yanayotolewa kwa ajili ya safari.” KKS (1981:210).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili mwanzo lina sauti kiyeyushi mdomo *w* chenye mkazo; sauti hiyo katika Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi nyuma juu /*u*/. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi kati lina irabu ndefu chini /*a*/. Irabu hiyo imefupishwa kwenye Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika lugha hiyo. Tatu, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Mwisho wa neno hili kuna irabu fupi nyuma juu /*u*/. Irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi mbele juu /*i*/ kwenye Kiswahili. Nne, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili nayo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia. Maana hiyo imejikita kwenye dhana ya malipo ya usafiri.

Uledi **وليد** : Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa kiyeyushi midomo *w* na irabu fupi nyuma juu *u*, na kufuatiwa na kitambaza ufizi *l* na irabu fupi chini *a* na kiyeyushi kaakaa *j* na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na

nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */wulajd/*. Neno hili katika Kiarabu linamaanisha “mtoto aliyekwisha zaliwa hivi punde; kijana mdogo, mtoto mdogo mwanamume.” El-Jar (1973:9298) .

Kwenye Kiswahili, neno hili linaanzia kwa irabu fupi nyuma *u* na kitambaza ufizi *l* chenye irabu fupi kati mbele *ε* na kumalizikia kwa kipasuo ufizi *d* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni */uledi/*, na lina maana ya “kijana mdogo wa kiume ambaye ni mtumishi katika jahazi.” BAKIZA (2010 : 428), KKS (2004:433).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti, kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu; neno hili mwanzo lina sauti kiyeyushi mdomo *w*. Sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa irabu fupi nyuma juu */u/*. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Mwisho wa neno hili kuna kiyeyushi kaakaa na irabu fupi chini */aj/* zinazojitokeza kama irabu pacha. Irabu pacha hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi kati mbele */ε/* kwenye Kiswahili; vilevile kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili mwisho lina irabu fupi nyuma juu */u/* nayo kwenye Kiswahili imekuwa fupi mbele juu */i/*. Tatu, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili nayo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia. Imejikita zaidi kwenye kijana mwanamume mtumishi wa jahazini.

5.2.8 Maneno ya Kiujenzi na Vifaa vyake

Jina la Kundi	Idadi ya maneno	Asilimia %
1. Vifaa vya Ujenzi	06	02.076

Jadweli Na.11 Maneno ya Vifaa vya ujenzi.

Dari *دار*: Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kipasuo ufizi meno *d* yenye ghuna na irabu ndefu chini *a*; na kumalizikia kwa kimadende ufizi *r* chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */da:r/*, na lina maana ya “majumba ya, mahali penye majengo, kiambo, mtaa; nchi, eneo, mkoa.” El-Jar (1973:519).

Katika Kiswahili linaanzia kwa sauti kipasuo ufizi *d* yenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kumalizikia kwa kimadende *r* chenye ghuna na irabu fupi mbele juu *i*. Neno hilo muundo wake wa msingi ni */dari/*, na lina maana ya “sehemu ya juu ya chumba katika nyumba; sehemu ya nyumba iliyo kati ya sakafu ya juu na paa.” BAKIZA (2010:62).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi, mwanzo lina irabu refu chini */a:/*. Irabu hiyo katika Kiswahili imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika lugha hiyo. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu. Mwisho lina irabu fupi nyuma juu */u/*. Irabu hiyo imebadilika na kuwa fupi mbele juu kwenye Kiswahili */i/*. Tatu, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili, umejikita zaidi kwenye sehemu ya juu tu kwenye nyumba au chumba.

Ghorofa **غرفة** : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa kikwamizi kaakaa laini y chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u , na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na kujiwa na kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a na kumalizikia kwa kipasuo meno ufizi t kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu u na *nazali n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni */yurfah/*. Neno hilo lina maana ya “ maji yachotwayo kwa mkono, kata n.k.; chumba cha juu katika nyumba.” El-Jar (1973:875), Ibnu Mandhour (-- : 363 Juz.ix).

Katika Kiswahili neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kidakatonge y chenye ghuna na irabu fupi nyuma kati ɔ , na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu fupi nyuma kati ɔ na kumalizikia kwa kikwamizi meno mdomo f kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini a . Kwenye lugha hiyo ya Kiswahili, neno hilo muundo wake wa msingi ni */ghorofa/*, na linamaanisha “sehemu ya nyumba iliyojengwa juu ya dari ya nyumba.” BAKIZA (2010:98).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiarabu, kwanza, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu; mwanzo wa neno hili kuna irabu fupi nyuma juu */u/*. Irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi nyuma kati */ɔ/* kwenye Kiswahili; vilevile kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili mwisho lina irabu fupi nyuma */u/* nayo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa fupi chini */a/*. Pili, kuna uongezaji sauti irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili, katikati kuna

konsonanti mkusanyiko /rf/. Irabu fupi nyuma kati /ɔ/ imeongezwa ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Tatu, kuna upanuzi semantiki; neno hili limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyoko kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana pana zaidi kimaana, ambayo imejikita zaidi kwenye nyumba inayojengwa juu ya nyumba nyengine.

Jasi جَسَّ : Kweye Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi kaakaa gumu *ǰ* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kikwamizi ufizi mtandazo *š* kisicho cha ghuna chenye mkazo na irabu fupi nyuma juu *u na nazali n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*ǰasš*/, na lina maana ya “chokaa inyopakwa kwenye nyumba” El-Jar (1973:396), Ibnu Mandhour (-- : 10 Juz.vii).

Kwenye Kiswahili neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi kizuio kaakaa gumu *J* chenye ghuna na irabu fupi chini *a*, na kumalizikia kwa kikwamizi ufizi *s* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*Jasi*/, linamaanisha “aina ya jiwe laini linalovunjika na kuvuruguka kiurahisi hutengenezwa saruji.” KKS (2004:128), bakiza (2010 :129).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili kati lina sauti kikwamizi ufizi /*š*/ mtandazo; sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa

kikwamizi ufizi /s/. Pili, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu; mwisho lina irabu fupi nyuma juu /u/. Irabu hiyo imebadilika kwenye Kiswahili na kuwa fupi mbele juu /i/. Tatu, kuna ufinyu semantiki; ufinyu huo wa maana katika Kiswahili umejikita zaidi kwenye jiwe laini linalovurugika.

Saruji **صارج** : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi ufizi ʃ nzito / matandazo isiyo ya ghuna yenye irabu ndefu chini $a:$, na kufuatiwa na kimadende ufizi r chenye ghuna na irabu refu nyuma juu $u:$ na kumalizikia kwa sauti kikwamizi kaakaa gumu dʒ chenye ghuna na irabu fupi nyuma juu u na nazali n . Hii un ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni $/\text{ʃ}a:ru:\text{dʒ}/$, na linamaanisha “mchanganyiko wa jasi/chokaa na maji unaopakwa kwenye kuta.” El-Jar (1973:733), Ibnu Mandhour (-- : 310 Juz.ii).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia kwa sauti kikwamizi ufizi s isiyo ya ghuna yenye irabu fupi chini a , na kumalizikia kwa sauti kikwamizi kizuio kaakaa gumu J chenye ghuna na irabu fupi mbele juu i . Katika Kiswahili, neno hili muundo wake wa msingi ni $/sarufi/$, na lina maana ya “udongo unaotengenezwa kutokana na mchanganyiko wa udongo wa ufinyanzi, mawe, chokaa na jasi ambavyo vyote hivyo husagwa na kupatikana udongo laini wa ungaunga unaotumika kujengea nyumba au kutengenezea matofali n.k.” KKS 2004:360), BAKIZA (2010: 356).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, mosi, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili mwanzo lina sauti

kikwamizi ufizi /s/ matandazo; sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa kikwamizi ufizi /s/. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi, mwanzo na kati lina irabu ndefu chini /a:/ na nyuma juu /u:/. Irabu hizo zimefupishwa kwenye Kiswahili ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika lugha hiyo. Tatu, kuna ubadili irabu; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, mwisho wa neno hili kuna irabu fupi nyuma juu /u/. Irabu hiyo imebadilika na kuwa irabu fupi mbele juu /i/ kwenye Kiswahili. Nne, kuna upanuzi semantiki; neno hili limepata maana jumuishi kuliko ile maana iliyoko kwenye Kiarabu. Pia neno hili limezidi upeo wa maana kutokana na kujumuisha dhana pana zaidi ambayo imejikita zaidi kwenye udongo laini wa ungaunga unaotumiwa kwa kujengea na kufyatulia matufali.

Sakafu **سقف**: Katika Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi ufizi *s* isiyo ya ghuna yenye irabu fupi chini *a*, na kumalizikia kwa sauti kipasuo kidakatonge *q* isiyo ya ghuna na kufuatiwa na kikwamizi meno mdomo *f* kisicho ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*saqf*/.

Kwenye Kiarabu neno hili lina maana ya “sehemu ya juu inayofunika nyumba; mbingu; ndevu laini ndefu.” El-Jar (1973:666).

Kwenye Kiswahili neno hilo linaanzia sauti kikwamizi *s* isiyo ya ghuna na irabu fupi chini *a*, na kufuatiwa na sauti kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a* na kuishia kikwamizi meno mdomo *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u*. Neno hili muundo wake wa msingi ni /*sakafu*/, na lina maana ya “sehemu ya chini

ardhini iliyotiwa saruji ndani ya nyumba au nje ya nyumba, eneo la chini la nyumba lililotandazwa na kutiwa saruji.” BAKIZA (2010:353).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, mosi, kuna ubadili konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu, neno hili kati lina sauti kipasuo kidakatonge /q/. Sauti hiyo kwenye Kiswahili imebadilika na kuwa kipasuo kaakaa laini /k/. Pili, kuna uongezaji sauti irabu; kwenye muundo wa msingi wa neno hili katikati kuna konsonanti mkusanyiko /qf/. Irabu fupi chini /a/ imeongezwa ili kuondoa mkusanyiko huo kwenye Kiswahili. Tatu, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili ambayo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia. Imejikita zaidi kwenye eneo la nje au ndani ya nyumba lililotiwa saruji chini.

Shubaka شبك : Kwenye Kiarabu neno hili linaanzia kwa sauti kikwamizi kaakaa ufizi /f/ kisicho cha ghuna chenye irabu fupi juu *u*, na kufuatiwa na sauti kipasuo midomo *b* chenye ghuna na mkazo na irabu ndefu chini *a*: na kuishia kwa kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u* na nazali *n*. Hii *un* ya mwisho wa neno ni tanwini ambayo ni irabu, kwa kuwa Waarabu hawasimamii irabu mwisho wa neno, kwa hivyo neno hilo katika Kiarabu muundo wake wa msingi ni /*u*ba:k/.

Neno hili katika Kiarabu linamaanisha “dirisha lililotengenezwa kwa vyuma au mbao; nyavu ya kuvulia samaki; wavuvi watumiao nyavu.” El-Jar (1973:697).

Kwenye Kiswahili vivyo hivyo, neno hilo linaanzia kwa kikwamizi kaakaa ufizi *f* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi nyuma juu *u*, na kufuatiwa na sauti kipasuo midomo *b* chenye ghuna na irabu fupi chini *a* na kuishia kwa kipasuo kidakatonge *k* kisicho cha ghuna chenye irabu fupi chini *a*. Neno hili muundo wake wa msingi ni */shubaka/*, na lina maana ya “nafasi iliyofanywa ndani ya ukuta juu ya mlango au dirisha ili kuwekea vitu; sehemu ndogo iliyojitokeza juu ya jengo.” BAKIZA (2010:366).

Mabadiliko ya neno hili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kwanza, kuna udondoshi konsonanti; kwenye muundo wa msingi katika Kiarabu. Neno hili katikati lina sauti konsonanti */b/* yenye mkazo inayoashiria kuwa ni konsonanti radidi/kariri */bb/*; moja kati ya hizo imedondoshwa. Pili, kuna ufupishi irabu; neno hili kwenye muundo wake wa msingi, katikati lina irabu ndefu chini */a:/*. Irabu hiyo katika Kiswahili imefupishwa ili kwenda sambamba na mfumo wa irabu katika lugha hiyo. Tatu, kuna ubadili irabu, kwenye muundo wa msingi wa neno hili katika Kiarabu; mwisho lina irabu fupi nyuma juu */u/*. Irabu hiyo imebadilika kwenye Kiswahili na kuwa fupi chini */a/*. Nne, kuna semantiki hamishi; neno hili limepata maana mpya kwenye Kiswahili. Pia maana hiyo haina mwelekeo wala uhusiano na maana iliyotangulia, nayo imejikita zaidi kwenye nafasi ya kuwekea vitu ndani ya ukuta na sehemu iliyojitokeza juu kwenye jengo.

5.2.9 Muhutasari wa Uchambuzi wa Data za Maktabani

5.2.9.1 Utangulizi

Katika ukusanyaji wa data za maktabani, Mtafiti alikusanya jumla ya maneno 289 yanayohusu utafiti huu, ambayo ni sawa na asilimia 100%. Kwenye mchakato wa

uchambuzi, maneno hayo yaligawiwa katika makundi 8. Kundi la Kwanza ni la maneno ya Kibiashara/Kiuchumi lenye maneno 14 ambayo ni sawa na asilimia 4.844 %. Kundi la Pili la Kiutawala/Kisiasa lenye maneno 17 sawa na asilimia 5.882 %. Kundi la Tatu la maneno ya Kidini lina maneno 19 ni sawa na asilimia 6.574 %. Kundi la Nne la maneno ya Kitaaluma lenye maneno 26 sawa na asilimia 8.996 %. Kundi la Tano la maneno ya Kijamii lenye maneno 150 sawa na asilimia 65.439 % ya maneno yote yaliyokusanywa. Kundi la Sita la maneno ya Kifedha/ Kibiashara lenye maneno 09 sawa na asilimia 3.114. Kundi la Saba la maneno ya Kibaharia/Usafiri lenye maneno 08 sawa na asilimia 2.768 %. Kundi la nane la maneno ya Vifaa vya Ujenzi lenye maneno 06 sawa na asilimia 2.076 %.

5.2.9.2 Mabadiliko

Katika uchambuzi wa maneno hayo, kwa upande wa kisemantiki na kifonolojia mabadiliko yafuatayo yalibainika :

5.2.9.2 Sababu za Mabadiliko ya Kisemantiki

Kabla ya kuyabainisha mabadiliko yaliyoonekana, ni vyema kubaisha sababu za mabadiliko hayo ya kisemantiki. Kwa kweli sababu hazijuilikani; hasa kwa maneno yaliyoingia tangu vizazi vingi vilivyopita, kutokana na kuwa hakuna maandishi yanayoonesha au kueleza jinsi ya matumizi na hatua mbalimbali za kisemantiki kwenye maneno hayo katika nyakati mbalimbali. Kutokana na hali hiyo, katika mabadiliko ya maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili yaliyotafitiwa katika kazi hii, kwa ujumla mtafiti anaona na kupendekeza kuwa sababu za mabadiliko hayo ni:

- a) Nguvu ya ukopaji wa maneno (*borrowing dynamics*) kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa.
- b) Kupatikana dhana iliyopo katika neno hilo kwenye lugha chanzi (Kiarabu). Dhana hiyo hatimaye inatoa haja inayokidhi katika maana inayohitajika kwenye lugha lengwa (Kiswahili).
- c) Kuongeza nguvu ya kuwepo msamiati imara katika lugha lengwa.
- d) Kukidhi kimsamiati katika mawanda mbalimbali hasa kwenye nyanja hii ya Semantiki.
- e) Kukuza maendeleo ya kilughawiya na ukuaji wa lugha lengwa yenyewe kwa kupitia kuwepo maana zilizokopwa au maana mpya zilizobuniwa kutokana na maneno hayo yenye asili ya Kiarabu.

5.2.9.2.1 Kisemantiki

Maneno 86 ambayo ni sawa na asilimia 29.757 % ya maneno yote yaliyokusanywa na kutafitiwa, yanaonekana kuwa yana ufinyu wa maana baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, hali hiyo ni kinyume na vile yalivyo katika Kiarabu.

Maneno 115 ambayo ni sawa na asilimia 39.792 % kati ya maneno yote yaliyotafitiwa yanaonekana kuwa yana uhamishi wa maana ikilinganishwa na ile maana asilia katika Kiarabu.

Asilimia 3.114% ambayo ni sawa na maneno 9 katika maneno yote yaliyochunguzwa, haya yanaonekana kuwa na uimarishi wa maana baada ya kuhamia katika Kiswahili.

Asilimia 3.460% ambayo ni maneno 10 kati ya maneno yote yaliyochunguzwa, yanaonekana kuwa hayana mabadiliko yoyote ya kimaana, kwa maana ya kwamba maana asilia ya Kiarabu haikubadilika baada ya maneno hayo kwisha kuingia kwenye Kiswahili.

5.2.9.2.3 Kifonolojia

Asilimia 39.792 ambayo ni sawa na maneno 115 yaliyotafitiwa yanaonekana kuwa yana mbadala wa konsonanti kwenye miundo yake ya msingi baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili.

Maneno 200 ambayo ni sawa na asilimia 69.204% kati ya maneno yote yaliyochunguzwa yamebainika kuwa yana mbadala wa irabu katika miundo yake ya msingi baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili.

Asilimia 29.411% sawa na maneno 85 kati ya maneno yote yaliyotafitiwa, yanaonekana yana badiliko la ufupi wa irabu baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili.

Kuna uimarikaji wa irabu kwenye maneno 9 sawa na asilimia 3.114 % kati ya jumla ya maneno yaliyochunguzwa kwenye utafiti huu.

Maneno 41 sawa na asilimia 14.186% katika maneno yaliyochunguzwa, katika muundo wake wa msingi baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili yana konsonanti mkusanyiko.

Kuna badiliko la udondoshi wa konsonanti kariri kwenye miundo ya maneno 39 yaliyochunguzwa ambayo ni sawa na asilimia 13.494% ya maneno yote.

Maneno 29 ambayo ni sawa na asilimia 10.034 % yaliyotafitiwa yanaonekana kuwa na badilikiko la udondoshi wa konsonanti mwanzo, kati na mwisho wa miundo yake ya msingi baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili.

Asilimia 2.076% ambayo ni sawa na maneno 6 katika jumla ya maneno yaliyochunguzwa yanaonekana na badiliko linalotokana na kudondoshwa konsonanti na irabu baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili.

Asilimia 4.498% ambayo ni swa na maneno 13 kati ya jumla ya maneno yaliyochunguzwa yana mabadiliko yanayotokana na kudondoshwa irabu katika miundo yao ya msingi.

Asilimia 1.038% ambayo ni sawa na maneno 3 katika jumla ya maneno yaliyotafitiwa yanaonekana kuwa na badiliko la kuongezeka kipashio cha kauli ya kutendeka baada kwisha kuingia katika Kiswahili.

5.3 Uchambuzi wa Data za Uwandani

5.3.1 Utangulizi

Mtafiti amezigawa data za uwandani katika sehemu mbili, data zilizopatikana kwa kutumia njia ya dodoso.

Njia hii ilishirikisha jumla ya wadadisiwa 26 ambao ni sawa na asimia 100 % waliulizwa kwa njia ya dodoso. Wanawake 14 sawa na asilimia 53.846% na wanaume 12 sawa na asilimia 46.153, kwa ujumla umri wao ni kati ya miaka 23 na 40. Wadadisiwa hao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu Ngazi ya Diploma Mwaka wa Pili na Shahada ya Kwanza Mwaka wa Pili na wa Tatu. Hawa ni wanafunzi wanaosomea lugha ya Kiswahili, Kiarabu na Kiingereza.

Dodoso iliyotumika ina sehemu mbili. Sehemu ya Kwanza inahusu taarifa binafsi za mdadisiwa, umri, jinsia, elimu na kazi yake.

Sehemu ya Pili ya dodoso ina vipengele 3 A, B, na C .

Kipengele A cha Semantiki .

Kipengele B cha Fonolojia.

Kipengele C cha Mofolojia.

Kipengele A kilikuwa na maswali kumi (10). Vipengele B na C kila kimoja kilikuwa na maswali matano (5). Angalia Kiambatisho A.

Kila mdadisiwa alitakiwa kujibu masuala yote kwenye vipengele vyote vitatu. Alitakiwa kujibu kwa kutia aalama ya $\sqrt{\quad}$ kwenye mabano katika jawabu zilizotolewa.

Uchambuzi wa data hizo ni kama hivi ifuatavyo:

5.3.2 Kipengele A - Semantiki

Katika kuonesha uelewa wa wadadisiwa juu ya maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili, wadadisiwa wengi sawa na asilimia 57.692% wanaonekana kuwa wanayajua maneno ya asili ya Kiarabu katika Kiswahili kwa kiasi kikubwa. Pia wapo wale wanaoyajua kwa kiasi cha kati na kati ambao hawa siyo wengi ni asilimia 38.461%. Wapo wachache sawa na asilimia 7.692% wenye uelewa wa kiasi tu kwenye maneno hayo yenye asili ya Kiarabu. Kinacho jitokeza hapa, ni kwamba watu wengi waliodadisiwa wana uelewa wa kutosha wa maneno yenye asili ya Kiarabu na wachache wenye uelewa wa kati na kati.

Kwa kuwa maneno hayo yenye asili ya Kiarabu yanaeleweka vilivyo kama ilivyokwisha bainika hapo juu, bilashaka maneno haya yanasikika na pia kupatikana katika nyanja za matumizi kwa njia mbalimbali.

Kuhusu unasibu wa dhana kwenye maneno hayo, watu wengi waliodadisiwa asilimia 80.769% wanafikiri kwamba maneno hayo yanabeba dhana mnasibu katika Kiswahili. Wapo wachache sawa na asilimia 15.384% wao wanafikiri kwamba maneno hayo hayana dhana mnasibu kwenye Kiswahili. Lakini pia wapo wale ambao hawana uhakika juu ya unasibu wa dhana za maneno hayo kwenye Kiswahili, hao ni wachache mno, ni sawa na asilimia 7.692%.

Ni jambo la kawaida kwa lugha yoyote kukopa maneno kutoka kwenye lugha nyengine. Katika hali hiyo ya ukopaji wa maneno hasa Kiswahili hivi sasa, njia inayotumika kukopa maneno kutoka kwenye Kiarabu na kutiwa kwenye Kiswahili watu wengi waliodadisiwa kwa asilimia 69.230% hawafikiri kwamba njia hiyo si sahihi, lakini wadadisiwa wachache sawa na asilimia 11.538% wao wanaona kwamba njia hiyo ni sahihi. Asilimia 7.692% ambao ni watu wachache sana, wao hawajui kabisa kama njia hiyo ni sahihi. Kutokana na hali hii, maana yake ni kwamba inaonekana njia hiyo inayotumika hivi sasa katika ukopaji wa maneno ya Kiarabu ni sahihi ingawa kuna kasoro ndogo ndogo kwa mujibu wa wale wanaosema kuwa si sahihi.

Baadhi ya wakati, maneno yanapokopwa kutoka lugha moja kwenda lugha nyengine, kwenye Kiswahili kuna baadhi ya maneno yenye asili ya Kiarabu yanapewa dhana mpya ili kukidhi haja iliyopo. Katika kuangalia usahihi wa dhana inayoyotolewa kwenye maneno hayo, watu wengi waliodadisiwa sawa na asilimia 61.538% hawakubali kuwa dhana hizo ni sahihi. Wasailwa wachache sawa na asilimia 26.923% wao wanaona kwamba dhana hizo sio sahihi, asilimia kama hiyo 26.923% wao wanakubali kwamba

dhana hizo mpya ni sahihi. Watu wachache mno waliosailiwa sawa na asilimia 7.692% wao hawajui kama dhana hizo ni sahihi. Kinacho jitokeza hapa, tafsiri inayopatikana inaonesha kwamba dhana hizo zipo zile ambazo bado zina walakini juu ya usahihi wake.

Kuhusu kufahamika kwa maana ya maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili, watu wengi mno kati ya waliodadisiwa sawa na asimia 76.923% wanafahamu kwa kiasi maana ya maneno hayo. Wadadisiwa wachache sana sawa na asilimia 7.692% hawa wao wanafahamu sana maana ya maneno hayo yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili. Hii inamaanisha kwamba maneno hayo yenye asili ya Kiarabu, kimaana yanafahamika vilivyo.

Wadadisiwa wengi sawa na asilimia 50% wanaona kuwa maana asilia ya maneno hayo yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili inabakia kama ilivyo na haina mabadiliko yoyote. Lakini wapo wale wanaoona kwamba maana hiyo inabadilika, nao hawa ni kwa asilimia 46.153%. Mdadisiwa mmoja tu ambaye ni sawa na asilimia 3.846% kati ya wadadisiwa wote, yeye hajui lolote juu ya kubadilika au kutokubadilika kwa maana hizo.

Kuhusu kinyume cha maana kwenye maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili, watu wengi waliodadisiwa sawa na asilimia 65.384% wanakubali kwamba kuna maneno hayo yenye kinyume cha maana. Wadadisiwa wachache ambao ni sawa na asilimia 15.384% wanakataa kabisa kwamba hakuna maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili yenye kinyume cha maana; lakini vilevile wapo wadadisiwa ambao kwa

asilimia hiyo hiyo ya 15.384% wao hawajui kabisa kama kuna kinyume cha maana katika maneno hayo.

Kuhusu kukubaliana na utaratibu mzima wa kupewa kinyume cha maana maneno hayo yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili, wadadisiwa wengi sawa na asilimia 88.461% hawakubaliani kabisa na utaratibu huo wa kupewa maneno hayo kinyume cha maana, watu wachache kati ya waliodadisiwa sawa na asilimia 11.538% wanakubaliana na utaratibu huo wa maneno hayo kupewa kinyume cha maana.

Watu wengi mno waliodadisiwa sawa na asilimia 96.153% wanaona kwamba kutoa maana yenye kinyume kwenye maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili si sahihi. Mdadisiwa mmoja tu ambaye ni sawa na asilimia 3.846% anaona kwamba utaratibu huo ni sahihi.

Watu waliodadisiwa ambao sio wengi ni sawa na asilimia 23.676% walitoa sababu ya kukubali usahihi wa utaratibu wa kupewa kinyume cha maana maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili, sababu hiyo ni uundaji wa maneno na istilahi ambazo huingizwa kwenye taaluma ya sarufi, lakini pia ni kwa utaratibu huo hueneza msamiati wa Kiswahili. Wadadisiwa ambao ni sawa na asilimia 19.23%, ingawa ni wachache, wao walitoa sababu ya kutokukubaliana na utaratibu huo kwa kujenga hoja kwamba kunatokea upotoshaji wa maana iliyokusudiwa kwa kupewa maana iliyotafauti na maneno hayo katika asili yake, lakini pia maana ya maneno hayo ya lugha chanzi (Kiarabu) inapotezwa. Wadasiwa wachache ambao ni sawa na asilimia 15.384% wanaona kuwa sababu kubwa ni tabu ya utumiaji wa maneno hayo kwa maana iliyokusudiwa.

Watu wachache kati ya wadadisiwa, ambao ni sawa na asilimia 7.692% walitoa sababu hasi ambayo ni upotoshaji wa maana, uepaji wa asili halisi katika maana ya neno, ugumu wa ufahamu wa maana, Kiarabu kupotosha Kiswahili kwa upande wa maana, kuchafua hadhi ya lugha, kuongeza ugumu katika tafsiri, kuongeza msamiati wenye sifa ya kutokukubalika kimaana na kupoteza lengo la waanzilishi katika kutoa maana za maneno hayo yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili.

5.3.3 Kipengele B - Fonolojia

Wadadisiwa wengi sawa na asilimia 50% wanaonesha kuwa na uelewa mkubwa katika sauti za Kiarabu. Wadadisiwa sio wengi sawa na asilimia 38.461% wanaonekana kwamba uelewa wao wa sauti hizo ni wa kiasi kidogo, mdadisiwa mmoja ambaye ni sawa na asilimia 3.846% anazielewa juu juu tu sauti hizo.

Kwa upande wa sauti za Kiswahili, wadadisiwa wengi sawa na asilimia 68.230% wanaonesha uelewa mkubwa sana katika sauti hizo. Watu wachache kati ya waliodadisiwa sawa na asilimia 34.615% wana uelewa wa kiasi katika sauti za Kiswahili ambapo mdadisiwa mmoja ambaye ni sawa na asilimia 3.846% anazijua juu juu tu sauti hizo za Kiswahili. Kinacho bainika hapa ni kwamba watu wengi sawa na asilimia 84.846% wana uelewa mkubwa wa sauti za lugha mbili hizi Kiarabu na Kiswahili..

Kwa upande wa tafauti baina ya mpangilio wa kisauti kati ya Kiarabu na Kiswahili, wadadisiwa wengi sawa na asilimia 68.230% wanaona kuwa kuna tafauti kubwa, ambapo wadadisiwa wachache sawa na asilimia 26.923% wanaona kwamba kuna tafauti ndogo. Lakini wadadisiwa wachache zaidi sawa na asilimia 7.692% wanaona kuwa hakuna

tafauti yoyote ya mpangilio wa kisauti. Mdadisiwa mmoja ambaye ni sawa na asilimia 3.846% yeye hajui lolote.

Kuhusu usawa wa kimatamshi wa sauti za maneno yenye asili ya Kiarabu kama vile yanavyotamkwa kwenye Kiarabu. Wadadisiwa wengi sawa na asilimia 65.384% wanaona kwamba matamshi ya sauti hizo hayako sawa na yale matamshi yake katika Kiarabu. Wapo wale wanaoona kwamba matamshi ya sauti hizo zinatamkwa sawa sawa kama katika Kiarabu, hawa ni wachache ambao ni sawa na asilimia 34. 615%.

Katika kuainisha mifano ya sauti za maneno yenye asili ya Kiarabu, watu ambao si wachache mno sawa na asilimia 46.153% kwa kutumia mifano ya maneno yenye sauti kikwamizi koromeo [ḥ]. Wadadisiwa wapatao asilimia 38.461% waliainisha sauti kipasuo kidakatonge [q]. Wadadisiwa sawa na asilimia 30.769% wao waliainisha kikwamizi ufizi [ʃ] vivyo hivyo, wadadisiwa asilimia 23.676% sauti kiwamizi [x], kipasuo koo [ʔ] na kikwamizi kaaka gumu [ʃ]. Wadadisiwa sawa na asilimia 11.538 waliainisha sauti kipasuo koromeo [ʔ] na kikwamizi kaaka laini [ɣ] na wadadisiwa wawili sawa na silimia 7.692% waliainisha sauti kikwamizi meno [ð].

5.3.4 Kipengele C - Mofolojia

Watu wengi mno waliodadisiwa sawa na asilimia 88.461% walibainika kuwa na fununu na maarifa ya wastani katika mofolojia ya Kiswahili. Wadadisiwa wachache mno sawa na asilimia 7.692% wao wana fununu na maarifa kwa kiasi kikubwa. Mdadisiwa mmoja sawa na asilimia 3.846% yeye hana maarifa wala fununu yoyote juu ya upande huo wa Kiswahili.

Kuhusu baadhi ya vishirikishi vya asili ya Kiarabu vinayounda viambishi awali vinavyoonesha umoja na wingi kwenye maneno ya Kiswahili, watu wasiokuwa wachache ambao ni sawa na asilimia 42.302% wanakubaliana na mjengeko wenye sura hiyo. Lakini pia asilimia kama hiyo ya 42.302% wadadisiwa wengine wao hawana uhakika wa hilo.

Kiambishi *mi* katika maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili kuchukuliwa kama ni sawa na kiambishi cha wingi ambapo umoja wake ni *m*. Watu wengi waliodadisiwa sawa na asilimia 53.846% wanakubaliana na mjengeko huo. Wapo wachache sawa na asilimia 19.230% wanapinga kabisa hali hiyo na kuona kuwa si sahihi pia wapo wa kiwango cha asilimia hiyohiyo ambao wao wanaonesha kuwa hapana uhakika wa hilo. Hapa inaonekana kwamba maneno hayo yenye mjengeko huo moja kwa moja yanakubaliana na kufuata utaratibu huo wa kimofolojia katika Kiswahili.

Wadadisiwa wengi sawa na asilimia 57.692% wanasema kwamba yapo maneno machache yenye asili ya Kiarabu yaliyofanywa kuwa na mfumo wa Kiswahili na viambishiawali vyake katika wingi kubadilika. Wadadisiwa wachache sawa na asilimia 19.230% wanakubali kwamba yapo maneno hayo kwa wingi, lakini wadadisiwa wachache mno ambao ni sawa na asilimia 11.538% wao hawana uhakika huo kwenye maneno hayo. Mdadisiwa mmoja sawa na asilimia 3.846% yeye anaona kwamba maneno kama hayo hayapo kabisa. Kutokana na hali hii, inaonesha kuwa baadhi ya maneno yanayotoka kwenye Kiarabu yanaweza kukubaliana na utaratibu huo.

Kwenye uhusiano wa kimofolojia baina ya Kiarabu na Kiswahili, wadadisiwa wengi sawa na asilimia 57.692% wanaona kwamba uhusiano uliokuwepo ni kwa sehemu ndogo.

Wadadasiwa wachache sana sawa na aslimia 15.384%, wao wanaona kuwa haupo kabisa. Wapo wadadasiwa wachache sawa na asilimia 26.923%, wao wanaona kuwa upo uhusiano mkubwa. Hapa inaonekana kuwa uhusiano huo upo lakini si kwa maeneo yote.

5.4 Uchambuzi wa Data za Njia ya Mahojiano

5.4.1 Utangulizi

Katika mahojiano aliyofanya Mtafiti na walimu/weledi wa lugha, bilashaka Wahojiwa wote hawa ni wazungumzaji wazawa wa Kiswahili. Mahojiano hayo yalikuwa na vipengele saba navyo ni: Unasibu wa dhana na maana, Usahihi wa utoaji wa dhana, Kubaki kwa maana asilia ya maneneno yenye asili ya Kiarabu, Kuwepo kwa uhusiano wa maana mpya na maana asilia za lugha chanzi, Kuwepo kwa kinyume cha maana hasa baada ya maneno yenye asili ya Kiarabu kwisha kuingia katika Kiswahili, Sababu zinazopelekea kuwepo hali hiyo ya kinyume cha maana ya maneno hayo yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili na Maoni juu ya utoaji wa maana iwe sahihi au si sahihi. Jumla ya wahojiwa 10 ambao ni sawa na asilimia 100% walishiriki katika mahojiano hayo.

5.4.2 Unasibu wa Dhana na Maana

Wahojiwa wengi sawa na asilimia 50% wanasema kwamba dhana pamoja na maana za maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili zina unasibu ndani yake MH 6,7,8,9 na 10 wamethibitisha hivyo. Wapo wahojiwa wachache ambao ni sawa na asilimia 40% wao wanaona kwamba kwenye maneno hayo hakuna unasibu wowote, MH.1,3 na 5. Asilimia 10% MH.4 anaona kwamba unasibu upo kwa baadhi ya maneno hayo na kwa baadhi ya

maneno hayo unasibu haupo. Kinachojitokeza wazi hapa kwa mujibu wa uchunguzi wa kipengele hiki, ni kwamba kwa kiasi kikubwa unasibu wa dhana na maana upo kwenye maneno hayo.

5.4.3 Usahihi wa Utoaji wa Dhana

Wahojiwa wengi sawa na asilimia 50 % wanasema kwamba, utoaji wa dhana ya maneno hayo yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili si sahihi hata kidogo. Hilo linathibitishwa na MH.3,5,6,8 na 9. Wahojiwa wachache ambao ni sawa na asilimia 40%, MH.1,3,6,7 na 9 hawa wao wanaona kuwa utoaji wa dhana ya maneno hayo ni sahihi. Mtu mmoja MH.5 ambaye ni sawa na asilimia 10 % anaona kuwa siyo sahihi kwa baadhi ya maneno tu, vilevile MH.6 ambaye ni sawa na asilimia hiyo hiyo 10 % anaona kuwa ni sahihi kwa baadhi ya maneno na kwa baadhi ya maneno mengine si sahihi. Kinachojitokeza hapa, kwa mujibu wa uchunguzi wa kipengele hiki, ni wazi kwamba utoaji wa dhana ya maneno hayo si sahihi au una kasoro nyingi.

5.4.4 Kubakia kwa Maana Asilia ya Kiarabu

Zaidi ya nusu ya wahojiwa ambao ni sawa na asilimia 70% wanaona kwamba baadhi ya maneno hayo maana hiyo asilia inabakia kama ilivyo na baadhi ya maneno mengine maana hiyo haibakii inaondoka moja kwa moja hilo linathibitishwa na MH.2,3,4,5,7,8 na 9. Lakini wahojiwa wachache sawa na asilimia 20% MH.4 na 5 wao wanaona kwamba maana asilia ya maneno hayo inabakia kama ilivyo. Asilimia 10 % mtu mmoja MH.10 anaona kwamba maana hiyo asilia haibaki asiliani. Kinachojitokeza hapa, kwa mujibu wa uchunguzi wa kipengele hiki ni kwamba, kwa kiasi kikubwa baadhi ya maneno hayo

maana yake inabakia na katika baadhi ya maneno kwa kiasi kidogo maana hiyo inaondoka kabisa.

5.4.5 Uhusiano wa Maana Mpya na Maana Asilia za Lugha Chanzi

Wahojiwa wengi mno ambao ni sawa na asilimia 80% wanaona kwamba hakuna uhusiano wa maana mpya na maana asilia za lugha chanzi MH.1,2,3,4, 7 na 8 wanathibitisha hivyo. Watu wawili MH.5 na 6 ambao ni sawa na asilimia 20 % wanasema kwa kuthibitisha kwamba upo uhusiano wa kulazimishwa kwenye maana hizo mpya na maana asilia. MH.9 mmoja ambaye ni sawa na asilimia 10 %, anaona kwamba upo uhusiano kwa baadhi ya maneno na kwa baadhi nyengine ya maneno hayo haupo. Katika uchunguzi wa kipengele hiki, kinachojitokeza ni kwamba hakuna uhusiano wa maana mpya na maana asilia za maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili.

5.4.6 Kinyume cha Maana

Watu wengi waliohojiwa sawa na asilimia 90% wanaona kwamba yapo maneno yenye kinyume cha maana baada ya maneno hayo kwishakuingia katika Kiswahili, hayo yanathibitishwa na MH.1, 2, 4, 5, 6,7, 8, 9 na 10 lakini mtu mmoja MH.6 ambaye ni sawa na asilimia 10% anaona kwamba hakuna kabisa kinyume cha maana katika maneno hayo. Kutokana na uchunguzi wa kipengele hiki, inaonekana kwamba kipo kinyume cha maana hasa kwenye maneno hayo yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili.

5.4.7 Sababu za Kinyume cha Maana

Watu wengi ambao ni sawa na asilimia 80% wameainisha sababu kubwa ni kutokujulikana kwa lugha ya Kiarabu, hali hiyo imethibitishwa na MH.1,4, 6,7, 8 na 10 . Watu wawili sawa na asilimia 20% MH. 3 na 5 wameainisha sababu ya hali nzima ya kutojua maana ya maneno ya Kiarabu lakini sababu kubwa zaidi ni upinzani wa ile dhana ya kuwa Kiarabu kina maneno mengi mno kwenye Kiswahili. Uchunguzi kwenye kipengele hiki umebaini kwamba sababu kubwa ni kutokujua Kiarabu hasa kwa wale wanaojaribu kuyachukua maneo kama hayo kwa mara ya kwanza na kuyatumia katika Kiswahili kwa njia isyosahihi na hatimaye kubakia katika hali hiyo ya kinyume.

5.4.8 Maoni ya Wahojiwa Juu ya Utoaji wa Maana Iwe Sahihi au si Sahihi

Watu wengi ambao sawa na asilimia 70% wanaona kuwa watu wajifunze lugha ya Kiarabu kutokana na umuhimu uliopo kwenye lugha hiyo, hali hiyo inathibitishwa na maelezo ya *MH. 1, 2, 4, 5, 6,7, na 10. Watu wawili, MH.3 na 7 ambao ni sawa na asilimia 20% wanatoa maoni yao kwa kutoa wito wa kufanywa utafiti zaidi. Maoni mengine ya wahojiwa kama vile hima ndogo ya ufundishaji wa Kiarabu, utunzaji wa lugha mbili hizi Kiarabu na Kiswahili, kutoogopa mambo mapya na mabadiliko katika Kiswahili, kuhusishwa maana asilia ya maneno ya Kiarabu katika Kiswahili, kubadilisha na kurekebisha kwa njia ya kutoa maelezo kwenye maneno hayo na maana zake, maneno yaliyoingia katika Kiswahili tangu zamani hayo yaendelee kutumika, kwa yale yatakayoingizwa hapo baadaye basi kwanza waulizwe wataalamu wa Kiarabu, maana ya

maneno yanayochukuliwa iwe sawa na maneno hayo katika lugha chanzi yaani Kiarabu.
Maoni yote haya yametolewa na wahojiwa wachache ambao ni sawa na asilimia 10 % .

SURA YA SITA

6.0 MATOKEOYA UTAFITI

6.1 Utangulizi

Baada ya mchakato mzima wa ukusanyaji na uchambuzi wa data, mtafiti aligundua matokeo mbalimbali yanayotokana na utafiti huu wa mabadiliko ya maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili. Matokeo hayo ni kama yafuatayo:

6.2 Semantiki

- Kwa kupitia utafiti huu, imebainika kwa asilimia 29.757% kwamba maneno yenye asili ya Kiarabu yana ufinyu wa maana baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili. Hali hiyo ni kinyume na vile yalivyokuwa maneno hayo katika Kiarabu.
- Utafiti huu umegundua kwamba, maneno hayo kwenye Kiswahili yana uhamishi wa maana kwa asilimia 39.792% ikilinganishwa na ile maana asilia ya Kiarabu.
- Kwa uchunguzi uliofanywa kupitia utafiti huu, imeonekana kwamba maneno haya yenye asili ya Kiarabu kwa asilimia 3.114 % yana uimarishi wa maana baada ya kuingia kwenye Kiswahili.
- Utafiti umebaini kwamba, maneno hayo kwa asilimia 3.460 % hayana mabadiliko yoyote ya kimaana, hapa inakusudiwa kuwa maana asilia ya Kiarabu haikubadilika baada ya kuingia kwenye Kiswahili.

6.3 Fonolojia

- Utafiti umegundua kwamba, kwa asilimia 39.792 % maneno hayo yanambadala wa konsonanti kwenye miundo yake ya msingi baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili.
- Kwa asilimia 69.204% maneno hayo yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili, yamebainika kuwa na mbadala wa irabu kwenye miundo yake ya msingi baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili.
- Kwa kupitia uchunguzi huu, imeonekana kuwa uimarikaji wa irabu kwenye maneno hayo una nafasi ya asilimia 3.114 %.
- Imeonekana kuwa, maneno haya kwa asilimia 14.186% yana konsonanti mkusanyiko katika miundo yake ya msingi baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili.
- Utafiti umebaini kwamba kuna udondoshi wa konsonanti kariri/radidi kwenye maneno hayo katika miundo yake ya msingi kwa asilimia 13.494 %.
- Kwa kupitia utafiti huu, imegundulika kuwa, kwa asilimia 10.034 % maneno hayo yana badiliko la udondoshi konsonanti mwanzo, kati na mwisho wa miundo yake ya msingi baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili.

- Uchunguzi kwa kupitia utafiti huu, umebaini kwamba kuna udondoshi wa konsonanti na irabu kwa asilimia 2.076 % ya maneno hayo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili.
- Utafiti umegundua kwamba, kwa asilimia 4.498%, maneno hayo yana badiliko la kudondoshwa irabu kwenye miundo yake ya msingi baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili.
- Kwa asilimia 1.038% imegunduliwa katika uchunguzi huu kwamba maneno hayo yana badiliko la kuongezeka kipashio cha kauli ya kutendeka mwisho hasa kwa vitenzi baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili.

6.4 Matokeo Mengine Kiujumla

6.4.1 Semantiki

- Utafiti umegundua kwamba maneno yenye asili ya Kiarabu yanaeleweka kwa kiasi kikubwa kwa asilimia 28.846 %, lakini pia ipo hali ya uelewa wa kati na kati ambao ni sawa na asilimia 19.230 % na hali ya uelewa mdogo na wa chini kwenye maneno hayo ni kwa asilimia 3.846 %.
- Kwa kupitia Utafiti huu, imebainika kwa asilimia 69.230% kwamba maneno yenye asili ya Kiarabu baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili yanachukua dhana mnasibu, ingawa kwa asilimia 20.384 % yanaonekana kinyume chake

kwamba hayana dhana mnasibu. Unasibu na kutokuwepo unasibu kwa baadhi ya maneno ni sawa na asilimia 9%. Zipo hisia za kutoeleweka unasibu huo, japo kuwa ni kwa kiasi kichache ambacho ni sawa na asilimia 1.390 %.

- Utafiti umebaini kwamba, namna ya ukopaji wa maneno hayo; hasa kwa wakati huu; unaonekana kuwa si sahihi kwa asilimia 69.230% pamoja na kasoro za hapa na pale ilibainika kwa asilimia 5.769 % usahihi wa wa ukopaji huo.
- Kwa kupitia utafiti huu, inaonekana, kwa asilimia 69.230 %, kwamba utoaji wa dhana mpya za maneno hayo kwenye Kiswahili si sahihi. Kinachojitokeza ni kuwa dhana hizi zina kasoro kwenye usahihi wake kwa hivyo usahihi wake ni kwa asilimia 23.846 %. Kwa baadhi ya maneno, usahihi wa dhana ni sawa na asilimia 5.555%, ile dhana ya kuwa baadhi ni sahihi na baadhi si sahihi ni sawa na asilimia 5.555%.
- Uchunguzi umebaini kwamba maneno hayo yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili yanafahamika kwa kiasi kikubwa kuwa ni maneno ya Kiswahili kama maneno mengineyo, hali hiyo ni kwa asilimia 76.923%. Lakini ufahamikaji wake kwa kiwango kikubwa au cha juu kama ni maneno ya Kiarabu, hali hiyo inajitokeza kwa asilimia 7.692 % kwa sababu wale wanaoyajua maneno haya ni wachache ambao wana uelewa wa kutosha wa Kiarabu.

- Utafiti umebaini kwa asilimia 60 % kwamba, maana asili ya maneno hayo inabaki kama ilivyo na haina mabadiliko yoyote kwa baadhi ya maneno katika Kiswahili. Hali ya mabadiliko ya maana asilia ipo kwa asilimia 33.076 %. Inajitokeza kwa asilimia 1.923 % hali ya bainabaina kwa maana ya kubadilika na kutobadilika kwa maana asili. Kutokubaki kwa maana ni sawa na asilimia 2.777%.
- Utafiti umebaini kwa asilimia 77.692 % maneno hayo yana kinyume cha maana, lakini kinyume chake hali hiyo ilibainika kwa asilimia 12.692% kuwa maneno hayo katika Kiswahili hayana kinyume.
- Uchunguzi umegundua kwa asilimia 44.230 % utaratibu wa kupewa kinyume cha maana ya maneno hayo yenye asili ya Kiarabu haukubaliki. Imeonekana kwamba utaratibu huo unakubalika kwa asilimia 5.769 %.
- Kwa kupitia utafiti huu, imebainika kwa asilimia 48.076% kwamba maneno hayo kupewa maana yenye kinyume si jambo sahihi. Hata hivyo zipo hisia kwa asilimia 1.923% kuwa hali hiyo ya kupewa kinyume cha maana ni sahihi.
- Utafiti umebaini kwa asilimia 11.838% sababu ya usahihi wa kupewa kinyume cha maana maneno hayo yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili, ni kutokana na uundaji wa istilahi na maneno. Istilahi hizo baadaye zinaingizwa kwenye taaluma k.v. sarufi; vilevile utaratibu huo unaongeza msamiati wa Kiswahili.

- Kutokukubaliana na utaratibu huo wa kinyume ni kwa asilimia 9.615 %, ni kwa sababu ya kutokana na upotoshaji wa maana iliyokusudiwa, maana ambayo ni tafauti kabisa na maneno yenyewe katika asili yake, lakini pia maana ya maneno hayo ya lugha chanzi inapotezwa.
- Utafiti umebaini kwa asilimia 43.846% ni kutokana na sababu ya tabu ya utumiaji wa maneno hayo katika maana inayokusudiwa. Hali ya kutokujua maana ya maneno ni pamoja na upinzani juu ya dhana kuwa Kiswahili kina maneno mengi ya Kiarabu, hali hii ni kwa asilimia 20%.
- Sababu hasi asilimia 23.846% ni upotoshaji wa maana, ukwepaji wa asili halisi ya maana, ugumu wa kufahamika, Kiarabu kupotosha Kiswahili hasa kwa upande wa maana ya maneno, kuchafua hadhi ya lugha, kuongeza ugumu wa tafsiri, kuongeza msamiati wenye sifa ya kutokukubalika kimaana na kupoteza lengo la waanzilishi katika kutoa maana za maneno hayo yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili, kutokujua Kiarabu vyema kwa wale wanaoyachukua maneno ya lugha hiyo kwa mara ya kwanza na kuyatia kwenye Kiswahili.

6.4.2 Mofolojia Kipengele B

- Utafiti umebaini kiasi cha wastani katika fununu na maarifa ya mofolojia ya Kiswahili kwa asilimia 88.461 %, kiasi kikubwa cha fununu ma maarifa ni kwa

na asilimia 7.692 %, na hali ya kutokuwa na maarifa wala fununu yoyote ni kwa asilimia 3.846%.

- Utafiti umegundua kwamba baadhi ya vishirikishi vya asili ya Kiarabu vinavyounda viambishi awali vya umoja na wingi kwenye maneno ya Kiswahili vinakubaliana kwa asilimia 42.302% na kwa asilimia hiyohiyo inaonesha hali ya kutokuwepo uhakika wa hilo.
- Utafiti umebaini kwamba, kiambishi *mi* katika maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili kuchukuliwa kama ni sawa na kiambishi cha wingi ambapo umoja wake ni *m* kwa asilimia 53.846% kukubaliana na mjengeko huo. Kwa asilimia 19.230% kuna hali ya kutokuwa sahihi pia kwa asilimia hiyo hiyo ya kutokuwa na uhakika wa hilo. Inaonekana kwamba maneno hayo yenye mjengeko huo moja kwa moja yanakubaliana na kufuata utaratibu huo wa kimofolojia katika Kiswahili.
- Kwa asilimia 57.692% utafiti umebaini maneno machache yenye asili ya Kiarabu yaliyofanywa kuwa na mfumo wa Kiswahili na viambishiawali vyake katika wingi kubadilika. Kwa asilimia 19.230% yapo maneno hayo kwa wingi, kwa asilimia 11.538% kuna hisia za kutokuwa na uhakika wa kuweco maneno hayo. Kwa asilimia 3.846% maneno kama hayo hayapo kabisa. Kutokana na hali hii, inaonesha kuwa baadhi ya maneno yanayotoka kwenye Kiarabu yanaweza kukubaliana na utaratibu huo.

- Utafiti umegundua kwa asilimia 57.692% uhusiano wa kimofolojia baina ya Kiarabu na Kiswahili ni kwa sehemu ndogo; kwa asilimia 15.384% inaonekana kuwa haupo kabisa na kwa asilimia 26.923% upo uhusiano mkubwa. Hapa inaonekana kuwa uhusiano huo upo lakini si kwa maeneo yote.

6.5 Mapendekezo na Maoni

6.5.1 Utangulizi

Baada ya kukamilika ukusanyaji, uchambuzi wa data na utoaji wa matokeo ya kazi hii ya utafiti; Mtafiti kwa mujibu wa kazi yake hii, anatoa mapendekezo pamoja maoni kutokana na yale yaliyojitokeza na kuonekana katika utafiti huu.

Kwa hivyo basi, maoni na mapendekezo ya mtafiti ni haya yafuatayo:

1. Kwa yale maneno ya asili ya Kiarabu yanayozushwa kimaana na yakawa yanatumika mitaani, maneno hayo hayana haja ya kushughulikiwa bali yaachwe kama yalivyo na hatimaye yatapotea na kuondoka wenyewe.
2. Kwa kuwa inaonekana mara nyingi, baadhi ya maneno yanapokopwa hasa haya yenye asili ya Kiarabu, unasibu wake unapungua. Kwa hivyo yanapochukuliwa maneno hayo ni vyema yakawa yana unasibu wake kimaana na ile maana asilia kwenye lugha chanzi yaani Kiarabu.
3. Kuna haja ya kutafutwa njia muafaka ya kuyaangalia maneno yenye kinyume cha maana, ikiwezekana kubadilishwa kinyume hicho. Kadhalika kurakibisha yale yanayotumiwa kwenye maandiko mbalimbali k.v. magazeti , vitabu n.k.

4. Utumiaji wa maneno ya Kiswahili usiozingatia usahihi wa maana, unaathiri pia kwenye maneno ya Kiarabu, utafutwe utaratibu maalumu utakaotumika kukosoa hali hiyo ilivyo.
5. Kutumika kikamilifu wataalamu wa Kiarabu katika utaratibu mzima wa kuyabaini maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili yanayohitaji kuangaliwa na kupitiwa tena kimaana.
6. Kutopuuzwa ushauri wa wataalamu hao wa lugha ya Kiarabu hasa kwa upande wa maana ya maneno yenye asili ya Kiarabu.
7. Kutiliwa mkazo ufundishaji wa lugha ya Kiarabu katika taasisi mbalimbali za kitaaluma ndani ya jamii yetu.
8. Hata kama si kwa kiwango cha aina moja, ipo haja kwa watu kujifunza Kiarabu.
9. Kwa kuwa Kiarabu nacho kina nafasi ya taaluma za kifiq-hi katika Kiswahili, hivyo ni lazima watu wajifunze na wasome lugha hiyo ya Kiarabu.
10. Kuwa na ufahamu japo mdogo kwenye neno linalokopwa kutoka kwenye Kiarabu na kuingizwa kwenye Kiswahili.
11. Kufanywa utaratibu wa mapitio ya maneno ya asili ya Kiarabu katika Kiswahili ambayo yana maana zenye kinyume.
12. Kwa vile kuna imani kwamba Kiswahili ni chetu, kutokana na nafasi ya lugha ya Kiarabu ilivyo kwenye Kiswahili, hapana budi kwa Vyuvo vya Zanzibar kushughulikia zaidi lugha mbili hizi, zifundishwe vilivyo ili hatimaye wapatikane watu wenye uwezo wa kufanya tafiti za kina kwenye lugha hizo.
13. Ikiwa kwenye Kiarabu kuna mambo mapya, basi si vibaya maneno yanayohusiana na mambo hayo mapya yakapendekezwa na kuchukuliwa na

hatimaye kutiwa kwenye Kiswahili hata kama yatabadilishwa matamshi lakini maana isiwe mbali sana na ile maana ya Kiarabu, hilo ni jambo la msingi.

14. Kuangaliwa vizuri kama kuna uwezekano wa kufanywa mabadiliko kwenye maana hasa kwa yale maneno yenye matatizo.
15. Ipo haja ya kuzingatiwa uasili wa maneno hayo yaliyoko kwenye Kiswahili, ili yawe kama lugha nyenginezo zinazokopa maana pia.
16. Kuacha kukurupuka hasa kwa wale wanaofanya kazi ya uundaji, utohoaji na usanifishaji wa maneno hasa yanayotoka kwenye Kiarabu.
17. Ipo haja ya kuhakikisha usahihi wa maana ya maneno ya Kiarabu kabla ya kuyachukua; hali hiyo itapatikana kwa kuyaulizia kwanza maneno hayo.
18. Kushirikishwa watu wengine wanaojua katika kuwauliza kuhusu maneno yanayokopwa, kwani hali hiyo itasaidia katika upatikanaji wa dhana sahihi na nzuri.
19. Kuepuka kuiga kutokana na kusikia maneno yasiyo na usahihi.
20. Kupimwa, kuthibitishwa maneno hayo na pia kutolewa maelekezo juu ya namna ya matumizi sahihi kimaana.
21. Wataalamu wanaohibitisha maneno hayo yatumike vipi kwenye Kiswahili, ni lazima wawe na uelewa na ufahamu wa lugha ya Kiarabu.
22. Mtafiti amechunguza eneo hili la mabadiliko kwenye uwanja huu wa maneno hasa kwenye nomino. Ipo haja kubwa ya utafiti zaidi, katika maeneo mengine ya uwanda unaohusiana na utafiti huu kwenye muundo wa vitenzi, vielezi na vivumishi vya maneno haya ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu.

6.6 Hitimisho

Kazi ya utafiti huu imeanzia kwa kutazama uhusiano wa kihistoria uliopo baina ya wenye lugha mbili hizi, Kiswahili na Kiarabu, pia imeangalia maingiliano ya watu hao kijamii, kiutamaduni na kidini. Maingiliano hayo yametazamwa kwa kiasi gani yalivyotoa mchango na kuathiri katika Kiswahili.

Kwa kuwa kazi hii imejikita zaidi kwenye lugha kwa ujumla na hasa kwenye maneno yenye usuli wa Kiarabu, ilionekana ni vyema kupata historia fupi za lugha mbili hizi. Mtafiti amefanya hivyo kwa ufupi sana.

Kutokana na mada ya utafiti huu ambayo ni “Mabadiliko ya Kifonolojia na Kisemantiki katika Maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu”, kwenye tatizo la utafiti, inaonekana kumekuwa na utaratibu wa kuchukuliwa maneno ya Kiarabu na kuingizwa katika Kiswahili. Imebainika kwamba maneno hayo au baadhi yake yanapewa maana nyengine kinyume na ile maana ya asili au wakati mwengine maana hizo katika Kiswahili zinakuwa hazina usahihi kwa mujibu wa maoni ya Mtafiti.

Kwa hivyo, lengo kubwa la Mtafiti ni kujaribu kuyachunguza maneno hayo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili. Katika hali hiyo, Mtafiti kwa umahasusi alilenga kuyatazama maneno hayo kwa kuyatafiti kisemantiki na kifonolojia kwenye Kiswahili na Kiarabu.

Umuhimu uliopo kwenye utafiti huu ni kwamba katika utaratibu mzima wa kukopa maneno ni kwa ajili ya kuongeza uelewa zaidi, lakini pia ni katika kazi ya uundaji istilahi na kuongeza baadhi ya msamiati wa maneno mengine yenye umuhimu mkubwa. Kwa hakika maneno 289 yenye asili ya Kiarabu yaliyotafitiwa katika kazi hii ni kidogo sana, kwani kuna maneno kama hayo zaidi ya 10,000 katika Kiswahili.

Bilashaka hili ni jambo zito hasa pale maneno na istilahi hizo pamoja na kupatiwa maana, hapa panahitaji uhakika wa maana inayotakiwa pamoja na uhalisia wake.

Utafiti umefanywa katika Kisiwa cha Unguja, Mjini Zanzibar. Mtafiti alitumia mbinu au njia ya dodoso ili kuweza kupata taarifa sahihi alizohitajia katika sehemu ya kwanza ya ukusanyaji wa data. Sehemu hii iliwahusisha zaidi wanafunzi wa ngazi ya Shahada ya Kwanza na Stashahada ya Lugha. Vile vile ilifanyika kwa njia ya mahojiano yaliyowahusisha watu mbalimbali pamoja ambao ni walimu tena weledi wa Kiswahili na Kiarabu. Hawa wote ni Waswahili wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kiswahili. Sehemu ya pili ya ukusanyaji wa data, ilifanywa kutoka maktabani kwa kupitia vitabu mbalimbali vya Kiarabu na Kiswahili pamoja na makamusi.

Eneo la utafiti huu, lilijikita kwenye nomino, maneno hayo yenye asili ya Kiarabu, katika Nyanja za Kijamii, Kidini, Kibiashara (kiuchumi), Kiutawala (kisiasa), Kitaaluma, Kifedha na Kiujenzi. Jumla ya maneno 289 yalikusanywa, kila neno kati ya hayo limeainishwa mabadiliko yake yaliyotokea kifonolojia na kisemantiki baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili.

Wakati wa utafiti huu, mtafiti alikumbana na matatizo yakiwemo ugumu na uchache wa upatikanaji wa fedha hili ndilo lililopelekea utafiti huu kufanywa zaidi Kisiwani Unguja. Pia kulikuwa na ucheleweshwaji wa taarifa mrejesho hasa katika hatua za awali baada ya uteuzi wa Pendekezo la Utafiti. Uchache wa marejeo hasa kwenye kazitangulizi, hali hii inatokana na kuwa nyanja hii haijafanyiwa kazi sana. Pamoja na kuwa nyanja hii haijaandikwa sana, hata hivyo mtafiti aliangalia kazi zilizokuwa na uhusiano na mada ya utafiti huu ambazo zimefanywa na watu wengine, lakini tatizo kubwa zaidi ambalo lilikuwa likimkwaza Mtafiti ni muda, pamoja na kazi hii ya

utafiti, Mtafiti alipewa majukumu ya kufundisha ngazi ya Shahada ya Kwanza na Stashahada.

Mtafiti amesainisha baadhi ya Nadharia alizozitumia katika Kazi hii pamoja na uchambuzi wa data kama vile Nadharia kuu kongwe ya istilahi ya Woster (1960); Nadharia Jamii ya Uundaji Istilahi; Nadharia ya Saikolojia ya Tabia Pavlo (1957) na Skinner (1971); Nadharia ya Uhalisia.

Baada ya ukusanyaji, uchambuzi wa data na taarifa, mtafiti amebainisha kwa kutoa matokeo ya Utafiti huu. Matokeo hayo ni mabadiliko ya maneno yaliyotafitiwa katika kazi hii, maneno ambayo ni ya asili ya Kiarabu katika Kiswahili kwa mujibu wa nyanja zilizoainishwa ambazo maneno hayo yamepatikana.

Baada ya matokeo hayo, Mtafiti anakamilisha kazi yake kwa kutoa mapendekezo kutokana na utafiti huu alioufanya.

Mtafiti anahitimisha kwa kutoa Muhutasari wa kazi hii. Mwisho kabisa amesainisha Marejeleo mbalimbali aliyotumia katika kazi nzima ya Utafiti huu pamoja na viambatisho muhimu.

MAREJELEO

Abdel-tawab, R. (1997). *Al-mad-khal ila Ilmi llugha wa Manahiji-l-bah-thi llughawiy*. Scnd Edition, Maktabatu-l-khanji. Cairo.

Abubakr, Y.E (1992). ‘ El-Huruwfu-l-Arabiya wa Llughatu-l-Afriqiya’. *El-Arabiya fi-llughaati-l-Afriqiyati* Uk. 11-41 ALESCO. Tunis

Akidah, M . A (2013) ‘ Phonological and Semantic change in Language Borrowing – The Case of Arabic words Borrowed in to Kiswahili’. *International Journal of Education and Research* Vol. 1 No. 4 April 2013.

Allen, James de Vere (1981). ‘ Swahili Culture and the Nature of East Coast Settlement’. *The International Journal of African Historical Studies*. 14.2 : 306-334. <[http:// links. Jstor.org/sici?03617882%289181%2914%3A2%3C306%3ASCATNO%3E2.0.CO%3B2-D](http://links.jstor.org/sici?03617882%289181%2914%3A2%3C306%3ASCATNO%3E2.0.CO%3B2-D)>.

Allen, J. de V. (1979) *Swahilisation: A Cultural Concept and Its Significance in Kenya Today*, Paper 125, Institute of African Studies, Nairobi.

Allen, J. W. T. (1970) *The Swahili and Arabic Manuscripts in the Library of the University of Dar es Salaam: a Catalogue*, Leiden.

Alidina, M. M. H., The Persian Factor in Kiswahili, *AFRICA EVENTS*, May 993:30–31, London.

Anna, W. (1992) . *Semantics Culture and Cognition*. Oxford University Press.

April, M. S.Mc Mahon (1994) *Understanding Language change*. Cambridge University Press.

Baalbaki , R. (1993). *Al-Maurid A Modern Arabic Dictionary*. Dar- El-Ilm Lilmalayin. Beirut.

- BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Oxford University Press. Nairobi.
- Bin ubaad, S. (). Al-muhytu fi-l lugha, <http://www.warraq.com>
- Bosha, I.A. (1993). *Taathari za Kiarabu Katika Kiswahili, Kamusi Tathlitha Kiswahili Kiarabu na Kiingereza*. Dar es Salaam University.
- Dereyd, A.M.H. (----). *El-shtiqaqu*. El-khanji Press, Juzuu ya Kwanza. Chapa ya Tatu. Cairo.
- Chaker, A. (2012). *Ilm Al-ḡwaut Al-Arabiyya* 1st ed. Dar Al-Kotob Al-Ilmiyah. Beirut.
- Chiraghdin, S. Mnyampala M.E. (1997). *Historia ya Kiswahili. Nairobi* . Oxford University.
- Craig, Albert M., et al (2006). *The Heritage of World Civilization Volume Two: since 1500* 7th ed. Upper Saddle River. Prentice Hall.
- David, S. (2000). *Language and the Lexicon. An Introduction*. NewYork. Oxford University Press.
- El-Farahidi, K. A. (-----). *Kitaab El-Ayni*. Chapa Mpya 2003 Dar El-Kutub El- Ilmiya. Beirut.
- El-Jar, K. (1973). *Larous Modern Arabic Dictionary*. Maktab Larous.
- El-jawhari, (---). *El-Sihahu Fil-lugha*. URL <http://www.alwarraq>.
- El-jawhari, I.H. (1987). *El-Sihahu Taj el-lugha wa Sihahu El- Arabiya*. Chapa ya Nne. Dar el- Ilmi li-l-malayin. Beirut.
- El-Mandhour, I. (-----). *Lisaan El-arab*. Dar El- Maarif. Cairo.
- El-Zubaidi, M.M.A (----). *Taj- El- Arous min Jawahir El-Qamous*. Juzuu ya II. <http://www.alwarraq>.

- Fairozabaadi, M.M.Y (-----). *Al-Qamoos Al-muhiytū*. Chapa ya Tatu Amiriya Printing Press 1302 H Beirout.
- Freeman-Greenville, G.S.P.(1988). *The Swahili Coast, 2nd to 19th Centuries*. London.Variorum Reprints.
- Ghanem, K.S.M. (1995). Lexical Relatedness Kiswahili and Arabic. M.A Thesis, Universty of Dar es Salaam.
- Grey, J. (1962). *History of Zanzibar from the Middle Ages to 1856*. London.
- Habwe, J. H. (2010). ‘Politeness Phenomena: A Case of Kiswahili Honorifics’. *Swahili Forum* 17 (2010) 126-142.
- Harries, Lyndon (1964). ‘The Arabs and Swahili Culture’. *Africa: Journal of the International African Institute*.34.3 : 224-229.
- <http://links.jstor.org/sici?sici-0001-9720%28196407%2934%3A%3C224%3ATAASC%3E0.CO%3B2-C>>.
- Kasper, G. (1990). ‘Linguistic Politeness’. *Journal of Pragmatics* 14 (1990) 193-218, North Holland.
- Krum, B. (1940) . *Words of Oriental Origin in Swahili*, The Sheldon Press, Northumberland Avenue W.C. 2
- Lee, G. (1981). *Semantics- The Study of Meaning*. Lodon.
- Lodhi, A.Y. (2000). *Oriental loans in Swahili- A Study in Language and Culture Contacts*. Gothenburg.
- Lodhi, A. (2015). *Oriental Loanwords in Swahili*. Oford University Press Nairobi.
- Maganga, C. (1997). *Historia ya Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Malberg, B.(1963). *Phonetics*. New York. Dover Publications, Inc.

- Masamba, D.P.B. (2002). *Historia ya Kiswahili 50 BK hadi 1500 BK*. Nairobi.
- Masamba, D.P.B. na wenziwe (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu Sekondari na Vyuo TUKI*. Dar es salaam.
- Middleton, John (1992). *The World of the Swahili*. New Haven. Yale University Press.
- Miles, M. , Huberman, M,(1999). *Qualitative Data Analysis*. London.SAGE Publication.
- Mshindo, H.B. (2010). *Kufasiri na Tafisiri*. Zanzibar Uviversity College Printing Press. Zanzibar.
- Moustafa, I. (----). *EL- Muujam el-wasiyt*. Juzuu ya Pili. Daru El-daawa.
- Mwita , L.C. (2009). ‘ The adaptation of Swahili Loanwords From Arabic: A Constraint Based Analysis’. *Journal of Pan African Studies*; (2009), P 46.
- URL [http:// connection. Ebscohost. Com/ articles/38213835/ adaptation-swahili-loanword- from- arabi...](http://connection.ebscohost.com/articles/38213835/adaptation-swahili-loanword-from-arabi...) Tarehe 10 / 07 / 2014.
- Nurse,Derek, and Thomas Spear (1985). *The Swahili*. Philadelphia: University of Philadelphia Press.
- Omar, H.A. (1995). Athari ya Kiarabu kwenye Mjengeko wa sentensi katika Kiswahil.M.A Thesis, International Institute for Arabic Language. Khartoum.
- Ronald, W. L (1973). *Language and its Structure: Some fundamental Linguistic Concepts 2nd ed*. New York.
- Suleiman, A.I. (2006). Maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu katika Mtazamo wa Maana ya Kiutamaduni na Kilughawiya. M.A Thesis, International Institute for Arabic Language. Khartoum.
- Omar, A. S. (2002). ‘Kiswahili Request. Performance of Native Speakers and Learners’. *Journal of Pragmatics* (2002) 227- 252.

- Omar, A. S. (1992). 'Conversational Openings in Kiswahili, The Pragmatic Performance of Native and Non native Speakers'. *Pragmatic and Language Monographs Series Vol.3.* 20-32.
- Omar, A. S. (1996). 'Kanga Captions: Social and political communication with Application to Kiswahili language Teaching and Learning'. *Journal of Pragmatics* 161-178.
- Onuigbo, G. N. (1992). 'Linguistic Politeness and socio-cultural Variations of the notion of the face' *Journal of Pragmatics* 18 (1992) 309 -328, North Holland.
- Rāzi, M.A.A. (2014). *Mukhtar al-sahāha*. 3rd ed. Dar Sader Beirut.
- Sani, I. Abdullah, M.A. , Ali, A. M. and Abdullah, F. S.(2010). 'Linguistic Analysis on the Construction of Satire In Nigerian Political Cartoon: the Example of newspaper cartoons'. *Journal of Media and Communication Studies vol. 4 (3)* 52 – 59.
- Suweid, A. S. (1999). Ulinganishi baina ya Kiarabu na Kiswahili kweye Mjengeko wa Sentensi changamano. M.A Thesis, International Institute for Arabic Language. Khartoum.
- TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. 2nd ed. Oxford University Press. Nairobi.
- Yahya-Othman, S. () 'If the Cap fits: Kanga Names and Women's Voice in Swahili Society'. *A A P* 51 135 – 149 .
- Wikipedia, The Free Ecyclpedia. 'Arabic Language' . URL: en.wikipedia.org/wiki/Arabic_Language tarehe 10 /07 /2014
- Wikipedia, The Free Ecyclpedia. 'Swahili Language' . URL: en.wikipedia.org/wiki/swahili_language tarehe 21 /07 /2014.

Zawawi, S. (2004). *Loan words and their effect on Classification of Swahili Juornal*.
Leiden.

MAHOJIANO

- Hamad, A.M Elimu Shahada ya Pili, Kazi Mwalimu wa somo la
Kiswahili . Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.
(04 / 02 / 2015).
- Hamad, A.K Elimu Shahada ya Uzamili, Kazi Mwalimu Skuli ya
Kiswahili na Lugha za Kigeni - Chuo Kikuu cha Taifa cha
Zanzibar. (16 / 03 / 2015).
- Khamis, A.A Mwalimu Mstaafu wa Kiswahil SUZA, mwanafunzi wa
Shahada ya Uzamivu Chuo Kikuu Huria Tanzania.
(29/ 01/2015).
- Makame, A.M Elimu Shahada ya Uzamili, Kazi Mwalimu Skuli ya
Kiswahili na Lugha za Kigeni - Chuo Kikuu cha Taifa
cha Zanzibar. (06/03/2015).
- Makallo, A.M Elimu Shahada ya Uzamili, Kazi Mwalimu Skuli ya
Kiswahili na Lugha za Kigeni - Chuo Kikuu cha Taifa cha
Zanzibar. (11/05/2015)
- Rai, R. A Mratibu Baraza la Kiswahili Zanzibar (mwanzo alikuwa
mwalimu. (29/01/2015).
- Said, D.A Elimu Shahada ya Uzamili, Kazi Mwalimu Skuli ya
Kiswahili na Lugha za Kigeni - Chuo Kikuu cha Taifa cha

Zanzibar (23/03/2015).

- Suleiman, A.I Mwalimu wa Kiarabu SUZA, mwanafunzi wa
Shahada ya Uzamivu *Internatioanal Islamic University*
Malaysia (10/10/2014).
- Suweid, A.S Mwalimu wa Kiarabu Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar,
mwanafunzi wa Shahada ya Uzamivu Chuo Kikuu Nileyn
Sudan (01/ 01/2015).
- Ziddy, I.H Mkuu wa Skuli ya Kiswahili na
Lugha za Kigeni na Mwalimu wa Chuo Kikuu cha Taifa
cha Zanzibar. Elimu Shahada ya Uzamivu. (16/02/2015)

VIAMBATANISHO**KIAMBATANISHO A****DODOSO**

Maswali yanayotarajiwa kutumika kwa wadadisiwa ni kama haya yafuatayo, mdadisiwa atatakiwa kutia alama ya \surd katika MABANO yaliyopo mbele ya jawabu iliyotolewa :

1. Kwa kiasi gani unajua kwamba kuna maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili?
Kiasi kikubwa () Kiasi cha kati na kati () Sijui hata kidogo ()
2. Unafikiri maneno kama hayo yenye asili ya Kiarabu unayoyasikia yana dhana Mnasibu katika Kiswahili?
Ndiyo () Hapana () Sina hakika ()
3. Unakubaliana na njia inayotumiwa hivi sasa ya ukopaji wa maneno ya Kiarabu katika Kiswahili ?
Ndiyo () Hapana () Sijui ()
4. Unafikiri utoaji wa dhana mpya katika maneno ya Kiarabu ndani ya Kiswahili ni sahihi?
Ni sahihi kabisa () Sifikirii hivyo () Sijui ()
5. Katika maneno yenye asili ya Kiarabu ndani ya Kiswahili, unayafahamu maana zake?
Ndiyo nafahamu () Nafahamu baadhi yake kidogo tu ()
Sifahamu ()
6. Unadhani maana asilia ya maneno hayo ya asili ya Kiarabu inabakia kama ilivyo yakisha kuingia katika Kiswahili ?

Yanabadilika mno () Yanabakia hivyo yalivyo () Sifahamu ()

7. Je, kuna maneno hayo yenye kinyume cha maana baada ya kuingia kwenye Kiswahili ?

Ndiyo () Hapana () Sina hakika ()

8. Unakubaliana na utartibu huo wa kupewa maneno hayo kinyume cha maana katika Kiswahili?

Bila shaka ndiyo () Hapana ()

9. Unafikiri utaratibu kama huo wa kutoa maana kama hivyo ni sahihi ?

Hapana () Ndiyo () Sijui ()

10. Kama Ndiyo / Hapana ni kwa nini ?

Andika kwenye mapengo haya :

.....

.....

.....

.....

KIAMBATANISHO B**MASUALI YA MAHOJIANO KWA WALIMU/WATU MASHUHURI****WELEDI WA KISWAHILI.**

Jina.....

Umri :

Jinsia :

Elimu :

Kazi :

1. Tangu zamani kumekuwepo utaratibu wa kukopa au kuchukua maneno ya Kiarabu na kutiwa kwenye Kiswahili, yanaonekanaje maneno hayo katika unasibu wake kidhana na kimaana?.

2. Hivi sasa Kiswahili kinapiga hatua za maendeleo, lakini pia wigo wake wa kimatumizi umeongezeka. Ili kukidhi haja hiyo ya maendeleo na uongezekaji wa wigo hivi sasa, mbali ya kukopwa maneno ya Kiarabu, lakini ule utoaji wa dhana za maneno hayo, je unafikiri kuwa ni sahihi?.

3. Bilashaka, maneno yanayochukuliwa au kukopwa kutoka kwenye Kiarabu na kutiwa kwenye Kiswahili yanakuwa na maana, na hapa maana hii tunasema ni asilia. Kwa kutazama hali halisi ya hivi sasa katika mwenendo wa uchukuaji wa maneno hayo ya Kiarabu, maana hiyo asilia inabakia kama ilivyo pale maneno hayo yanapokwisha

kuingia katika Kiswahili?.

4. Ni kweli kwamba, neno linaweza kukopwa kutoka lugha moja kwenda lugha nyengine na likapewa maana tafauti na ile ya asili katika lugha ya mwanzo, kwa kukiangalia Kiswahili hivi sasa jinsi kinavyopewa maneno ya asili ya Kiarabu ambayo maana zake mpya katika Kiswahili zikawa hazina uhusiano kabisa na maana asilia kinyume na maneno ya lugha nyenginezo k.v Kiingereza n.k tunaona kuwa uhusiano wa maana asilia na zile maana mpya bado unakuwepo kwa kiasi fulani. Hili unalionaje?.
5. Kwa kuwa sisi ni mashahidi wa myenendo hiyo ya ukopaji wa maneno hasa ya Kiarabu, kwa muktadha huo unafikiri kwamba kuna maneno ambayo yana kinyume cha maana hasa baada ya kwisha kuhamia katika Kiswahili?.
6. Pengine kama yapo hata kama si mengi, au hata yakawa mengi maneno hayo, ni jambo gani au sababu zipi zinazopelekea hali hiyo?.
7. Katika kujaalia vyovyote, ikiwa utaratibu huo wa utoaji wa maana hasa iwe sahihi au si sahihi, una maoni gani juu ya kadhia hii ya maneno hayo?.

Ahsante sana

KIAMBATANISHO C

Tafsiri za maelezo ya Wahojiwa

Utangulizi

Baada ya mahojiano kufanyika baina ya Mtafiti na Wahojiwa, mara tu baada ya kwisha kupata maelezo yaliyotolewa na wahusika; Mtafiti alitoa tafsiri ya maelazo yao hayo kwa kuzingatia vipengele muhimu vilivyofanyiwa mahojiano wakati wa kukusanya data za utafiti huu. Tafsiri hiyo ni kwa kila mhojiwa kati ya wahojiwa kumi. Tafsir hiyo iliyofanywa ni kama hivi ifuatavyo:

Mhojiwa Na.1 miaka 46. Tarehe 10/10/2014

Kwa uapande unasibu wa dhana na maana ya maneno yanayokopwa kutoka kwenye Kiarabu, kwanza ni ukweli usiopingika kwamba Kiswahili kina maneno mengi kutoka kwenye Kiarabu. Baada ya maneno hayo kuingia kwenye Kiswahili kuna mwengezeko wa maana katika baadhi ya maneno na vilevile kuna ufinyu wa maana katika baadhi ya maneno. Lakini pia yapo yale yaliyobakisha maana yake ya asili iliyoko katika Kiarabu kwa maana ya kwamba, hiyo maana haikubadilika.

Unasibu wa dhana na maana upo katika baadhi ya maneno, bali yapo yale yaliyokuwa hayana unasibu wa dhana kutokana na kuacha kabisa uasili wake wa kimaana na matokeo yake maneno hayo yamechukua maana nyengine mpya katika Kiswahili. Vilevile yapo yale ambayo hayana unasibu wa dhana lakini yamepata maana.

Katika usahihi wa utoaji wa dhana mpya ya manenano yanayokopwa kutoka kwenye Kiarabu. Maneno yanayopewa dhana mpya kwenye Kiswahili, yanaingizwa hivi hivi tu pasi na kuwa na vigezo vya kitaalamu, alimradi tu madamu jamii inayakubali na kwa kuwa hayana ukakasi na karaha. Lakini ipo haja kubwa ya kuzingatiwa uasili wake wa dhana katika lugha ya awali. Kwa hali hii ya hivi sasa jinsi inavyokwenda, mtiririko wa utoaji wa dhana unakuwa si sahihi.

Katika muktadha wa kubaki kwa maana asili, kama ilivyo katika Kiarabu baada ya maneno kama hayo kuingia katika Kiswahili, kuna hali ya kutozingatiwa uasili wa maana, hususan katika hizi istilahi zinazobuniwa kwa kukopa maneno yake kutoka kwenye Kiarabu. Inaonekana kinacholetwa hapa ni maana nyengine ambayo ni mpya kabisa na ni tafauti na ile maana ya asili ambayo ndiyo ya msingi inayohitaji mazingatio kwanza. Jambo bora ni kupata maneno yanayobeba maana asili na katika hali kama hiyo, maneno hayo yangeweza kuchangia katika kutoa maana madhubuti na nzuri tena ya kutegemewa kabisa. Lakini kinachoonekana hapa ni kuwa zaidi linaangaliwa neno kutokana na uzuri wake wa matamshi, na si kwa maana yake asili halisi ilivyo. Kinachokosekana ni kutokuchunguza maneno au istilahi hizo tangu mwanzo katika muktadha huu.

Suala la kuwepo uhusiano wa maana asilia katika maneno yanayochukuliwa kutoka kwenye Kiarabu na kuingizwa katika Kiswahili, hili linakosekana. Inaonekana kwamba, katika maneno kama hayo hususan yale yanayochukuliwa siku hizi hayana ufungamano huo katu, zile maana zake asilia na zile maana mpya ni mambo mawili tafauti.

Kwenye kinyume cha maana ya maneno, katika huu mtiririko wa ukopaji wa hivi sasa; pamoja na kwamba kuna maneno yaliyoingia kwa kupitia vinywa vya watu wa kawaida tu; si vyema kuchukua neno na hasa kama istilahi kutoka kwenye Kiarabu likapewa maana ya kitaalamu bila ya hata kuchunguzwa jinsi vile linavyostahiki kufanyiwa.

Sababu kubwa ya hali hii inatokana na kutokujua lugha yenyewe ya Kiarabu au kukosekana utaalamu wa lugha ya Kiarabu, lakini kubwa zaidi ni kutokana na chuki ima za kisiasa au za kidini ambapo mambo haya ndiyo yanayopelekea dharau ya aina fulani. Kwa kuwa Kiswahili, kwenye uga wa msamiati, kwa kiasi kikubwa kiko karibu na Kiarabu, kwa hivyo neno lolote linalotokea karibu ya watu huwa linachukuliwa au kwa lugha ya sasa linabambikizwa maana wanayoiona wao kuwa inaelekea na hasa kwa kuzingatia raha na ladha inayosikika masikioni.

Kutokana na tafsihi inayopatikana kwa kupitia maoni ya mtafitiwa, ni kuwa bidii na hima ya kufundisha Kiarabu ni ndogo au haipo kabisa, hivyo basi yale mahusiano ya kilughawiya yaliyokuwepo baina ya Waswahili na Waarabu hayapo tena na kama yapo basi ni historia tu. Watu wa kaumu mbili hizi na lugha zao ndani yake kumekuwa na vipengele vya utamaduni ulioingiliana. Iliyokuwa lugha hiyo ya Kiarabu ina mahusiano na Kiswahili ni vizuri ikatiliwa mkazo katika kufundishwa tangu ngazi ya Elimu ya Maandalizi, Msingi, Sekondari na Vyuho Vikuu, kwani hapo baadae si tu kutakuwa na watu wanaoielewa lakini pia kutakuwa na wataalamu ambao wataweza kufanya tafiti za lugha ya Kiarabu na Kiswahili kwa umakini na uhakika. Na hapo itawezekana zaidi

kuchukua au kukopa maneno kutoka kwenye lugha hiyo katika hali ya kuwa na uhakika wa maneno na kuyapatia maana mnasibu inayostahiki.

Mhojiwa Na. 2 maiaka 67. Tarehe 16 / 12 / 2014

Unasibu wa makubaliano juu ya dhana na maana kwenye maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili. Hali hii ipo, lakini kwenye maana, kuna hali ya uepukaji na pia kuwa mbali na uasili wa maana ya maneno. Hali hii ni kwa maana ya kwamba kuna mabadiliko yenye maana mpya katika Kiswahili.

Kutokana na ukuaji na maendeleo ya Kiswahili hivi sasa, utaratibu wa utoaji wa dhana hauko makini na una mashaka mashaka. Utoaji huo wa dhana unasababisha kengeuko kubwa la maana. Hii maana yake ni kwamba hauna usahihi. Hali hiyo ya kutokuwa na usahihi imesababishwa na wachukuaji/waazimaji wa maneno hayo hawakufanya na hawafanyi uchunguzi wa kutosha kwenye maneno hayo yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili kabla ya kuyaazima.

Suala la kubakia kwa maana asilia, hasa kwa yale maneno yanayochukuliwa wakati huu. Maana asilia inaondoka kabisakabisa katika baadhi ya maneno hayo yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili. Katika jumla ya hali inayochangia, ni utandawazi na mazingira nayo yanachangia kwa kiasi fulani katika suala hili.

Kwenye uhusiano wa maana asilia na zile maana mpya, tatizo kubwa ni kuwa hakuna mazingatio juu ya hili. Kwa maana hiyo hakuna uhusiano wowote wa mambo mawili haya katika kadhia hii.

Kuwepo kwa maneno yenye kinyume cha maana baada kwisha kuingia katika Kiswahili. Kwa muonekano mkubwa hilo lipo tena kwa kiasi kikubwa sana, ni kutokana na kuacha kufuata taratibu na kanuni zilizopo katika suala zima la kukopa maneno hayo. Ndio maana mfumo mzima huu wa upande wa maana unaendelea kimakosa.

Sababu za maneno hayo kuwa na kinyume cha maana, inaonekana kwamba kuna makosa yanayotendeka katika uteuzi wa maana. Kuwaiga watangulizi katika kuendelea na mkumbo wa makosa, kwani wao huko mwanzo walilifanya hili pengine iwe si kwa kukusudia au hata kama kwa kukusudia. Kuwa na pupa ya kuandika bila ya kufanya uchunguzi lakini na hao waandishi kutoijua lugha yenyewe ya Kiarabu.

Maoni juu utaratibu wa utoaji wa maana hasa kwenye maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu, jambo muhimu kabla ya kitu chochote ni kusoma na kufanya utafiti. Mambo mawili haya yakifanywa utapatikana ujuzi zaidi. Kuepuka makosa yaliyofanywa huko nyuma, lakini pia kusahihisha makosa kama hayo endapo yatagundulika. Kiarabu ni kimoja katika vyanzo vya taaluma za Kiswahili, kwa hivyo si umuhimu tu bali kuna na ulazima wa kujifunza na kukisoma Kiarabu.

Mhojiwa Na. 3 miaka 55 .Tarehe 01/01/2015

Maneno mengi, katika upande wa dhana ni mnasibu. Lakini yapo machache hayana unasibu wa dhana na maana.

Utoaji wa maana unaonekana kuwa na usahihi, kwa kuwa tayari maneno kama hayo ndiyo yanayotumiwa na jamii. Maana hiyo wakati mwengine si lazima iwe mia juu ya mia kama maana asilia ya Kiarabu.

Maneno mengi yaliyochukuliwa au yaliyokopwa yana maana ile ile, lakini mengine yanapewa dhana nyengine.

Uchukuaji na upewaji wa maana ni wa kulazimisha

Hakuna kinyume cha maana, bado maneno yanaendelea na yanakwenda kwa misingi ya uelewa wa lugha ya Kiarabu kutokana na watu kuielewa Kuraan.

Sababu kubwa ya baadhi ya maneno kuwa na kinyume ni ukosefu wa utaalumu na ujuzi wa lugha ya Kiarabu pamoja kukurupuka katika kutoa / kukopa maneno ya Kiarabu.

Maoni juu ya maneno yaliyokopwa:

Kwanza kufanywa utafiti wa kina juu ya maneno yaliyoingizwa kwenye Kiswahili.

Kuyatazama maneno yaliyoingia kwenye Kiswahili hivi karibuni, yanaingia vipi na vyombo vinahusika vipi mpaka yakakubalika.

Kupigwa marufuku kutumia istilahi na maneno ambayo siyo.

Kuwa na utaratibu maalumu wa kuingiza istilahi/maneno pamoja na kuwa na vyombo makini vyenye wataalamu wanazuoni wa lugha na fani hizo.

Kupimwa, kuthibitishwa na kuelekezwa vipi maneno na istilahi zitumike.

Watu wanaolazimisha ni wale wenye mamlaka ya juu, wanaharibu kutokana na uwezo wao mdogo wa Kiarabu kwenye kadhia hii.

Mhojiwa Na. 4 miaka 58. Tarehe 29/01/ 2015

Unasibu wa dhana na maana kwa baadhi ya maneno haupo.

Ubadilikaji wa maana unakuja katika maneno mengi yanayokopwa kutoka kwenye Kiarabu. Baadhi ya maneno yanasaza maana yake ile ya asili na baadhi ya maneno yanabadilika maana yakisha kuingia katika lugha ya pili.

Ili kuthibitika kuwa neno lililokopwa kuwa ni la lugha ile iliyokopa, kuna mambo matatu yafanyike, kwanza matamshi ya tahajia yake, pili tafauti ya matamshi yake, tatu, neno lenyewe ndilo kutoka kwenye lugha asili.

Si sahihi, kwani kuna maneno mengine kwenye lugha asili yana athari zake ambazo Waswahili hawazijui. Watu wanavutiwa na uzuri wa neno jinsi linavyosikika na siyo maana linayoibeba. Mnasaba wa maneno ni lazima uzingatiwe wakati maneno yanapokopwa kutoka kwenye Kiarabu, lakini pia yaangaliwe kikazi, kidhana na kimaana kama hayana ukaraha. Uhuru wa matumizi ya lugha isiwe ni kisingizio cha kufanya makosa.

Baadhi ya maneno yanabadilika maana, lakini kuna mengine yanabakia kama yalivyo.

Baadhi ya maneno, uasili wake unakosekana, sababu kubwa ya hali hiyo ni kutokana na kutokujua lugha yenyewe. Neno linapokopwa, ihakikishwe kuwa haliopotoshwi kimaana. Kutokana na utaratibu huo wa kutokuhakikishwa, ndipo unapotokea uharibifu wa lugha. Maneno yenye kinyme cha maana yaainishwe kwa kufanyiwa utafiti.

Sababu kubwa ni kutokujua lugha ya Kiarabu, hali hii ndiyo inayopelekea mazoea yasiyosahihi.

Kuhusishwa matumizi ya maana ile ya asili ya maneno yaliokopwa baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili. Maana iangaliwe kwanza kwa umakini, kusoma na kujifunza lugha ya Kiarabu. Kufanya utafiti, kuepuka kuiga kutokana na kusikia tu.

Mhojiwa Na. 5 - miaka 46. Tarehe 04/ 02/ 2015

Kutokana na kufuata fonetiki na fonolojia ya Kiswahili, unasibu wa kidhana na kimaana unaonekana kuwa ni mzuri. Kwa upande wa maana, kuna tafauti kwa kuwa dhana inakwenda sambamba na maana ili kukidhi kile kilichokusudiwa ingawa inakuwepo na tafauti.

Baadhi ya wakati, utoaji wa dhana unakwenda sawa, lakini wakati mwengine unakiuka hali nzima lakini pia unatoa dhana finyu kabisa. Utoaji wa dhana wa

ya aina hii si sahihi, ndani yake kuna makosa ingawa wakati mwengine kuna ishara ya usahihi kidogo. Hiyo ishara ndogo ya usahihi ndiyo inayochukuliwa kuwa ni kigezo na kuhalalisha dhana.

Maana asilia haibaki na kuna tafauti kubwa, kwa baadhi ya maneno inabakia.

Kuna tatizo, tatizo lenyewe ni kwamba maneno yanajitokeza na maana ambayo hailingani na kule neno linakotoka. Ilivyo, maneno yakiingia kwenye lugha nyengine yanakubaliana na ule uasili wa lugha chanzi ijapokuwa kuna mengine hayalingani.

Maneno yenye kinyume cha maana yapo, hapa pana tatizo; maneno haya yanakwenda kinyume na uasili wake.

Sababu kubwa ya hali hiyo ya kuwa na kinyuma cha maana kwa baadhi ya maneno ni kukurupuka katika kuchukua dhana tu bila ya kuzingatia asili ya neno. Waundaji na wasanifishaji wa maneno hawakufanya na hawafanyi utafiti wa kutosha.

Maoni:

Kama upo uwezekano wa kubadilisha yale maneno yenye matatizo ambayo tayari yameshaingia kwenye Kiswahili basi ni vyema kufanywa.

Kufanywa marekebicho na kutolewa maelzo ingawa hapa patakuwa na suala la kukubalika mbele ya jamii kutokana na maneno kama hayo kuzoeleka na kupata mashiko.

Kuzingatiwa uasili wa maneno kama hayo yaliyoko kwenye Kiswahili ili iwe kama lugha nyenginezo.

Watu wasikurupuke hasa wanaofanya kazi hii ya usanifishaji na uundaji wa maneno hasa ya kukopa kutoka kwenye Kiarabu.

Jambo la busara ni kufuatilia na kuuliza juu ya maneno yanayokopwa au yaliyokopwa kutoka kwenye Kiarabu.

Kushirikishwa watu wengine katika kuwauliza kuhusu maneno ya Kiarabu yanayokopwa.

Kwani hali hiyo itasaidia katika upatikanaji wa dhana sahihi na nzuri.

Kwa kuwa Kiarabu kina nafasi muhimu katika taaluma za Kiswahili, watu wasome na wajifunze lugha ya Kiarabu.

Mhojiwa Na. 06 miaka 53. Tarehe 16/02/2015

Kwanza, kwenye unasibu wa dhana na maana katika maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu ni wa kawaida hasa kwa wale wanaokijua Kiarabu na wale watu wa zamani.

Pili, kuchukuliwa kwa maneno ya Kiarabu kwenye Kiswahili ni jambo lenye ufungamano na Historia. Watu wengi walikuwa wanakifahamu Kiarabu na Kiswahili, kwa hivyo kukopa maneno lilikuwa ni jambo la kawaida. Lakini katika wakati wetu huu wanaozungumza Kiswahili ni wengi laikini hawajui Kiarabu kwa hivyo kumekuwepo na ugumu wa aina fulani hasa katika kuelwa lugha hiyo.

Katika usahihi wa utoaji wa dhana. Hapa panajitokeaza makundi mawili. Kundi lile linalojua Kiarabu na hasa wale wenye umri mrefu kidogo, kundi hili bilashaka

halikotayai na mabadiliko ambayo yanakwenda kinyume na vile lilivyo zoea huko mwanzo. Kundi jengine la pili ni lile ambalo halifahamu Kiarabu. Kwa kundi hili haitakuwa rahisi kwao kukubali, kwani lugha inakua kwa hivyo ni lazima ipate maneno ili yende na wakati.

Kubaki kwa maana asilia baada ya neno kwisha kuingia kwenye Kiswahili. Katika hali hii, kuna yale maneno ambayo maana yake asilia inabaki takriban kama ilivyo, hili ni kundi la kwanza. Lakini kundi la pili ni la ya yale maneno yanayobadilika maana asilia hata kama maneno hayo siyo mengi. Ambapo maana yake ni kuwa ubadilikaji wake huo pamoja na maana unakuwa hautoki moja kwa moja kwenye eneo husika kimaana.

Kuhusu mtazamo wa maneno ya Kiarabu yanayopata maana nyengine kwenye Kiswahili, kwanza hivi sasa maneno ya Kiarabu siyo mengi kama inavyosemwa kuwa yanaingizwa katika Kiswahili. Ni kweli yapo yaliyoingizwa lakini si kwa kiasi kikubwa, na hali hiyo inatokana na sababu ya kwamba hao wataalamu wengine wenyewe, Kiarabu kiko mbali nao yaani kwa lugha rahisi ni kuwa hawakijui na kwa hivyo hata hayo maneno yanayoingizwa wao hawayajui kama ni ya Kiarabu.

Kuhusu kinyume cha maana na ule uasili wake. Maneno kama hayo yapo na yanakuwa yakipewa maana nyengine ambayo ni tafauti na yenye kinyume cha maana hasa.

Kwanza ni vyema kutambua kwamba siku hizi, Kiarabu kwa kiasi kikubwa kinawapa watu tabu yaani hawakijui. Ama kuhusu sababu zinazopelekea maneno hayo kuwa na

kinyume cha maana, kwanza kutojua maana halisi za maneno yenyewe kwenye Kiarabu, inawezekana mtu kalisikia tu neno linatajwa mahali na yeye akalichukua na kulitumia visivyo na baadaye kuenea katika vinywa vya watu. Pili upinzani juu ya maneno yanayo asili ya Kiarabu kuonekana mengi kwenye Kiswahili. Hii maana yake ni kwamba lengo kubwa ni kuiondoshia ile nadharia inayosema kwamba kwenye Kiswahili kuna msamiati mkubwa na mwingi wenye asili ya Kiarabu.

Maoni :

Kwa kuwa lugha ni lazima ikue kama inavyokua jamii yenyewe na watu wake, na kwa kuwa ni lazima ibadilike kama mambo yanavyobadilika. Kwa hivyo basi yasiogopwe mabadiliko na pia kupata mambo mapya. Ikiwa kwenye Kiarabu kuna mambo mapya basi si vibaya maneno ya mambo mapya hayo yakapendekezwa na kuchukuliwa na hatimae kutiwa kwenye Kiswahili hata kama yatabadilishwa matamshi lakini maana isiwe mbali sana na ile ya Kiarabu, hilo ndio jambo la msingi.

Kujifunza lugha ni muhimu, watu wajifunze hasa lugha ya Kiarabu.

Ni vizuri kutunza lugha zetu na kuzisoma kwa sababu hiyo ndiyo asili yetu.

Mhojiwa Na. 7 miaka 50. Tarehe 06/03/2015

Kwenye unasibu wa dhana na maana, kwa baadhi ya maneno yana mnasaba wa dhana na maana kwenye Kiswahili lakini pia yapo yale ambayo hayana unasibu wa dhana na maana. Kuna haja ya kuangaliwa upya kwenye nyanja hii ya unasibu wa dhana na maana.

Kuhusu utoaji wa dhana, ingawa siyo mia juu ya mia, kwa kiasi fulani utoaji wa dhana sio sahihi. Hali hiyo zaidi iko kwenye yale maneno yanayozushwa hasa hivi sasa, kwani

wanaofanya hivyo hawana ufahamu na uelewa wa lugha ya Kiarabu. Kwa hivyo basi, yanapatikana maneno ingawa ni machache, yenye dhana tafauti baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili.

Katika kubakia kwa maana asilia kama ilivyo baada ya kwisha kuingia kwenye Kiswahili, kuna baadhi kubwa ya maneno ambayo maana yake asilia hiyo inabakia. Na ipo baadhi ndogo ya maneno hasa yanayochukuliwa hivi sasa, yanapata maana mpya na kuacha kabisa ile maana asilia.

Kuhusu uhusiano wa maana mpya. Kutokana na kutokuwepo uhusiano huo, inaonekana ule umuhimu wa kuyapatia maneno hayo na udurusu stahiki ili kuweza kubaini kasoro na kuzirekebisha kasoro hizo. Uzoefu wa nyuma unaonesha kwamba maneno yenye maana iliyo na ukakasi au maana iliyokuwa siyo yanaweza kuzuilika, kwa hivyo na hata hiyo maana pia nayo inawaza kurekebisha.

Kuhusu kuwepo maneno yenye kinyume cha maana, yapo maneno yanayoidadika ambayo yana kinyume cha maana. Maneno hayo yanahitaji kufanyiwa uchunguzi zaidi. Mtafitiwa ameonesha hali ya utayari wake wa kushiriki katika kazi ya kuyakusanya maneno kama hayo.

Kuhusu sababu zinazopelekea kinyume cha maneno hayo, kubwa zaidi ni kutokufahamu lugha ya Kiarabu. Lakini pia kusikika kwa neno na neno hilo likawa linapendeza masikioni, kwa hivyo neno hilo huchukuliwa pasi na kuzingatiwa dhana ya neno hilo.

Maoni:

Kufanya mapitio ya maneno yenye kinyume cha maana.

Kuwa na ufahamu japo mdogo kwenye neno linalochukuliwa/ linalokopwa na kuingizwa kwenye Kiswahili.

Ingawa si kwa kiwango cha aina moja, watu ni vyema wakajifunza.

Kwa kuwa kuna imani ya kuwa Kiswahili ni chetu, kutokana na nafasi ya lugha ya Kiarabu katika Kiswahili ilivyo, hapana budi kwa Vyuho vya Zanzibar kushughulikia lugha mbili hizi yaani Kiswahili na Kiarabu na zifundishwe vilivyo ili hatimaye wapatikane watu watakao kuwa na uwezo wa kufanya utafiti kwenye lugha hizi.

Mhojiwa Na 8 miaka 61. Tarehe 16/03/2015

Kwa upande wa unasibu wa dhana na maana ya maneno yenye asili ya Kiarabu, maneno kama hayo yapo mengi katika Kiswahili. Watu wengi hawana uelewa wa maneno hayo na kwa hivyo hata ufahamu wao juu ya hili ni mdogo au haupo kabisa. Kuna watu wachache sana wenye uelewa pamoja na ufahamu wa kutosha. Kwa kuwa wale wengi wao, wanaona hayo maneno ni ya Kiswahili tu, kwa hivyo unasibu wa dhana na maana wanauona uko kwa kukiangalia Kiswahili tu ambacho ndio lugha yao wanayoifahamu.

Kuhusu usahihi wa utoaji wa dhana, kutokana na azma ya kutumiwa Kiswahili katika usomeshaji na ufundishaji, hapo mwanzo lugha hii ilikuwa haina msamiati na istilahi za kutosha zinazoweza ufundishaji kwa kutumia lugha hii wende vizuri na kwa ufanisi. Kwa hivyo maneno mbali mbali yalichukuliwa kutoka kwenye Kiarabu na kupewa dhana mpya katika Kiswahili, kwa kipindi chote hicho utoaji huo wa dhana ulionekana

kukidhi haja, hivyo bado unaonekana kuwa ni sahihi kutokana na kupatikana maneno na istilahi mbali mbali zinazohitajika katika taaluma.

Kubaki kwa maana asilia baada ya maneno hayo kwisha kuingia katika Kiswahili.

Pamoja na kwamba kutafuta usuli wa neno na kulipata lina maana gani kwa sasa hivi hilo ni jambo jengine. Lakini kila unapoongezeka utaalumu wa watu wetu kwenye Kiarabu ndipo hizi tafauti zilizopo na zitakazojitokeza zitapatiwa ufumbuzi kama si wa kuondoshwa kabisa basi ni kupunguza kwa kiasi kikubwa.

Kuhusu kuwepo uhusiano wa maana asilia ya maneno. Kuna matatizo ya kutumia maneno ambayo ukiangalia hata ile maana yake asilia inakuwa haina nafasi yoyote. Kuna haja ya kupata maelekezo juu ya maana asilia pamoja na hizo maana zinazozushwa. Bilashaka maelekezo haya yatatoa muongozo sahihi unaotokana na weledi au wataalamu.

Kuhusu kinyume cha maana. Maneno yenye kinyume cha maana yapo, lakini maneno hayo hayafahamiki kwa maana ya kuwa yana kinyume cha maana. Katika hali hiyo ya kutofahamika kumepelekea makundi mawili, kundi la wale wanaoona kuwa hali hiyo ya kinyume ibadilishwe hata kama maneno kama hayo yamekuwepo tangu zamani na kwa kiasi kikubwa yamekubalika na kuzoeleka. Kuna wale wanaoona kwamba yaachwe yaendeleo hivyo hivyo kutokana na kuzoeleka kwake kwa muda mrefu hata kama yalifanywa hivyo kimakosa kutokana na kutojua maana.

Sababu za kinyume cha maneno kama hayo. Kubwa zaidi katika hili ni kutokujua na kuifahamu lugha chanzi iliyotoa maneno hayo hasa kwa wale walioyachukua kutoka huko kwenye Kiarabu, katika mchakato wa awali kwenye ukopaji. Pili ni pupa ya kutaka lugha lengwa ipate msamiati na istilahi zitakazoweza matumizi muafaka katika ufundishaji kwa kutumia lugha lengwa yaani Kiswahili. Tatu uchache wa weledi na wataalamu wa Kiarabu kwa wakati huo kwenye mwendelezo au mchakato mzima wa kuyachukua maneno kama hayo.

Maoni juu ya maneno jinsi yanavyotolewa, utaratibu wa utolewaji wa maneno hayo una kasoro; kasoro hizo zitaondoka au kupungua kwa kiasi kikubwa kwa:

- Maneno yajayo yatakayokopwa kutoka kwenye Kiarabu, ni vyema na kwanza kuangaliwa namna gani yalivyo huko kwenye Kiarabu hasa kimaana kimatumizi. Uchunguzi mkubwa ufanywe.
- Yale maneno yaliyoingia na yakawa yana kasoro k.v. kinyume cha maana na makosa mengine ya kiisimu, hayo yaendeleo kubakia kutokana na kuwa ni ya muda mrefu na yameshapata mashiko kwenye jamii.
- Kuwa na makubaliano kwanza kabla ya maneno hayajatumiwa katika jamii.

Kwenye unasibu wa lugha kidhana na kimaana; unasibu wa dhana na maana uko katika hali mbili kwenye maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili, kuna yale yenye unasibu wa lugha hasa ile lugha chanzi, lakini pia yapo maneno mengine katika maneno hayo hayo hayana unasibu huo baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, hali hii ni kutokana na kupata maana nyingine ambayo ni tafauti na ile ya asili katika Kiarabu.

Kuhusu usahihi wa utoaji wa dhana, kwa baadhi kubwa ya maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili, upewaji wake wa dhana ni sahihi. Kuna maneno mengine ya kawaida na yale ya kiistilahi katika hayo yanaonekana kuwa na matatizo katika maana zake. Hali hii inaonesha kwamba dhana iliyotolewa siyo sahihi. Kinachojitokeza wazi ni kwamba yale maneno yanayokubaliana kimaana, upewaji wake wa dhana ni sahihi na yale ambayo hayakubaliani basi upewaji wake wa dhana sio sahihi.

Kuhusu kubaki kwa maana asilia ya maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili, kuna baadhi ya maneno ambayo maana yake kwa kiasi ina bakia na baadhi kati ya maneno hayo maana yake haibakii na inabadilika na kuwa tafauti na ile maana ya asili. Pamoja na kwamba lugha ni nasibu, lakini si kwa kukopa maana na baadaye kubadilishwa maana zake. Katika hali kama hiyo, unasibu kama huo unakuwa na kasoro.

Kuhusu namna yanavyoonekana maneno hayo yanayotoka kwenye maana asilia; labda iwe umetumika mtindo wa kuongeza msamiati, lakini kama kusudio ni kukopa maneno, basi ni kuchukuliwa maneno na kuwekwa katika utaratibu wa kisarufi wa lugha lengwa.

Lakini katika hali hiyo, vyovyote iwavyo, ile dhana ya neno au maneno hayo lazima iwepo, inawezekana ikatanuliwa au ikabanwa katika kutoa maana.

Kuhusu kuwepo kwa maneno yenye kinyume cha maana. Kutokana na ule utaratibu wa kutoa dhana isiyo sahihi, hali hiyo imechangia katika kupatikana kwa yale maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili yenye maana iliyo kinyume na maana asilia za maneno hayo.

Katika sababu zinazopelekea kuwepo kwa maneno yenye kinyume cha maana katika maneno yenye asili ya Kiarabu ndani ya Kiswahili, kama inavyojuilikana kwamba lugha ni ya jamii. Si jambo la kawaida kwamba katika kuundwa kwa maneno yote ya lugha kuwa wanajamii wote hukutana katika kikao chenye madhumuni hayo. Mara nyingi yule mhusika wa mwanzo anayelitoa neno kwa mara ya kwanza, ama neno hilo litakuwa lina ufinyu wa kimaana au tafauti kubwa ya kimaana vilevile, kwa hivyo watu hulipokea neno kama hilo katika hali yake hiyo ya mara ya kwanza na kuendelea kutumika.

Wakati mwengine migongano ya mawazo tafauti inayoibuka baina ya watu kilugha, mwishowe hali kama hiyo hupelekea kuzuka kinyume cha maana ya maneno fulani kwenye lugha.

Maoni:

Maneno ya zamani ambayo tayari yapo, yaendeleo kutumika kutokana na kuwa yameshapata mashiko kwa muda mrefu, kwa hivyo si rahisi kuyabadilisha.

Maneno mapya yatakayoingizwa katika Kiswahili, kabla ya kufanya hivyo ni vizuri kwanza kutafutwa wataalamu wa Kiarabu ili kupata ushauri wao hasa kwa upande wa maana.

Kwa kuwa inaonekana mara nyingi baadhi ya maneno yanapokopwa hasa haya yenye asili ya Kiarabu, unasibu wake unapungua, kwa hivyo yanapochukuliwa maneno hayo, ni vyema yawe na unasibu wake wa kimaana na ile maana asilia katika lugha chanzi.

Mhojiwa Na.10 miaka 44 Tarehe 11 /05/2015

Kwa upande wa unasibu wa dhana na maana ya maneno yenye asili ya Kiarabu. Kuwepo kwa unasibu wa dhana na maana kwenye maneno hayo, kuna kundi kubwa na lenye maneno mengi yenye sifa ya unasibu na dhana. Pia kuna kundi jengine lenye maneno si mengi ambayo hayana unasibu wa dhana na maana.

Kuhusu usahihi wa utoaji wa dhana, kukosekana kwa maana asilia, kunapelekea dhana tafauti ya matumizi ya neno, hali hii yote inasababishwa na ukopaji wa lile neno tu na si zaidi ya hapo. Kawa hivyo basi, ukopaji wa neno usiwe kwenye sauti na umbo lake tu, bali likopwe lote zima umbo, sauti, dhana na maana yake. Kubadilishwa kwa maana katika ukopaji huo, itakuwa tayari neno hilo husika limebaguliwa na kwa hivyo litakosa uhusiano kwa kiasi fulani kule lilikokopwa.

Kuhusu kubaki kwa maana asilia ya maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili baada ya kwisha kuingia katika Kiswahili. Hali hii inachangia kutokubaki maana asilia za

baadhi ya maneno hayo. Ni kigezo kipi kinachotumika katika ukopaji wa maneno hayo. Hilo la kigezo kwa kweli linakosekana kabisa kabisa.

Kuhusu namna yanavyoonekana maneno hayo yanayotoka kwenye maana asilia; maneno hayo yamechukuliwa na kupewa maana nyengine jambo ambalo kwa kiasi kikubwa ni kupotosha utaratibu mzima wa utoaji wa maana.

Kuhusu kuwepo kwa maneno yenye kinyume cha maana. Kinyume cha maana ya baadhi maneno ya asili ya Kiarabu katika Kiswahili, kinatoa taswira mbaya kwa yule mzungumzaji wa Kiarabu katika kujifunza Kiswahili kwa mara ya kwanza anapoyaangalia maneno hayo kwa upande wa maana.

Katika sababu zinazopelekea kuwepo kwa maneno yenye kinyume cha maana katika maneno yenye asili ya Kiarabu ndani ya Kiswahili, ni kwa kuyasikia maneno hayo na kwa kutoyajua maana, watu wanayatumia jinsi vile wanavyoona wao kwamba ndio sahihi, hali hiyo inakwenda kama hivyo mpaka maneno hayo kufikia kuingizwa katika makamusi ya Kiswahili.

Maoni :

Kutafutwa njia muafaka ya kuyaangalia upya maneno yenye kinyume cha maana na kuyabadilisha, kadhalika pia kuyarekebisha yale yanayotumika kwenye maandiko mbali mbali kama vile magazeti n.k.

Kwa yale maneno yenye asili ya Kiarabu yanayozushwa kimaana na yakawa yanatumika mitaani, hayo hayana haja ya kushughulikiwa bali yaachwe kama yalivyo na hatimae yatapotea na kuondoka wenyewe kabisa.

Utumiaji wa maneno ya Kiswahili usiozingatia usahihi wa maama, utumiaji kama huo hivi sasa nao unaathiri pia kwenye maneno ya Kiarabu.

Kutumika kikamilifu, wataalamu wa Kiarabu katika utaratibu mzima wa kuyabaini maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili yanayohitaji kuangaliwa na kupitiwa.

Lugha ya Kiarabu itiliwe mkazo wa kusomeshwa kwenye taasisi mbalimbali za elimu katika jamii.